

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 25 Aprili, 2019

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano, Kikao chetu cha leo ni cha Kumi na Sita. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu sana. (*Makofii*)

Swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali ifuatalo:-

Kwa kuwa Dira ya Maendeleo ya Nchi yetu ya Mwaka 2015 ni kufikia uchumi wa kati na uchumi wa viwanda ni kigezo kimojawapo; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza kwenye uchumi wa viwanda na imejitahidi kutengeneza mazingira mazuri kwa wawekezaji ili waweze kuja kuwekeza; hata hivyo, wawekezaji wengi wanakwamishwa na kusumbuliwa sana:-

Je, nini kauli ya Serikali kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasmine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nchi yetu imejikita katika kuboresha uchumi wake kupitia viwanda ambapo tumetoa fursa kwa Watanzania kwa mtu ye yeyote kutoka Taifa lolote kuja kuwekeza hapa nchini. Suala la uwekezaji tumelipa nafasi muhimu sana kwenye uwekezaji hasa kwenye viwanda.

Awali tulikuwa tunatumia tu Taasisi ya Uwekezaji nchini, lakini Serikali imefanya maboresha makubwa kwenye uwekezaji pale ambapo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli alipoianzisha Wizara Maalum ya Uwekezaji na kumteua Mheshimiwa Angellah Kairuki kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), kumteua pia Katibu Mkuu ili kusimamia uwekezaji kwa ukaribu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo hapa ni kuhakikisha kwamba tunaondoa usumbufu ambao wanaupata wawekezaji hao ili kuweza kuwekeza kwa urahisi zaidi. Hata

hivyo, kwenye uwekezaji sasa tumefikia hatua nzuri sana. Kwanza tumetengeneza andiko maalum (*blueprint*) ambayo imeonyesha njia rahisi za uwekezaji hapa nchini kwa lengo la kuondoa usumbufu kwa wawekezaji wetu. Kwa hiyo tumetengeneza mazingira rahisi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, pili, tumeboresha kituo cha uwekezaji kwa kukaribisha Wizara zote zinazoguswa na uwekezaji kwa kuwa na mtu wao pale kwenye Taasisi ili mwekezaji anapokuja, huduma zote kama mtu alitakiwa kwenda Wizara ya Ardhi, mtu wa ardhi yuko pale; akitaka kwenda *BRELA*, mtu wa *BRELA* yuko pale; anakwenda sijui *TFDA*; mtu wa *TFDA* yuko pale. Kwa hiyo, tuna idara kama 10 au 11 ambazo ziko pale za kumhudumia mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, badaa ya kuwa Wizara ile imeletwa Ofisi ya Waziri Mkuu, tumeanzisha mfumo wa kielektroniki ambao mwekezaji sasa anaweza kuomba leseni kutoka popote alipo. Tunatambua kuna wawekezaji wako nje ya nchi, haimlazimishi yeye kuja moja kwa moja Tanzania kuanza kujaza makaratasi. Anajaza huko huko Marekani kuomba nafasi, kupata ardhi, kupata ithibati ya uwekezaji hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumetengeneza hayo yote kurahisisha mfumo wa uwekezaji kwa lengo la kupanua wigo wa uchumi hapa nchini kuititia viwanda, kilimo, madini na kila eneo ambalo mwekezaji anataka kuwekeza, sasa Tanzania imefungua nafasi, imetengeneza mazingira rahisi ya uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito kwa Watanzania, kwa yeote kutoka Taifa lolote kuja kuwekeza nchini Tanzania, fursa tunazo na ardhi tunayo. Fursa hizi sasa tumezikaribisha hata kwenye Mikoa na Wilaya kutenga ardhi kwa ajili ya kukaribisha wawekezaji ili pia kuendelea kuongeza mapato ya Halmashauri yenyewe, Mkoa wenyewe na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Suala la vitambulisho kwa wajasiriamali wadogo wadogo imekuwa ni kero kubwa sana katika maeneo mbalimbali nchini na limekuwa ni kero kubwa zaidi kwa wajasiriamali wale wanaouza mboga mboga kama mchicha, nyanya, tembere, maandazi na vitumbua. Kibaya zaidi, maeneo mengine hata wale wanaotoka shambani, amechuma mchicha wake, anaambiwa naye ni Mjasiriamali aweze kutoa shilingi 20,000/= apewe kitambulisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala hili kwa mtazamo wangu mimi naona kama vile halijatafsiriwa vizuri kule chini hasa wale wanaolitekeleza kwa sababu maeneo mengine pia hata wapiga debe na walimu maeneo mengine wanaambiwa kwamba ni wajasiriamali waweze kulipia vitambulisho vyatya shilingi 20,000/=.

Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa swalilangu: Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka hili jambo lingeweza kusitishwa kwanza ili tuweze kufanya tathmini na kupanga vizuri kwamba hasa ni watu gani ambao wamelengwa na wenye mitaji ya namna gani? Kwa sababu kuna wengine wana mitaji ya shilingi 1,000/= wengine shilingi 2,000/=, lakini wanaambiwa walipe shilingi 20,000/= kwa ajili ya vitambulisho vyatya ujasiriamali?

SPIKA: Nilidhani ungeuliza swalibadala ya kuhutubia; lakini kwa ujumla umeeleweka. Hiyo habari ya walimu kupewa hivyo vitambulisho, wapi iko hivyo? Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu, tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalila Mheshimiwa Mwalimu Haonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeweuka utaratibu mzuri sana wa kuwafanya wajasiriamali wadogo

kuweza kuchangia pato la Taifa; na Mheshimiwa Rais alibuni njia nzuri ambayo inawatambulisha hawa wajasiriamali. Hata hivyo, wajasiriamali hawa tumewaweka kwenye madaraja yao. Wako wale wadogo, wako wafanyabiashara wa kati na wale wajasiriamali wakubwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliwalenga Serikali imewalenga hawa wadogo ambao kipato chao kutokana na kazi wanayoifanya hakizidi zaidi ya shilingi milioni nne kwa mwaka ili nao wapate nafasi ya kuweza kuchangia pato la Taifa lakini kuwaondolea usumbufu kwenye maeneo wanayofanya biashara kwa kutozwa kodi kila siku ambayo pia na yenye we inasaidia kupunguza mapato wanayopata kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa vitambulisho vile vilipotolewa kwa Wakuu wa Wilaya, tambua kwamba kuna maeneo mengine utekelezaji wake siyo mzuri, kwa sababu wako wengine wanalazimisha watu badala ya kuwaelimisha namna ya kupata vitambulisho hivyo. Yako maeneo wanapewa hata wale wajasiriamali wakubwa wenyepato la zaidi ya shilingi milioni nne, linawafanya na wao wanashindwa kuchangia kulingana na biashara wanazozifanya kwa sababu wao kwa *category* yao wanachangia *TRA* moja kwa moja, lakini wale wadogo hupitia vile vitambulisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maelekezo ambayo tumeyatoa tena baada ya kuwa tumepata malalamiko kutoka kwenu Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa watumie muda wao kuelimisha nani anapaswa kuwa na kitambulisho badala ya kutumia wakati mwingine nguvu au kwenda kulazimisha au kuwapa wajasiriamali wakubwa wenyepato zaidi ya shilingi milioni nne na kuondoa maana ya uwepo wa vitambulisho? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kupitia Mheshimiwa Mbunge Serikali tumeipokea hiyo. Tunaendelea kutoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watumie nafasi hiyo

kuelimisha zaidi kuliko kulazimisha, ni nani wanatakiwa wapate kitambulisho hicho ili kuwaondolea usumbufu wa kuwa wanatozwa fedha tena shilingi 200/=, shilingi 500/= kila siku anapoendelea kufanya biashara yake ya mchicha, maandazi, wale wanaokimbiza mahindi vituo vya mabasi.

Mheshimiwa Spika, watu wa namna hii ndio ambao Mheshimiwa Rais aliwalenga ili nao waone uchangiaji wa uchumi, pato la nchi ni sehemu yao lakini pia waendelee kufanya biashara yao bila kusumbuliwa ndani ya mwaka kwenye Halmashauri zao. Kwa hiyo, niseme tu, tumeipokea tena hiyo na tutaifanya kazi zaidi ili kuleta utendaji ulio sahihi na wajasiriamali waweze kujitoa kuchangia kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu katika swali lake amesema pia kwamba walimu wanalazimishwa wapewe vitambulisho vya wajasiriamali. Sijui hilo nalo unasemaje Mheshimiwa Waziri Mkuu?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Sawasawa, hilo limetokea Jimboni kwangu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la swali la Mhehsimiwa Mwalimu Haonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, inawezekana pia uko utekelezaji usio sahihi. Mwalimu kama Mwalimu ni mionganii mwa watu wenye pato la zaidi ya shilingi milioni nne kwa mwaka. Kwa hiyo, mwalimu anapofanya biashara, ile biashara anayoifanya kama yenye haimfikishi kwenye pato hilo, Mkuu wa Wilaya ambaye yuko kwenye eneo hilo, anajua mwenedno wa pato la huyo mtu ambaye yuko pale.

Mheshimiwa Spika, sasa suala la mwalimu na mfanyakazi mwingine, muhimu zaidi ni ile biashara anayoifanya, lakini pia namna ambavyo anaweza pia akachangia pato kupitia biashara hii anayoifanya ambayo

uzalishaji wake haifiki kiwango hicho cha shilingi milioni nne kwa mwaka. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Kama mtu ni mjasiriamali, ndiyo Waziri Mkuu ameeleza hivyo, kwamba unakwenda katika *category* hizo. Tunashukuru. Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kabisa katika Taifa hili kwamba sasa mazingira ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wetu katika nchi hii bado ni tete sana. Huwezi kuamini sasa hivi watu ambao walikuwa wanakuja kufanya biashara katika Jiji letu la Dar es Salaam, mfano watu wanaotoka Zambia, Congo, Zimbabwe, Angola na maeneo mengine, wamepungua sana kuja kufanya biashara, kununua mizigo Dar es Salaam na sasa wanakwenda Kenya, Uganda, wameanza kwenda Dubai wenyewe hata wenyе mitaji midogo ambao walitegemea kwamba Dubai yao iko Dar es Salaam kwa sababu ya usumbufu uliojitokeza kwenye Jiji letu la Dar es Salaam. Sasa hivi kimeundwa kikosi kinaitwa *Task force* ambacho kinakagua risiti za *EFD*:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imetengeneza rushwa kubwa sana kutokana na *fine* ya shilingi milioni tatu. Sasa hivi Maafisa *TRA*, Maafisa ambao wanajifanya Polisi na Maafisa ambao wanajifanya Usalama wa Taifa na wengine ni vibaka ambao sasa hivi siyo watumishi wa Umma, wameingia baada ya wafanyabiashara wengi kuwa na hofu na sasa wamejifanya nao ni watumishi wa Umma wameanza kuomba rushwa ya shilingi milioni moja, shilingi 1,500,000/= ili mradi tu...

SPIKA: Swali lako ni nini Mheshimiwa Mwakajoka?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo linarudisha uchumi nyuma. Kwa hiyo,

nilikuwa najaribu kujenga hoja ili Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu aweze kutoa majibu vizuri na kuhakikisha kwamba...

SPIKA: Uliza swali basi. (*Kicheko*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo, nataka kujua, ni lini Serikali itaondoa kero kwa wafanyabiashara hawa ambao wanalamika kila siku? Kwa sababu mwaka uliopita nilikueleza hapa ndani ya Bunge nikasema kwamba...

SPIKA: Mwakajoka nakuuliza kwa mara ya mwisho. Unajua mpaka sasa hivi hujauliza swali? Yaani swali lako ni nini hasa?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ninasema hivi; ni lini kero kwa wafanyabiashara zitaondoka ambazo zinalalamikiwa kila siku katika Taifa hili?

SPIKA: Ni kero ipi?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Kero za kodi, kero za *fine* za shilingi milioni tatu...

SPIKA: Nchi hii ifute kodi au ni nini?

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Siyo kufuta kodi.

SPIKA: Huna swali. Mheshimiwa Amina Mollel. (*Makof*)

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Swali langu ninapenda kufahamu, kwa kuwa takwimu za Taifa kwa sasa zinaonyesha kuwa kila mwaka watu 82,000 wanaambukizwa virusi vyatya UKIMWI hapa nchini na ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya UKIMWI na Dawa za Kulevyaa.

Mheshimiwa Spika, kati ya hao wanaoambukizwa ni kuanzia miaka 15 mpaka 64 na asilimia kubwa inaonyesha

kwamba vijana ndiyo wanaoongoza hivi sasa kwa asilimia 40 na kati ya hao vijana, watoto wa kike ndiyo ambao wanaoongoza kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Spika, watu wanaoishi na virusi vyatukwimu za Taifa...

SPIKA: Sasa swali Mheshimiwa Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, swali langu; nilipenda kufahamu mkakati wa Serikali, tamko la Serikali juu ya hali hii kwa sababu hali ni mbaya. Nini tamko la Serikali katika kusaidia Taifa na hasa vijana ambao ndiyo tunawategemea katika nguvu kazi ya Taifa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ongezeko la tatizo la UKIMWI linakuwa kubwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ufanuzi.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la UKIMWI nchini limekuwa likiratibwa vizuri sana na Serikali toka tulipoanza kampeni ya kupambana na maambukizi ya UKIMWI kwa kushirikisha Wizara zote ambazo zinahusika katika kulinda afya ya Mtanzania. Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo hasa inasimamia suala la mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kuwa tumeshaunda Taasisi inayoitwa *TACAIDS*. Tunafanya kazi kwa pamoja na Wizara ya Afya ambayo ndiyo ina wajibu wa kusimamia afya ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, pia Bunge Ietu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ambayo inashughulikia masuala ya UKIMWI nayo pia imekua ikishiriki kikamilifu. Kwa hiyo, mkakati huu wa pamoja ndiyo unaowezesha sasa kupambana na maambukizi ya UKIMWI ambayo sehemu kubwa yanaathiri sana maisha ya vijana

kama ambavyo umeeleza na takwimu ambazo unazo mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi ni kwamba mkakati wetu sasa ambao tunao ni kuhakikisha kwamba wale Watanzania wote kwanza tunatakiwa kupima ili kujitambua afya yetu na malengo yetu kufikia mwaka 2020 kila Mtanzania awe ameshapima. Ndiyo maana tumeweka kampeni ya upimaji karibu maeneo yote na kila mahali wanapokutana, wananchi zaidi ya 100 lazima pawe na eneo la kupimia ili kutoa fursa kwa Watanzania kwenda kupima. Kwa hili pia tuna kampeni kubwa, tumegundua wanaopima sana ni akina mama kuliko wanaume, nami ni Balozi wa wanaume wa upimaji. Kwa hiyo, tunahamasisha kwa ujumla wake watu wapime.

Mheshimiwa Spika, pili, wale wote walio pima na wamegundulika kuwa na maambukizi, kufikia mwaka 2020 tunataka wote wawe wameshaanza kutumia dawa za kufubaza hivyo virusi vya UKIMWI. Tunataka kufikia mwaka huo kila ambaye amepima, akishajitambua aanze kutumia dawa. Malengo yetu ni wale wote ambao wamepima na kukutwa na virusi wawe wameanza kutumia dawa, ifikapo mwaka 2020 tupate idadi kubwa ya watu ambao tayari wamefubaza virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, nini ujumbe hapa? Ujumbe ni kwamba Serikali inaendelea na mkakati wa kuhakikisha kwamba tunapunguza kwa kiasi kikubwa maambuki ya UKIMWI nchini kuititia Kampeni, Kuititia Programu zetu ambazo tunazo, pia tunaendelea kuwa elimisha Watanzania kuendelea kutambua afya zao pale ambako wanajikuta wana maambukizi waende wakapime moja kwa moja na hasa vijana ambao umewalenga wa katiba ya miaka 18 mpaka 25 ambayo sehemu kubwa ndio waathirika wakubwa hao ndio tunafanya kampeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hiyo kama haitoshi, tumeendelea kutoa elimu hii kwenye shule za msingi na sekondari ya maambukizi ya UKIMWI na kuwatakiwa watoto sasa, vijana

wetu kwenye shule za msingi na sekondari wawe na tahadhari ya maambukizi, waaache kujingiza katika maeneo ambayo yana maambukizi ili waendelee kuwa salama na wao ndio wawe Walimu wa Watanzania wengine katika kujikinga na maambuki ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo programu za kujikinga na UKIMWI zinaendelea na Serikali inaendelea na mpango wa kuwahamasisha Watanzania na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kupitia Kamati kazi nzuri wanayoifanya kuisaidia Serikali ya kuhakikisha kwamba Watanzania wanatambua umuhimu wa kupima, kupata madawa na umuhimu wa kujilinda wakati wote hapa tunapoendelea na shughuli zetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana. Mheshimiwa Venance Methusalah Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, uliza swali lako, tafadhalii.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nchi yetu ilipata heshima kubwa ya kuandaa mashindano ya AFCON, lililotokea Watanzania wote wameshuhudia lakini tumejifunza mambo mengi. Sasa kwa kuwa tumejepata heshima nyingine tena ya kuandaa mashindano ya watu wenye ulemavu ya Afrika Mashariki. Je, Serikali sasa inasemaje ili watuondoe kimasomaso?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchi yetu sasa tumeanza kushuhudia na kuona mwamko wa Watanzania kushiriki katika michezo mbalimbali. Pamoja na mwamko huu tuliokuwa nao tumeanza kuona pia hata mashirikisho mbalimbali duniani na Afrika wanaendelea kututambua Watanzania na kutupa heshima ya kuendesha mashindano

mbalimbali. Leo hii nchini tunayo mashindano ya vijana wetu wa umri chini ya miaka 17 yanaendelea nchini na sisi tulipelekea timu yetu, hatujafanya vizuri lakini tumejifunza mambo mengi kuititia mashindano haya.

Mheshimiwa Spika, pia nafurahi kusikia kwamba nchi yetu pia imepata heshima ya kuendesha Mashindano ya Waleavu ya Afrika Mashariki. Jambo hili kwetu kama Tanzania ni tunu kwa sababu tunaanza kuona mashirikisho mbalimbali ya michezo duniani na Afrika yakitupa hadhi ya kusimamia mashindano hayo, maana yake ni nini? Maana yake nchi yetu inatambulika au kwa upande wa usalama au uwezo wa kusimamia pia inatutengenezea fursa kwa Watanzania kutumia mashindano hayo kuboresha pia masuala ya uchumi. Hili litatufanya pia na sisi sasa tuondoke hapa tulipo kimichezo katika michezo mbalimbali na tuweze kufikia hatua nzuri ya kuweza kushindana mpaka ngazi ya dunia.

Mheshimiwa Spika, mashindano ambayo yanaendelea na hayo ambayo yatakuja, tutaendelea kujifunza na kuandaa vizuri timu zetu za ndani zinapokwenda kushiriki zipate kombe lilitotarajiwu na ambalo tumeletewa hapa nchini ili tuweze kuboresha. Vile vile Serikali sasa tumeanza kusimamia michezo hii ikichezwa kutoka umri mdogo kwenye shule za msingi na sekondari, kwenye vyuo ili kuweza kupata kuunda timu za Kitaifa ambazo sasa tunaanza kuona mwelekeo huo mkubwa. Hiyo ndiyo ilifanya hata mashindano haya ya vijana wa umri chini ya miaka 17 kuruhusu vijana wote wa shule za msingi, sekondari walioko likizo na Watanzania wote kuingia bure kwenda kushuhudia michezo inayochezwa kwa lengo la kujifunza zaidi kwenye michezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hadhi na heshima ambayo tunaipata Serikali ni pamoja na kupata fursa za kuongeza uchumi, kutangaza nchi, kuboresha sekta ya utalii na kila mmoja hasa watoa huduma kupata fursa ya kuweza kutoa huduma. Nitoe wito kwa Watanzania, tuanze sasa kuona michezo kuwa ni fursa kwetu na tuendelee kuungana

pamoja kuhakikisha kwamba michezo inachezwa katika maeneo yote na michezo yote, tuunde vilabu, tuvisimamie vizuri, viingie kwenye mashindano na kila shirkisho la kila michezo lishawishi kwenye ngazi yake ya Afrika, ngazi ya Dunia michezo iweze kuchezwa hapa ili fursa zile sasa ziwewe kunufaisha Watanzania. Kwa hiyo kwa kupitia michezo sasa Serikali na Watanzania tunaweza kunufaika zaidi. Ahadi ya Serikali kwenye hili ni kusimamia michezo. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli tunashukuru michezo hii imefanyika hapa tumejifunza mengi, Serengeti Boys tunawapongeza, lakini mawili hivi nimeyaona. Moja, timu yetu ilijaa sana Wanyamwezi, walikuwa wengi sana mle kwenye timu, safari ijayo tukiweka na wa katikati hapa naamini, tutashinda. La pili, hivi wale watoto wa wenzetu kweli chini ya 17 wale, mmh, wengine vijeba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Zainab Athuman Katimba, Mbunge wa Viti Maalum, swali la mwisho kwa siku ya leo.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kumekuwa na matukio ya uhalifu katika maeneo ya mipakani na ni kutokana na mwingiliano wa wageni kutoka nchi jirani. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na kuimarishwa na kudhibiti hali ya usalama katika mipaka yote nchini hususan katika maeneo ya Mkoa wa Kigoma ambako kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya uhalifu ambayo yanahusisha matumizi ya silaha za moto? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katimba, Mbunge wa vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na usalama nchini ni jukumu letu sote, suala la ulinzi na usalama nchini napenda kuwahakikisha Watanzania na wote ambao wanakuja nchini

Tanzania kwamba, ulinzi na hali ya amani na utulivu nchini inaendelea vizuri kwa sababu vyombo vyetu vya ulinzi vinaendelea kufanya kazi katika maeneo yote na kuhakikisha kwamba Tanzania inabaki kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge amezungumzia wasiwasi wake wa hali ya ulinzi na usalama kwenye mipaka na ameeleza hasa Mkoani Kigoma ambako natambua yeye pia anatoka Mkoani Kigoma. Nimefanya ziara Mkoani Kigoma, yako matukio kadhaa yameripotiwa, lakini hasa matukio haya ni kutokana na mchanganyiko tulionao na hasa kwenye mikoa yote iliyoko pembezoni.

Mheshimiwa Spika, nimeenda Kigoma, Kagera na Mkoani Kilimanjaro nimeona dalili hizo na taarifa za Jeshi la Polisi, lakini sehemu kubwa ni salama. Nini tahadhari ya maeneo haya, ni kutokana na mwingiliano wa nafasi ambazo tunazo na nchi jirani ambazo zinazunguka kwenye maeneo haya, tahadhari kubwa imechukuliwa. Nataka pia nitumie nafasi hii kuwasihii Watanzania hasa wale tulioko mipakani kushiriki kikamilifu katika kulinda mipaka yetu na kubaini vyanzo vyote vinavyoashiria kuleta uvunjifu wa amani nchini tukishirikiana na vyombo vya dola ambavyo vyenyewe vina nafasi ya moja kwa moja kwenye ulinzi wa usalama hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya ni nini kwenye mipaka? Kwanza, tumeimarisha mipaka hiyo kwa kuweka maeneo maalum ya wanaoingia nchini ili kuweza kuwatambua wote wanaoingia na kukagua wamengia na zana gani kwa lengo la kudhibiti uingajaji wa silaha ambazo haziruhuswi kuingia hapa nchini. Pia vyombo vyetu vya ulinzi vimeweka tahadhari kubwa sana na nchi jirani ambazo sasa tunashuhudia huko kuwa na migogoro mingi ya ndani, kwamba migogoro hiyo kwenye nchi hizo jirani isihadie kwenye nchi yetu.

Kwa hiyo, Majeshi yetu na vyombo vyote vya dola vinaendelea na umakini huo ikiwemo na Mkoa wa Kigoma

ambako tunapakana na nchi jirani zisizopungua mbili, tatu, nne ambazo na zenyewe pia tunaendelea kujenga mahusiano ya kiulinzi kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine anaweza kuhamishia migogoro nchi nyingine ili kufanya nchi hizi kuendelea kuishi kwa umoja, mshikamano pia kuwa na ulinzi wa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nataka niwahakikishie wananchi wote wanaoishi maeneo ya pembezoni matukio yote madogo yanayoripotiwa yanachukuliwa hatua lakini udhibiti wa mipaka hiyo unaendelea kuimariswa lakini nitoe wito sasa kwa Watanzania wenyewe tushirikiane, tushikamane katika kubaini viashiria vyote vinavyoleta uvunjifu wa amani nchini kwa lengo ya kuifanya Tanzania kuendelea kuwa salama, kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa ni kimbillio la wale wote wanaopenda amani, kwa lengo la kuwafanya Watanzania wenyewe kufanya shughuli zao za maendeleo wakiwa na uhakika wa maisha yao, wakiwa na uhakika wa shughuli zao.

Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana kuhakikisha kwamba vyombo vyaya usalama vinalinda maeneo yote ili kuhakikisha kwamba nchi inabaki salama. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda wako umekamilika, tunakushukuru sana kwa kutupa fursa ya kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Swalii la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura.

Na. 132

Upungufu wa Walimu wa Sayansi Mkoa wa Dodoma

MHE. FELSTER A. BURA aliuliza:-

Mkoa wa Dodoma una upungufu wa Walimu 527wa Sayansi:-

Je, ni lini Serikali italeta Walimu wa kutosha wa sayansi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo muhimu la upungufu wa Walimu katika Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kongwa peke yake kwa shule za msingi, Walimu wanaopungua ni zaidi ya 1,000 majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Dodoma una shule 221 za sekondari zikiwa na wanafunzi 72,254. Mahitaji ya Walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati ni Walimu 1,641 na Walimu walipo ni 916, hivyo pungufu ni Walimu 527 sawa na asilimia 32 ya mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri Walimu wa masomo hayo kwa awamu na kwa sasa kibali cha kuajiri Walimu 4,549 kimetolewa ambapo kati ya hao Walimu 1,374 ni wa masomo ya Sayansi na Hisabati. Taratibu za kuajiri Walimu hao zinakamilishwa ili kuwapanga Walimu hao katika Halmashauri zenye upungufu ikiwepo Halmashauri za Mkoa wa Dodoma. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Bura, swali la nyongeza tafadhali.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, kama uhitaji wa Walimu wa Sayansi kwa Mkoa wa Dodoma ni 916. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba uhitaji wa Walimu wa Sayansi ambao ndio Madaktari na Wahandisi na Wauguzi unakamilika kwa kuwaajiri Walimu wanaotesheleza mahitaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na uhitaji mkubwa wa Walimu wa Sayansi kwa shule za sekondari, kuna uhitaji mkubwa wa Walimu wa shule za msingi. Kwa mfano, Wilaya ya Kongwa kuna uhitaji wa Walimu 1,088; Chembu, Walimu 786; Kondoa, Walimu 618; Dodoma Jiji, Walimu 656, hapo ni Wilaya nne tu nimezitolea mfano. Je, ni lini sasa Serikali itaamua sasa kuwaajiri Walimu wa shule ya msingi kwa sababu elimu ya msingi ni kujenga msingi wa mwanafunzi, Je, Serikali iko tayari kuwaajiri Walimu wa kutosha pamoja na halmashauri zetu kujenga miundombinu, Jiji wamepanga bilioni 8.3 kwa ajili ya kujenga miundombinu kwa ajili ya shule za msingi na sekondari. Je, serikali iko tayari sasa kuwaajiri na Walimu wa shule za msingi ili kukidhi mahitaji? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Mwita Mwikabwe Waitara, swali hili la leo tunauliza muhimu kweli, majibu tafadhali. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli swali lake la kwanza anauliza upungufu mkubwa Walimu na naomba nikiri kwamba ni kweli kwamba tuna uhitaji mkubwa sana wa Walimu wa Hesabu na Sayansi, takribani nchi nzima na Wilaya zote na Wahesimiwa Wabunge wote hawa ukiona wanapiga makofi wanazungumza hilo. Hii ni ajira ya awamu ya kwanza, bado tathimini ile ya Walimu hewa na wengine, hii tumeomba kibali kupata Walimu 8,500 kama nilivyosema, lakini

tunataraja kupa kibali kingine mwezi wa Tano au wa Sita ambao watakuwa wengi zaidi ya hawa. Kwa kweli makusudi yetu ni kulenga kuajiri Walimu wengi wa Hesabu na Sayansi, lakini kama nilivyosema pale ambapo wana mahitaji makubwa sana, kwa mfano, unakuta kuna shule haina Mwalimu wa Hesabu, haina Mwalimu wa fizikia na kemia tutazingatia maeneo yenye upungufu mkubwa zaidi wakati tunapeleka Walimu hawa katika shule zetu za sekondari.

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pili, ameuliza ajira ya Walimu wa shule za msingi. Katika hao niliovataja Walimu 4,500 nimesema 1,300 ni masomo ya sayansi na hisabati, maana yake Walimu 3,200 wanaobaki wote hawa ni Walimu wa shule ya msingi pamoja na Walimu wa watoto wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, tutazingatia kupeleka pia na Walimu wa shule za msingi katika maeneo mbalimbali ambayo yana upungufu mkubwa. Tumefanya mawasiliano na Waheshimiwa Wabunge, wanafahamu, tatalizingatia, lakini tukipata kibali mwezi wa Tano kama nilivyosema au wa Sita tutazingatia maeneo gani ya kwenda.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna upungufu mkubwa, lakini tuna maelekezo mengine ambayo kama kutakuwa kwa mfano kwenye vibali vya muda, tukianza kutangaza nafasi unakuta pia inakuwa ni pungufu. Tumetoa vibali vya muda, Walimu ambao wamesoma masomo ya sayansi na hesabu lakini sio Walimu wanapata mafunzo ya muda mfupi ili waweze kuziba *gape* hili la Walimu wa Sayansi na Hisabati. Ahsante.

SPIKA: Tunaishukuru Serikali kwa mipango mizuri ya kutaka kuajiri Walimu, lakini Waheshimiwa Wabunge tutakubaliana hata Serikali ikiwijiri namna gani kwa jinsi ambavyo darasa la kwanza na chekechea kila mwaka ile idadi inayoandikishwa ile tusipoifanyia kazi...

Mheshimiwa Suzan swalı la nyongeza.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nasema tu kwamba Wilaya ya Kilombero na hasa

kutokana na miundombinu yake ina upungufu wa Walimu 1,018 na sio wa sayansi tu, wa kada zote. Kwa mfano, Jimbo la Mrimba unakuta shule ina Walimu watatu lakini ina wanafunzi 800 au 1,000. Je ni lini sasa Serikali katika hawa Walimu wanaosema wanawaajiri sasa hivi watatupelekea Walimu kwenye Wilaya ya Kilombero, ikiwemo na wanawake kwa sababu kuna shule haina Mwalimu mwanamke hata mmoja. Sasa wale watoto wanaokuwa wakamuone nani? Kwa hiyo, ni lini sasa mtapeleka walimu hususan Jimbo la Mrimba ili watoto wale waendelee kukua wakiwa na chakula cha akili. Ahsante? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri na hasa wa shule hizo ambazo hazina Mwalimu wa jinsia mojawapo, shule zingine Walimu wote wa kike wa kiume hata mmoja hakuna.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba njibui swali la Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mbunge wa Mrimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshatoa maelekezo zile shule ambazo zina Walimu wa kike peke yake au wa kiume peke yake ni lazima wachanganywe. Hii kwa kweli ni kazi ambayo inafanywa ndani ya Wilaya na Mkurugenzi mwenyewe kwani ana uwezo kupata taarifa na Mheshimiwa Mbunge anawasiliana naye halafu wanawabasilisha ndani, kama ni Mwalimu kutoka nje ya mkoa mwingine hilo ndio unakuja ngazi ya TAMISEMI. Kwa hiyo, nadhani hilo lifanyike na ningepeda kueleza kwa kweli itakuwa sio sawasawa kama kuna shule ina Walimu wa kiume tu na shule ile ni mchanganyiko. Kwa hiyo, naomba nitoe maelekezo kwa Wakurugenzi wote na Maafisa Elimu wa Mikoa na Makatibu Tawala, hili jambo walifanyie kazi sio zaidi wiki mbili kwa sababu inawezekana na ndani ya mazingira yao.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyozungumza, ajira hizi ambazo tumetangaza tutazingatia maeneo ambayo yana upungufu mkubwa na tuliomba Mheshimiwa Mbunge anajua

kuna shule ambayo, shule za msingi inaweze kana kwamba unaweza ukawa na Walimu wachache kwa sababu wanafundisha masomo mengi kwa wakati mmoja, lakini sekondari lazima kila mtu ana somo lake au masomo mawili ambayo anafundisha, haya maeneo ambayo yana changamoto kubwa na tutahakikisha kwamba tunapeleka Walimu katika maeneo haya. Ndiyo maana tumezia pia na uhamisho, labda niliseme hili, kwa maana kwamba kuna maeneo ya halmashauri kwa sababu yana mazingira magumu, watu wamekuwa na sababu nyingi sana za kuwahamisha na kuomba uhamisho.

Mheshimiwa Spika, maelekezo yametoka kwa Serikali kwamba tusimamishe uhamisho kwanza wa Walimu nchi nzima ili tutengeneze mifumo ambayo, anapoomba uhamisho kwa sababu yoyote ile hata kama ni mgonjwa, kumfuata mume wake au mke wake au vyovyote itakavyokuwa tujuje je, anapotoka kule Kaliua, Mrimba, Kilosa anapooenda kule *balance* ikoje kule ya Walimu, kwa maana ya kuangalia ikama hiyo. Kwa hiyo, tumelichukua hatua hiyo baada ya kugundua kwamba kuna maeneo wanakimbia mazingira magumu ya kazi, wanaenda sehemu ambayo kuna unafuu, anapaswa kufundisha mahali popote kulingana na mkataba wake wa kazi. Ahsante.

SPIKA: Tunashukuru sana. Bado tuko TAMISEMI, tuendelee na swali la swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 133

Fedha za Uchaguzi – Serikali za Mitaa

MHE. AIDA J. KHENANI aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali inatenga na kutumia fedha kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji?

SPIKA: Hili swali la Mheshimiwa Aida sijui linataka kuuliza nini? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, maana

maswali mengine bwana, ngoja tusikilize majibu labda tutajua ultaka kuuliza nini.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, tuna majibu yake. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba nimjibu Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ilivyotajwa kwenye Katiba, Ibara ya 146(2)(a) mpaka (c) ni kuimarisha demokrasia na kutumia demokrasia katika kuharakisha maendeleo. Katika kutekeleza Jukumu hili muhimu, vlongozi wanaoongoza vyombo vya Serikali za Mitaa huchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia kuititia uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya vijiji, mitaa na vitongoji.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Mitaa unahitaji rasilimali fedha ili kuwezesha upatikanaji wa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi ikiwemo vifaa vya uchaguzi yani masanduku, lakiri, fomu na kadhalika. Pamoja na vifaa hivyo, zipo gharama mbalimbali zinazohusiana na uendeshaji wa uchaguzi huo ikiwemo mafuta ya magari, matengenezo ya magari na posho mbalimbali kwa ajili ya watu watakaoshughulikia mchakato mzima wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile zipo taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama vile kutoa matangazo ya Kiserikali yanayohusu uchaguzi, kufanya vikao mbalimbali na wadau wa uchaguzi, kuhakiki maeneo au majimbo ya uchaguzi na kuanda Daftari la Wapiga Kura, kuratibu shughuli hizo zote zinahitaji rasilimali fedha. Hivyo, kukamilisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni lazima Serikali itenje fedha za kugharamia shughuli hizo, kama ilivyo kwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa taarifa tu ni kwamba na mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, kwa hiyo, hiki nilichokuwa nakiuliza nahitaji Wenyeviti wengine wapate ufanuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali inatenga fedha nydingi kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Majibu ya Naibu Waziri amenukuu Katiba, Ibara ya 146, wanasema madhumuni ya kuanzisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kuharakisha maendeleo ambapo kuchaguliwa huku na sisi Wabunge, Madiwani pamoja na Rais tunachaguliwa hivyo lakini sisi tunalipwa posho na mshahara. Kama Serikali inaweza kutenga fedha kwa ajili ya uchaguzi, kwa nini haitengi fedha kwa ajili ya kuwalipa Wenyeviti hawa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwenye ngazi ya Serikali za Mitaa na Vijiji kuna Watendaji wa Vijiji na wa Serikali za Mitaa ambao wanalipwa na Serikali, wanaofanya kazi saa tisa lakini Wenyeviti wanaochaguliwa na wananchi wanafanya kazi saa 24 hawalipwi. Serikali haioni sasa kwa kuwa mpaka sasa hajjawalipa Wenyeviti wala hakuna sheria yoyote iliyoletwa kwa ajili ya kuwalipa, kwa nini isiufute Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wabaki hawa wanaolipwa na Serikali? (*Makof!*)

SPIKA: Mbona uko mkali sana asubuhi yote hii?
(*Kicheko*)

Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimjibu Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, maswali yake ya nyongeza mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kuhusu posho za Wenyeviti wa Serikali za Mitaa. Mimi pia ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa kabla ya kuwa Mbunge tangu 2014 mpaka 2017. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba haya ni maswali ya uchonganishi na naomba niwaambie Wenyeviti wa Mitaa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawapenda sana na ndiyo maana inataka kuwaeleza ukweli na naomba wanisikilize. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kwenda kugombea kunakuwa na maelezo na kanuni zimetaja sifa za nani anapaswa kuwa Mwenyekiti wa Mtaa. Sifa mojawapo muhimu sana ni kuwa na kipato cha kumfanya aweze *sustain* maisha yake binafsi. Kwa hiyo, mtu yejote anapoenda kuchukua fomu na bahati nzuri mwaka huu mwezi Novemba tunafanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kila anayetaka kuwa Mwenyekiti wa Mtaa au Mjumbe wa Serikali ya Mtaa au Kijiji, Kitongoji, anapaswa asome sifa, ajiridhishe ndiyo achukue fomu, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Wenyeviti wa Mitaa kwa mujibu wa maelezo ya Serikali watalipwa kwa viwango mbalimbali kulingana na uwezo wa Halmshauri yao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge anapouliza swalii ningetaka aseme kwenye Halmashauri yao wamejipangaje kuwalipa posho Wenyeviti wa Halmashauri kwa sababu pesa ziko kule na miradi iko kule wanalsimamia.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa uwezekano wa Serikali kulipa posho za Wenyeviti wa Mitaa kwa maelekezo tuliyotoa makusanyo yakipatikana kinachotakiwa kirudishwe kwenye Halmashauri asilimia 20 walipwe. Ni muhimu kuzingatia Mheshimiwa Diwani anapochukua fomu anafahamu mimi sina mshahara nitalipwa posho, anajiridhisha Sh.350,000 kwa mwezi inatosha.

Mheshimiwa Spika, tunaomba watenganishe kati ya kazi na posho. Wafanye kazi kwa weledi lakini wasiache kuwahudumia wananchi kwa sababu hawajaliwa posho, kwa sababu hayo ni makubaliano na wameridhika kabla ya kugombea. Serikali ikipata uwezo wa kutosha itapeleka posho kwa Wenyeiti wa Mitaa, kwa sasa uwezo haujapatikana, tunawaomba waendelee kufanya kazi kwa weledi, wanafanya kazi kubwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo pamoja na Wenyeiti wa Mitaa kinyume na hapo.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kwamba kwa sababu Wenyeiti wa Mitaa hawalipwi posho na Watendaji wa Mitaa na Vijiji wanalipwa kwa hiyo tufute wabakie wanaolipwa. Hawa Watendaji wa Mitaa, Kata na Vijiji ni watumishi wa Serikali, wanatajwa kwenye orodha ya watumishi wa umma.

Kwa hiyo, huyu ni mtumishi na ndiyo maana anapotaka kupata nafasi hii tunatangaza nafasi kwa uwezo wa Halmashauri na Serikali Kuu, analeta vyeti, anakuvavetted, anakaguliwa, anapewa mkataba wa kazi yake na huyu anapaswa kufanya kazi kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwenye ngazi ya Kijiji na Mtaa huyu Mtendaji ndiyo Mkurugenzi wa Halmashauri na kama kuna jambo lolote hawa wanawajibika. Kwa hiyo, naomba tutofautishe huyu ni mtumishi wa Serikali na huyu ni mtumishi wa wananchi kwa kazi ya kujitolea na wote ni watu muhimu sana katika eneo hili. Huyu Mtendaji na watu wengine watapata kile ambacho kinastahiki kwa kadiri ambavyo tumekubaliana. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri sana, mwaka huu kimbembe Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mwisho wa mwaka tutajua nani ni nani.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swalii la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini.

Na. 134

Ujenzi wa Barabara ya Kinyanambo – Madibira

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA aliuliza:-

Barabara ya kutoka Kinyanambo A – Isalavamu – Igombavanu – Sadani hadi Madibira ilikuwepo kwenye llani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010 na 2010 – 2015 lakini hadi sasa haijajengwa kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizofanya Serikali kutoanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi wa Wilaya za Mbarali na Mufindi?

(b) Je, ni lini sasa ujenzi wa barabara hiyo utaanza?

(c) Je, ni lini Serikali itaanza uthamini kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara hiyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Naibu Waziri, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, lenye Sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kinyanambo (Mafinga) – Madibira ni barabara ya Mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na inajulikana kama Barabara ya Rujewa – Madibira – Kinyanambo yenye urefu wa kilometra 152. Barabara hii ambayo kwa sasa ipo katika kiwango cha

changarawe, ikiunganisha Mkoa wa Iringa, sehemu ya Kinyanambo na Mkoa wa Mbeya sehemu ya Madibira, imepita maeneo muhimu yenye kilimo cha mahindi na mpunga.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) tayari imefanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kazi hii ilikamilika mwaka 2009 ikiwa ni pamoja na kufanya uthamini kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi watakaopisha ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, wakati Serikali inatafuta fedha za ujenzi barabara hiyo, itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali kila mwaka ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

SPIKA: Mheshimiwa Mgimwa, swali la nyongeza.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, alipokuwa kwenye ziara yake Wilaya ya Mufindi alisema ahadi ni deni na hii barabara ni ya muda mrefu. Akaahidi kwamba hii barabara itajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Mufindi na Rujewa na ni *short-cut* kwa wasafiri wanaotoka Mbeya. Nini *commitment* ya Serikali, lini wataanza kujenga barabara hii hata kwa kilometra mbili-mbili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuja Wilaya ya Mufindi kukutana na wananchi wote waliopo kandokando ya barabara hii kusudi uweze kuwaambia hatma ya tathmini na malipo yao?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mufindi - Rujewa, utaenda lini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgimwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mgimwa kwa sababu anafuatilia kweli siyo barabara hii tu peke yake lakini pia barabara inayoenda kumuunga kule Kihansi na kila wakati yuko Wizarani kufuatilia barabara hii. Kwa hiyo, nampongeza sana naamini kwamba wananchi wa Mafinga hawakukosea kumpa nafasi ya Ubunge.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba ahadi ni deni ni kweli na ndiyo maana tumeendelea kuiwekea kipaumbele barabara hii ili tuweze kujenga kwa lami. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mgimwa nakubaliana na wewe lakini tatizo ni fedha, tukipata fedha tutaendelea kupunguza kwa maana ya kujenga kwa awamu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba kadiri tunavyopata fedha tutaendelea kujenga barabara hii muhimu kwa sababu inapita maeneo ya uzalishaji mkubwa wa mpunga kule Mbarali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutembelea eneo hili, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge mara baada ya Bunge hili nitatembelea eneo hili ili kuweza pia kuwashakikishia wananchi wa Tarafa hii ya Sadani na maeneo mengine kwamba tumejipanga kuwaleta barabara ya lami lakini pia kuwalipa fidia ili kupisha mradi huu muhimu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Haule na Mheshimiwa Ally Keissy mtamalizia maswali ya nyongeza.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami napenda niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisimama mara kwa mara nikimuomba Waziri atujibu ni lini wataleta pesa na kujenga barabara ya kilometra 142 kutoka Dumila – Kilosa mpaka Mikumi ambayo kwa sasa imejengwa kuanzia Dumila mpaka Ludewa na bado kilometra 21 Ludewa – Kilosa? Kila siku nimekuwa nikijibiwa kwamba tuko kwenye upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na vitu kama hivyo. Wananchi wa Kilosa wanataka kujua ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii muhimu kwa uchumi wao? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo na barabara hiyo ni muhimu kwa kweli.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Haule, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara hii muhimu inayotoka Dumila - Kilosa, inapita maeneo ya Ulaya mpaka Mikumi, niseme tu kimsingi barabara hii imeanza kujengwa lakini tunaenda kwa awamu. Mheshimiwa Mbunge unafahamu eneo hili la Ludewa – Kilosa ambalo sasa tuna mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami na katika bajeti inayokuja kipande hiki tutaanza kujenga ili tupunguze uelekeo wa kwenda Mikumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe tu Mheshimiwa uvute subira, tumejipanga na tunaendelea kujenga kama unavyofahamu ili kuweza kuwaunganisha wananchi hawa wa Mikumi. Hii njia kwa kweli ni fupi, itapunguza gharama na muda lakini pia inapita maeneo muhimu ya uzalishaji na utalii kwenye maeneo yetu ya Mikumi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri tuliambatana naye mpaka *Kipiri Port*. Sasa namuuiliza lini usanifu wa barabara ya Namanyere – *Kipiri Port* utanza?

SPIKA: Majibu ya swai hilo, Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa John Elias Kwandikwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Keissy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimetembelea eneo la Kipili, Mheshimiwa Mbunge anafahamu yapo mambo mengi, nimpongeze tu kwa kweli kwa ufuatiliaji wake kwa sababu hata hii Bandari ya Kipili kule iko vizuri, tumeona maendeleo mazuri lakini uko umuhimu sasa wa kuunganisha kwamba tunakuwa na bandari nzuri lakini tunahitaji pia tuwe na barabara nzuri ya kuwapeleka wananchi katika maeneo hayo. Tumeona pia kuna uchumi mzuri, kuna samaki wanavuliwa maeneo yale wananchi hawa wanahitaji hii barabara.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Keissy, kama tulivyojipanga katika mwaka huu wa fedha tulilitengea fedha kwa ajili ya usanifu, harakati za awali zinaendelea, lakini katika mwaka unaokuja pia tutaweka mapendekezo ya fedha, ili tukamilishe usanifu na tuweze kuanza kujenga kipande hiki cha barabara kilometra kama 72 hivi kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Asante sana. Mambo ya Ndani ya Nchi sasa, swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Wingwi.

Na. 135

Kukithiri kwa Vitendo vya Utekaji Nchini

MHE. JUMA KOMBO HAMAD aliuliza:-

Vitendo vya utekaji kwa watu wasio na hatia na kuwatesa, kuwahujumu na hata kuwaua vinaendelea kukithiri nchini:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia, kulinda na kuhakikisha inakomesha vitendo hivyo haraka sana?

(b) Je, hadi sasa ni watu wangapi ambao wamekamatwa na kuchukuliwa hatua kutokana na uhalifu huo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Hamad Masauni, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Serikali ni kuhakikisha raia wake wanakuwa salama wakati wote na wanaendelea na shughuli za uzalishaji mali na shughuli nyingine za kijamii kwa amani na utulivu pasipokuwa na hofu. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwenye taarifa za utekaji, utesaji ama mauaji zinapotolewa lengo likiwa ni kuwabaini, kuwachukulia hatua za kisheria watu ambao wanajihuisha na vitendo hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutumia taarifa za kitielijensia imekuwa ikiweka mikakati mbalimbali ya kudhibiti mipango ya wahalifu kwa kufanya operesheni na doria

mbalimbali kwa lengo la kuzuia na kukomesha vitendo vyatia hii ambapo hadi sasa mtuhumiwa mmoja amekamatwa kwa makosa ya utekaji nyara.

SPIKA: Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, swali la nyongeza.

MHE. JUMA KOMBO HAMAD: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ni ukweli usiopingika kwamba yapo matukio ambayo yalitikisa sana ya aina hii Tanzania. Matukio haya ni pamoja na kitendo cha jaribio la mauaji ya Mheshimiwa Tundu Lissu, kutekwa kwa Mohamed Dewji, kutekwa, kupigwa na hatimaye kuuawa kwa Mheshimiwa Ali Juma Suleiman pale Unguja, matukio ya Kilwa na matukio ya kutekwa vijana saba pale Mkao wa Kaskazini Pemba, Jimbo la Mtambwe. Je, Serikali inatuambia kwamba pamoja na matukio haya makubwa na mazito na ya kutisha, ndiyo ni mtu mmoja tu hadi sasa ambaye amekamatwa na kuchukuliwa hatua?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba kutaka kufahamu, je, Serikali ipo tayari sasa kuunda Tume ili kuchunguza matukio haya ili kuyabainisha na kuwabainisha wanaohusika na matukio haya ili kuchukuliwa hatua za kisheria? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Eng. Hamad Massauni, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ametaja matukio mbalimbali ambayo yametokea kwa wakati tofauti. Nataka tu

nimthibitishie kwamba matukio haya kila moja Jeshi la Polisi liliyachukulia kwa uzito unaostahili na yapo katika hatua mbalimbali za upelelezi, yako ambayo upelelezi wake umeshakamilika na yameshawasilishwa kwa *DPP*, mengine yamepiga hatua hata zaidi ya hapo. Kwa hiyo, kuyazungumzia kwa pamoja matukio ambayo ni tofauti na yana mazingira tofauti inakuwa ni changamoto. Hata hivyo, nimthibitishie kwamba, kwa sababu suala la upepelezi mchakato, ni imani yetu kwamba matukio haya yataweza kufikia katika hatua nzuri na hatimaye haki itaweza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na hoja yake ya kuundwa Tume, sijui sijaelewa anazungumzia Tume ya aina gani lakini nataka nimthibitishie tu kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pale ambapo imekuwa ikipokea malalamiko mbalimbali ambayo yanapelekwa katika vyombo vyetu vya usalama ikiwemo Jeshi la Polisi, tumekuwa na utaratibu wa kuunda Tume. Kuna Tume mbalimbali tumekuwa tukiunda na zimekuwa zikifanya kazi vizuri, kwa hiyo, si jambo geni.

SPIKA: Ahsante. Swali la mwisho, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa siku ya leo. Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga, tafadhalii.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, asante sana. Kwanza naomba niipongeze Serikali yangu, jana tumelipa shilingi bilioni 668 kwa ajili ya mradi wa *Stiglier's Gorge*. Nilikuwa namuuliza mtu wa benki, bilioni 668 zinafafanaje? Akaniambia shilingi bilioni 668 ni kontena moja la futi 40, kama malori ya fuso ni manne, kama vile vikiriku ni 22. (*Makofi*)

SPIKA: Kuna watu kushoto kwangu wametoa macho hawaamini, watani zangu. (*Kicheko*)

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, naomba swali langu namba 136 kwa niaba ya Wanaulanga, lijibiwe.

Na. 136

Hitaji la Chuo Ulanga

MHE. GOODLUCK A. MLINGA aliuliza:-

Wilaya ya Ulanga ina Shule za Msingi zaidi ya 50 na Sekondari zaidi ya 17 lakini haina Chuo chochote ambacho Wanafunzi wanaomaliza masomo kwenye shule hizo wanaweza kujunga:-

Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

SPIKA: kuna watu kushoto kwangu wametoa macho hawaamini, watani zangu. (*Kicheko*)

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa William Ole Nasha Tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa vyuo vya elimu na mafunzo katika kuandaa rasilimaliwatu itakayochangia katika kufikia azma ya Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inatekeleza mpango wa kuboresha vyuo vilivyopo kwa kukarabati na kujenga miundombinu mipyaa pamoja na kuongeza vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia ili kuongeza nafasi za udahili na kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo. Aidha, Serikali inatekeleza mpango wa ujenzi

wa vyuo vya VETA za Mkoa na Wilaya kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ulanga ni moja kati ya Wilaya zenyе uhitaji mkubwa wa vyuo vya elimu na mafunzo. Wilaya ina chuo kimoja tu cha ufundi stadi cha Mtakatifu Francis Kinachomililiwa na sekta binafsi. Wakati Serikali inaendelea na jitihada zake za upanuzi na ujenzi wa vyuo, natoa wito kwa Wilaya zote zenyе uhaba wa vyuo vya elimu na mafunzo kutumia vyuo vilivyopo nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga nilikuona.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimpongeze Mkuu wangu wa Wilaya kwa jitihada zote za kunyanya Elimu ya Ulanga Bi. Ngoro Malenya.

Mheshimiwa Spika, chuo anachoongelea Mheshimiwa Waziri ni cha *mission* na kinachukua wanafunzi wachache sana na fani chache ambazo haziendani na rasilimali zinazopatikana Ulanga kama madini, misitu na uvuvi. Wanafunzi wanaomaliza Ulanga kidato cha nne kwa mwaka ni 1000 hadi 1200 na hiki chuo kinachukua wanafunzi chini ya 150.

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa Serikali isishirikiane na misheni ili kuongeza kukipanua chuo hiki ili kiweze kuchukua wanafunzi wengi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna eneo ambalo tulilitoa kwa ajili ya VETA wajenge Chuo cha Ufundi eneo la Mwaya. Je, Serikali inasemaje ipo tayari kutoa hela kwa ajili ya kuanza ujenzi wa chuo hiki?

SPIKA: Majibu ya maswali hilo Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama tulivyosema kwamba Wilaya

ya Ulanga kwa sasa ina chuo kimoja tu cha binafsi lakini tumeshauri kwamba wananchi wa Ulanga waendelee kutumia vyuo vingine vilivyopo, kuna vingi viro katika Mkoa wa Morogoro lakini vilevile nchi nzima kwa sababu ndio utaratibu tunaoutumia kwa sababu sio kila Wilaya ina vyuo.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuhusiana na Serikali kushirikiana na wa-misionari wanaoendesha Chuo cha Mtakatifu Francis, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kuendesha vyuo kwa utaratibu wa *PPP*. Tupo tayari kuona ni namna gani tutajenga Chuo cha Ufundı Stadi Ulanga kwa sababu hata hivyo ni mpango wa Serikali kujenga chuo cha Ufundı Stadi kila Wilaya na Mkoa.

Kwa hiyo, kuhusu eneo ambalo limetengwa, wizara yangu haina shida ya kushirikiana na Wilaya ya Ulanga kuangalia namna gani kile chuo kitajengwa kwa sababu tayari ni mpango wa Serikali kulingana na upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa makusudi kuweza kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Kaliua ili vijana wa Kaliua ambao wanakua haraka sana ni wengi wanaokosa nafasi za kuingia masomo ya juu waweze kupata stadi za kazi na ujuzi waweze kujajiri na tunapoelekea kwenye uchumi wa katni na uchumi wa viwanda? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kulieleza Bunge lako tukufu na ningeshukuru kama Waheshimiwa Wabunge wote watasikiliza kwa sababu jibu nitakalotoa linafanana kwa kila Jimbo kwa sababu jibu ni hilo hilo.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kujenga *VETA* katika kila Wilaya na Mkoa. Kwa sasa tunavyoongea kuna ujenzi unaendelea katika Wilaya 17 Vyuo vya *VETA* lakini vilevile kuna *VETA* tano zinaendelea kujengwa. Sasa mpango wetu ni kwamba nikuhakikisha kila Wilaya inapata *VETA* kwa hiyo tutaendelea kujenga nyingi iwezekanavyo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ushauri wa ujumla ambao ningependa kutoa kwa Waheshimiwa Wabunge, ukiweza kujongeza na kwenda mbele zaidi katika kujenga sehemu inakuwa ni rahisi Serikali kuleta fedha kwa sababu hata hivyo tunachotaka ni kuongeza nafasi za udahili kwa wengi nchi nzima.

SPIKA: Mheshimiwa Almas Maige swali la mwisho kwa siku ya leo.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, ni majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Je, yupo tayari kufuatana na mimi kwenda kuangalia eneo ambalo tayari Wilaya ya Uyui tumeliweka kwa ajili ya *VETA?* (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, sina shida ya kuandamana na Mheshimiwa Mbunge na akipenda vilevile anaweza akawa na Wabunge wa Viti Maalum wa Mkoa husika wakati wa kutembelea eneo hilo. kwa hiyo, tukitoka tutapanga ili tuweze kutembelea huko. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge mtaona muda wetu umetimia, ni-*manage* kidogo meza ili tuweze kwenda kwa wakati.

Wageni waliopo Bungeni nitaanza na wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni pamoja na hawa wafuatao; Ndugu Said Seleman Kahondo, Ndugu Barnabas Esau, Ndugu Kasambe Hokororo karibuni sana Bungeni. Pia leo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa na Mabaloz wawili

kutoka nje ya nchi watakaokuja kumuona ofisini kwake; Balozi wa Kenya Ndugu Kidam Kazungu na Balozi wa Kuwait Ndugu Mubarak.

Wageni wangu kutoka Dayosisi ya Anglikana Mpwapwa akiwemo Mchungaji Elibariki Kutta kutoka Boston Marekani, karibu sana Mchungaji, karibu sana kututembelea hapa Dodoma. Ndugu Albert Galahenga na Ndugu James Senyegalo, karibu sana. Huyu ni Katibu wa Uaskofu wa Anglikana kule Mpwapwa na Kongwa. (*Makofi*)

Pia nina wageni 25 ambaao ni Maafisa Eliu wa Kata kutoka Hal mashauri ya Wilaya ya Kongwa wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Joseph Manisi; Maafisa Elimu Kata kutoka Kongwa, karibuni sana. Hawa ndio wanaosimamia elimu kule na kwa sasa Wilaya ya Kongwa inapaa kielimu. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 32 wa Mheshimiwa Mussa Sima, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ambaao ni Wajumbe wa Baraza la Madiwani Kata ya Kindai Manispaa ya Singida, wakiongozwa na Diwani Mheshimiwa Omari Salum. Karibuni sana, wale mliotoka Kindai karibuni sana na Singida kwa ujumla. (*Makofi*)

Wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa ambaao ni walimu wa Shule ya Msingi Longido, wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Charles Ephata, karibuni kutoka Longido; karibuni sana Dodoma walimu wetu. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Hasna Mwilima ambaao ni familia yake wakiongozwa na mdogo wake Ndgr. Hafsa Rusagara, karibuni sana wale kule. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Khamis Ali Vuai, ambaao ni wapiga kura wake wakiongozwa na mke wake Ndugu Mwanaisha Machano; karibu sana. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni familia yake kutoka Kinyerezi Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu David Cosato Chumi; karibuni sana pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni 28 wa Mheshimiwa Felister Bura ambao ni viongozi wa CCM Kata ya Nkuhungu, Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT wa Kata Ndugu Mahija Mataka. Karibuni sana; Hapa Kazi Tu. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Morogoro Ndugu Nazareth Mwampeta, Happyness Mollel na Junior, ahsante. Junior sijamuona yuko wapi, asimame Junior haloo jamani kitinda mimba wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya; kama nimevuruga utaratibu utanisamehe kama bado bado kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Zainab Mussa ambao ni ndugu zake kutoka Pemba wakiongozwa na Ndugu Warda Juma, karibuni sana wageni wetu kutoka Pemba. (*Makofi*)

Wageni 32 wa Mheshimiwa Kiteto Koshuma ambao ni Kwaya ya Vijana wa St. Nicholaus Anglikana kutoka Mkoani Mwanza wakiongozwa na Mchungaji Kiongozi Joseph Kitwe. Wanakwaya hawa kutoa Mwanza, karibuni sana Mtakatifu Nicholaus. Lakini Wasukuma ninyi mnajua kuimba? Aah! hebu acheni mambo jamani, mnajua kuimba kweli ninyi? Baadaye tutafutane. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni 33 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni kwaya ya vijana wenye ulemavu wa akili kutoka Mkoani Tanga, wakiongozwa na Ndugu Prisca Mwakasendile; ooh! karibuni sana kutoka Tanga. (*Makofi*)

Hii kwaya bahati mbaya tu muda haupo upande wetu lakini waheshimiwa Wabunge ingekuwa vizuri saa saba tukitoka hapo ukatuimbia kidogo, hizi kwaya mnatuimbia kidogo hapo nje mmh! Tukishamaliza saa saba angalau

wimbo mmoja mmoja. Sasa hii ya wenyewe ulemavu wa akili sidhani kama Wabunge wengi mmewahi kuona kwaya za aina hiyo. Kwa hiyo, ni vizuri wakati mwingine wanapofunga safari kama hivi basi tukapata nafasi ya kuwasikiliza kidogo ndugu zetu kwa upendo. (*Makofi*)

Wageni 24 wa Mheshimiwa Ritta Kabati kutoka Taasisi ya *Tanzania Music Foundation (TAMUFO)* ya Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Donald Kisanga; karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambao ni ndugu zake kutoka Mkoani Tabora wakiongozwa na babu yake Ndugu Jabir Kagombe; haya Wanyamwezi nao wamekuja, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni 18 wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, ambao ni viongozi wa CCM wa Wilaya ya Mufindi kutoka Mkoani Iringa wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya Ndugu Daudi Yasin; karibuni sana kutoka Iringa. (*Makofi*)

Wageni saba wa Mheshimiwa Aysharose Matembe ambao ni viongozi wa UWT kutoka Mkoani Singida, wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT wa Mkoa Jane Kashari pamoja na Mwenyekiti wa Wilaya Rudia Kidaila. Wako wapi wa Singida wale? Eeh! wale kule, karibuni sana wakina mama. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Mwanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Ndugu Theresia Msuya. Mwanga, karibuni sana popote pale mlipo maana yake leo *Gallery* zetu leo zimejaa kweli kweli inawezekana wengine wamekosa nafasi. (*Makofi*)

Wageni 44 wa Mheshimiwa Joseph Selasini ambao ni wanafunzi 32 na walezi 12 kutoka Shule ya Msingi ya Watoto ya Ngorika Happy ya Jijini Arusha ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi yake. Haya wageni wa Ngorika

Happy, wale pale; karibuni sana wageni wetu kutoka Arusha.
(*Makofii*)

Wanafunzi 42 na walimu nane kutoka Shule ya Msingi ya Libembeni iliyopo Kondoa Mkoani Dodoma, wakiongozwa na Waheshimiwa Madiwani Wawili. Wale wa Kondoa, Karibuni sana; ninyi ni Kondoa Mjini nadhani, asante sana.

Kabla hatujaendelea, jana palijitokeza sintofahamu kidogo na kabla ya hapo pia kuhusiana na hotuba ya Kambi ya Upinzani kutokusomwa ambapo msemaji wake aliona bora asiisome kwa vile palikuwa na mabadiliko fulani fulani.

Naomba Waheshimiwa tungesikilizana hasa upande wa CCM, nawaombeni sana wale wote mnaoongea ongea tuwe tunasikilizana kidogo. Wale wenye kamera mkiona watu wanaongea sana hawafuati mambo ya Bunge mnaelekeza kamera kwao ili wapiga kura wao wawe wanawaona huko kwamba kumbe wapo hapa wala hawafuatilii kinachoendelea.

Jana ilijitokeza kidogo sintofahamu hapa kwa hiyo Upinzani hawakusoma hotuba yao na imejitokeza tena na nyuma na nyuma kidogo jambo hilo. Tumelitazama na kulizingatia na kuliangalia tukaona kuna shida kidogo, sijui shida hiyo tutaitatua vipi, lakini ukweli ni kwamba kuna shida.

Baadhi ya hotuba namna zinavyoandikwa zina matatizo, tena matatizo mengine makubwa ya Kikanuni na mengine ya kiutaratibu na mengine Maofisa wetu pia ambao wamekuwa wakiziangalia wamekuwa nao wana-*overlook* baadhi ya vitu.

Ninachojifunza, mtanisahihisha huko mbele, wako watu mahali wanaandika hizi hotuba na baadhi ya Mawaziri Vivuli wanaokuja kusoma hizi hotuba hawapati muda wao wenyewe wa kuzipitia hotuba zenu. Kwa hiyo, anasaini anakuja hapa anasoma kitu ambacho kimeandikwa nje ya Bunge na watu ambao sio Wabunge na kadhalika. Kwa hiyo, wanajikuta wale kwa sababu wapo kule hawajui Kanuni zetu

kidogo na baadhi ya mambo, unakuta kwenye hotuba kule kule kuna mambo mengine yapo mahakamani na kadhalika. Kwa hiyo, tukiruhusu tu tunaleta mgongano mkubwa sana kati ya Taasisi ya Bunge na Taasisi ya Mahakama na mambo mengine ambayo kwa kweli kimsingi hayakubaliki.

Sasa ushauri wangu ni kwamba ni vizuri Waziri Kivuli kwa kweli ukasoma wewe mwenyewe hata kama hayo mambo unaona ni sawa basi baadaye tukubane wewe mwenyewe kwa nini hili limo? Itatusaidia sana uki-own kile kitu wewe mwenyewe.

Basi uamuzi wetu tumeamua kwamba sisi tutaruhusu zije, basi kwa upande mwingine nao tutakuwa na ubishi ubishi hapa kidogo basi tutaendelea kwa ubishi ubishi huo, lakini ambacho nakiomba ni kwamba... (*Makofi*)

Mnielewe tu mnapiga makofi ndio lakini yale mambo ambayo ni ya msingi msifanye kwa sababu kwa nini unafanya? Kama jambo lipo mahakamani, lipo mahakamani au mengine yameshapata majibu ya uhakika hayana sababu ya kuyaleta. Hotuba nyininge unakuta ni ya mwaka jana ile ile mambo yalishajibiwa au ya mwaka juzi, imeibuliwa mambo ambayo leo wala hayapo wala sio ajenda na kadhalika.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni huo na makosa makosa mengine mengi unakuta makosa hata Waziri Kivuli mwenyewe wale jamaa wanaoandika hotuba wamekosea hata jina, wamekuandikia majina ambayo hayapo. Kwa mfano, hotuba ya Mheshimiwa Ally Saleh badala ya kuandikwa Ally Saleh Ally, wamemuandika Ally Saleh Abdallah, kwa hiyo, inabidi watu wangu wasahihishe hata majina yenu. (*Makofi/Kicheko*)

Katibu tuendelee!

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Katibu tuendelee.

NDG. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE: Kauli za Mawaziri.

SPIKA: Tuendelee, Katibu.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Miongozo tutachukua kesho. Katibu.

NDUGU. STEPHEN N. KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

KAULI ZA MAWAZIRI

SPIKA: Kauli za Mawaziri, namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Ningombwa Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, kauli hii ni muhimu.

Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha kauli ya Serikali hapa Bungeni kuhusu upandishwaji vyeo kwa watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kama itakavyokumbukwa, zoezi la upandishaji vyeo watumishi waliokasimiwa katika ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ilahirishwa mwezi Mei, 2016 kupisha mazoezi ya uhakiki wa watumishi hewa na mishahara batili pamoja na vyeti vya watumishi wa Umma. Baada ya kukamilika kwa mazoezi hayo tajwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliridhia upandishwaji vyeo watumishi kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza, ilianza tarehe Mosi Novemba, 2017, ilihuisha upandishwaji na uidhinishaji wa taarifa za watumishi 59,967 ambao taarifa zao za kupandishwa vyeo zilikuwemo kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*Human Capital Management*

Information System) lakini zilikuwa hazijaidhinishwa wakati wa usitishwaji tajwa hapo mwezi Mei, 2016.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili, iliyoanza tarehe Mosi Aprili, 2018 ilihusisha watumishi zaidi ya 53,553 ambao walipandishwa vyeo lakini taarifa zao zilikuwa hazijaingizwa kwenye mfumo wakati wa zuio tajwa. Uidhinishwaji wa taarifa za watumishi wapatao 113,520 kwenye makundi haya mawili kupidia mfumo wa *Human Capital Management Information System* umekamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa upandishwaji vyeo, watumishi wa Umma 113,520, Serikali imewaelekeza waajiri kuendelea na upandishwaji vyeo kwa watumishi 193,166 waliokasimiwa katika ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuanzia tarehe Mosi Mei, 2019.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza zoezi hili, waajiri wanaelekezwa kwamba kipaumbele cha kwanza kitolewe kwa watumishi wenyе utendaji mzuri ambao wanataraja kustaafu hivi karibuni ili waweze kushughulikiwa mapema iwezekanavyo kabla ya kustaafu kwao. Kipaumbele cha pili kitolewe kwa watumishi wenyе utendaji mzuri, waliokaa kwenye vyeo walivyonyavyo sasa kwa muda usiopungua miaka minne na kukasimiwa kwenye ikama ya bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa rai kwa waajiri wote nchini kuhakikisha kwamba wanaliendesa zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi stahiki kwa wakati na kwa kuzingatia *seniority list* ya taasisi husika, sifa za kimuundo, kuwepo kwa nafasi iliyoidhinishwa katika ikama kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa Matokeo ya Tathmini ya Utendaji Kazi (*OPRAS*).

Mheshimiwa Spika, waajiri na maafisa watakaotekeleza zoezi hili kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Serikali kuhusu upandishwjai vyeo

watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais kwa kauli hiyo ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyojua kuna kimbunga kinaendelea huko, tumeona kwenye vyombo vya habari baadhi ya maeneo ya nchi yetu yanaweza yakahatarika, nimemwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama atueleze kwa kifupi tu nini kinachoendelea.

Karibu hapa mbele Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama. Karibu tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kutoa maelezo haya kama taarifa kwa Umma mzima wa Watanzania kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kufuatia utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini ambao umetolewa muda siyo mrefu uliopita.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utabiri wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini kuna uwezekano mkubwa wa kimbunga na mafuriko kutokea katika maeneo ya Pwani ya Mikoa ya Mtwara na Lindi na mikoa mingine ya jirani kuanzia usiku wa tarehe 24, yaani jana, kuamkia tarehe 25; na kwa mujibu wa utabiri huo hali hiyo inaweza ikaendelea mpaka tarehe 26 Aprili, 2019.

Mheshimiwa Spika, hali ya hewa inatarajiwa itaanza kubadilika usiku wa tarehe 24 kama nilivyosema. Kama nilivyosema, itaendelea hivyo mpaka tarehe 25 na 26 Aprili, 2019 na kwa msingi huo, inatarajiwa kutokea kimbunga chenye upepo wa kasi ya kilometra 130 kwa saa katika ulekeo wa mashariki umbali wa kilometra 175 kutoka Pwani ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kimbunga hicho kinatarajia kuendelea kusogea kuelekea Pwani ya Kusini mwa nchi yetu na kitaambatana na mafuriko hasa ikizingatiwa kwamba Pwani ya Mikoa ya Lindi na Mtwara iko chini ya usawa wa bahari.

Mheshimiwa Spika, hali hii inatarajia kuleta athari mbalimbali ikiwa ni pamoja na mtawanyiko mkubwa wa mafuriko na upemo mkali vinavyoweza kusababisha athari kwa maisha, uharibifu wa makazi, mali, mazao mashambani, miundombinu na mazingira kutokana na kuongezeka kwa kina cha maji ya Bahari ya Hindi katika kipindi kifupi. Aidha, shughuli za usafirishaji kwa njia ya anga, kwenye maji na nchi kavu vinaweza vikaathirika hasa kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi na maeneo jirani kutokana na hali mbaya ya hewa inayotabiriwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaelekeza mamlaka zote na wananchi wote wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na jirani kuchukua hatua za tahadhari ikiwemo kuwahamasisha wananchi wanaoishi kando kando ya Bahari ya Hindi kujiepusha kwa kuondoka maeneo hayo kabla hali hatarishi haijatokea. Aidha, shughuli mbalimbali zinazofanywa kando kando na ndani ya Bahari ya Hindi, hususan shughuli za uvuvi, biashara ndogo ndogo, usafirishaji wa majini na anga, tunashauri kwa kiasi kikubwa zisimamishwe katika kipindi hicho kinachotabiriwa kuwa hatarishi kuepusha athari zinazoweza kujitekeza kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kusitiza Kamati za Maafa katika ngazi zote katika maeneo husika, kwa mujibu wa sheria tuliyonayo, kufuatilia kwa karibu na kwa kina jambo hili ambalo limeshatabiriwa.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuelekeza uongozi wa ngazi zote kutoka katika Mikoa ya Mtwara na Lindi na hata maeneo ya jirani kuchukua na kutoa tahadhari katika mitaa mbalimbali ya mikoa yao juu ya uwepo wa hali hiyo hatarishi ya kiutabiri pamoja na hatua muhimu za kuchukuliwa ili kupunguza athari za kimbunga hicho.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa taasisi mbalimbali za Serikali na taasisi binafsi nchini kuendelea kufuatilia kwa karibu sana hali hii na kujiardaa kutoa misaada mbalimbali ya kibinadamu endapo hali hii itakuwa imejitokeza. Nachukua fursa hii pia kutambua hatua mbalimbali ambazo zimeshaanza kuchukuliwa na viongozi na Kamati za Maafa na watalam katika sekta mbalimbali kwa kushirikiana na wananchi katika kukabiliana na hali hiyo endapo itatokea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika kwa sasa, ninaendelea kuelekeza hatua stahiki ziendelee kuchukuliwa kuhakikisha tunakuwa na hali ya utayari wa kutosha ili kupunguza madhara makubwa ya kimbunga na mafuriko kama yatatokea kama ilivyotabiriwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia Sheria yetu ya Usimamizi wa Maafa Na. 7 ya Mwaka 2015 na Kanuni za Usimamizi wa Maafa za Mwaka 2017, imeendelea kusisitiza Kamati za Maafa kuanzia ngazi ya kijiji hadi mkoa kuhakikisha zinakuwa pamoja katika jukumu hili zito na kuhakikisha zinashirikiana kwa karibu na wananchi katika, kuzuia kukabili na kurejesha hali endapo utabiri huu utakuwa umetekelzeza.

Mheshimiwa Spika, vilevile, wananchi wote wanaelekezwa kuchukua tahadhari na kuchukua hatua katika suala zima la kushughulikia kujikinga na maafa kisheria kwa mujibu wa utabiri ambao umekwishakutokea. Suala la kujiardaa kukabili na kurejesha hadhi ni suala ambalo linahitaji ushirikiano wa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu na hasa Idara ya Maafa, itaendelea kuchukua hatua stahiki katika kuhakikisha maisha na mali za Watanzania zinakuwa salama kutokana na majanga yanayotabiriwa. Hivyo, Idara ya Maafa imeendelea kutoa taarifa kwa taasisi zote husika kufanya maandalizi muhimu yanayohitajika.

Ndugu zangu, wananchi wote Watanzania tunaomba kufuatilia hatua kwa hatua utabiri wa taarifa hizi za tahadhari mara kwa mara zinazoendelea kutolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha taarifa hii kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na *Chief Whip*, tunakushukuru sana.

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka
2019/2020 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano yanaendelea. Kwanza niseme kwamba wachangiaji nikikutaja jina kama utakuwa haupo ndiyo imetoka hiyo, mradi uko kwenye orodha. Maana yake orodha imetoka kwenu; wewe kaa sawa, nafasi utapata, lakini ukiwa umetoka tu, nafasi imechukulia. Maana yake nina wachangiaji wengi, karibu 20 hivi.

Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa kwa siku ya leo, atafuatiwa na Mheshimiwa Machano Othman Said.

Mheshimiwa Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza wa hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nitumie fursa hii kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa usikivu wake wa kujali mahitaji ya wananchi wanapomililia katika shida zao.

Mheshimiwa Spika, ni wiki moja tu imepita tulipotoa kilio kwamba hali ya chakula ni tete katika Kanda ya Kaskazini na wananchi waliouza mifugo yao hata hawana pa kununulia chakula maana bei ya mahindi ilipanda mpaka shilingi 20,000/= kwa debe, lakini Mheshimiwa Rais alitoa tamko kwamba kwa kuwa tuna maghala ya Serikali yanayoweka chakula, wananchi waliouza mifugo yao, wapelekewe chakula kwa bei ya Serikali na chakula hicho kimefika.

Naomba niishukuru Serikali, nimshukuru Waziri wa Kilimo na timu yake yote kwa ushirikiano waliotoa. Wanalongido wamefurahi, chakula kimewafikia, na hata wale walanguzi sasa wameshusha bei baada ya kuona kwamba Serikali sikuvi imewaletea wananchi wake chakula. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi na shukrani hizo, nitasema mambo machache sana kuhusiana na hotuba ya Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sababu mengi yameshasemwa na sipendi kurudia yaliyosemwa, lakini nina machache ya kusema kuhusu Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Jeshi la Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa Jeshi la Polisi, naungana na wenzangu waliotangulia kusema kwamba mazingira yao ya kuishi na kufanya kazi ni duni. Serikali iwaangalie kwa jicho la karibu. Ukija kwa mfano katika Jimbo langu la Longido ukaenda katika Kituo cha Polisi kilichopo Kamwanga, wale Polisi wanaishi katika *shacks; shacks* ni kama banda la kuku. Kwa kweli sisi kama wananchi wa Longido pia tunajali hivyo vyombo vyaya usalama na hata tulijitolea kabisa tukajenga na Kituo cha Polisi ambacho kinakaribia kumalizika, lakini Polisi wetu hawana makazi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri; na nilishaongea naye kwamba atuunge mkono kumalizia kile Kituo cha Polisi kipya kilichojengwa kupisha barabara ya lami inayounganisha Wilaya za Rombo na Siha na baadaye Longido.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Magereza, napongeza sana kazi wanayoifanya na uzaishaji ambao wameonesha. Pia nategemea kwamba baada ya kuanzishwa kwa *Mobile Courts* msongamano wa wafungwa utapungua. Pia nitoe rai kwamba kama zilivyoundwa na Serikali yetu sikuvi, tume mbalimbali za kuhakiki masuala ambayo yalikuwa hayaendi sawa katika nchi hii, kwa mfano uhakiki wa watumishi hewa, wale wenye vyeti feki na watu wengi wakabainishwa, naomba pia tume iundwe na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhakiki wafungwa wallosahauliwa ndani ya Magereza.

Mheshimiwa Spika, wako wafungwa ambao wametuhumiwa tu, ni mahabusu. Wamekamatwa kwa tuhuma za kuhujumu uchumi. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Longido, kuna waliotuhumiwa tu kwamba wanajihuisha na biashara ya ujangili kwa sababu sisi ni Wilaya ya Wanyamaporini na wanatupwa kule Gerezani, wengine wana mpaka miaka miilli; wanaitwa tu Mahakamani wanarudishwa, wanasema uchunguzi bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba suala hili litapewa kipaumbele baada ya Mahakama kuongezewa wigo wa kuwa na *Mobile Courts* na Vyombo vya Usalama vifanye uhakiki wa uhalifu wao kwa haraka, wasikae Gerezani pasipo sababu kama mahabusu ambao hata hawajahukumiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Zimamoto; ni ukweli usiopingika kwamba bado tuko nyuma sana katika kuendeleza Sekta ya Zimamoto na kunusuru maisha na mali za Watanzania wanaoweza kuathirika kwa majanga ya moto; na wilaya nyingi nchi hii ambazo nimeshazipita hazina

miundombinu kabisa ya uzimaji moto; na katika Wilaya yangu ya Longido pia hatuna hata gari la Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, naomba katika bajeti hii iongezwe fedha ya kuhakikisha kwamba kila Wilaya angalau inapata gani moja la Zimamoto maana tunapata majanga ya moto kila wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sisi katika Shule yetu ya Sekondari ya Longido karibu kila baada ya mwaka mmoja au miwili tunapata janga la moto. Hata Kituo cha Polisi Longido mwaka 2018 nyumba ya Askari iliungua moto tukishuhudia; tunazima kwa mchanga na udongo, hatuna chombo chochote cha kuzimia moto. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, pia niklenda katika huduma za uhamiaji, napongeza Serikali kwa sababu ya huduma ya kielektroniki na kwa kutengeneza *passports* zilizokidhi hadhi ya Kimataifa na kuwa moja ya *passports* bora duniani; lakini niombe kutoa rai kwamba hizi paspoti za kielektroniki zitengenezewewe mazingira ya kuwa rafiki kwa waombaji na Watanzania wote wenye haja ya kupata *passport*.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa sababu Watanzania wengi uwezo wao wa kutumia mitandao bado uko chini, hizi *passports* za muda mrefu ambazo mtu ukitaka kupata, mpaka ujaze fomu iende kanda, iende Makao Makuu; nasi watu tunaoishi mipakani tumekuwa tunategemea zaidi hizi hati za dharura tu. Unaona katika taarifa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba idadi ya wasafiri wa dharura ni kubwa mno ukilinganisha na wasafari wa aina nyingine. Siyo kwamba kuna dharura ni kwamba ndio hati ya pekee ambayo ni rahisi kuipata mtu unapotaka kusafiri nchi ya jirani.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu sasa hivi adha wanayopata wananchi wanaotaka kusafiri nchi ya jirani kwa biashara au kwa shughuli za kifamilia au kwa matibabu ni kubwa, maana kila akienda akirudi ile *passport*

inayoitwa hati ya dharura ina-expire; akitaka kuomba nyingine labda ameambiwa arudi ndani ya wiki hiyo hiyo, mpaka apeleke tena zile nyaraka zote; apeleke *birth certificate*, apeleke sijui barua ya mtendaji na akirudi tena wiki ijayo anaitishwa tena *back up* ya zile *documents* zote.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali najua kwamba ni njema, Waziri wa Mambo ya Ndani alishakuja akatoa elimu katika Jimbo langu, lakini naomba *passport* za muda mrefu, angalau zile za *East African Community* zirahisishwe wananchi waweze kupata katika ngazi ya Wilaya. Mtu akija, ajaze fomu, atoe vielelezo vyake, apewe *passport* ya muda mrefu kwa sababu naamini haki ya kuwa na *passport* ni haki ya kila Mtanzania mwenye kuwa na haja nayo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niongelee kidogo suala Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, vitambulisho hivi kasi yake ya kutoa ni ndogo mno, wananchi wangu wa Longido kuna waliopigwa picha za kupewa hivyo vitambulisho tangu mwezi wa Kumi mwaka jana lakini mpaka leo hawajapata.

Mheshimiwa Spika, pia niunganishe hapa kwa sababu ya ufinyu wa muda suala zima la kupatiwa hivi vitambulisho ili mtu aweze kuhakikiwa na *line* yake ya simu. Naomba kuuliza na Waziri anijibu baadaye atakavyohitimisha hoja, Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa wale raia ambao siyo raia wa Tanzania lakini wapo nchini kihalali aidha kwa *work permint* au huku kwa sababu ni *dependants*, wao ni vitambulisho gani watahitajika kuonyesha ili *line* zao za simu zisifungiwe itakapofika wakati wa kuzifunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, niipongeze Wizara, Waziri wenyewe ambao ni mmoja ya Mawaziri wasikivu sana ambao mimi nimewafahamu katika Bunge hili, yupo tayari usiku na mchana kukuhudumia ukimpigia simu, nimpongeze yeye na timu yake yote kwa kazi nzuri waliyofanya katika kuandaa hotuba ya bajeti na pia katika utendaji wao tunaouona katika vyombo vya kitendaji wanavyovitumia. Kazi yao ni

nzuri, Mheshimiwa Waziri aendelee hivyo hivyo, tupo nyuma yake kum-support kwa sababu kazi anayofanya inawasaidia Watanzania kubaki salama, lakin tuendelee kuongeza bidii katika kupunguza urasimu na hasa rushwa katika Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Spika, polisi bado wanakula rushwa, naomba hata kwa sababu tumekuwa *electrified* hizo *electronic agency* zitumike tu kumsoma mtu anayefanya uhalifu kwa mfano barabarani akakutane na faini yake mbele ya safari na sio polisi kuanza ku-negotiate naye. Teknolojia imeendelea, kuna nchi ukienda unapigwa picha tu barabarani unatumiwa kwenye barua kwa sababu gari yako inajulikana, ni ya nani, unatumiwa barua ya madai na usipopeleka gari yako inataifishwa. Kwa hiyo, naomba pia sera hiyo ya kufanya *Electronic Traffic Monitoring System* iweze kuboreshwa zaidi, maaskari waondokane na hadha ya kusamisha wasafiri barabarani na kuanza kuwahoji na kupatana na hatimaye kudaiwa rushwa ndipo mtu aweze kwenda au vinginevyo atapigwa faini kubwa.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kiruswa.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema naunga mkono hoja na ahsante kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Machano Othmani Said nilishakutaja, dakika kumi utafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, dakika tano.

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kuweza kufika leo katika Bunge letu Tukufu. Pia napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uchapakazi wao, wamefanya kazi nzuri katika kulitumikia Taifa kwa kipindi chote tangu Mheshimiwa Waziri ameteuliwa.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maeneo matatu ambayo ni Polisi, Uhamiaji na *NIDA*. Kwanza nianze na Jeshi la Polisi na kwa upande huu pia niwapongeze sana polisi na zaidi kwa upande wa Zanzibar Kamishna wa Polisi kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kwa miaka karibu mitatu sasa hali ya utulivu katika Mji wa Zanzibar na maeneo mengine ni nzuri. Maeneo ya ujambazi yamepungua sana na vitendo vyta uhalifu pia vimepungua, tatizo ambalo bado lipo kwa polisi na kwa upande wa Zanzibar ni mapambano dhidi ya madawa ya kulevyta, tunamuomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Maafisa wao waendelee kupambana na suala hili ambalo ni janga la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa polisi yapo matatizo ambayo tunaomba wayatatuwe na moja ya tatizo kubwa la polisi ni makazi miundombinu ya makazi kwa polisi kwa upande wa Zanzibar bado ni madogo sana. Katika maeneo mengi ya vituo vyta polisi, askari polisi hawana makazi, wanakaa katika hali ngumu, lakini hata vituo vyenyewe vyta polisi vimechakaa sana. Mfano, kwa Mkoa wa Mjini Magharibi ambao wananchi wa Zanzibar karibu nusu wanaishi Mjini Magharibi, hali ya vituo ni vichache na vichakavu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulifurahi sana Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara Zanzibar na kuzungumza na Maafisa wa Polisi na tunaomba Mheshimiwa Waziri afanye tena ziara kutembelea baadhi ya maeneo ya vituo vyta polisi ili ajionee hali halisi ya uwepo wa vituo hivyo katika hali mbaya. Tunashukuru kwamba wameanza kujenga nyumba za askari katika Kituo cha Polisi cha Fuoni, lakini waangalie na maeneo mengine zaidi ya Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo hali ya uchakavu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa polisi Zanzibar ni ukosefu wa vitendea kazi kama magari na *uniform* ambazo zinawakabili kwa muda mrefu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, jambo hili nalo alifikirie sana na aweze kulipatia ufumbuzi zaidi magari katika maeneo ya vituo vyta polisi.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, naomba nizungumzie Uhamiaji; namshukuru na kumpongeza Kamishna uhamiaji Zanzibar Ndugu Sururu kwa kufanya kazi vizuri sana, lakini naomba hapa nimshukuru Waziri wa Utawala Bora kwa tamko lake ambalo amelitoa hivi punde kuhusu kupandishwa vyeo kwa madaraja. Maafisa wengi wa Uhamiaji Zanzibar walikuwa wanalamika kwamba wameshakwenda kozi kwa muda mrefu, lakini bado kwa miaka mitano hawajapandishwa vyeo. Nafikiri hili tangazo la Mheshimiwa Waziri leo litawapa nafuu na mategemeo kwamba hali hii itamalizika na wataweza kupandishwa vyeo kama ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupandishwa vyeo na kuisifu Uhamiaji, ukizungumzia kwa ujumla Uhamiaji Tanzania tazito ambalo nalionia ni biashara ya binadamu. Biashara ya binadamu kila siku tunaisiklia na tunaomba Serikali ijitahidi sana kukabiliana na changamoto ya biashara ya binadamu. Pia kuna uhaba wa wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji ambao hawajaa jiriwa kwa kipindi cha miaka mitatu, minne hivi. Sasa baadhi ya Taasisi za kiaskari kama Polisi, Jeshi na wengine wamepata fursa za ajira, lakini wa Uhamiaji bado hawajapata nafasi za ajira, kwa hiyo, naomba nalo hili liangaliwe sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea naomba nizungumzie *NIDA*; Taasisi hii ina umuhimu mkubwa katika maisha ya wananchi wa Tanzania, kwa sababu ndiyo inashughulika na kutoa vitambulisho vya Mtanzania, vitambulisho vya Taifa lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wako, hii *NIDA* naiomba sana ishirikiane na Wakala wa Usajili wa Zanzibar ambao nao wanatoa vitambulisho vya Mzanzibari, vitambulisho hivi vina umuhimu sana kwa watu wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla. Jambo ambalo lipo hivi sasa ni kwamba kama vile vitambulisho vya Mzanzibari havitambuliki, tukienda kwenye *passport* havitambuliki, katika usajili wa simu havitambuliki, kwa hiyo tunaomba *NIDA* wafanye mashirikiano ya karibu na Mamlaka ya Usajili wa Mzanzibari.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia *NIDA* ni deni la JKU, Zanzibar Mamlaka hii ya *NIDA* inadaiwa karibu milioni 489 na JKU Zanzibar kutokana na ulinzi wa ofisi zao mbalimbali. Kule Pemba sehemu ya Micheweni wanadaiwa milioni 82, lakini ukija Ofisi Kuu ya Idara wanadaiwa milioni 222, Mwanakwerekwe wanadaiwa milioni karibu 110 na Gamba hivyo hivyo. Madeni haya yamemalizika tangu Julai, 2018, kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri akija hapa aje atueleze kuna mpango gani wa kulipa madeni haya ya JKU kwa upande wa *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Machano Othumanli Saidi. Mheshimiwa Leah Komanya, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel, dakika tano.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia muda ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mambo ya Ndani. Awali ya yote, naomba nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya, Mheshimiwa Rais amekuwa akiguswa na matukio yanayohusishwa na wananchi kuuawa kutokana na ajali na matukio mbalimbali na Mheshimiwa Rais amekuwa akichukua hatua mara moja bila kusita. Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri toka ateuliwe, akishirikiana na wasaidizi wake pamoja na Naibu Waziri wameweza kusimamia vizuri Wizara ya Mambo ya Ndani na kuweza kudhibiti matukio makubwa ambayo yalikuwa ni tishio kwa usalama wa raia yakiwemo uvamizi mkubwa katika mabenki yetu ambao ulikuwa ukigharimu maisha ya raia pamoja na askari wetu.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya watu wenye albino, mauaji ya watu wenye albino yameweza kudhibitiwa, tumekuwa hatusikii yakiripotiwa. Naomba niwapongeze sana. Naomba pia nipongeze kwa upande wa mauaji ya vikongwe; sisi tunaotoka Kanda ya Ziwa, jambo hili lilikuwa kero na lilitutia aibu wananchi tunaotoka Mikoa ya Kanda

ya Ziwa, lakini nipongeze Jeshi hili limeweza kudhibiti mauaji ya wazee wetu vikongwe. Vile vile ajali za mabasi zimekwisha ama zimepungua, matukio yamekuwa hayaripotiwi. Naomba waendelee hivyo hivyo walivyoanza kwa kuendelea kutoa elimu kwa madereva pamoja na raia.

Mheshimiwa Spika, Askari hao wanafanya kazi nzuri sana lakini wana changamoto katika mazingira ya kufanya kazi pamoja na vitendea kazi ofisini. Ukipifika vituo vya polisi hata karatasi za kuandikia maelezo ya mtuhumiwa wanapata shida, inalazimu wakati mwingine kuomba waletewe na hii pia itaweza kusababisha wasitende haki kwa sababu hata vitendea kazi havipo.

Mheshimiwa Spika, nyumba wanazoishi ni shida, naomba waongezewa bajeti ya kutosha ili askari wawewe kujengewa nyumba bora, wawewe kutoka uraiani. Vile vile nishukuru kwa kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha maboma katika Wilaya ya Meatu ambayo yalikuwa ya mwaka toka 1999. Maboma haya nimekuwa nikiyaaongelea toka nilipoingia Bungeni na swali langu la pili lilikuwa kukamilisha maboma hayo. Nawashukuru kwa sasa wametenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha maboma.

Mheshimiwa Spika, pia niongelee upande wa dawati la jinsia. Dawati la jinsia lipo kwenye *level* ya wilayani katika kituo cha Polisi, lakini ukatili mkubwa unafanyika katika ngazi ya chini. Naomba waboreshe waone namna gani wanaweza wakafanya ili kuweza ku- *accommodate* yale matukio kwa wakati yanayotokea katika ngazi za chini, kwa sababu matukio mengi ya ukatili yanafanyika katika ngazi ya nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti ajali za bodaboda, pia naomba elimu itolewe kwa raia pamoja na waendesha bodaboda hususan katika uvaaji wa *helmet*, nashauri ili wawewe kuvutia uvaaji wa *helmet*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Usafi uzingatiwe.

Mheshimiwa nashukuru na naunga mkono hoja.
(Makofii)

SPIKA: Ahsante sana Leah Komanya. Mheshimiwa Ruth Mollel, dakika tano, tafadhalii.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia nami pia kwenye hii Wizara. Jambo kubwa ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu mikutano ambayo tunanyimwa kufanya, wakati kikatiba tunaruhusiwa kukusanyika na kukaa na kuzungumza mambo yetu kama vyama, lakini imekuwa ni vigumu kufanya hilyo kwa sababu tunazuiwa kufanya mikutano, hata mikutano ya ndani.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Diwani wa Mkuranga, mwezi wa jana nilikuwa na kikao tume-book ukumbi kwa ajili ya kuwa na vikao vyetu nya chama kwa ajili ya kuchagua viongozi wa chama. Nimekwenda Mkuranga, polisi wamekwenda wamemtisha yule bwana mwenye *hall* pale Mkuranga, akakataa kutupa *hall* la kufanya mikutano. Tukaondoka pale, tukaenda kwenye Ofisi za chama, tukakaa nje, lakini bado huwezi kuamini *defenderzimekuja zina-patrol*, *wana-patrol*/watu ambao tumekaa tunazungumza mambo yetu, hatuna silaha, hatuna kitu chochote, *patrol* inapita mpaka tumemaliza mikutano pale nje, tena nje ya Ofisi ya Chama, nikajiuliza yaani Tanzania tumefikia kiasi hiki. *(Makofii)*

Mheshimiwa Spika, wananchi tumekaa tunazungumza mambo yetu, hiyo petroli ya walipakodi inayozunguka na *defender* muda wote na maaskari wamejaa kwenye *defender*, ni sisi kweli wanatuchunga au wanatutisha. Nafikiri hapa tulipofikia si penyewe, tunataka tuirudie Tanzania yetu ambayo tulikuwa tunakaa, tunafanya mikutano yetu kama ni mikutano ya ndani ambayo imeruhusiwa, basi Mheshimiwa Waziri aje na kauli anapokuja

kuhitimisha hoja yake atuambie kwanza ni sheria gani ambayo inatunyima sisi kuwa na vikao vyetu vya ndani, wakati chaguzi zinakuja ni lazima sisi kama chama tujipange kwa ajili ya kuingia kwenye chaguzi, tutajipangaje kama hata mikutano ya ndani wanatuzuia kufanya. Naomba Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha hoja yake aweze kutuambia ni kanuni gani anayoitumia kutokuruhusu sisi kufanya vikao vyetu.

Mheshimiwa Spika, maandamano; maandamano ni namna moja ya wananchi kutoa...

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

SPIKA: Taarifa, pokea taarifa Mheshimiwa Ruth Mollel.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Ruth Mollel, kwanza mimi namheshimu sana na nafikiri kwamba yeche kwa fursa kubwa aliyopata katika Jimbo langu la Mkuranga na namna ya kazi anayoshiriki kufanya pale, sikutegemea kama angeweza kuwa ni mmoja katika Wabunge wanadolishutumu Jeshi la Polisi. Nataka awe mkweli kwamba Mheshimiwa Ruth Mollel anafanya mikutano katika Kata ya Kitomondo amekutana na akinamama hadharani wala siyo mikutano ya ndani na anatoa vifaa na vitu mbalimbali. Amekwenda Kata ya Vikindu, amefanya mikutano, ametoa pesa misikitini, amefanyaje, hadharani wala siyo kwa kificho na Ofisi ya Chama cha CHADEMA Mkuranga haijawahi kuwepo. Sasa nadhani wakati Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani atakapo kuja kumjibu kwa kuwa anataka ayapate hayo anayoyaomba hapa, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, basi mpeni hiyo ladha ambayo anaitamani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Mheshimiwa Ruth Mollel taarifa hiyo.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa kwanza siipokei, kwanza kama Mbunge ni haki yangu kwenda kwenye huo Mkoa kuna kutoa msaada na vile vile kunizua kufanya, hili jambo limetokea na ni lazima nitalisema kwamba walituzuia kufanya mukutano na *defenderzilikuwepo*.

SPIKA: Kengele imelia kwa sababu ulikuwa umenani kidogo, nakuongeza dakika moja ili umalizie hicho cha mwisho.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa nazungumzia suala la maandamano, kwamba watu wanapoandamana wanatoa hisia zao kwa sababu siyo kila mtu ana nafasi ya kumwona Rais, saa nydingine Rais haambawi ukwelli, lakini watu wanapoandamana kwa amani, wanatoa hisia zao kusudi Mheshimiwa Rais aweze kujua wananchi wake waliomteua na kumuweka madarakani wanamawazo gani na maeneo gani ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maandamano yaruhusiwe, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani atuambie ni kwa nini anazuia maandamano ya watu kutoa hisia zao. Wananchi wanahitaji kusimamiwa na kulindwa, waende waandamane kwa salama watoe hisia zao na hiyo ni namna mojawapo ya watu kutoa vitu ndani ya roho zao, ukiwafungia watu ndani yanakuwa matatizo makubwa sana

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Mollel. Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Bobali.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayofanya, tunajuwa wanafanya kazi kubwa lakini vilevile wanafanya kazi hiyo katika mazingira magumu, tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nitazungumzia mambo mawili, kwanza nizungumzie hali ya uraia kule Mkinga. Wilaya ya Mkinga ni wilaya inayopakana na nchi jirani ya Kenya na kwa muda mrefu sasa tumekuwa na tatizo ambalo limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wangu, kero ya uraia. Bahati nzuri jambo hili unalifahamu lilifika Mezani kwako ukataka nikupe ufanuzi tukafanya hivyo lakini jambo hili mpaka leo bado halijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ipo changamoto kubwa sana kwa wananchi wangu wa makabila ya Wataita, Wakamba, Waduruma, ambayo haya ni makabila ambayo unayapata vilevile upande wa pili wa nchi jirani ya Kenya. Hili jambo la kuwa na makabila ambayo unayakuta kwenye nchi mbili tofauti si jambo geni. Kwenye maeneo yetu ya mipakani hili ni jambo la kawaida lakini wananchi wangu kule Mwakijembe wanapata usumbufu mkubwa sana kwa kuambiwa siyo raia kwa sababu tu wanaasili ya makabila ya Kenya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo sawa kwa sababu wananchi hawa wamekuwepo kwenye maeneo yetu kabla ya Uhuru. Wamekuwa wakitambulika kama raia wa Tanzania lakini imeingia sasa kadhia tulipoanza kuandikisha raia wetu, wale wananchi wote wanaoonekana wanamajina ya makabila haya moja kwa moja wanaambiwa siyo raia, hii siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri jambo hili nimeshawasiliana na Waziri tangu mwaka jana, nikamuomba ikiwezekana afanye ziara aje aone kadhia hii. Naamini muda bado upo na Waziri atajipanga ili tuje tutatue tatizo hili lakini kwa kweli ni jambo linalowaumiza sana wananchi wangu kwa sababu wananyimwa haki yao ya msingi ya kuchagua na kuchaguliwa kama viongozi lakini vilevile wananyimwa haki ya kushiriki kwenye shughuli nyingine za kimaendeleo kama wananchi halali wa Tanzania. Naiomba Serikali yangu ilifanyie jambo hili uharaka ili wananchi hawa wasione wananyanyasiaka katika nchi yao wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni vitendea kazi. Wilaya yetu ya Mkinga baada ya kuanzishwa, pale Makao Makuu ya Wilaya hatuna kituo cha polisi. Kituo tunachokitumia kama kituo cha polisi kiko takriban kilomita 40 kutoka makao makuu ya wilaya, hili si jambo zuri. Naiomba Serikali ione umuhimu wa kujenga kituo cha polisi kama Makao Makuu yetu ya Polisi katika Wilaya ya Mkinga pale kwenye mji wetu mkuu wa wilaya pale Kasera.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa Tarafa ya Maramba ambayo hii inajumuisha kata 10 tuna jengo la kituo ambalo limechoka, jengo hili ni *condemned* lakini ndipo kilipo kituo chetu. Wananchi wamejitätahidi kwa nguvu zao kujenga jengo la kisasa. Tunachohitaji ni msaada wa Serikali tuweze kumalizia jengo lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali ifahamu kwamba tuna askari wale wanaohudumu katika kata 10 hawana makazi, hii haiwezi kuwa sana. Naiomba Serikali yangu iliangalie jambo hili na iangalie jambo hili ikijua kwamba maeneo haya ni ya mpakani. Sasa unapokuwa na kituo cha polisi kwenye kata kinachohudumia kata 10 lakini kiko kwenye jengo ambalo ni *condemned*, Mheshimiwa Waziri wewe unajua mambo ya kiusalama silaha na kadhalika, unajua nisiendelee kwa *details* hapa, lakini tuna changamoto kubwa tunaomba msaada huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini viro vitendea kazi vingine ni changamoto kubwa kwa askari wetu kule Mkinga ambao wanafanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama katika maeneo ya mpakani inakuwa shwari. Tunawaomba sana muwaangalie kwa jicho la pekee. Gari moja kwa eneo lile halitoshi, lile gari lililoko kwenye Kata ya Maramba ni bovu. Tunaomba msaada wetu tuweze kupata gari ambalo litasaidia kulinda usalama kwenye maeneo yetu ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dunstan Kitandula, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Hamidu Bobali na Mheshimiwa Deo Sanga atafuatia.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Nataka nianze na hoja ya vijana wa bodaboda wa pale Mchinga kutakiwa kuwa na kitambulisho cha Sh.20,000, hivi vitambulisho vilivyotolewa na Mheshimiwa Rais. Nataka kupata majibu kwamba huu ndio utaratibu? Mimi nimesoma ule Waraka unaoainisha ni watu gani wanapaswa wachangie ile Sh.20,000, suaona sehemu ya bodaboda. Kwa Mchinga pekee bodaboda baada ya kuwa na leseni wanatakiwa pia wawe na kitambulisho cha Sh.20,000.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri akija aje atueleze kwamba haya ni maelekezo yanafanyika kwa ajili ya kukusanya kodi na ikiwa kama bodaboda wanatakiwa wachangie Sh.20,000, je, madereva wa gari taxi kwa nini nao wasilipe? Kwa hiyo, hili jambo nataka nipate majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mimi nakubali kama wenzangu wanavyokubali kwamba Jeshi la Polisi linafanya kazi nzuri na kubwa ya kulinda raia na mali zetu tulizonazo lakini yapo mapungufu lazima tuyaseme na Jeshi la Polisi wayachukue waweze kuyafanya kazi yabadilike. Dhamira ya mtu inapimwa kwa maneno na vitendo, wakati mwingine unaweza ukachafuka kwa ajili ya maneno yako tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano anapotokea Polisi akasema nitawapiga na kuwachakaza, hili neno linaudhi lakini pia halina tafsiri njema kwa raia ambao umeapa utakwenda kuwalinda wao na mali zao. Kwa nini usitumie lugha nyingine ambayo inaweza ikatumika kuzuia lakini pia wewe ukaonekana kwamba dhamira yako ni njema katika kulifanikisha jambo lile.

SPIKA: Kwa mfano Bobali, hebu mfundishe lugha ya kutumia, asemeje?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, kwa mfano tu aseme maandamano haya yamezuiwa na msiandamane, inatosha. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

SPIKA: Sasa huyo anayesema hivyo ni Mwenyekiti wa Mtaa au askari huyo? (*Kicheko*)

Endelea Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Askari ni askari tu, kama umepita JKT hutashangaa hivi vitu.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini katika tamaduni za kawaida kabisa Polisi walioapa kulinda raia na mali zao si vyema kuwatisha kwamba watawapiga na watawachakaza, si vyema kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi yako mambo Jeshi la Polisi lazima tuyaseme wamefanya vizuri. Kwa mfano, katika jambo la kupambana na ujambazi, kiwango cha ujambazi kimepungua, hili ni jambo la kupongeza, wanafanya kazi nzuri sana lakini yako mambo yanatia doa Jeshi la Polisi. Kwa mfano, *very recently* Jimbo la Mchinga kulikuwa na uchaguzi, Diwani mmoja alikuwa amefariki mwezi Machi, kwa hiyo, uchaguzi ukatangazwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi wakiwa kwenye gari ya polisi, wakiwa na silaha zao wamekwenda nyumbani kwa mgombea wa Chama cha CUF kumlazimisha asaini barua kwamba yeye anajitoa. Jeshi la Polisi usiku wamemvamia nyumbani kwake. Bahati nzuri tulijua kabla hawajakwenda

tukamwambia toka akakimbia. Sasa Mheshimiwa Waziri, haya ndio majukumu ya Jeshi la Polisi? Tena wakiwa wameambatana na msimamizi wa uchaguzi, unakwenda nyumbani unamwambia saini hapa kwamba unajitoa halafu baadaye wanatangaza kwamba wamepita bila kipingwa, *this is not fair. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mambo kama haya yanatia doa Jeshi la Polisi. Tukikaa nao hawa Polisi wakati mwingine ni rafiki zetu wanatuambia kabisa jamani eeh sisi tunaambiwa. Sasa ni nani anayewaambia Jeshi la Polisi kufanya kazi hii? Ukija utuambie kwamba wewe Waziri ndio umewaambia kwa sababu tunakuona muda wote unashika llani ya CCM unatembea nayo ...

SPIKA: Mheshimiwa Bobali, tukikutaka utuletee hao Askari walokwambia haya unayoyasema humu utaweza kuwaleta?

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, mimi natekeleza jukumu langu la kumfahamisha Mheshimiwa Waziri.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

SPIKA: Unatekeleza jukumu lako lakini hupaswi kutudanganya kama Bunge, hili ni Bunge.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, sidanganyi.

SPIKA: Kwa hiyo, kama ulipewa taarifa hizo *inconfidence* basi ni vizuri ukae nazo *inconfidence, as long as* unaziweka hapa maana yake uko tayari kutuletea hao Askari waliosema hayo na kama hauko tayari kuleta hao Askari maana yake wewe uko tayari kuwa *liable* kwa unayoyasema. Yaani lazima upime kama kiongozi kuna habari unapewa kwa matumizi yako mradi umeamua kuyaanika hapa maana yake uko tayari kusimama nayo.

Sikukatazi kusema endelea mradi uwe tayari kwa hayo naku-*caution* tu.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Spika, nimekuelewa ila nachosema tunakokwenda kwenye mwaka wa uchaguzi huu Serikali za Mitaa, jeshi letu litumike kwenye kutulinda na kuhakikisha kwamba vyama vyote vinatendewa haki. Hilo ndiyo hoja yangu, nimekuelewa.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kwenye suala la uhamiaji. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Kamishna Mkuu wa Uhamiaji lakini kuna jambo lina dosari. Kumekuwa na wahubiri *especially* wa Kiislamu wamekuwa wakija miaka mingi hapa wanapita kwenye maeneo yetu wanakuja kuhubiri hasa karibu na mwezi huu wa Ramadhan. Mheshimiwa Waziri anajua kwamba wako wahubiri mwaka jana waliondolewa hapa nchini kwa kupewa *warranty* saa 24, ikawa shida sana. Sasa hivi kumekuwa na shida nyingine wahubiri wakiomba visa inakuwa shida sana wakati mwingine mpaka hata ule muda wenyewe uliokusudiwa kwamba twende tukaelimishe au tukaseme hili unapita.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri jambo hili mliangalie. Tunajua kwamba mnaangalia mambo ya ugaidi na kadhalika lakini wako wahubiri mkiangalia *records* zao wamekuwa wakija kwenye nchi hii miaka yote. Kwa mfano, mimi toka nimekuwa na akili timamu wako watu nimewahi kuwaona wanapita maeneo yetu wanakuja wanahubiri wale Wapakistanilakini sasa hivi wakiomba visa kuja Tanzania inakuwa shida sana. Sasa Mheshimiwa Waziri wakati mwingine mnapozuia watu hebu tazameni na *records* zao kwamba hawa wana *record* gani zilizopita?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga nilikwishakutaja utafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ajiandae.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweza kuchangia. Kwanza naunga mkono hoja kwa kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi ikisimamiwa na Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wanafanya kazi nzuri sana ya kutulinda sisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa nasikiliza wachangiaji wenzangu hasa upande fulani, hebu fikiria Jeshi la Polisi na Mahakama visiwepo angalau kwa siku moja nini kitatokea? Ni lazima tumpongeze Waziri kwa kazi nzuri ambayo anafanya kupitia Jeshi la Polisi la kutulinda sisi na mali zetu na nchi kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Njombe tulipata tatizo la mauaji ya watoto. Jeshi la Polisi lilitanya kazi kubwa ya kuwakamata wahusika, hivi sasa wanajibu tuhuma walizifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nzungumzie kwenye Jimbo la Makambaku, mwaka 2016/2017 kulikuwa na mauaji vijana wengi walikuwa wananyang'anywa bodaboda zao na wanauwawa. Jeshi la Polisi limeweza kuwakamata wote waliokuwa wanafanya vitendo hivyo. Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama - Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya - Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama, *RPC* na *OCD* na wapelelezi wake wa Jimbo la Kiwilaya la Kipolisi pale Makambaku. Wamefanya kazi nzuri sana, walikamata mpaka magaidi pale Makambaku, wale ambao walikuwa wanafanya mauaji kule Kibiti wamekamatwa pale na Jeshi hili hili la Polisi. Kwa hiyo, ni lazima tulipongeze sana kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niwapongeze kwa kujenga nyumba za askari wetu kwa nchi nzima na hususan kwenye Mji wetu wa Makambaku. Tangu tupate uhuru hatujawahi kupata nyumba za Jeshi la Polisi, safari hii tumejengewa nyumba na wanaendelea kujenga nyumba nzuri za kukaa Askari wetu. Hata mimi Mbunge wao nimeweza kuchangia kwa asilimia kubwa kufanikisha nyumba zile ambazo Serikali ya Magufuli imetupa fedha. Nawapongeza

sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya.
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, Makambaku ndiyo njia panda ya kwenda Songea, Mbeya, Iringa, tunaomba utupe gari ili Askari hawa waweze kufanikisha shughuli zao za kidoria kwenye Mji wetu wa Makambaku. Tunaomba sana tupate gari ambalo litasaidia kufanikisha shughuli za kiusalama katika Mji wetu wa Makambaku.

Mheshimiwa Spika, vilevile gereza liko Wilayani Njombe, kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani tunaomba waone umuhimu wa kujenga gereza katika Halmashauri yetu ya Mji wa Makambaku. Sisi wa Makambaku tutawatafutia eneo la kujenga gereza kwa ajili ya wahalifu ambapo kwenda Njombe ni mbali. Kwa hiyo, eneo lipo, nikuombe sana Waziri mwenye dhamana uone namna ya kutenga fedha kwa kipindi kinachokuja ili kujenga gereza katika Mji wetu wa Makambaku.

Mheshimiwa Spika, nzungumze jambo la mwisho, pamoja na kazi nzuri si vizuri kuwataja hawa Askari lakini kupitia Bunge lako naomba niwataje kwa sababu ya kazi nzuri wanayofanya, akiwepo *OCD* wa Mji wa Makambaku, Mkuu wa Upelelezi pamoja na timu yake ya askari kadhaa wanaofanya kazi nzuri ambapo waliweza kufanikisha kukamata silaha mbalimbali katika mji wetu. Naomba muone namna ya kuwapandisha madaraja hawa askari kwa namna ambavyo wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo askari kadhaa ambao labda wakati fulani wanaweza kuwa si wazuri ...

SPIKA: Mheshimiwa Sanga, unawapongeza askari wako wa Makambaku lakini hapa Dodoma Wabunge wote mnakaa kwa amani kabisa, salama kabisa lakini *RPC* wa Dodoma hamumpongezi, hii inakuwaje? *(Kicheko/Makofi)*

Eendelea Mheshimiwa Sanga.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, ni kweli na ndiyo nilikuwa nakuja huko kutokana na kazi nzuri wanazozifanya na hata sisi Wabunge hapa, sisi kule lringa kuna msemo wanasema '*tukikala kilega*', tukilegea ni kwa sababu ya usalama wa hawa wanaotulinda. Kwa hiyo na Dodoma hapa tunalindwa, tunakaa majumbani salama huko tunakokaa hakuna bughudha mitaani, tunatembea mpaka usiku wa manane ni kwa sababu ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho baada ya maelezo haya, Mheshimiwa Waziri na timu yako kaza buti, endelea kuchapa kazi, askari mmoja anayeharibu si jeshi zima bovu. Kwa hiyo, hawa askari ambao wanataka kulichafua Jeshi la Polisi kuititia Kamanda wako Siro muendelee kuwadhibiti ili warudi kwenye mstari vinginevyo kazi ni nzuri na mnadhibiti vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hili suala la mikutano ambalo wenzangu wamelizungumzia hapa, kwenye mikutano watu walikuwa wanafanya kazi ya kuja kutokana si kufanya shughuli za maendeleo. Sasa hivi mikutano tunafanya kila watu kwenye maeneo yao, shughuli zinakwenda vizuri, Waziri kaza kamba. Nikutakie kila la kheri katika shughuli hizi ambazo ziko mbele yetu, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Jacqueline jiandae, dakika kumi kumi.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ingawaje kwa kweli haukuwa mpango wangu hasa kuongea lakini imebidi niongee kwa sababu zifuatazo.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa namtania Mama Makilagi hapa aliposema haongei na watoto na mimi nikasema mimi ndiyo baba yao na Bunge likacheka kidogo. Kwa muktadha huo nataka niseme hivi, imetokea lugha hapa

kwamba kambi yetu hii hatuthamini kazi ambazo zinafanywa na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niseme kwamba hii si kweli. Nichukue fursa hii kwa niaba ya wenzangu kuwapongeza askari wote wa jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Uhamiaji, Jeshi la Zima Moto ambao wanafanya kazi yao vizuri. Rai yetu hapa ni mbili tu ya kwanza ni kulikumbusha na kuliomba Jeshi la Polisi kufanya kazi zake kwa kufuata sheria hiyo ndio rai yetu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa hili hakuna anaweza kusema kwamba Jeshi la Polisi lifuata sheria mia kwa mia hakuna kwa sababu yapo matukio kadhaa katika nchi yetu ambayo yana-*prove* tofauti. Kwa mfano juzi, juzi kuna kijana alikamatwa Waziri Dhahiri pale Lembeli amekamatwa asubuhi saa mbili amepigwa na askari mpaka kafia kituoni. Sasa askari kama huyu ni moja katika maskari ambao hawafuati sheria, hawafuati taratibu na matukio kama haya yapo maeneo mengi. (*Makofi*)

Kwa hiyo sio sahihi kusema kwamba tunaosema Jeshi la Polisi lijirekebishe lifanye tathimni ya baadhi ya askari wake sio sawa sawa na kusema kwamba hatulipendi jeshi la polisi wala asitokee mtu akasema eti kwamba ikitokeo polisi wasiwepo kwa masaa machache itakuaje haitatokea mpaka dunia itakapokwisha.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Selasini pokea taarifa Mheshimiwa *Chief Whip*.

T A A R I F A

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa mchangiaji anaochangia nimpende kumkumbusha kwamba moja ya mambo ambayo jana yalifanya kiasi kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wakafikia kusema kwamba hawa hawawapendi polisi wetu

ni kwamba mchangiaji wao mmoja alifikia kusema kwamba polisi ni kansa ya Taifa. Nakupa taarifa kwamba hilo neno sio nzuri na tunafahamu kabisa kwanza kansa hata nikisikia kansa naogopa polisi hao hao wanaolinda usalama wetu na sisi tupo salama hapa wanapotamkwa kwamba wao ni kansa la Taifa hilo neno linaukakasi nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa bado Mheshimiwa Selasini kidogo. Sikupata *privilege* ya kulifahamu hilo lakini kama limesemwa na Mbunge ningeomba nifahamu tu wala usifiche ni Mbunge nani?

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda wakati anachangia jana alisema kabisa wazi na Hansard zitaeleza kwamba polisi ni kansa ya Taifa.

SPIKA: Ahsante naomba mnilettee hiyo hansard sijui kama Mheshimiwa Sophia yupo lakini kama Wabunge haya ni majeshi yetu, hata uwe na chuki kiasi fani kuna mstari ambaao huwezi kuvuka. Kwa hiyo, ni vizuri *Chief Whip* unaongea basi endelea.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ahsante natumai utanihifadhia muda wangu.

Mheshimiwa Spika, nilivyoanza kusema nimesema nasimama kama kiongozi wa kundi hili, na Mbunge aliyeongea angekuwa amesoma saikolojia angekuwa amesoma kitu kinaitwa *furious of generation* haiwezekani kauli ya mtu mmoja ikawa kauli ya wote, na Mbunge hili lina taratibu zake kama kuna mtu mmoja amezungumza Bunge hili lina namna ya kumdhibiti huyo aliyezungumza. Lakini kama kiongozi wa kundi hili nasema hatuna msimamo wowote wa kulidharau jeshi la polisi kwa namna yoyote ile na ninawapongeza polisi ambaao wamekuwa wakifanya kazi vizuri *full stop* hakuna zaidi. (*Makof*)

TAARIFA

SPIKA: Almas Maige

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kutoka CHADEMA huko nje, huko nje amesema mambo mengi na kulikashifu Jeshi la Polisi na ndiye Msemaji wa Kambi ya Upinzani, sasa wanakanusha au wanakubali?

SPIKA: Mheshimiwa Selasini unaipokea taarifa?

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ninampa pole rafiki yangu katika utu uzima huu alipaswa vilevile awe amezijua kanuni. Pamoja na hayo sote kwa pamoja kama Wabunge wajibu wetu ni kulisaidia Jeshi la Polisi. Tunasema kwa pamoja jeshi letu lina matatizo, askari wetu wanahitaji nyumba bora wote, wa polisi, wa magereza, wa uhamiaji hili sio suala la upinzani ni suala letu wote na kila Mbunge akisimama hapo anazungumza kuhusu nyumba za askari kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, tunazungumza juu ya vitendea kazi vya polisi, tunazungumza habari ya vituo bora vya polisi, jeshi letu kwa sasa ni jeshi ambalo unakwenda kituoni wanahangaika na makaratasi na mafaili na kadhalika. Watu wameshaenda sasa hivi kisasa watu wana komputa na kadhalika na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumza hayo, tunazungumza habari ya mishahara na posho za askari wetu. Tunazungumza habari ya *uniform* za askari wetu haya ndiyo mambo ya kuzungumza na Mheshimiwa Kangi Lugola Waziri ametuletea hotuba hapa tuijadili sisi kama Wabunge sio kumjadili Mheshimiwa Tundu Lissu hayumo humu kwenye hotuba ya Waziri. Kwa hiyo, wakati mwingine tunatumia muda Wabunge vibaya kugeuza kila jambo kuwa jambo la siasa wakati huu muda ni muda wa wanaotulipa mshahara, wanaotuliapa posho ambaao ni wananchi wa Tanzania wanaolihitaji hili jeshi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wako askari ambaao wanalifedhehesha jeshi la polisi na ushahidi ni

kwamba limekuwa likichukua hatua dhidi ya askari wa namna hiyo. Tunachosema kasi ya kuchukua hatua iendelee.

Mheshimiwa Spika, na wewe unakumbua hotuba za Mwalimu Nyerere, Mwalimu Nyerere alikwisha kusema kuna vyombo viwili tu sasa hivi tunavitegemea sana watanzania. Chombo cha kwanza ni mahakama, chombo cha pili ni polisi. Mwalimu alisema polisi na mahakama wakiingia kwenye rushwa au kutotenda haki itakuwa ni balaa. Tunazungumza habari ya mikutano hapa, kusumbuliwa hapa, pilipili usizozila haziwezi kukuwasha sisi tunazungumza kwa sababu tunajua kinachotokea lakini polisi hawa lazima wawe mfano katika kutekeleza sheria. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati sheria ambayo wanapaswa watekeleze, polisi hawaruhusuwi kuingia kwenye *active politics* kwa sababu wao wanafanya maamuzi, jeshi hili ni la wote. Sasa polisi kuwa *tamed* na Watanzania kwamba ni la CCM na la Chadema watu wa upande mwingine hawatawapa ushirikiano na matokeo yake utendaji wa jeshi la polisi hautakuwa sawa. Kwa hiyo, ndugu zangu tunapozungumza habari ya kuriboresha jeshi la polisi hatuzungumzi kwa sababu ya chuki na jeshi la polisi. Tunazungumza kwa sababu tunalipenda na tunapenda lifanye kazi vizuri zaidi. Tunazungumza ili Waziri na Naibu wake wapate uwezo wa kulisaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, na mwisho pale kwangu Rombo lile ni jimbo ni jimbo la mpakani Mheshimwa Waziri angalia uwezekano wa kusaidia wale polisi ili ule mpaka uweze kufanya kazi vizuri. Na sisi watu wa Rombo tunashirikiana vizuri na Jeshi la Polisi tumejenga kituo pale Useri kwa nguvu zetu tumekabidhi Serikalini sasa hivi tuna msingi kwenye Kata ya Mahida unakwenda, tuna msingi umeshafika leta kwenye Kijiji cha Kilongo chini msingi wa kituo cha polisi na wa nyumba za polisi. Huo ni ushahidi kwamba tunasaidiana na jeshi lenyewe na Serikali katika kuliboresha.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kusema kama tunatendelea na vijembee katika hoja kubwa kama hii ya

jeshi tunaiweka nchi yetu katika hatari kubwa sana kwa sababu tunaligawa jeshi tugawa na wananchi. Kwa hiyo, naomba tu ni rai yangu chukueni hoja ambazo zinaweza kusaidia jeshi upande huu zichukuliwe zinaweza kuisaidi jeshi upande tuweze kujenga jeshi bora kwa ajili ya nchi yetu. Ahsante sana nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushuru. Lakini litegemea ungesema chochote kuhusu Mbunge wako endapo kweli alisema maneno mazito kama hayo *at list* ungesema chochote kama kweli kambi yako *hai-subscribe to that kind of a statement.* Lakini kwa kuwa umechangua kutokusema chohote basi nakupa dakika moja zaidi nasema sikuwepo lakini kama kweli huyu amesema maneno hayo si dhani kama kambi mnawenza mkanyamza.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, *ruling* ilifanyika jana.

SPIKA: Sidhani kama kuna nchi yoyote ambayo Mbunge wake anaweza akasimama aka-*accuse* jeshi zima la polisi yaani jeshi *as a unity* kama jeshi kwamba ni kansa nasubiri hiyo Hansard. Lakini sidhani kama ninyi hapo mtakubaliana mnyamaze na mkadhani you *will get away with that kind of the statement* eeh! if that, thus *what she said*, ni vizuri abaki nao huo msalaba wake yeye mwenyewe mkiamua kucaa pamoja nao sio mbaya ni chagua kupanga ni kuchagua tuendelee Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. (*Kicheko*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunipa fursa hii ya kuweza kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu ili nami niweze kuchangia katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha bilioni 10 kwa ajili kwenda kuboresha makazi ya askari wetu. Hali kadhalika vituo vya

polisi vingi vimetengewa fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo na Wabunge wengi wamesimama humu wametoa ushuhuda na mpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika,nimpongeza Waziri mwenye dhama ya Wizara hii ndugu Kangi Lugola unafanya kazi nzuri sana chini ya majeshi yako yote ya Polisi, Magereza, Uhamiaji pamoja na Zima Moto. Ukisikia jirani yako anapiga kelele ujue sindano zinaingia vizuri na unafanya kazi vizuri. Itakuwa ni ngumu sana kwa jeshi la polisi kupewa sifa ya kwamba mnafanya vizuri yaani mpokuwa mnaambiba hamfanyi vizuri kwa upande wa pili kwamba mpo sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasihi kwamba kamanda Sirro endelea kufanya kazi sisi wenyewe nia njema tunaona kabisa kazi unayofanya ni nzuri ulinzi umeimalika katika nchi yetu ya Tanzania watu wamekuwa na nidhamu kazi zinafanyika kwenye maeneo mbalimbali hata vijana waliokuwa wanashinda vijiweni vibaka nao pia wamepungua sana hongera sana kama Sirro. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kasma ya mafuta kwa jeshi la polisi, magereza na maeneo mengine. Pesa imekuwa inatengwa kidogo kuelekea kwenye maeneo hayo ili waweze kutimiza shughuli zao. Inafika kwa muda mfupi sana unakuta pesa inaisha wanashindwa kutimiza wajibu wao. Kwa hiyo, naomba majeshi haya yote yatengewe fedha ili waweze kufanya shughuli zao kwa maana ya kupata mafuta yanayotosheleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kasma ya vipuli magari yameongezwa nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuongeza magari katika jeshi la polisi. Lakini pia vipuli navyo viongezwe kwa sababu vipuli bado ni vichache kwa hiyo wanashindwa kufanya mategenezo pale inapotokea magari yanapata uharibufu.

Mheshimiwa Spika, zipo stahiki za maskari ambazo wanashindwa kuzipata kwa mfano kuna suala *plainclothes*

ambalo ni *allowance* kwa ajili ya CID. Hii *allowance* hawaipati kwa hiyo nilikuwa naomba sana watengewe fedha kwa ajili ya kupata hiyo *allowance* ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Lakini pia kuna *house allowance*, *house allowance* inatakiwa 15% ya mshahara wa kila askari lakini hawapati kwa hesabu hiyo ya 15% naomba wapigiwe kwa 15% ili waweze kupata *allowance* hiyo.

Mheshimiwa Spika, mafao ya askari polisi, askari polisi wamekuwa wakipata mafao lakini hayo mafao yanachewa sana, siku za nyuma walikuwa wanatumia karibu mwaka mmoja na nusu ili waweze kupata mafao baada ya kustaaifu. Lakini sasa hivi imepungua walau mwaka mmoja. Niombe Serikali ipunguze zaidi sababu askari wetu wanapokuwa wamestahafu kuendelea kukaa katika hali ya manung'uniko hawapati fedha zao kwa wakati nayo pia haileti tija kwa sababu kazi yao ni gumu na wanafanya kazi pia wakati mwingine katika mazingira magumu wamapate fedha zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Iakini pia hawa askari inapotokea askari amefariki wanaobaki ndugu zao kuhusu suala la mirathi wanapata shida sana wanatumia muda mrefu sana kupata mirathi ya ndugu zao. Kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie suala hili hasa pale tunapojuu kwamba umuhimu wa jeshi la polisi kama ambavyo Wabunge wengine wamezungumza humu kwamba jeshi la polisi linafanya kazi nzuri na sisi tumo humu ndani kwa utulivu kwa sababu jeshi la polisi linafanya kazi yake barabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia suala la fidia kwa askari magereza na askari polisi. Inapotekea kwa majeshi haya inapotekea amepata madhara kazini, ameumia kazini sheria ya tume ya polisi namba 25 inaeleza kwamba askari huyu baada ya kuumia alipwe pesa apate fidia. Lakini haielezi kwamba fidia ile anayoilipwa inatoka katika fungu gani? Sasa leo hii naomba nishauri Serikari yangu, kwamba kwanini Serikali isikae pamoja na jeshi la polisi wakazungumza na wakaweza kuchukua utaratibu wa hawa askari wote wakaunganishwa kwenye mfuko wa fidia badala

ya hawa askari baada ya kupata matatizo wanajikuta kwamba wanasubiri yale mafao ambayo hayajulikani yanatoka fungu gani ni mpaka waombe benki kuu. Kwa hiyo, naomba sana suala hili lisimamiwe na lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, askari wetu hawa nao pia ni binadamu, ambao wameumbwa kwa mfano wa kila binadamu hapa ndani kwa maana ya Mungu. Hawa askari hawana moyo wa chuma wana moyo wa kibinadamu, wana moyo wa nyama.

Mheshimiwa Spika, inapotokea mtu anasimama humu katika Bunge lako hili Tukufu anawatuhumu askari. Jana amesimama Mbunge mmoja humu ndani akazungumzia suala la askari kuwabaka, kuwalawiti wanawake wanaokwenda kwenye vituo vya polisi. Miongoni mwa vituo ambavyo alivitaja ni pamoja na kituo cha Mtakuja Dar es Salaam na Staki shari na vingine lakini mionganoni mwa hivyo. Sasa najiuliza ni kweli askari hawa wanafanya vitendo vya aina hii? Na kama ndivyoo ni kwa nini aleze kwa maana askari wote...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. JACQUELIN N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, na kama ndivyoo kwa nini asichukuliwe akatoa ushahidi?

SPIKA: Mheshimiwa Jacqueline kuna taarifa.

TAARIFA

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa yangu kwanza nisikitike, anayechangia ni mwanamke. Jana nimechangia nikasema mabinti wanabakwa, wanatendewa kinyume na maumbile wanaambukizwa na *UK/MW/niseme* tu hii sio mara ya kwanza nimeongelea Bungeni. Alikuwa anakuja *RCO* kutoka Kanda Maalum gerezani tulimueleza na mifano. Nilipotoka tu gerezani niliongea na waandishi wa habari nilisema sasa ukiona Mbunge anabisha badala kwenda kusema!

SPIKA: Ulisema kwamba?

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, kwamba kuna mabinti wanatendewa ndivyo sivyo na wapo wanabakwa, wanaingiliwa kinyume na maumbile wanaambukizwa na UKIMWI na nikataja maeneo ya vituo ambavyo wametaja, na walivyokuja gerezani walisema wanaenda kufuatilia. Sasa na RCO kutoka Kanda Maalum sasa ukiona Mbunge ambaye amekuja kuwatete wananchi anatetea vitu anapindua, inabidi aombewe na inasikitisha sana. Polisi nimetaa taarifa ni chombo ambacho tunaongea huku Bungeni, wataeenda watafuatilia wataona *the validity* ya hiyo kitu na sio vinginevyo. Naomba sana Bunge hili litumike kushauri na kukemea na sio kutetea. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, nafikiri ulikuwa unampa taarifa

MHE. ESTHER N. MATIKO: Kama mnawapenda polisi mgeweza kubadilisha hata leo bajeti tukaingoza tukawajengea majumba wanateseka au tukawaongezea mshahara.

SPIKA: Ahsante sana inatosha Mheshimiwa Msongozi unapokea taarifa hiyo!

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, ninayezunguza ni Mwanamke na nina uchungu na wanawake wenzangu na walionileta ndani ya humu ndani ya Bunge hili ni wanawake. Siwezi kufurahia mwanamke mwenzangu analawitiwa, amekuwa na haraka ya kuyadaka maneno kabla ya kusikiliza nini ninachokisema angesubiri akaona *concernyangu* nini. Nasikitika sana kwa kudaka daka maneno. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hivi, huyo Mbunge ambaye ameeleza habari hii kama kweli vitendo hivyo viro awataje hao polisi wanaofanya hivyo ili waweze kuchukuliwa hatua, kwa sababu vitendo hivyo kwa wanawake wenzetu sisi hatukubaliani kama wanawake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini isiwe kwamba Askari wote wanapakwa matope hayo, *a-specify* ni nani na nani? Ina maana kwamba leo hii kwa watu ambao wamesikiliza ile *clip* wanawake wote wataogopa kwenda kwenye Vituo vya Polisi, wanaogopa kubakwa na kufanyiwa vitendo vya ulawiti. Kwa hiyo, *a-specify*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba hili suala lisichukuliwe kimzahazaha asaidie Polisi ili kutoa ushuhuda wa kina ili Polisi na Serikali walifanyie kazi kwa sababu mwisho wa siku isiwe ni katika hali ya udhalilishaji kwa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi, nakubaliana na wale wote ambao hawakubaliani na suala la maandamano, lakini pia hawakubaliani na suala la mikutano holela holela. Sisi kama Wabunge ziko kazi tumepewa na wananchi kwenda kuzifanya. Nashangaa sana Mbunge anasimama hapa, toka lilianza Bunge ye ye anazungumzia maandamano tu. Nawea nikafananisha na mnyama mmoja anaitwa nyumbu.

Mheshimiwa Spika, tabia ya mnyama anaitwa nyumbu anafanana hivi; mmoja akiongoza njia kwenda, basi wote wanakwenda huko hata kama kule kuna samba, wote wataelekea huko; hata kama kuna shimo, wote wataelekea huko. Sasa hivi humu ndani ya Bunge hamna agenda nyingine, ni kuongelea tu suala la maandamano, suala la Askari wamefanya nini.

Mheshimiwa Spika, suala la mikutano nasema nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, mikutano yote isiyokuwa na tija ikomeshwe. Hakuna mikutano, watu wakafanye kazi. Watu walikuwa wamezoea kuchukua vijimambo vidogo vidogo, anabeba kama dili anaenda nalo kwenye mkutano kupotosha watu na kufanya mambo yasiyostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba sana nipongeze Jeshi la Polisi, Kamanda Sirro kazia hapo hapo, endelea kufanya kazi

yako, tuko nyuma yako. Sisi tutakutetea na tutakusaidia.
(Makof)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, tunataka nchi iwe na amani, nchi iwe na utulivu badala ya watu kufanya mambo yao binafsi.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia kwa asilimia mia moja. *(Makof)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitoe tangazo moja kidogo. Tunao wageni. Hizi *gallery* zimejaa wageni wengi, wengine hawakuwepo asubuhi. Leo tulikuwa na wageni wengi sana. Tunao wanachuo 170 na viongozi watano kutoka Shirikisho la Wanafunzi wa Kozi ya Manunuzi na Ugavi kutoka Vyuo Vikuu vyote Nchini ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi yake.

Wanachuo wa Manunuzi na Ugavi popote mlipo simameni. Karibuni sana, sana, sana. Wanatoka vyuo mbalimbali hapa nchini Tanzania; na kama mnavyosemaga mara nyingi Waheshimiwa Wabunge eneo la Manunuzi na Ugavi ni moja ya eneo ambalo lina matatizo makubwa katika utendaji, lakini tunaona na tunashuhudia jinsi ambavyo vijana wetu wanakuwa *trained* na kuwa *experts* katika eneo hilo. Tunaamini huko tunakoenda hali ya Manunuzi na Ugavi katika nchi yetu itakuwa bora zaidi kuliko tunakotoka. Tunawapongeza sana, karibuni sana Bungeni.

Anayefuata ni Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mwamtumu Dau na Mheshimiwa Haonga, ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru sana kupata nafasi hii. Awali ya yote

namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia uhai kufika hapa leo kuchangia bajeti hii ya Taifa. Pia nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na pongezi na shukrani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani. Shukrani zangu, mwaka 2018 nilikuja hapa nikasikitika kwamba kuna familia 120 ambazo zina wakazi au zina watu ambao wanafikia 480 walikuwa wakitumia choo kimoja. Hivi sasa Jeshi la Polisi kule Ziwanji, Jimboni kwangu Jang'ombe tayari kuna choo kinajengwa na sasa hivi kipo katika hatua za mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba kuna choo pale cha zamani cha tokea Mkoloni mimi nimeanza kukikarabati pale, tumeshaingiza fedha kadhaa, lakini tumekwama katikati. Hata kama tukipata shilingi milioni mbili hivi au tatu, basi tunaweza tukatengeneza kile choo kikachangia pale kikaweza kuondoa matatizo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, hili nalitupa kwake, nkipata fedha hizo kile choo kitamalizika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine, nizungumze kwa Wabunge wenzangu kwamba kuna msemo unasema, "asiyelijua chozi, amtazame aliaye." Kuna msanii mmoja Marehemu John Komba alisema kwamba, "amani duniani imetoweza na pia Afrika imetoweka"; lakini kumbe Tanzania imejichimbia na kama hujui hayo, kaangalie Kongo. Kama hujui kufa, kaangalie Somalia.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu hii, ukiona vyaelea, basi ujue vimeundwa, amani iliyokuwepo ni kwa sababu ya mifumo ya kazi ya majeshi yetu ambayo yanafanya kazi ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuyapongeza majeshi yetu yote ambapo sasa hivi sisi tuko katika amani na usalama.

Kwa hiyo, kama kuna watu ambao waliwahi kubeza, wasifanye hicho kitu kwa sababu siyo kitu kizuri na wale ambao wanataka kutulizia ndege mbaya, washindwe na walegee. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *vote 28* - Jeshi la Polisi huwa mara nydingi linafanya kazi zake kwa kutegemea taarifa na mara nydingi mawasiliano ndiyo kitu muhimu kinachowezesha Jeshi la Polisi kufanya kazi. Sasa nilivoangalia randama na kitabu hiki cha bajeti, pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nikagundua *sub-vote 2036* ambayo iko katika mkoa wangu wa mjini kuna kifungu 22012 ambacho kinaelezea *communication and information*. Kifungu hiki kinahusiana na mambo ya mawasiliano ya simu pengine na mambo ya masunduku ya barua.

Mheshimiwa Spika, kwenye *sub-vote* hii ya Mjini Magharibi, kule hakuna hata senti tano: Je, kule Jeshi litafanya kazi vipi? Nikadhani labda zimewekwa Makao Makuu, nikaenda katika *sub-vote 2005* ambayo ni Polisi Zanzibar. Kuangalia pale nikakuta zimewekwa shilingi 180,000/= na hizi ni kwa ajili ya kulipia masunduku ya posta. Sasa nilikuwa najiuliza: Je, Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Mjini tunakoishi sisi pale, litafanya kazi zake vipi bila kuwa na vitu hivi vya mawasiliano? Watafanya kazi vipi?

Mheshimiwa Spika, nilipoangalia maeneo mengine kwenye mikoa mingine kama Kusini, Kaskazini, nimegundua kila sehemu kumewekwa shilingi 15,600,000/=, huku kwetu Mjini Magharibi, hakuna kitu. Nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, aniambie sisi tutafanya kazi vipi pale Mjini Magharibi? Aje anipe ufanuzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo niliombwa katika bajeti iliyopita, nilisema kuna jengo la Kilimanjaro, Ziwani Polisi. Jengo lile liko katika hali mbaya na wakati wowote linaweza likaleta madhara kwa wakazi wa jengo lile. Familia zinazokaa pale zinaweza zikaadhirika. Serikali jambo hili hawajalichukua.

Mheshimiwa Spika, nimeenda kuangalia katika kifungu cha *repairs and maintenance of buildings*, nimetazama, hakuna fedha iliyotengwa pale kwa ajili ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Nimetazama katika kifungu hicho

chicho kwa Polisi Zanzibar 2005, hakuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya jengo hili kulikarabati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimwulize Mheshimiwa Waziri: Je, pale Jeshi la Polisi amewahi kufika katika lile jengo akaona ile hali pale? Usipoziba ufa, utajenga ukuta. Kwa nini tusikarabati? Nimetazama katika fedha za ukarabati, kuna fedha zimebekwa chache sana lakini ziko katika mkoa mwingine. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia hiki kitu. Nasi tulikizungumza hiki, lakini sasa hakuna ambacho kimetengwa.

Mheshimiwa Spika, zimetengwa pesa katika kifungu cha Polisi Zanzibar cha 2005 ambapo fedha zilizotengwa, zimetengwa katika kifungu cha 2019 ambayo ni kwa ajili ya ukarabati mdogo wa Vituo vya Polisi. Kwa hiyo, hakuna ukarabati unaolenga nyumba za Polisi. Mheshimiwa Waziri hili mimi ni ombi langu tokea nimeingia katika Bunge hili. Moja nimepata, lakini hili sjapata. Kwa hiyo, hili nalitupia kwa Mheshimiwa Waziri tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine kwenye bajeti ya maendeleo; sisi pale Zanzibar Polisi viwanja vya kujenga majengo vimo, lakini Mkoaa wa Mjini hatujatengewa fedha. Nimetazama kwa Zanzibar nzima kwenye bajeti hii, ukienda katika bajeti ya maendeleo, utakuta kuna shilingi milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Mkokotoni Kaskazini Unguja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pale Zanzibar ukija ni aibu. Nyumba ya *IGP* wamebekwa maofisa wane. Watu wanaohamishwa wakazungushwa vituo, huwa wanakuja pale Mkoaa wa Mjini Magharibi na wanafikia Ziwan Polisi. Kwa hiyo, hali ya makazi mle haiko vizuri. Nilipotazama katika kifungu cha 6303 *construction of offices and quarters* cha Zanzibar, ndiyo nimegundua kwamba kuna hiyo shilingi milioni 500. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuangalia hivi vitu kwamba vitafanyika vipi ili nasi mjini pale tuweze kupata majengo.

Mheshimiwa Spika, kingine, nakwenda katika *vote* ya vitambulisho, hapa kwenye *vote* ya vitambulisho nizungumzie kitambulisho kule kwetu tunachokiita kitambulisho cha Mzanzibar. Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar iliingia gharama na mpaka sasa hivi inaendelea kuingia gharama kutoa vile vitambulisho ili viweze kufanya kazi; na kweli vikatoka. Vilitoka mwanzo kabla ya Kitambulisho cha Taifa. Vitambulisho hivi vimetoka, sasa hivi eti hata benki unapokwenda wanakwambia lete namba yako ya leseni ya gari wanakidharau hiki kitambulisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hapa sasa hivi kuna usajili wa simu kwamba mtu anaweza akasajiliwa hata na leseni ya gari au kadi ya kupigia kura, lakini kitambulisho kilichomtambulisha kwa taarifa zake zote kinakataliwa. Kwa nini kitambulisho hiki kisiende sambamba na kitambulisho hiki cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Kwa nini tunakidharau hiki kitambulisho wakati tayari Serikali moja imeshaingia gharama na bado Ofisi ya Vitambulisho ipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikwenda benki moja nikasema kwamba kadi yangu ya Uraia ya Utanzania sijachukua, nikawatolea kadi ya Zanzibar wakasema, aah bora ulete leseni ya gari. Hivyo kweli kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi kikadharaulike ikapate hadhi leseni ya gari katika kupita huduma!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kupitia Idara hii ya Vitambulisho vya Taifa ajaribu kuliweka sawa au kutupa ufanuzi, kwa nini watu wasiweze hata kusajili simu kwa kutumia Vitambulisho vya Uzanzibar? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa nami naweza nikajilandikisha kukamata shilingi, kwa sababu kule Ofisi ya Vitambulisho ipo na bado inafanya kazi na gharama kubwa zimetumika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie katika masuala ya ufanisi kwenye Jeshi la Polisi hususan nazungumzia

utendaji kazi katika mikoa yote. Natoa mfano tu, mikoa yote ina Askari tofauti. Mkoa wa kwangu mimi wa Mjini Magharibi, takribani sitaji namba, ukienda kwenye randama ipo, lakini ina Askari wengi zaidi ya mara nne au mara tano ukilinganisha na mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, ukiacha tofauti ya mshahara, ukienda kwenye kifungu cha *fuel*, ukienda kwenye kifungu cha *utilities, military services, travel in country, communication and information*, ukiangalia vifungu hivi vyote vimepewa idadi sawa. *Amount ya fedha sawa. Hivi kweli hii bajeti ni realistic?*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mjini tumewazidi watu mara nne. Watu wanaoishi pale Mkoa wa Mjini ni wengi, Mkoa wa Mjini Magharibi ni sehemu kubwa, kuna *population* kubwa, matukio ni mengi. Kwa nini katika kulihudumia Jeshi la Polisi tupewe sawa na Mkoa ambao uko chini mara nne?

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu pale tunapokaa wakati mwingine Askari hutumia pesa zao kupiga simu kwa ajili ya kazi, kwa ajili ya kujaza gari mafuta na kufuatilia matukio mengine. Kwa hiyo, aje anipe ufanuzi, kwa nini viko hivi? *Is it realistic?*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana. *(Makof)*

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makof)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwamtumu Dau Haji, dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Haonga.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya. Pia namshukuru kuwa

na uhai na uzima wa kusimama kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa jitihada kubwa wanazozichukua kufanya kazi zao hizi za Wizara ya Mambo ya Ndani. Naendelea kuzungumzia suala la amani na utulivu na usalama. Wenzangu wengi waliosimama wamezungumzia suala hili lakini kila mmoja kazungumzia kwa mtazamo wake.

Mheshimiwa Spika, mtazamo wangu ninaouzungumzia ni kwamba usalama, amani, utulivu umeimarika, Jeshi la Polisi wanafanya kazi kubwa sana kuhusu suala hili la amani na utulivu. Hivi sasa hatuna wasiwasi wa kwamba nina safari yangu hivi sasa saa tatu nitoke nirande, basi huko njiani labda nitakutana na jambo gani. Unitembea kifua mbele, unakwenda kutoka hapa Dodoma mpaka Dar es Salaam bila ya wasiwasi na tunafika salama salimini Dar es Salaam na magari yanakwenda bila kuzuiliwa. Kwa hili, nalipongeza Jeshi la Polisi liendelee kufanya kazi hii kubwa sana wanayoifanya ili tupate amani na utulivu na tujitanue katika Tanzania yetu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nazungumzia suala la ujenzi wa makazi na Vituo vya Polisi. Kwa kweli Serikali imechukua jitihada; na sasa hivi nilivyoipitia hotuba hii, inazungumzia kwamba kila mkoa utajengwa nyumba ishirini ishirini.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sisi Mkoa wetu wa Kusini kuna nyumba pale Paje na kuna baadhi ya nyumba zile nne pale tayari zilishakuwa zinakalika na nyingine bado kidogo kupauliwa. Nasema hivi, nyumba zile ziendelee kuboreshwa ili Polisi wapate kukaa vizuri waweze kufanya kazi zao vizuri na hasa ukizingatia ukanda ule ni wa watalii. Hili nalizungumza kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado vituo havijakarabatiwa. Kwa Mkoa wetu wa Kusini kuna vituo baadhi tu; kuna Kituo cha Dunga tayari kiko kinajengwa, kuna Kituo cha Chwaka tayari

kinafanya kazi; lakini kuna baadhi ya vituo bado havifanyi kazi vizuri, havijakarabatiwa ukaridhika Polisi wako katika mazingira mazuri juu ya vituo vle. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Makunduchi wameweka *foundation* toka 2015, *foundation* ile mpaka leo bado haijapata msaada wowote. Serikali haijaweza kuinyanya ili kile kituo kiendelee kiwe cha kisasa. Bado Serikali, juu ya jitihada zake inazozichukua lakini bado haijafikia malengo hasa tunayoyataka.

Mheshimiwa Spika, nasema Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake waifanye hii kazi hasa kwa Mkoa wangu wa Kusini na huu mkoa ni mkubwa sana, maana mkoa huu ni mkoa wa watalii. Watalii wote wanapokuja Kusini Unguja, basi lazima wafike Chwaka, Paje, Makunduchi, Jambiani, kote huko kuna vikazi vyao vyaa kupita wakienda wakafanya utalii wao.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mafao ya polisi na mahitaji yao ambayo polisi wanapokuwa tayari wameshapandishwa vyeo, basi polisi anapandishwa cheo na anakaa muda mrefu bado hajapata stahiki yake inayotakiwa. Hili nimeshalizungumzia mpaka katika swali langu la msingi, nikazungumza kwamba mafao ya polisi ni bado, polisi wanalamika mafao bado hawajayapata. Mheshimiwa Waziri ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, Mheshimiwa Waziri anapokuja hapo aje atuambie kuhusu habari ya mafao ya polisi, maana alisema mpaka mwezi wa Tano itakuwa tayari hapa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri angalia mambo ya Paje huko. Mheshimiwa Pascal Haonga, dakika tano.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nami niweze kuchangia kwenye hii Wizara ya Mambo ya Ndani. Nimesikiliza karibu wazungumzaji wote, Wabunge wote wa pande zote mbili kwa maana ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ambao ndiyo wengi, lakini pia na Wabunge wa CHADEMA na *CUF* na wengine waliochangia wanazungumzia sana suala la maslahi kwa maaskari wetu kwa maana ya Polisi, Zima Moto, Magereza na Uhamiaji, wamezungumza vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wabunge wote kwa jinsi walivyowapigania maaskari wetu kwa maana ya kutaka kuongeza mishahara. Siyo jambo baya, lakini nakuwa na hofu kidogo na hofu yangu hii labda naomba inawezekana ikaondolewa na Bunge hili kupitia kitie chako kwa sababu wakati mwininge haitakiwi tuwapende maaskari kwa maneno tu, kwa kuzungumza tu, leo ndiyo siku tunayojadili bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, na leo hapa inaonekana fedha zinazoombwa ni bilioni 921.2.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, pamoja na mambo mengine Wabunge kazi kubwa inatakiwa pia tujadili namna ya kuongeza mishahara ya maaskari wetu. Nashauri, kama kweli tunayozungumza kwamba tunawapenda maaskari na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi ndiyo wengi zaidi na ndiyo wanaweza wakapitisha akidi, hebu tufanye maamuzi hapa leo hii kwamba maaskari wetu waongezwe mishahara leo na mishahara hiyo angalau ianzie shilingi milioni mbili kwa askari mmoja na kuendelea kima cha chini na baada ya hapo kila askari apewe angalau gari nzuri ya kutembelea, kila askari apewe nyumba bora na baada ya hapo mambo yaweze kwenda vizuri kwa Jeshi la Polisi. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Siyo kwa maneno.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, tusiende kwa maneno.

SPIKA: Mheshimiwa Haonga, kama kweli husemi uongo kwa nini hukuleta hoja mahsus kwa ajili hiyo. Unajua kabisa kwamba hayo unayoyasema Kanuni hatuwezi kuyafanya kazi, unajua kabisa. Kwa hiyo kwa nini hukuleta hoja mahsus ukajenga hoja kwa ajili ya jambo hilo.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, mimi najua, wewe ni mzoefu sana na Bunge hili unaweza ukatuongoza vizuri, kwa sababu jambo lenyewe lina maslahi mapana ya maaskari wetu tukalijadili hapa, kwa sababu CCM ni wengi tuongeze maaskari wetu mishahara milioni mbili mbili wapate magari, wapate fedha kwa sababu wao ni wengi zaidi. Kwa hiyo naomba... (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa *cheap politics* haikusaidii, lazima ufuate Kanuni za Bunge. Haya nipe Kanuni ya kuweza kufanya hilo unalolisema maana yake unawadanganya askari nchi nzima kwamba Bunge hili linaweza hilo unalolisema, *instantly* nipe kuhusu utaratibu sasa. Nifungulie ni mahali gani!

MBUNGE FULANI: Ipo, kuna *page* inayozungumzia mishahara.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, *with due respect*, naomba niseme kwamba, tunapokuwa tunaijadili bajeti, bajeti hii hapa tunaweza tunakafanya...

SPIKA: Nimekwambia nipe Kanuni gani.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Tunaweza tukafumua bajeti, tukaifumua *then* baada ya hapo tukajadili kuboresha maslahi ya maaskari wetu.

SPIKA: Mheshimiwa Haonga kaa chini! Kaa chini, unachofanya ni uchochezi tu. Taratibu za Kibunge zinahamika, kama kweli una nia hiyo ungeleta katika utaratibu wa kawaida. Tunazungumza habari ya jeshi hapa,

unachochaea wanajeshi, ileté katika utaratibu wa kawaida, kama kweli wewe ni Mbunge *serious* ili lifanyiwe kazi. Pita kwenye Kamati ya Bajeti kule na kadhalika, maana yake mnavyosema namna hii mnawafanya watu waamini kwamba Wabunge hawa hawawatakii mema askari, hivi na hivi, kitu ambacho si kweli hata kidogo.

Mheshimiwa Fatma Toufiq dakika tano.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hii hoja iliyopo mbele yetu. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Mambo Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi Lugola pamoja na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba hii ambayo wameiandaa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naomba niwapongeze Askari Polisi wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuitetea na kuilinda nchi yetu. Hali kadhalika nawapongeza Majeshi ya Magereza, Idara ya Uhamiaji, *NIDA* na Jeshi la Zimamoto tunaelewa wanafanya kazi yao nzuri pamoja na ufinyu wa bajeti iliyopo, pongezi zao sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kujitahidi kuboresha ustawi wa Jeshi la Polisi kwa kuona umuhimu kwanza wa kuboresha ukarabati wa Chuo cha Taaluma cha Polisi, Dar es Saalam, lakini pia na ujenzi wa nyumba za Jeshi la Polisi pamoja na Askari Magereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kuhusu suala la usalama barabarani nikirejea ukurasa wa tisa hadi wa 10 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Imebainisha kwamba sasa hivi ajali zimepungua kwa asilimia 38, napongeza hatua hiyo. Sambamba na hilo, naomba nichukue fursa hii kuiomba Serikali yangu Tukufu kuona umuhimu sasa wa kuipitia Sheria ya Usalama Barabarani kwani bado ina upungufu mwingi na upungufu huu iwapo kama utaondolewa ina maana

kwamba tutawalinda wananchi wetu waweze kuepukana na vifo pamoja na ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, naungana na maoni ya Kamati yangu, na-*declare interest* mimi ni mjumbe wa Kamati hii, kwamba kuiomba Serikali iharakishe marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168 kwani hatuoni sababu kwa nini inachelewa. Kwa sababu tukirekebisha sheria hii kuna baadhi ya mambo ambayo yanaweza yakaleta tija kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia nataka kujua, kwa nini Serikali imechelewesha kuleta marekebisho ya sheria hii, kwa sababu sasa hivi kumekuwa kuna matumizi ya teknolojia na baadhi ya madereva wetu wamekuwa hawafuati Sheria za Usalama Barabarani kwa sababu wanaendesha vile vyombo vyao moto huku wakitumia simu. Kwa hiyo wanapokuwa wakitumia simu hizi ina maana kwamba umakini wao katika kuendesha vyombo hivi unakuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo kama ikipatikana Sheria ina maana kwamba itawabana hawa madereva ambao ni wazembe na itasaidi kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika kurekebisha sheria hii, naamini kabisa hili suala la kiwango cha kilevi ambalo liko katika sSheria ya nchi yetu kwamba madereva wanaruhusiwa kuwa na asilimia 0.08 ya kiwango cha kilevi. Je, kwa nini Serikali isione umuhimu sasa wa kubadilisha kiwango hiki ili kiwe asilimia 0.05 ambacho kinaendana na kiwango cha kimataifa chini ya *World Health Organization*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 17 wa hotuba hii, Waziri amezungumzia kuhusu kuongeza rasilimali watu na fedha na kubainisha kwamba, kuna baadhi ya maaskari wamehitimu mafunzo. Ningependa kujua, Je, katika mafunzo haya kuna jicho la kijinsia? Ni wanawake wangapi ambao wamepata fursa ya kwenda katika mafunzo haya na kupandishwa vyeo katika maeneo mbalimbali. Kwa sababu naamini kabisa sote tunafahamu kwamba nchi yetu imeridhia

matamko mbalimbali ya kuhakikisha kwamba usawa wa kijinsia unakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa kuna malalamiko ya baadhi ya Maafisa au Polisi (askari) wa kike ambapo wakipangija mafunzo na ikitokea bahati nzuri wakawa wajawazito...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Muda hauko upande wako Mheshimiwa Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Toufiq. Mheshimiwa Hussein Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Migila. Mheshimiwa Hussein Bashe, tafadhali.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Jambo la kwanza nitumie nafasi hii kwanza kwa dhati kabisa kulipongeza Jeshi la Polisi na nawapongeza tukiwa *honest* sasa hivi katika Taifa letu wamefanya kazi kubwa sana ya kudhibiti uhalifu na ujambazi mkubwa hasa katika maeneo ambayo yalikuwa yanaathirika ya pembezoni mwa nchi na ambayo yamezungukwa na nchi ambazo zina *instability*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi wamefanya kazi kubwa sana ya kudhibiti na kuleta utulivu na amani hasa sisi tunaotoka Mikoa ya Kanda ya Magharibi, zamani ilikuwa ukifikiria kusafiri kukatiza kutoka Dodoma hapa ukaseme ukalale Bukoba, ilikuwa ni mtihani. Kwa hiyo wamefanya kazi kubwa sana tunawashukuru na Mwenyezi Mungu awajalie kwa kazi hii wanayofanya. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Amina.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, nataka niongee mambo machache kuhusiana na polisi. Polisi wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu, ni muhimu sana ndani ya Serikali kuangalia ni namna gani stahiki za polisi na majeshi mengine zinakuwa *harmonized*, kwa sababu suala la usalama linaanza na *intelligence* kwa maana ya kukusanya taarifa, lakini suala la kuzuia, suala la *ku-enforce*, hizi ni kazi ambazo zinashabihiana. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuangalia ni namna gani stahiki za askari wa Jeshi la Polisi zinakuwa *harmonized* na majeshi mengine ili kuleta uwiano ulio sawa kwa sababu majukumu yao yanategemeana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo askari wetu wanafanya kazi *over time*, hawapati kulipwa *over time*, wanafanya kazi masaa 12, akiingia kwenye lindo ni masaa 12 na hii ni kutokana na uchache wa askari katika maeneo yao. Kwa hiyo ni muhimu sana Serikali iangalie. Nataka niishauri Serikali, watafakari, mfano, sasa hivi huwa tunasikia kwenye TV kwamba kutokana na makosa ya barabarani askari wamekusanya bilioni 700, hivi *is it not possiblendani* ya Serikali wakatengeneza utaratibu katika kila kituo angalau *twenty percent* ya hizi fedha wanazokusanya zibaki kituoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano, pale Nzega kwangu leo ni mwaka wa tatu askari wamekatiwa maji, Jeshi la Polisi. Pale Nzega kwetu *LUKU* wanaweka kutoka mfukoni kwao na *it's an average* ya shilingi laki moja kwa mwezi wanayotumia. Kwa hiyo wananchi wanachanga changa na wenyewe saa nyingine wanatoa fedha zao mfukoni, Mkuu wa Kituo hawezi kukubali usiku pasiwe na taa katika kituo chake cha polisi na ni kwa sababu ya ukata.

Mheshimiwa Spika, pale Nzega tuna *household* za askari familia 17, leo sisi katika halmashauri tumeamua kuanza kutafuta fedha ili tuanze kujenga makazi ya askari, tunaiomba Serikali iangalie, ni vizuri sana kuangalia hawa watu kazi wanayoifanya ilivyo ngumu iweze kwenda na stahiki zao. Tunaweza tukaja hapa ndani tukawalaumu kuwa wanachukua rushwa, je, tumeangalia, nimemsikia Haonga

rafiki yangu amesema tuwape *two million*, nadhani tusingeanzia kwenye *two million*, tunganeanzia namna gani tunatengeneza uchumi imara ambao utakuwa na mapato imara ili tuwalipe vizuri askari wetu. Hili ndiyo jambo la msingi kabisa, lazima tuanze na kutazama haya mambo *in a broader perspective*, itatusaidia kama nchi kwenda mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niongelee, ni vizuri Serikali ikaangalia *custodian* wa *border control* ni *migration*. Je, *equipments* tunazowapa watu wa Uhamiaji, kwa sababu ndiyo mwenye jukumu la kuangalia mipaka, wanaoingia na kutoka, ni vizuri hili Jeshi la Uhamiaji likawa *a unit* inayojitegemea, inayojiendesha, iwe na *resources* zake, iwe na *proper plan* tujue ndani ya miaka mitano *border control* zetu zitaendeshwa namna gani. Hii ni muhimu sana ili kuweza kuingiza *efficiency* katika kazi wanazofanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee jambo lingine mahsus. Kwa miaka mitatu ambayo nimekuwa humu ndani ya Bunge na kabla sijaja Bungeni, kumekuwa na mjadala mkubwa sana juu ya suala la Masheikh waliowekwa magereza. Leo ni mwaka karibu wa sita, nataka niiombe Serikali kwa heshima kabisa na mwaka jana walitoa ahadi hapa, hawa watu kama wana makosa wapelekeni mahakamani dunia ijue kwamba hawa watu wana tuhuma moja, mbili, tatu kuliko kuendelea kuwa-*hold* ndani *with no clarity*, inaleta maswali mengi, ina *distort image*, inasababisha watu wengine kupata hoja ya kujadili jambo ambalo halina sababu. Nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya *wind up*, hebu tuelezeni *faits na direction* ya suala la Masheikh walioko magereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nataka niiombe Jeshi la Polisi na Mheshimiwa Rais alisema hili, alisema Watanzania siyo wajinga, Watanzania wanaona, nami nitaongea kuhusu hili ninalolisema na lingine linaloitwa la *task force*. Kuna mambo yanasemwa halafu *response* inayopatikana kutoka kwenye *authority is just a political response*, kuna mambo

ambayo yanatajwa ya ki-*criminal*/yanatakiwa yapate majibu *complete*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano, imesemwa sana hapa na Mheshimiwa Bwege amewahi kuisema mara nyingi, nataka nimwombe Mheshimiwa Kangi hebu wamwambie Mheshimiwa Bwege awasaidie. Kuna hoja inayosemwa sana sana na inaenda kwa umma, inayozungumzia Masheikh wa Tablíj waliopigwa risasi inayosemwa huko Kilwa sijui, *this things need answers*. Kama ni taarifa za uongo, wanaotengeneza taarifa hizi za uongo wachukuliwe hatua, *we should not allow mambo ya uongo yanasemwaa semwa, yanaachwa, halafu siku ya mwisho yana-distort heshima na image ya Taifa hili*. *This country* imejengwa katika misingi imara ya utu, hili ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nataka niseme kuhusu *minority society*, nataka niiombe Serikali, pale Uhamiaji waanzishe dawati maalum linalohudumia wahamiaji katika nchi hii. *Community ambazo ni minority*, Idara ya Uhamiaji zimegeuka ni mradi, halafu jambo la kushangaza anakwenda mtu akionekana Msomali anaambiwa wewe siyo raia, leta cheti cha bibi na bibi yako watano, anatoa wapi? Kwa sababu hata huyo Afisa ye ye ukimuliza cheti cha bibi yake wa nne hana, basi fanyeni *audit*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Nzega kuna familia tano za Wasomali zinajulikana ambao familia ile hawako watu hata arobaini. Suala la uhamiaji jamani siyo dhambi, *today* Rais wa Taifa kama Ireland ni Mhindi, kwa hiyo Uhamiaji na *migration* nataka niwaambie, hivi mnajua neno sukuma! Hawa Wasukuma ni wahamiaji kwenye nchi hii, ni *Northerner*. Neno sukuma, kisukuma maana yake ni Kaskazini. (*Makofi/ Kicheko*)

SPIKA: Ilikuwa ni Mheshimiwa Ndassa au nani alisimama! (*Kicheko*)

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Yupo. (*Kicheko*)

SPIKA: Au Mheshimiwa Chegeni!

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Wote.

SPIKA: Nilisikia kama taarifa hivi, Mheshimiwa Bashe endelea. (*Kicheko*)

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Spika, ninachotaka niseme ni hivi, dunia leo *you cannot restrict migration*, tengeneza *proper administrative measures* zitakazokusaidia wewe *migrants* kukusaidia kwenye nchi, *because the world is village*, hili ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niongelee, Mheshimiwa Kangi nitampa majina. Sasa hivi kuna watu wanahama nchi yetu *especially business community* na wanassumbuliwa na watu wanaoitwa *task force*. Kinachotokea na nitampa Mheshimiwa Kangi majina hapa, *transporters* walioko Wilaya ya Temeke ambao wana asili ya Kisomali na ni Watanzania, mfano mtu anaitwa Abdigul Abdi Kulane ambaye ana kampuni inaitwa *Kulane and Sons Company Limited* alifuatwa nyumbani kwake Kinondoni akachukuliwa, leo ni miezi miwili hajulikani alipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mtu anaitwa Abushir Ally, huyu mtu kachukuliwa, leo hayupo, walichukuliwa wane, wenzao wawili wameachiwa baada ya kutoa fedha na wao walichokifanya, angalia hiki kitu, wametoka wamehamisha *Transport Company* yao wamehamia Zambia.

Mheshimiwa Spika, kuna mtu anaitwa Abushir Ally, huyu mtu kachukuliwa leo hayupo. Walichukuliwa wanne, wenzao wawili wameachiwa baada ya kutoa fedha na wao walichokifanya, angalia hiki kitu, wametoka wamehamisha *Transport Company* yao kwenda Zambia. *This is happening.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hawa wakubwa kwa hizi *task force* wanachokifanya sasa hivi, wengi wanahamisha biashara. Nakuomba Mheshimiwa Waziri,

tazameni hizi *task force* zinavyoundwa na bahati mbaya Kituo cha Polisi mtu akienda anaambiwa huyo wala usihangaike yuko chini ya *task force*, wala sisi hatuna *control/naye*. Sasa hizi *task force* ambazo hazina *controls* zitaathiri *image* ya nchi yetu, kazi kubwa inayofanywa *image* yake itakuwa *distorted*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Kangi, angalieni hizi *task force* zinazoundwa, lazima ziwe zina *TOR*, majibu. Watu wasipokuwa na majibu juu ya *family members* wao, inaleta shida na ukakasi mkubwa sana katika *community*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka ni-*conclude* kwa kuiomba Wizara ya Mambo ya Ndani, mnafanya kazi kubwa sana ya kulinda usalama wa raia. Niwaombe, moja, angalieni maslahi ya askari kuya-*harmonize* na majeshi mengine, ni muhimu sana ili kuwajengea *confidence* askari wetu.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba Idara ya *Migration* waache kugeuza *minority society* mradi. Tengenezeni Dawati Maalum litakalohudumia na ikiwezekana familia zilizoko hapa nchini ambazo ni *migrants*, *minority* zinaweza kujulikana, *it's easy* kuwa na *database* ambayo itaondoa hii shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mdogo wangu mimi kaenda siku ya kwanza kapata shida, siku ya pili mmoja kaangalia jina la mwisho alivyoona Bashe akasema wewe ni mdogo wake na Mbunge. Sasa yule ana *privilege* ya mdogo wake na Mbunge, wangapi hawana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka niiombe Serikali, ni vizuri sana haki za raia zilindwe na mwenye wajibu wa kutoa majibu juu ya masuala yenye ukakasi ni Wizara ya Mambo ya Ndani, toeni majibu juu ya haya mambo yanayosemwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge. Nilikwisha kukutaja Mheshimiwa Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na uzima mpaka leo nipo humu ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpe pongezi sana Mheshimiwa Kangi na Naibu wake, kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Mkoani kwangu Tabora yalitokea matatizo ya watoto kukamatwa, nilishirikiana na Mheshimiwa Kangi kuhakikisha hali hiyo inakuwa shwari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, napenda nimwambie Mheshimiwa Kangi wanafanya kazi nzuri lakini bado wanahitaji maboresho katika maeneo yafuatayo. Nitaanza na usalama barabarani, hawa watu wanafanya kazi nzuri sana, tumeona ajali za barabarani zimepungua na watu wanaendesha magari yao vizuri sana lakini eneo hili kuna shida mpaka baadhi ya Askari wa Usalama wa Barabarani wamebadilishwa majina badala ya kuitwa *traffic* wanaitwa *MaxMalipo* au *TRA* ndogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, dhana nzima ya kulinda usalama wa barabarani wa watembea kwa miguu na wa magari haipo tena badala yake wamefanya kama kile ni kitengo cha kukusanya kodi. Mtu anakamatwa badala ya kuambiwa kosa lake kwanza anaulizwa leseni. Baada ya hapo wanamwambia njoo nyuma huku. Sasa unampeleka kule nyuma kufanya nini?

MBUNGE FULANI: Nyuma wapi?

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Namaanisha nyuma ya gari. Akirudi tayari lile kosa limekwisha anaendelea na safari.

SPIKA: Mheshimiwa Rehema, nakukumbusha lugha za Kibunge. (*Kicheko*)

Endelea kuchangia Mheshimiwa Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi napenda niishauri Serikali, tunaomba dhana nzima ya hawa Askari wa Usalama Barabarani iwe ni kuelimisha hawa watumiaji wa magari na watembea kwa miguu na isiwe ni kitengo cha kukusanya kodi. Leo hawatoi elimu wanakaa kufanya kazi ya kukusanya kodi. Mheshimiwa Kangi, tunataka utuambie hivi Kitengo cha Usalama Barabani na chenyewe ni *source* ya mapato ya Serikali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikisalia hapo hapo kuna hawa watu wanaitwa *PT*, kiukweli hawa mfano kwa kule kwetu Tabora imekuwa ni shida. Badala ya kutembea mipakani mwa mji sasa wanasumbua bodaboda kila kukicha yaani bodaboda hawafanyi kazi kwa amani. Tukumbuke kwamba hawa watu wamejiajiri wenye na wengine pikipiki sio zao, aweze kupata hela ya tajiri na ya kuhudumia familia yake lakini hawa *PT* kila bodaboda akijipindua wako naye na wanataka chao na hiyo haina risiti wala nini, wanaweka mifukoni mwao. Mheshimiwa Kangi tunaomba hawa watu wa *PT* uwaangalie kwa jicho lingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la upoteaji wa vithibitisho pindi vinapofika Polisi. Nasema hili nikiwa na uhakika, mimi namiliki bodaboda. Kuna siku bodaboda yangu imekamatwa ilivyofika Polisi, kesho yake nakwenda kuchukua pikipiki yangu haina mafuta wala betri. Sasa tunaamini kabisa kwenye Kituo cha Polisi ni mahali salama na wana kazi ya kulinda usalama wa raia na mali zao. Kwa hiyo, nataka utuambie Mheshimiwa Kangi...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ajenda hiyo naomba uiache kwanza ni *conflict of interest* lakini pilli biashara nyingine tuwaachie wananchi jamani, Mbunge unafanya biashara ya bodaboda inakuwaje? (*Kicheko*)

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, ndiyo ni katika kuongeza uchumi.

SPIKA: Endelea na ajenda nyingine Mheshimiwa Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Suala lingine nataka tuambiwe maana ya *VTS* (*Vehicle Tracking System*). Tunajua Jeshi la Polisi linafanya kazi na Idara nyingine kama *SUMATRA* na tumeona magari ya mizigo na mabasi yamefungiwa hivi ving'amuji lakini mimi sijajua lengo halisi la kufunga hivi vidubwasha ni lipi? Kwa sababu nimepanda kwenye basi yaani dereva akiongeza spidi kinachofanyika pale ni ule mliontu unasiakia chwi, chwi, chwi lakini hakuna kusema kama ni kile kifaa kinapunguza ule mwendo wa gari. Kama lengo ni kusikiliza tu ule mliontua haja ya kuwawekea hao wenye magari hivi vitu.

Mheshimiwa Spika, tunataka tujue, hii sauti inavyolia mule kwenye basi hatua gani zinachukuliwa dhidi yake kama hatapunguza mwendo? Atakapoamua kuongeza mwendo kwa sababu kuna magari siku hizi yana *TV* na *music* dereva akaamua tu kuchapa mwendo kwa sababu abiria hawatasikia ile sauti matokeo yake atasababisha ajali na huyu mtu bado akienda kule mbele kwa sababu ameenda spidi kubwa atakutana na tochi, je, atakuwa *charged* mara mbili au vipi? Maana tunaambiwa ikilia ile sauti kwa bosi na *SUMATRA* inasoma, je, huyu mtu atakuwa anachajiwa mara mbili?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ucheleweshwaji wa upelelezi wa makosa mbalimbali. Haki ya mtuhumiwa ni kupelekwa Mahakamani. Tunajua kabisa muda wa kumpeleka Mahakamani mtuhumiwa ni saa 48 au 24 lakini kuna watu leo wako mahabusu takriban miaka sita hawapelekwi Mahakamani na hata wakipelekwa Mahakamani wanaambiwa hii Mahakama haina uwezo wa kusikiliza kesi yao. Kwa nini waendelee kukaa mahabusu ilhali Mahakama ambayo itashughulia kesi zao haipo? Wanaongeza msongamano na gharama kubwa ya kuhudumia mahabusu wengine. Tunaomba tuambiwe, je, hawa watu wanaokaa mahabusu muda mrefu mfano hawa Mashekhe wa Uamsho, kuna watu walikamatwa kule Arusha

mpaka leo takriban miaka sita hawajasomewa hukumu yao, ni lini upelelezi wao utakamilika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni utumikaji wa Polisi kama sehemu ya wasimamizi wa uchaguzi. Inahuzunisha sana Polisi kutumika kama wasimamizi wa uchaguzi ilhalii wao kazi yao ni kusimamia usalama wa raia na mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumefanya chaguzi za marudio sehemu mbalimbali lakini unakuta Polisi anakwenda mpaka chumba cha kuhesabia kura, Polisi huyu naye anakuwa ni msimamizi. Kweli leo Polisi wanaacha kutekeleza majukumu yao wanayopaswa kufanya wamekuwa wasimamizi wa uchaguzi. Tunaomba hawa Polisi wasitumike, wafanye kazi wanazopaswa kufanya na kama wanafanya hivyo, basi wafanye kwa pande zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu maslahi ya Polisi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Tayari dakika zako. Nakushukuru sana Mheshimiwa Rehema Migilla, msemaji kweli, kumbe Mnyamwezi huyu, doooh! Taabu kweli, wamejaa kweli humu. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa namna ya pekee, naomba nilipongeze Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri wanayoifanya na ma-RPC wakiwakilishwa na Bwana Mroto – RPC wa Dodona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanawalaumu Polisi wakati sisi usiku tumelala na wake zetu tunapata joto wenyewe wamekumbatia bunduki wanapata ubaridi kwa ajili ya kuhakikisha sisi tunalala salama mpaka asubuhi. Inasikitisha kuona sisi Wabunge kama wawakilishi tukitumia Bunge kama

jukwaa kwa ajili ya kuwapiga na kupambana na Jeshi la Polisi, hiyo haipendezi kabisa.

Mheshimiwa Spika, watu wanashindwa kutofautisha kati ya Polisi na Afisa Maendeleo ya Jamii. Polisi siyo Afisa Maendeleo ya Jamii ndiyo maana imeitwa *Police Force*, sawa? *IGP* Siro kama upo humu ndani wewe siyo Kamishna wa Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo, asikuchezee mtu, umepewa nguvu kwa mujibu wa Katiba, kwa hiyo komaa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanalalamika kuhusu shughuli za kisasa, hao wanaolalamika ni wale waliovamia treni kwa mbele. Kwa wanasiasa sisi wenyewe wakongwe wa siasa ambao tunajua allichofanya Nyalandu kutoka CCM kwenda CHADEMA ile ni siasa siyo mpaka ufanye mikutano wa hadhara, allichofanya Maalim Seif kutoka *CUF* kwenda *ACT* ile ni siasa kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata anachofanya Lipumba kuondoa wasaliti ndani ya *CUF* ile ni siasa tosha siyo mpaka mikutano ya hadhara. Wanachofanya akina Zitto Kabwe, wale wanaoongea na waandishi wa habari, ile ni siasa kubwa sana katika nchi siyo mpaka mfanye mikutano ya hadhara, hizo ni siasa za zamani na zinaharibu maendeleo ya nchi. Kwa hiyo, naomba Jeshi la Polisi likomae.

Mheshimiwa Spika, pia mnaozuiliwa siyo ninyi tu, kwa mfano mimi Ulanga niligundua ujisadi wa shilingi bilioni 2.9, wananchi wangu waliandaa mikutano mkubwa na mapokezi ya kunipokea mimi. Polisi waliniambia Mheshimiwa Mlinga utakapofanya hilo, kuna wahalifu wako ndani ambao wanaumia na ule ujisadi ulioungundua kwa hiyo usifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo wao tu, siyo kila kitu lazima tuseme na siyo kila barua unayopewa na Polisi lazima uweke katika vyombo vya habari, hiyo haiwezekani. Kwa hiyo, Polisi wanawazuia siyo ninyi tu hata sisi sehemu yoyote, sasa mkiachiwa mkadburika mtasema Polisi hawafanyi kazi. Kwa mfano, Mheshimiwa Tundu Lissu alipopigwa risasi

angepewa tahadhari tangu mwanzo mnge sema kaonewa. Kwa hiyo, muwe mnawasikiliza, hawa wanafanya kazi kwa taaluma, wameenda wamesomea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote, kuna matatizo katika Jeshi la Polisi la nyumba za askari. Sisi Morogoro pale tumeanza mkoani tunajenga nyumba kwa ajili ya maaskari wetu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *uniform* kwa Polisi. Juzi wakati tunaangalia Ripoti ya CAG shilingi bilioni 16 za *uniform* za polisi ni hewa, wanasema nyaraka hazionekani lakini hata nilipopita karibu na IGP nikagundua hata ile *uniform* yake bado ni ya zamani. Kwa hiyo, najua kabisa hii bilioni 16 hakuna *uniform* hata moja iliyounuliwa na Polisi hawawezi kusema wao wenyewe kwa sababu mfumo wao wa chini hawezi kumhoji wa juu. Kwa hiyo, *uniform* Polisi mpaka wanaokwenda kucheza gwaride tena katika sherehe kama za Uhuru yaani mtu baada ya miaka mitano ndiyo anapata *uniform*, kwa hiyo, bado hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Spika, suala la vitendea kazi, siku moja nilishuhudia askari anaenda kuchukua maiti hawana hata ile mifuko ya kuwekea maiti kwa hiyo hawana vitendea kazi. Kwa mfano, camera, posho, mtu anapewa kazi akachunguze kesi ya mauaji hapewi hata shilingi 10, unategemea nini kitakachotokea? Yule anayetuhumiwa si anamhonga hela kiasi tu anaachana nayo?

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa Jeshi la Polisi bado yanatolewa kwa upendeleo yaani mtu mpaka awe anamjua mtu wa juu ndiyo anapewa nafasi kwa upendeleo. Hilo hamuwatendei haki polisi wetu.

Mheshimiwa Spika, bado kuna mapungufu mengine kwa mfano, Dar es Salaam, eti unakuta katikati ya Mji Dar es Salaam kuna tochi yaani askari anakaa anapiga tochi katikati ya Da es Salaam. Kwa mfano, maeneo ya Tegeta, Mbezi, Oysterbay kuna tochi, hivi tochi Dar es Salaam inafanya kazi gani? Tunajua Sheria za Usalama Barabarani hazihitaji gari

moja kukaa mbele ya lingine mita tatu, sasa Dar es Salaam hiyo mita tatu unaitolea wapi, Askari anakukamata. Eti Dar es Salaam umekanyaga Zebra askari anakukamata. Kwa hiyo, hapa naomba muwe mnaangalia hizi sheria zenu ziwe zinaendana na mazingira.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ulevi, sizungumzii askari wote. Ulevi unaruhuswa lakini mahali pa kazi hauruhusiwi. Siku moja nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri nampa taarifa na yeye akanipa kesi yake siku moja na yeye alilindwa na askari ambaye ameleta, nikamwambia wasiwe wanapewa silaha, wawe wanachunguzwa kwanza kama wameleta au la.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *counseling*, askari kabla hawajapewa silaha wawe wanafanyiwa *counseling* kwa sababu hujui mtu ametoka katika mazingira gani huko alipotoka. Ndiyo maana ukichunguza wako maaskari wanaua wenzao maeneo ya kazi, wako maaskari akipewa silaha baada ya saa mbili anajipiga risasi. Kwa hiyo, muwe mnawafanyia *counseling* mgundue wana shida gani kwa sababu hata mishahara yenye ni midogo.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine tena nilipewa na askari. Kuna maaskari mwaka 2013 walilipa fedha kwa ajili ya kupatiwa viwanja Chalinze Mzee na kampuni moja inaitwa *Ardhi Plan International*, askari zaidi ya 1,000 na wamelipa hiyo hela ikiwa ni pamoja na hati lakini hakuna hata askari mmoja aliyepewa hati. Naambiwa hizo pesa zimepigwa na viongozi wa Polisi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri unapo-*wind up* tafadhalii nahitaji majibu, hawa askari wanapata lini hati zao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la Uhamiaji, ameongea Mheshimiwa mwenzangu Bashe. Uhamiaji ndiyo jeshi ambalo linafanya vibaya kwa sasa hivi. Uhamiaji mmegeuza watu kuwa mitaji yenu. Mtu akigundua kijana anatembea na mke wake anaenda kuongea na watu wa Uhamiaji wanampa nchi nydingine.

Mheshimiwa Spika, leo hii wanakukamata wanakwambia wewe siyo raia wa Tanzania na ni wengi. Kuna kesi moja nilipeleka mimi kwa Mheshimiwa Waziri na hata Kamishna wa Uhamiaji nimemwaambia, kwa hiyo, Uhamiaji imegeuzwa silaha kwa ajili ya kuwapigia watu. Kama alivyoongea Mheshimiwa Bashe, tukianza kuchokonoana kutafutana uraia tutakaobaki raia halali wa nchi hii ni Wapogoro na Wazaramo peke yetu, wengine wote ni wahamiaji. (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Aaaa.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Ndiyo! Kwa sababu Wangoni tunajua mmetoa Afrika Kusini, Wachaga ninyi ni Wasomali, kwa hiyo, tutakaobaki ni sisi peke yetu. (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Mlinga, taarifa. Watakaobaki ni Wagogo peke yake maana ndiyo wa katikati. (*Makof/ Kicheko*)

Endelea Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Uhamiaji imegeuka fimbo kwa wananchi wetu wa Tanzania. Pia Uhamiaji wamewageuza hawa watu wanaoishi sasa hivi, kwa mfano, watu wa Congo wa Dar es Salaam ndiyo mitaji yao. Leo Afisa Uhamiaji akiona mambo yake magumu anamtafuta mtu mmoja wa Congo anampiga blahblah pale anachukua hela, watu wa Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la zimamoto. Tunashukuru kwa kutupa Maaskari wa Zimamoto hata Ulanga tumepata. Hata hivyo, unatuletea Askari wa Zimamoto Ulanga hata koleo la kubebeta mchanga hana, gari hana, anafanyaje kazi? Ina maana moto unapowaka naye anasaidia kuja kutuangalia? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la *NIDA* kuhusu vitambulisho. Leo miaka minne *NIDA* wametengeneza vitambulisho milioni nne. Sasa hata tukiwapa huo mwezi

Novemba bado hawatakuwa na uwezo wa kutengeneza hivyo vitambulisho kwa Watanzania. Watanzania tuko zaidi ya milioni 50, kwa hiyo, muda tulio wapa ni mdogo na kazi yao wanayoifanya ina changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nimalizie na suala la kupata uraia. Kuna shida kubwa, watu wana muda mrefu hawajapata uraia. Mtu ameomba uraia miaka 10/15 iliyopita hajapewa mpaka leo, hili linatengeneza mazingira ya rushwa. Wako hata hapa Wabunge wana wake ambao siyo raia lakini wameshughulika sana na imeshhindikana. Kwa hiyo, hili linachangia kuleta rushwa katika kitengo hicho cha kuwapa watu uraia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Lusinde, dakika 10.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya asubuhi ya leo ili na mimi niweze kuchangia hili Fungu 28 la Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamempongeza sana Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola pamoja na Naibu wake Masauni pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa vyombo vya ulinzi na usalama walioko chini ya Wizara hiyo wanafanya kazi nzuri sana. Mimi niwe shuhuda tu kuthibitisha kwamba Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji ni miongoni mwa vyombo muhimu sana kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunajadili leo, kuna tofauti kubwa sana kati ya mjadala wa leo na mjadala wa jana Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana nami. Jana tulifikia mahali hata kuambiwa kwa nini mnawapa pole Polisi ya kung'atwa na mbu wakati ni kazi yao. Sasa mimi nikawa napata taabu sana, hii ni kazi ya kizalendo, si tu kazi yao kazi wanayoifanya ni ya kizalendo ambayo ina mazingira magumu yanayohitaji kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, aliyesema maneno hayo akasema ninyi wengine hamjawahi kulala hata ndani ninyi, wewe si umelala ndani kwa kujitakia mwenyewe? Kwani ukiwa hutaki kulala ndani utalala ndani jamani! Siyo rahisi, maana Polisi wanashughulika na watu waovunja sheria. Polisi hawashughuliki na kila mtu barabarani hapa, ingekuwa kila mtu basi kakamatwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *nature* ya chombo chenyewe tunachokijadili, kwanza ni chombo chenyeye mafunzo, lakini chombo kina watu wanahenya, kuna watu wanasoma na kuhenya juu.

Mheshimiwa Spika, unajua hapa Wabunge, Bunge lilitopita muliamua wewe na Mheshimiwa Spika Anna Makinda, tukaenda JKT, tulikwenda na mdogo wangu Mheshimiwa Neema hapa, nadhani tulijifunza kidogo utofauti wa hivi vyombo, kwa hiyo, nataka nikupongeze Mheshimiwa Neema kwa ajili ya ukakamavu, kumaliza. Jamani *counter* ya jeshi la polisi haiwezi kufananishwa na *counter* ya hoteli, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *counter* ya polisi lazima umkute mtu ana sura ya jiwe, ametulia, anakusikiliza umasema nini, ya hoteli utamkuta mtu anatabasabu, karibu, chumba kipo, hiyo ni ya hoteli, siyo polisi! (*Makofi/Vicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, polisi lazima wawe wakakamavu, siyo kitu cha mchezo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Tena ndiye ninayemtaka huyo.

SPIKA: Wewe unampa taarifa Lusinde, haya toa taarifa. (*Kicheko*)

TAARIFA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, mzungumzaji anayezungumza, ni vizuri tukaweka rekodi sawa hapa, anayesema hajanitaja lakini najua ananisema kwa hiyo, lazima niweke rekodi sawasawa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, na ni rafiki yangu, hoja niliyozungumza jana kwamba polisi wanatimiza majukumu yao, Serikali huwa inatoa nafasi za kazi, mtu ye yeyote anapokwenda kuomba kazi yoyote huwa wanajua *consequences* zake, anajua polisi wana kazi gani, Askari wana kazi gani.

Mheshimiwa Spika, hata wewe hapo unafanya kazi ya kizalendo, tunategemeana kama Taifa. Tulichokizungumza jana, na nilivyosema jana wengine hamjalala polisi, na nimetoa ushahidi kwamba nimesingiziwa nimelala kwa makosa. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, kufanya kazi ngumu kisiwe kisingizio cha kuvunja sheria, hiyo ndiyo hoja tunayoizungumza, lakini siyo kwamba tunadhalilisha kazi ya polisi.

MWENYEKITI: Mbona unahutubia sasa si taarifa iwe fupi!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, ndiyo hiyo.

SPIKA: Mchungaji ahsante sana, Mheshimiwa Lusinde unapokea taarifa!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, ukipenda kachumbali upende na pilipili. Watu wote, wanaofanya upinzani kwenye maeneo yao, wote wanaingia kwenye matatizo! Mheshimiwa Zitto alijaribu kufanya upinzani ndani ya CHADEMA, kumpinga Mheshimiwa Mbewe, yupo CHADEMA? Amemalizwa, ameondoka, alijaribu Kafulila, yupo salama CHADEMA! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, muelewe kazi mnayoifanya ina hatari yake, ndiyo ninachotaka kukwambia ukweli hapa, yaani huwezi ukajiita upinzani, yuko wapi, Mheshimiwa Komu alijaribu juzi kumteteta Mwenyekiti na mwenzake, wako wapi! Kwa hiyo, ninachotaka kusema, hamuwezi kuwa wapinzani, halafu mkawa salama tu, haiwezekani! (*Makofi/Vicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwasaidie, kwamba kazi wanayoifanya ni kazi inayoweza kuwapa matatizo wakati wowote! (*Makofi/Vicheko*)

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nitulie kaka yangu kasimama amua.

SPIKA: Mheshimiwa Komu, nini tena rafiki yangu! (*Kicheko*)

TAARIFA

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Haya, dakika moja bwana maana yake tunakaribia mwisho.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Lusinde, ambaye tuna historia nzuri sana na yeye kwa sababu tumemkuza sisi na anajua. Sasa nipo, na sijazurika, sijateteleka, nipo, maana yake yeye amesema yuko wapi, nipo hapa. (*Makofi*)

SPIKA: Ila jambo moja tu, hajakanusha kama alimteta Mwenyekiti wake. (*Makofi/Vicheko*)

Mheshimiwa Lusinde, endelea!

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema, kwanza namheshimu sana kaka Komu

na ni mmoja wa watu waaminifu sana na alichokuwa anakisema Komu kwa kweli, naweza nikakiamini kwa upande wangu, kwamba kweli kuna matumizi mabaya ya ruzuku mle ndani. Na ye ye ndiye aliyekuwa mhasibu wa chama, kwa hiyo, hata, alichofanyiwa alisema ameonewa. Nilitaka kumuonyesha Mheshimiwa Msigwa, kwamba wanaoonewa hawako huku tu, hata ndani ya chama chenu mnaonea watu, mmojawapo mmemuonea Mheshimiwa Komu! Mheshimiwa Komu amesema, kuna matumizi mabaya ya ruzuku, amevuliwa nafasi zake zote, ameonywa, yuko kwenye uangalizi hapo alipo. Sasa hii siyo sawa na Mheshimiwa Kubenea, (*Makofi/Vicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jeshi la polisi linafanya kazi nzuri sana. Niombe Waziri wa Mambo ya Ndani, nichukue fursa hii kumpongeza sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, Mroto. (*Makofi/Vigelele*)

Mroto anafanya kazi nzuri, jeshi la polisi ni *beat*, huwezi kucheka na waharifu, kwamba hapa kuna Bunge, Wabunge wanavaa cheni za dhahabu kama unavyowaona wengine humu, halafu Mrotoacheze na maandamano maandamano hapa, Wabunge mtaporwa hiso cheni. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, Mroto anaposema hataki mchezo watu watachakaa, yuko sahihi kwa ajili ya kuwalinda ninyi. (*Makofi/Vigelele*)

Mheshimiwa Spika, jeshi la polisi kazi zake nyngi, kazi za *operation*, kwa hiyo, tunaomba Makao Makuu yamehamia hapa Dodoma na jeshi la polisi liimarishwe hapa Dodoma! Wapeni magari ya kufanya kazi, njia nzima ya kutoka Dodoma kwenda Iringa, kuna vituo viwili tu vya polisi navyo vyote havina gari na wanapita Wabunge wengi, wanapata matatizo huko, kwa hiyo, wapeni, wapeni magari waweze kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mtera tuna Tarafa tatu, tumeomba pipipiki tatu tu Mheshimiwa Kangi, mpaka leo! Tusaidieni, ili wale polisi waweze ku-move kwenda sehemu

moja hadi nyingine. Majuzi hapa kuna mtu alijinyonga, ilichukua karibu siku nzima, mtu kuweza kufika pale, polisi hana pikipiki, hana nini mpaka Mbunge nimetoa gari kwa ajili ya kwenda ku-rescue hiyo *situation*. Kwa hiyo, sisi tunaomba jeshi la polisi liimarishwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa, mikutano ya hadhara, kuna mikutano ya hadhara kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, kila mkutano ulikuwa unasababisha mauaji! Iringa alikufa mtu, Morogoro alikufa mtu, Singida alikufa mtu, ni mikutano gani hiyo, Arusha, mikutano hiyo imetuletea matatizo. Kwa hiyo, jeshi la polisi wakati mwingine linapima, hivi kama Bungeni tu tunaongea kwa mihemko hivi, Mbunge anaongea mpaka anasema *rubbish*, jana hapa. Sasa unajiliza huyo Mbunge akiwa kwenye mkutano wa hadhara wa kwake binafsi ataongea maneno gani huyu! Lazima jeshi la polisi lipige marufuku, jamani uchaguzi ukishakwisha siasa zinahamia humu, nje tuache watu wachape kazi, tutakutana 2020! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimewaambia siku zote nazidi, unajua wakati mwingine huwa natema madini sijui kama huwa mnasikiliza, uchaguzi ukiisha, mnaachia washindi wafanye kazi waliochaguliwa, na washindi ni Chama cha Mapinduzi. Wapeni nafasi watekeleze Ilani, maswali mtatuuliza mwakani kama yapo, na nina uhakika yatakuwa hayapo, vituo vya afya vinajengwa, maji yanapatikana, sasa kutakuwa na maswali gani tena, hakuna! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema, baadhi ya Askari wachache ambao wametajwa, kwamba siyo waaminifu, hao waendelee kuchukuliwa hatua, kama sheria inavyosema, lakini tusiliharibu jeshi la polisi lote kwa sababu ya mtu mmoja kakosea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jamani ikitokea bahati mbaya *Padre*, au Shekhe kakamatwa ugoni, siyo dini mbaya, haiwezekani, ni huyo huyo aliyeshikwa, dini inaendelea kuaminika, dhehebu linaendelea kuaminika ila ye ye

aliyevunja masharti ya imani yake huyo ndiye anayechukuliwa hatua. Tusiwatukane Askari wote kwamba wote hawafai, wote wanakosea, hapana, lakini kuna mambo yamezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, jana kilizungumzwa kitu hapa na nataka nikiseme, kwenye taarifa ya CAG iliguswa hapa jana kwamba, Mbunge wa CHADEMA alikopeshwa fedha za kununua gari. Nasema, jambo lile lina harufu ya ukwepaji wa kodi, kwa nini nasema hivyo, Wabunge tuna *exemption*, leo CCM wakinitumia kununua gari la chama, maana yake CCM wanataka kukwepa kodi, kwa sababu wanajua mimi nitasamehewa kodi fulani, lakini ukiniambia kwamba eti alikopeshwa na chama, halafu ameshindwa kulipa chama kimemnyang'anya, si kweli, hapo CHADEMA msikwepe mlitaka kuwepa kodi! (*Makofi*)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

SPIKA: Nini tena *Chief Whip*!

KUHUSU UTARATIBU

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, jambo analolizungumza rafiki yangu anayeongea sasa hivi, Mheshimiwa Chenge akiwa kwenye Kiti chako, alishatolea uamuzi na hiyo hoja anayoisema haiko kwenye taarifa ya CAG! (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Selasini ni hoja gani.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, ni suala la Mbunge wa CHADEMA kukwepa kodi. Sasa CAG hakuliweka hivyo, hoja ni kwamba kuna gari lilinunuliwa kwa mkopo kutoka CHADEMA na ile gari iko kwa jina la mwanachama, haliko kwenye jina la Baraza la Wadhamini la chama. Kwa hiyo, agizo ni kwamba lile jina liondoke kutoka kwenye jina la mwanachama liende kwenye jina la Baraza la Wadhamini na siyo kukwepa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na Mheshimiwa Chenge akiwa kwenye kiti chako alitoa hiyo *ruling*.

SPIKA: Hivi huyo mwanachana ni nani!...

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, huyu mwanachama hatajwi, huyu mwanachama ni Mbunge, Mbunge, siyo mwanachama wa kawaida, na CHADEMA ituambie kabla ya mwaka huu, au mwaka gani iliwahi kumkopeshwa mtu fedha ya kununua gari, wakati Wabunge wote tunakopeshwa hapa! Jamani kuna harufu ya kukwepa kodi, ndicho ninachosema na niko wazi, niiteni popote hata kwenye maadili niiteni nthibitisha, nyie mnataka kukwepa kodi kwa kumtumia Mbunge mwenye *exemption!* Ninyi siyo watu wasafiki kiasi hicho! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kuhusu mauaji, jeshi la polisi...

SPIKA: Mheshimiwa malizia.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, jeshi la polisi tunaliomba sana. Kuna watu wengi tu, siyo wale wanaotajwa maarufu, kwamba wameuawa taarifa zao hazipo, wako wengi, nina mjomba wangu anaitwa Nikanoli, amepotea tangu mwaka 1979 mpaka leo. (*Kicheko*)

Tunaomba jeshi la polisi lipewe vifaa vya kisasa vyenye weledi ili viwasaidie katika uchunguzi hasa wa mauaji, hasa wa mauaji. Watanzania wengi, siyo hawa tu wanaotajwa, wako wengi ambao wamepotea wengine wameuliwa, bila sisi kujuwa wala bila familia zao kuelewa.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabisa, niombe suala la uraia limezungumzwa sana, hili suala halijawahi kujadiliwa humu Bungeni, lakini kwa kuwa limeanza kusemwa humu, tuombe mamlaka za Serikali zilifanyie kazi. Watu wamezungumza sana kuhusu wafanyabiashara maarufu, kuna siku hapa ametajwa Vedagri wa Mwanza ni mfanyabiashara mkubwa amewekeza sijui Mafya, wapi,

Mwanza, hawa watu wote ambao wengine siyo maarufu wakulima ambao wanataka kuhamia nchi hii wapewe huo uraia, kama ni haki yao na kama kuna matatizo vyombo vichunguze, viangalie ubaya wao, viwakatalie kama ambavyo wengine wamewahi kukataliwa bila kusemwa Bungeni na wengine wamewahi kupewa bila kusemwa Bungeni, Serikali iendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo kwa namna moja au nydingine imefanyiwa uchambuzi na Serikali na kuondosha aya nyngi ambazo kama Kambi tuliona ni muhimu kutoa maoni yetu, kuishauri na kuihoji Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu Polisi kukamata raia na kuwaweka mahabusu ya Polisi muda mrefu hadi miezi sita bila kuwapeleka Mahakamani na wengine kuwaweka mahabusu ya magereza hadi miaka kumi na kuendelea na kusema upeletezi haujakamilika. Naongea haya nina ushahidi kwa Magereza ya Idete, Kiberege, Morogoro Mjini (Manispaa). Hivi kwa nini hii Serikali inawatesa raia/nguvukazi namna hii? Napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu uvunjaji huo wa haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo inayosababisha mlundikano wa mhabusu magereza ni *DPP* kuchelewesha uchunguzi kwa kifungu cha 225. Je, lini Serikali itakifuta kifungu hicho ambacho ni cha ukoloni wakati huo kunyanyasa watu weusi? Kifungu hiki kinasababisha mazingira ya rushwa kwa waendesha mashtaka na kuangamiza familia/raia.

Mheshimiwa Spika, mhabusu ya wanawake Gereza la Morogoro Manispaa ina hali mbaya kwa wanawake

kutumia choo kimoja ambacho kiko nje ya maselo hayo matatu ambapo kuanzia alasiri wanapofungiwa na ikiwa mahabusu amepata tumbo la kuhara inampasa ajisaidie kwenye ndoo ambayo ni moja (mtondoo) uliopo ndani na kulala nayo hadi asubuhi. Je, huu ni uungwana kwa wanawake kufanyiwa ukatili huo?

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi mahabusu hao wanatumia choo kimoja na maaskari walio zamu na kuhtarisha maisha ya maaskari hao. Je, ni lini Serikali itaboresha selo za gereza hilo? Kibaya zaidi selo hiyo haina bomba la maji ya kunywa, bomba liko moja tu chooni ambako hutumiwa kupata maji ya kunywa, hivi sisi hapa tunakunywa maji ya chooni? Naomba Serikali iweke miundombinu haraka katika gereza/mahabusu hiyo ambayo ina wanawake waliowekwa hapo zaidi ya miaka mitatu hadi mitano bila kesi zao kuisha au wafungwe ama waachiwe.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ipeleke trekta na vifaa vingine vya kilimo Gereza la Idete ili wazalishe kwa tija. Trekta moja walilopewa halitoshi kwa kuwa wana eneo kubwa la kilimo.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mlimba liko kilometra 235 hadi Ifakara ambapo ndipo kilipo Kituo cha Polisi cha Wilaya hivyo kupelekea wananchi wengi kukosa haki zao. Serikali imeomba jengo la TAZARA kuhifadhi askari wachache kujibanza hapo kutokana na kutokuwepo kwa jengo lao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na umbali huo na ukosefu wa barabara ya lami na uwingi wa mvua zilizopo Mlimba, askari hao hawana gari la uhakika. Halmashauri na watu wa Mlimba kwa kuona umuhimu wa uwepo wa Kituo cha Polisi walitoa eneo la ardhi bure ili Serikali ijenge Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa Serikali itajenga kituo cha kikubwa cha Polisi, Jimbo la Mlimba ili kuepusha usumbufu kwa wananchi? Napenda kupata majibu ya Serikali, je, bajeti hii imetenga kiasi gani cha fedha kuanza

ujenzi wa kituo hicho? Kuhusu gari, ni lini Mlimba itapata gari la uhakika kutokana na mazingira yake?

Mheshimiwa Spika, nilishaongea na Waziri, Mheshimiwa Kangi mara nyingi kuhusu matatizo mbalimbali ya rushwa zinazofanywa na baadhi ya maaskari wa barabarani kwa watoa huduma ya usafiri kwa wananchi wa Mlimba ambao ni waendesha Noah, pikipiki na kadhalika. Wao wenyewe wako tayari kumueleza Waziri kuhusu kero hiyo kubwa ya rushwa. Pia nilimwambia kuna rushwa ndani ya Ofisi ya Upelelezi kwa baadhi ya maaskari. Vilevile nilimuomba afanye ziara Jimbo la Mlimba lakini pamoja na ahadi alizonipa hadi leo hajatekeleza. Je, ni lini sasa Mheshimiwa Kangi Lugola, Waziri, atafanya ziara hiyo kama alivyoahidi? Ahsante.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza wote Waziri na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wote ndani ya Wizara kwa kazi nzuri iliyotukuka kwa nchi yetu na wananchi wake. Pia, pongezi za dhati kwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jinsi anavyoyajali majeshi yetu. Hivyo, nasi wawakilishi tuna kila sababu tukubaliane na tuunge mkono jitihada za Rais kwa kazi kubwa anayofanya kwa majeshi yetu kwani wanafanya kazi katika mazingira magumu hasa makazi, ofisi, sare na miundombinu mingine kutokarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwa Serikali yangu sikuvi kuisukuma na kuvisitiza Hazina kutoa fedha zote za maendeleo zinazopitishwa na Bunge kwa bajeti ya Wizara hii kwa Mafungu yote 14, 28, 29, 93 na 51 ili Wizara iweze kutatua changamoto zinazowakabili ambazo ni sugu kwa sasa. Kwa kuwa, hakuna fedha ya maendeleo zilizotoka kwa mwaka 2018/2019 za shilingi bilioni 1.027 na kwa kuwa mwaka haujakamilika ni vema zikatolewa kwa sasa. Mfano Chuo cha Polisi Kidatu kutokana na kutotolewa fedha za maendeleo kimechakaa na kupelekea kupunguza idadi ya wanachuo wanaodahiliwa chuoni hapo na zinahitajika shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti kiutendaji na tunahitaji wanajeshi wetu kuwa na mpangilio mzuri wa maisha ya kila siku, hivyo maji na umeme ni huduma muhimu kwao. Ni vema tuweke mkakati madhubuti wa kuhakikisha madeni yote ya huduma hizo yanalipwa kikamilifu na yasijirudie.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu na kazi ngumu waifanyayo wanajeshi wetu na changamoto lukuki walizonazo ambazo zinawadhoofisha lakini inabidi wafanye kazi ya ziada katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi na umakini mkubwa. Wizara inatambua uzito wa changamoto hizo kwa majeshi yetu lakini inapoandaa bajeti wanajielekeza zaidi na ukomo wa bajeti waliopewa na Hazina. Nachokiona ni kwamba ukomo wa bajeti wa sasa haukidhi mahitaji na hawawezi kupata ufumbuzi wa changamoto walizonazo kwa wakati na ukizingatia tabla iliyodumu kwa Hazina kutotoa fedha za maendeleo kwa wakati na zote kama zilivyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana. Katika hotuba nimeona kwa Wilaya ya Nyang'hwale tumejengewa nyumba za askari wetu kwa familia saba. Naomba kwenye bajeti hii tujengewe mahabusu kwani iliyopo imezidiwa, imekuwa ndogo sana sababu kuu ni kuwa na Makao Makuu ya wilaya.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata muda wa kuchangia kwa maandishi. Kumekuwa na mamalamiko kutoka kwa baadhi ya maaskari wa kike kutopangwa mafunzo ikitokea bahati nzuri askari huyo ni mjamzito. Aidha, nafasi ya vyeo kwa wanawake inaonyesha bado ni finyu. Je, Jeshi la Polisi linawapa fursa gani maaskari polisi wanawake wanaaoahirisha mafunzo kutokana ujauzito na fursa zipi za mafunzo hupata maaskari hasa baada ya kujifungua?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono maoni ya Kamati kuendelea kutoa msisitizo kwa Serikali kutoa fedha kwa wakati ili kuimarisha utendaji kazi na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mafunzo 14,28,51 na 93.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika suala la uvunjwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa katika utundikaji au upeperushaji wa bendera za vyama kwenye Ofisi na mabango mbalimbali. Hivi karibuni katika Mkoa wa Iringa umetokea mtindo anakuja kiongozi wa nchi bendera za CHADEMA zinaondolewa zote na kutundikwa bendera za CCM. Hii haikubaliki tuko katika mfumo wa vyama vingi ni vyema Jeshi la Polisi likalinda mali za jamii na watu wake. Bendera ziliondolewa Mafinga na Iringa Mjini.

Mheshimiwa Spika, askari wanahitaji kuongezewa mishahara na pia kupata posho za mazingira magumu ya kazi yao. Mara nyingi wanakosa karatasi, *printer* na mafuta ya kuendesha programu mbalimbali. Nashauri waongezewe fungu ili wafanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza wamekuwa hawana mavazi/sare kwa kugharamiwa na Serikali, wananaunuwa kwa fedha zao wenyewe kinyume na taratibu. Serikali ifanyie kazi suala hili ili wapewe sare za kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la maadamano na mikutano ya hadahara limekuwa ni changamoto kufanya hasa kwa vyama vya upinzani. Nashauri Jeshi la Polisi lifuate sheria na Katiba inayotaka kuwapo kwa maandamo pamoja na mikutano ya hadhara na mikutano/vikao vya ndani. Jukumu la Jeshi la Polisi ni kulinda amani katika mikutano/vikao na maandamano.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mlundikano wa mahabusu. Nashuri kuanzishwe Kitengo Maalum cha Usuluhishi Polisi ambacho kitasuluhisha migongano ya

waliofika kituoni ili kuwajengea umoja wananchi na kuwaweka karibu na Polisi kama sehemu ya kimbilio.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani na majeshi yote. La msingi ni kuhakikisha fedha za maendeleo zinatolewa ili kuwezesha majeshi hayo kumaliza miradi kusudiwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Katavi unalao tatizo kubwa la makazi ya askari sambamba na makao Makuu ya Mkoa (Jengo la Polisi la Mkoa). Suala hili limepelekea kutumika kwa yaliyo kuwa Makao Makuu ya Polisi Wilaya.

Mheshimiwa Spika, limekuwepo tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Gereza la Mpanda Mjini. Ombi langu ama ukarabati ufanyike katika gereza hilo au ujenzi wa magereza hasa katika Wilaya Mlele ili kufanya mahabusu toka Mlele wapatiwe huduma huko huko.

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi/sare hasa za Askari Magereza na wafungwa naomba litazamwe kwa namna ya pekee maana vazi pia linaakisi kiwango cha utu na ubinadamu ambao ni haki ya msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyenzi Mungu kunipa fursa kuchangia siku ya leo. Nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fusa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara pamoja na viongozi wetu wakuu wa majeshi chini ya

Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Pamoja na changamoto kubwa ya uhaba wa vifaa na nyenzo za kufanya kazi, hongereni kwa kazi kubwa na nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri katika baadhi ya maeneo ili kuboresha huduma katika majeshi yetu. Nianze na Jeshi la Magereza, wanafanya kazi kubwa na nzuri. Wana majukumu makubwa sana ya kuwahifadhi wahalifu walioshtakiwa kwa makosa mbalimbali na zaidi ya hapo kutoa elimu ya kuwarekebisha wahalifu (*re-habilitation*). Jambo hili la kuwarekebisha wahalifu wakiwa katika kutumikia adhabu zao huwa gumu kwa sababu ya kukosa nyenzo, vifaa na mazingira ya kufanya hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ingeweza kulisaidia Jeshi letu la Magereza kupata mkopo wa kupata vifaa vya kufundishia, vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kujenga karakana na madarasa. Jeshi letu hili lina wataalam wa kutosha, mfano mainjinia wa majengo (*civil engineers*), wachora ramani, mafundi umeme, mafundi bomba na wengine.

Mheshimiwa Spika, tukitumia *force account* wanaweza kujenga na kupanua magereza mbalimbali. Tukifanya hiyo tutakuwa tumesaidia Watanzania wengi sana watakaopata adhabu na wakitoka baada ya kifungo wawe na utalaam. Gereza liwe ni chuo cha ufundi, wafungwa wapewe vyeti vya kuhitimu mafunzo. Baadhi ya mafunzo yanayoweza kutolewa ni ufundi uashi, umeme, seremala, bomba, gesi, kuchomelea (*welding*), *IT (computer)*, ushonaji, lugha mbalimbali na uchoraji.

Mheshimiwa Spika, pia kwa wale wanaosubiri kesi (mahabusu) wapate huduma bora zaidi kwa upande wa chakula, makazi, kupata taarifa mbalimbali kuititia redio au TV sababu inawezekana mwisho wa siku anatoka bila kuwa na kesi au adhabu kuititia mahakama.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Magereza lina uzoefu na wataalam wa kutosha katika fani mbalimbali, mfano, ujenzi wana usajili wa daraja la kwanza, kilimo, ufugaji,

useremara na hata katika kuzalisha mali kupitia miradi mbalimbali na viwanda vidogo. Mfano Babati Magereza imeshirikiana na VETA kujenga jengo lenye thamani ya shilingi milioni 495 ambapo likiisha itafikia shilingi milioni mia tatu wameweza kuokoa shilingi milioni 195 kupita *force account*. Vilevile jengo la Uhamiaji Arusha lilijengwa na Magereza. Naomba jeshi letu lipewe vifaa vyaa kisasa vyaa ujenzi ili kitengo chao cha ujenzi kiweze kufanya kazi ya ukandarasi na washindane katika soko.

Mheshimiwa Spika, pia katika kilimo, ufugaji na uzalishaji mali (kusindika), Jeshi letu likopeshwa zana za kufanya kazi kama matrekta, vifaa vyake (*implements*) ili wawewe kuzalisha chakula chao na cha biashara na iwe sehemu ya shamba darasa. Kila mwaka katika Maonesho ya Nane Nane hupata kikombe cha ushindi ya kwanza. Wanafuga kuku, bata, ngombe, samaki, mbuzi na sungura kwa ufanisi mkubwa. Siyo lazima baadhi ya hivi vitu viwe kupitia bajeti, wanaweza kukopeshwa mfano matrekta na zana zake kupitia mfumo wetu unaokopesha raia wengine na pia kupitia *TADB*, Mfuko wa Pembejeo na taasisi zingine za fedha. Pia Serikali kupitia ruzuku na Magereza ipewe mashamba darasa ya kilimo, mifungo na usindikaji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ni suala la mazingira na matumizi ya nishati. Tunashauri Magereza zetu ziwe mfano ya matumizi bora ya nishati (kuni, mkaa na umeme). Leo hii magereza mengi hutumia kuni nyingi sana kwa ajili ya kupikia. Nashauri kwa kupitia *CAMARTEC*, magereza yote yajenge mifumo ya nishati ya kutumia gesi inayotokana na vyoo na mifungo (*biogas* na *bio-latrine*). Hii inaweza kupunguza matumizi ya kuni, pia kuweka mifumo ya *solar*, upepo na hiyo gesi utakayozalishwa kwa wingi (*bio-latrine*) wanaweza kupata nishati ya umeme na kupunguza gharama za umeme.

Mheshimiwa Spika, nashauri magereza yetu yote yawekewe mifumo ya kuvuna maji ya mvua. Hii itasaidia kupata maji ya matumizi ya kawaida na pia kupunguza gharama za malipo ya ankara za maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashauri taasisi chini ya magereza zinazozalisha mali ziimarishwe. Pia tuangalie namna ya kuwakopesha Askari wetu wa Magereza usafiri wa pipipiki au magari kutokana na nyadhifa zao na wawe wanalipa kwa mwezi. Vilevile kuwe na *bulk procurement* kwa vifaa vya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na walio chini yao ikiwa na Viongozi Wakuu wa Majeshi yaliyoko chini ya Wizara hii. Naomba nishauri katika maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; naomba nishauri kwanza Jeshi hili lipatiwe zana za kutosha za kufanyia kazi yao vizuri. Leo hii kwa jina la Zimamoto tunatoza kila biashara, viwanda, mgodi na hata kilimo kwa ekari, gharama za *fire inspection fee*, ni fedha nyngi sana zinazokusaywa. Nashauri badala ya kuweka bajeti ya kununua vifaa vya kuzima moto na fedha huwa haitoki kwa wakati, makusanyo ya tozo tunayokusanya aslimia 20 ziende katika Mfuko Maalum wa Zimamoto ili waweze kununua vifaa vyao vyote.

Mheshimiwa Spika, hapo pia watapata bajeti ndogo ya kutoa elimu juu ya uokoaji wakati wa dharura kwa raia. Pia Wizara ifanye kazi karibu na mipango miji na taasisi za maji kuweka *fire hydrants* mabomba ya kutolea maji katika kila eneo ili wakati wa dharura zitumike. Huko miaka ya nyuma ilikuwa ni lazima kila eneo liwe na bomba la kutolea maji (*fire hydrants*).

Mheshimiwa Spika, pia nishauri Idara ya Uhamiaji ambao wanafanya kazi nzuri sana mifumo yao iunganishwe na *NIDA*, Polisi na Idara ya Kuandikisha Vifo na Vizazi. Itasaidia kupata taarifa mapema na ya uhakika. Nashauri Wizara kupitia Uhamiaji pia iangalie suala la uraia wa Watanzania

ambao wamezaliwa Tanzania, wamekulia Tanzania, wazazi wao walizaliwa Tanzania ila hawakujua sheria na utaratibu wa kukaa na uraia wa awali na kupata cheti cha uraia wakati wa uhuru.

Mheshimiwa Spika, nipongeze jitihada za Wizara kupunguza ada ya kupata vyeti vya uraia kwa Watanzania ambao hawakufanya hivyo awali kutoka Dola za Kimarekani 5,000 hadi milioni mbili *dependant pass* kutoka Dola za Kimarekani 500 hadi 100,000 kwa *dependant* wa Kitanzania. Nashauri hawa Watanzania waliokuwa na vyeti hivyo tuweke muda maalum, mfano mwaka mmoja wapatiwe kipaumbele na viwango vya milioni mbili vipunguzwe na iwe angalau laki tano kwa kipindi hiki maalum na tuwaondoe hofu Watanzania hawa. Wengi hawana uwezo wa milioni mbili baada ya hapo tubaki na wanaoomba uraia wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, pia haki ya kuomba uraia wa mwanaume aliyeoa mwanamke Mtanzania na mwenye watoto ambao Watanzania iwe na fursa ya usawa kwa uraia wa wanawake raia wa nje walioolewa na mwanaume Mtanzania, *Fast Track*.

Mheshimiwa Spika, pia Somo la Uraia litolewe kuanzia ngazi ya shule ya msingi na sekondari, itasaidia kuongeza uzalendo.

Mheshimiwa Spika, nayapongeza Majeshi yetu ya Zimamoto na Idara ya Uhamiaji kwa kazi nzuri inayofanywa.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuweza kuchangia leo hii katika hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, nipongeze Wizara hii kwa jitihada ambazo zimekuwa zikifanyika katika kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarika katika nchi yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola na Naibu wake kwa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Wizara hii lakini bado kuna changamoto katika mipaka yetu. Mimi natokea Mkoa wa Kigoma, huu ni mkoa ambao tunapakana na nchi nne za Congo, Burundi, Zambia na Rwanda ambapo mwingiliano na wenzetu hawa ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mipaka yetu haina ulinzi wa kutosha kwani wakimbizi hawa wamekuwa wakifanya matukio ya kihalifu. Tumeona matukio ya ujambazi yakishamiri kila kukicha kwa kutumia silaha za moto, wananchi wamekuwa na hofu hawana amani na maisha yao. Hivyo niombe sana Serikali tupate askari wa kutosha katika Wilaya zote za Kasulu, Kibondo, Buhigwa, Kigoma na Mkoa wetu kwa ujumla watu wake waishi kwa amani pasipo hofu ya ujambazi huu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie tena suala la hawa ndugu zetu askari. Hawa ni ndugu zetu lakini ni watu muhimu sana kwani hawalali wakilinda usalama wa raia na mali zao, lakini pia amani ya nchi yetu. Niombe sana Wizara iwaangalie hawa askari wetu kwa jicho la pili kwani wanaishi katika mazingira magumu sana, hawana makazi bora na imara, wengi wanaishi mpaka kwenye nyumba za mabati, hii si sawa. Naomba sana Wizara iwathamini wapate nyumba za kutosha bora na imara, hii itawasaidia hata kuongeza bidii katika kazi. Pia watu hawa wamekuwa wakifanya kazi muda mrefu bila kupandishwa vyeo, niombe sana tuwalipe fadhila wapande vyeo kwani wanafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, niguse suala la Vitambulisho vya Taifa. Kiukweli bado wananchi wengi sana hawajapata hivi vitambulisho, leo watu milioni 16 ndiyo ambao wamepata vitambulisho hivi wakati Tanzania ina watu zaidi ya milioni 50. Niombe sana Serikali iongeze kasi kuhakikisha wananchi wote wanapata vitambulisho na tumeona Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano wanassema kuanzia mwezi ujao watu watasajili *line* kwa kutumia Vitambulisho hivi vya Taifa. Niseme hili zoezi lisitishwe kwanza mpaka pale wananchi wote watakapopata hivi vitambulisho kama kweli tuna nia ya kuwasaidia hawa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nigosie suala la ujenzi wa vituo vya polisi. Kiukweli hali ni mbaya sana yaani kuna vijiji ukifika unaweza lia kwa huruma, kwani majengo yao yapo katika hali mbaya sana. Unajuliza hii ofisi kweli ndiyo wanafanya kazi hawa askari wetu wanaolala usiku kucha wakilinda mipaka, usalama wa raia na mali, ofisi inataka kuanguka, hakuna hata vitendea kazi, kiukweli hii siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, leo katika Kijiji cha Mwindiga ninapotoka kituo cha polisi kina hali mbaya sana, kituo kidogo lakini hakuna hata vitendea kazi, hawana magari. Naomba sana Wizara mkarabati vituo vya polisi lakini magari ya kutosha yapelekwe katika maeneo mengi kwani hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, kwa leo niishie hapa, nashukuru kwa kuweza kupata muda wa kuchanglia leo kwa maandishi.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo. Makatazo ya vikao vya ndani. Jeshi la Polisi limeendelea kukataza vikao vya ndani vya Vyama vya Upinzani hasa kwa kipindi hiki ambapo wanafanya changuzi za ndani ya chama. Mfano, kikao cha ndani cha wanawake huko Geita tarehe 8 Machi, 2019 Jeshi la Polisi lilizuia kikao cha ndani cha BAWACHA na kulazimisha wanawake hao wa CHADEMA kuungana viwanjani na wanawake wa CCM ambao walikuwa kiwanjani, hii siyo sawa na siyo halali. Naomba Serikali itende haki iache wananchi wafanye vikao vyao vya ndani bila bughudha. Vyama vyote viko kwa mujibu wa Katiba ya nchi, halafu utekelezaji unakuwa kinyume chake.

Mheshimiwa Spika, Polisi wa Barabarani wamekuwa kero kubwa sana kwa wananchi hasa kwa madereva wa *hiace* na kirikuu. Madereva wanasihamishwa kila kituo ambapo wapo Polisi na wanatozwa fedha. Naiomba Serikali itafute utaratibu wa kudhibiti makosa ya barabarani kwa kutumia mashine badala ya Polisi kuwa barabarani. Wafunge maeneo yote mashine za kubaini makosa mbalimbali na

madereva waweze kwenda kulipa faini na kodi zingine kwenye vituo vya polisi bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo. Nashauri Serikali kuhakikisha haki na amani inalindwa na itambue amani ni tunda la haki. Pale tu ambapo Polisi watatenda haki ndipo amani itashamiri Tanzania. Mfano, Polisi wanapozua vikao vya ndani kwa Upinzani wakati Chama Tawala wakifanya vikao, hiyo siyo haki. Nimeshuhudia kwa macho yangu nikiwa kwenye kikao cha ndani Kibaha, nikiambiwa kuvunja kikao hicho eti kutatokea vurugu wakati ni kikao cha Kikatiba cha chama.

Mheshimiwa Spika, nishauri Serikali ifuatilie rushwa zinazoendelea kwa Askari wa Usalama Barabarani. Mfano, magari yanayotoka Saba Saba kuelekea Nane Nane, siku moja kwa macho yangu nimeona Polisi wanasimama Kilimo Kwanza kila daladala wanatoa Sh.2,000, hivyo halikaguliwi linaendelea na safari hata kama kuna shida kwenye gari.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie kwa upya maisha ya Askari Magereza na Polisi, makazi yao siyo rafiki. Hawawezi kufanya kazi zao kwa weledi kama Serikali haitawaangalia kwa jicho la ziada.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iangalie ajira za Polisi kwani zinatolewa kwa upendeleo bila kujali sifa tarajiwa za Polisi zilizoainishwa katika ajira hizo.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya katika kutekeleza majukumu yake, ikiongozwa na Waziri, Mheshimiwa Kangi Lugola na Naibu wake Mheshimiwa Mhandisi Hamadi Masauni.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu maeneo matatu. Kwanza ni nyenzo za kufanya kazi. Kuna changamoto kubwa ya vitendea kazi kwa Majeshi yetu ya

Polisi, Magereza na lile la Zima Moto. Naomba Serikali kuangalia kwa karibu suala hili kwani imefika mahali ikitokea dharura, Polisi wanategemea msaada wa vyombo vyaya usafiri kutoka kwa watu binafsi kwa kutokuwa na gari au gari kukosa matengenezo. Si ajabu kuona Magereza nao wanaomba kusaidiwa usafiri kutoka kwa watu binafsi ili kwenda kusaga chakula cha wafungwa. Nashauri majeshi haya yapewe fedha za kutosha kugharamia vitendea kazi, ununuzi wa mafuta, posho za askari na stahili zao zingine pamoa na sare zao.

Mheshimiwa Spika, pili, Kituo cha Polisi Nanyamba. Kituo hiki kilijengwa kama *Police Post* kuhudumia Tarafa ya Nanyamba miaka ya nyuma. Kwa sasa Nanyamba ni Halmashauri ya Mji na Jimbo na idadi ya watu imeongezeka na matukio ni mengi. Naomba yafuatayo yafanywe: Kituo hiki kiboreshwe ili kukidhi haja ya kuhudumia eneo husika; idadi ya askari waongezwe; na wapewe usafiri wa magari na pikipiki.

Mheshimiwa Spika, tatu, magari ya Zimamoto ni ya muda mrefu, machache na hayatoshelezi. Nashauri zitengwe fedha za kununua magari zitakazopelekwa kila Halmashauri hata kwa kununua awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha, naunga mkono hoja.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, Serikali iliondoa maduka ya *duty free* yaliyokuwa yaktumika kutoa huduma kwa watumishi wa vyombo vyaya ulinzi na usalama, ikiwepo Polisi, Magereza, Zimamoto na kadhalika na imeleta utaratibu wa kulipa kiasi cha fedha kama mbadala wa *duty free*.

Hata hivyo, watumishi wa Uhamiaji wamekuwa hawalipwi licha ya kuwa nao ni sehemu ya vyombo vyaya ulinzi na usalama. Hali hii inaleta hali ya unyonge hasa kwa kuzingatia kuwa kazi zao ni za ulinzi na usalama. Nashauri Serikali ione umuhimu wa kuwajumuisha Uhamiaji ili na wao wapate huu unafuu.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa gari ya polisi kati ya Dodoma na Iringa. Barabara ya Dodoma – Iringa hivi sasa inatumiwa na magari mengi ya mizigo, abiria na binafsi. Hata magari ambayo ni *transit* kati ya Tanzania na nchi za jirani yanatumia barabara hii ambayo ni sehemu ya barabara kuu ya Cairo-Johannesburg. Pamoja na umuhimu huu, hakuna huduma ya gari la polisi hali ambayo ni hatari sana, hasa inapotokea ajali ambayo ina majeruhi wanaohitaji huduma ya haraka. Pamoja na kuwa siyo jukumu la Jeshi la Polisi kubeba majeruhi lakini uwepo wa gari unasaidia kufika eneo la tukio kutoa msaada wa kiusalama.

Mheshimiwa Spika, siku ya tarehe 19/4/2019 (Ijumaa Kuu) nilipata ajali kati ya Chipogolo na Mtera. Nawashukuru sana Askari wa Kituo cha Chipogolo, pamoja na usafiri wa kuunga-unga walifika kutoa msaada. Nikiwa eneo la ajali, nillishuhudia magari ya vlongozi wakiwemo Wabunge, Mawaziri na mengine ya Serikali yakipita na ndipo nilipobaini kuwa barabara hii inahitaji kuwezeshwa hasa kwa vyombo vya usafiri walau katika Kituo cha Chipogolo (upande wa Dodoma) na Migori (upande wa Iringa).

Mheshimiwa Spika, naamini aina yoyote ya gari itawasaidia. Nasema haya nikiwa ni mhanga wa hali halisi kwa sababu baada ya ajali ambayo haikuwa na madhara kwa maana ya majeruhi, ilituchukua zaidi ya saa zima kupata msaada wa lifti ya gari. Sasa nilijiliza ingekuwaje au inakuwaje pale ambapo kumetokea majeruhi wanaohitaji msaada wa haraka? Naamini hata kupitia wadau, Jeshi la Polisi wanaweza kupata msaada wa gari.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri na hotuba yenye kuleta matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mafia inakabiliwa na ukosefu wa gari la doria baada ya gari lililokuwepo kutumbukia baharini na kuharibika vibaya. Wilaya ya Mafia ni kisiwa kilichopo pembezoni mwa nchi Kusini Mashariki na

kinapakana na nchi ya Comoro. Kutokana na ukweli huo, kuna umuhimu mkubwa suala la ulinzi na usalama kuimarishwa sambasamba na kupatiwa boti ya kisasa ya doria ili kuweza kukabiliana na matishio hususani ya ugaidi kutoka nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, makazi kwa Askari Polisi na Magereza, Wilaya ya Mafia ni kero ya muda mrefu sana. Tunaiomba Serikali ijenge nyumba za askari wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Spika, kwanzা nimpongeze Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii pamoja na timu yake zetu kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliyotoa shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Lushoto lakini mpaka sasa kituo kile hakijakamilika. Nilipofuatilia nikaambiwa fedha zimeisha na wakati jengo lipo kwenye usawa wa lenta. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu ifuatilie fedha hizo ili jengo lile liweze kuisha na kama unavyofahamu Kituo cha Polisi Lushoto ni cha tangu Mkoloni, kwa hiyo ipo haja kubwa kumalizia kituo kile.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kuna tatizo kubwa sana la nyumba za Askari Polisi na Askari Magereza. Kama niliviotangulia kusema kuwa Kituo cha Polisi pamoja na Magereza majengo haya ni ya tangu Mkoloni na hii imefanya Askari wetu kuishi katika mazingira magumu mno. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu Tukufu ipange bajeti mwaka huu ili tupate hata nyumba kidogo za wafanyakazi wa Polisi pamoja na Magereza.

Mheshimiwa Spika, sambasamba na hayo, Gereza la Wilaya Lushoto lipo katikati ya mji ambapo siyo salama kwa Askari wetu wa Magereza, kwani wanakuwa na kazi ya ziada na hii inapelekea kutoroka kwa wafungwa. Kwa hiyo, niiombe

Serikali yangu itenge fedha ili kujenga gereza lile eneo ambalo tayari limeshatengwa la Yogui.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na baadhi ya Askari wanafanya vitendo vya kihalifu lakini yote haya ni kutokana na kukaa kwa muda mrefu katika kituo kimoja, ndiyo maana Askari hawa wanatumika na wenyiji hasa wenyewe uwezo wa kifedha kufanya matukio watu ambaao hawana hatia, hasa kuwabambikia kesi, ili mradi tu hakupewa rushwa na mhusika. Kwa hiyo, niishauri kama siyo kuiomba Serikali kuwahamisha Askari hawa, hasa katika Wilaya ya Lushoto kuna Askari wanataka kuzeeka hapo hapo Lushoto.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi wetu kucheleweshewa Vitambulisho vya Taifa, hasa wale waliopo vijijini kwani tumekuwa tukikosa majlibu ya kuwalibju wananchi wetu. Kwa hiyo, nilombe Serikali yangu ifanye haraka iwezekanavyo, iwapatie wananchi vitambulisho hivyo na kama unavyo jua vitambulisho hivyo ni muhimu katika usajili wa mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ni ya milima na mabonde, kwa hiyo, kwa jiografia hiyo wananchi wengi hasa wa pembezoni hawapati huduma hasa ile ya usalama pamoja na mali zao. Hii imepelekeea wananchi kuvamiwa mara kwa mara na kupoteza maisha pamoja na mali zao au kujeruhija mwisho wa siku anakuwa ni mlemavu wa viungo. Kwa hiyo, nilombe Serikali yangu Tukufu ijenge vituo vidogo vya Polisi katika kila Kata ili kupunguza changamoto hizi zinazoendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Barabarani wamekuwa wakiwanyanyasa madereva wa magari hasa wa Noah, bodaboda pamoja na wa magari ya mizigo. Hali hii imekithiri katika Wilaya ya Lushoto. Nimuombe Waziri atume hata wataalamu wake ili wakajionee jinsi madereva wale wanavyonyonyasika, hasa hawa wa bodaboda, ukizingatia bodaboda hawa, pikipiki nyingi wamezaminwa utakuta mwisho wa siku anarudi mtaani na kufanya vitendo vya kihalifu. Niendelee kuiomba Serikali yangu kuwasimamia

vijana hawa wa bodaboda waweze kufanya kazi zao bila ya bughudha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Mheshimiwa Waziri alitoa tamko la zile pikipiki zilizokamatwa kwa makosa madogo madogo ziachiliwe lakini ukifika Kituo cha Polisi Lushoto, pikipiki hizo zimejaa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na hili ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Spika, naomba nami nichangie hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani kutokana na umuhimu wake katika suala zima la usalama wa raia na mali zetu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema katika vipaumbele vya Wizara yake ni kuhakikisha amani na utulivu unaendelea katika nchi yetu na kuhakikisha kuwa wanajitosheleza kwa chakula kupitia miradi inayoendeshwa chini ya Jeshi la Magereza. Haya ni malengo mazuri sana na ya kuungwa mkono lakini ni lazima ukweli huu hapa chini uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, moja, amani na utulivu ni tunda la haki na uzingatiaji wa sheria kwa kila mtu yaani watawala na watawaliwa, raia na viongozi. Suala la kuzuia mikutano ya hadhara na sasa karibu shughuli zote za kisiasa za wanasiasa ni uamuzi usio sahihi, wa haki na wala siyo wa kisheria. Hii inaweza kuwa sababu ya uvunjifu wa amani siku za baadaye. Ni vyema Jeshi letu la Polisi likatumia weledi wake kuhakikisha shughuli za kisiasa zinafanyika kulingana na sheria na mtu mmoja mmoja anayetumia fursa hii vibaya achukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, hivi majuzi nimeona katika vyombo vya habari Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mara akitoa maelekezo na vitisho kwa *OCD* wa Tarime eti awakamate Wabunge wa CHADEMA waliofanya mkutano wa hadhara

huko Tarime Mjini na kama hatawakamata basi aondolewe mara moja katika nafasi yake. Hii inatia mashaka sana kauli kama hizi zinapoachwa bila ukemeaji wowote kutoka kwa Waziri mwenye dhamana. Naomba atakapokuja kuhitimisha na hili alitolee maelezo na kukemea tabia hii ili Jeshi letu liendelee kuaminiwa na kuheshimiwa na watu wote.

Mheshimiwa Spika, mbili, pawepo na ushirikiano wa karibu baina ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Katiba na Sheria na Idara ya Mahakama juu ya uwepo wa mahabusu wengi ambaao kwa sababu mbalimbali wanakaa katika magereza yetu kwa muda mrefu bila mashauri yao kuamuliwa au hata kuanza kusikilizwa tu. Masuala kama haya yanatumia gharama nyingi sana za jeshi letu mfano chakula, magari, rasilimali watu na hata hali ya afya ya mahabusu wenyewe kutokana na msongamano wa mahabusu wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeeleza katika ukurasa wa 11 na 12 jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kukabiliana na uhaba/uchache wa Vituo vyta Polisi na nyumba za askari. Katika Jimbo la Moshi Vijijini, sisi wananchi wa Jimbo hili, Kata za Uru Kusini, Shimbwe, Uru Kaskazini na Uru Mashariki wamejenga kituo kikubwa cha kisasa sana cha *Class 'C'* na kimekamilika. Nilishamuarifu Mheshimiwa Waziri juu ya kukamilika kwa kituo hiki nikimuomba aje kukipokea na kutambua mchango wa wananchi hawa wa zaidi ya Sh.100,000,000. Naomba wakati Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atuambie ni lini atakuja kupokea kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa maombi yangu kwa niaba ya wananchi ninaowawakilisha *TANAPA* (*KINAPA*) wameunga jitihada hizi za wananchi na kujenga nyumba kwa ajili ya askari watakaohudumu katika kituo hiki, nayo imekaribia kukamilika. Jitihada kama hizi zilishafanyika pia katika Tarafa ya Kibosho ila sasa uhudumiaji wa kituo hicho ambacho kilijengwa katika Kata ya Okaoni leo kinahitaji ukarabati na huduma nyingine kama gari la uhakika kutokana na ukubwa wa eneo linalohudumiwa na kituo hicho.

MHE. MARTIN M. MSUHA: Mheshimiwa Spika, naungana na wachangiaji waliotangulia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazoendelea kuzifanya. Nilipongeze pia Jeshi letu la Polisi kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kutulinda usalama wa raia na mali zetu. Hivi karibuni kumezuka madhehebu mengi sana hususan ya imani ya Kikristo (Pentekoste). Madhehebu hayo mara nyingi hawana ratiba ya kuendesha ibada zao na mara nyingi huendeshwa kwenye makazi ya watu na mara nyingi wanapiga miziki kwa sauti ya juu usiku kucha.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo ni kero kwa wakazi wa maeneo mengi. Hivyo naishauri Serikali kuwatengea maeneo maalum madhehebu hayo ya kuendeshea shughuli zao za ibada.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa wasilisho zuri, lakini pamoja na hilo, bado kuna changamoto kadhaa ambazo zinahitajika zaidi kuangaliwa na kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, nianze na vitambulisho vya uraia. Ni haki ya kila Mtanzania kupata kitambulisho hiki ambacho kimekua ni mojawapo ya sifa za kupata baadhi ya huduma za muhimu kabisa. Upatikanaji wake umekuwa ni changamoto sana. Ili kufanya zoezi hili kuwa rahisi, kwa nini vitambulisho hivi visiwe zoezi endelevu mfano mashulenii, vyuoni, sehemu za kazi hata Ofisi za Kata kiasi kwamba mtu anapotaka kupata kitambulisho hiki ni zoezi jepesi kuliko iliyivo sasa. Pia mianya ya rushwa iangaliwe sana ili kuondoa uzoroteshaji wa zoezi hili. Elimu itolewe kwa wananchi jinsi ambavyo anaweza kupata kitambulisho na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni wageni wanaokuja katika nchi yetu kufanya kazi za mikataba. Watu hawa mara nyingi wanajenga mahusiano na Watanzania wanawazalisha, mwisho wa siku wanaacha watoto bila

malezi ya kueleweka na kuongeza watoto wa mitaani katika Taifa letu. Serikali iangalie inawasaidiaje hawa watoto wasio na hatia ili wapate malezi wanayostahili toka kwa wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, pia wengine wamekuwa wakifunga miradi yao ghafla na kuacha wale waliowaajiri katika wakati mgumu na kukosa stahiki zao ikiwemo michango yao ya kila mwezi kwa Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Mara nyingi kesi za namna hii zimekuwa zikichukua muda mrefu sana na hivyo kuwafanya waishi maisha magumu sana. Serikali iangalie ni namna gani inawabana katika mikataba yao ikiwemo aidha kuwa na bima ambazo *zita-take off* linapotokea tatizo kama hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine ni suala la bima hasa za magari. Unapokwenda kukata bima, kunakuwa hakuna milolongo wala kucheleweshwa kwa namna yoyote ile. Ila unapopata ajali sasa ndiyo balaa juu ya balaa. Inachukua muda mrefu sana na wakati mwingine hadi watu wanaghairi kufuatilia, jinsi usumbu unavyokuwa mkubwa. Mimi tayari nimepata ajali, sina usafiri na inachukua mwaka hadi miaka miwili mtu unafuatilia tu malipo. Sasa hamwon kama badala ya kumsaidia huyu mtu mwenye matatizo, tayari ndiyo kwanza unamwongeza gharama ambazo hata baada ya malipo anakua amepata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi shirikishi ni muhimu sana kwa jamii zetu. Serikali isisitize zaidi juu ya suala hili ikiwezekana kuwe na utaratibu rasmi wa kuhakikisha ulinzi shirikishi unafanyika ipasavyo. Tumeona kumekua na matukio ya wizi majumbani hasa vifaa vya magari na magari yenye we pamoja na matukio ya ujambazi na mauaji ambayo yanaweza kupungua zaidi au kutoweka kama suala la ulinzi shirikishi litawekewa mkazo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuiomba Serikali izidishe elimu hasa Zimamoto majumbani, maofisini na mashulenii ili kupunguza au kuondoa kabisa majanga haya ya moto, wakati huo huo pia mazingira ya kazi ya maofisa

wetu wa ulinzi yaboreshwe maana hawa watu ni muhimu sana kwa ustawi wa nchi yetu ili akili zao zitulie katika kazi ya ulinzi wa nchi yetu na wafanye kazi zao wakiwa na furaha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa Hotuba na Hoja iliyowekwa mezani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia eneo moja tu la hali ya usalama wa wananchi katika Mikoa inayopakana na nchi jirani hususan katika Mkoa wa Kigoma. Katika Mkoa wa Kigoma kuna mwingiliano wa wahamiaji/wageni haramu ambaao mara kwa mara wanavuka mpaka wa nchi na kuingia nchini wakati mwingine wakiwa na silaha, tena za kivita. Wakati mwingine wahalifu hawa wanaingia nchini kwa kisingizio cha kufanya vibarua mashambani na baadaye wanafanya uhalifu. Uhalifu wa mara kwa mara ni pamoj na kuteka magari, kuua na kuwaibia mali abiria, kuvamia nyumba, kuiba na kubaka wanawake na wasichana na kufanya uhalifu mwingine.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimekuwa nafanya mawasiliano ya mara kwa mara na Mheshimiwa Waziri ili kuonesha uzito wa tatizo. Kwa kuwa wahalifu wanavuka mpaka tena wakiwa na silaha, nashauri Wizara yake ishirikiane na Wizara ya Ulinzi na JKT kudhibiti wahalifu kuvuka mpaka wa nchi wakiwa na silaha. Aidha, pale ambapo wahalifu wanafanikiwa kuvuka na kuingia nchini, Wizara yako iangalie uwezekano wa kuanzisha Kanda Maalum ya Kipolisi itakayodhibiti maeneo korofi hususan katika Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Ngara, katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyomweleza Mheshimiwa Waziri tulipokutana katika kikao chake na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Mkoa wa Kigoma, kuna kila dalili kwamba wageni na wahamiaji haramu wanaofanya uhalifu wana ushirikiano mkubwa na wananchi wenyeji wa maeneo

husika. Naishauri Wizara itumie ujuzi na pengine kuwaruhusu wananchi kufanya/kupiga kura za siri ili kuwabaini wananchi wanaoshirikiana na wahalifu kutoka nje. Naamini Wizara ina wataalam wa kuendesha zoezi hilo kwa ufanisi bila kuathiri wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Wana Namtumbo wanafurahia utendaji wao na wanaomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wanachi wa Namtumbo wanaomba wapewe Vitambulisho vya Taifa, maana taarifa zao na picha vimechukuliwa muda mrefu sana lakini hawaoni matokeo.

Mheshimiwa Spika, lingine, baadhi ya Askari Polisi wasio waaminifu wanaodai hawajalipwa haki zao wanawanyanya wakazi wa Namtumbo kwa kuwabambikizia kesi na kwa waendesha bodaboda kushikwa mara kwa mara na kutakiwa walipe faini bila kosa lolote. Mtusaidie tuishi kwa amani bila bugudha ya baadhi ya Maaskari wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, Polisi wanatumika vibaya na *WMA* ya Mbarang'andu na Kimbanda kwa kuwanyanya wakazi wa Namtumbo wanaoishi karibu na maeneo ya Hifadhi za Jamii (*WMA*) kwa kuwapa adhabu za kuwatweza utu wao na kutakiwa kulipa faini ama tozo za malaki na mamilioni ya shilingi eti kwa sababu wamekutwa majumbani mwao wamepika samaki au uyoga wakidai lazima watakuwa wameingia kwenye maeneo ya Hifadhi za Jamii kinyume na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nashauri Polisi wasitumike kwa operesheni za aina hii, badala yake hizo *WMA* zjisimamie zenyewe. Polisi walipwe stahiki zao kwa wakati ili

wasirubuniwe na viongozi wa *WMA* wanaowalipa posho zinazotoka kwa *NGO* za Kimataifa ambazo zina dhamira mbaya za kuwagombanisha wananchi na Serikali yao inayoongozwa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, kwa kuanza kabisa, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Kigoma maeneo ya Wilaya ya Kibondo, hali ya usalama bado siyo nzuri. Hakuna utulivu pamoja na Serikali imejitahidi lakini bado matukio yapo ya mara kwa mara. Naomba Serikali ituwekee Mkoa Maalum wa Kipolisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

MHE. SHAMSIA A. MTAMBA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima. Naomba Askari wetu waongezewe mishahara katika bajeti hii kwani wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, usiku na mchana, jua lao mvua yao. Kwa hiyo, naishauri Serikali iwaangalie Askari wetu hawa waongezewe posho kwani hali ya maisha ni ngumu sana. Posho ya shilingi 300,000/= kwa mwezi ni ndogo sana, haitoshi. Ina maana Askari huyu pamoja na familia yake inabidi atumie shilingi 10,000/= kwa siku kuanzia asubuhi mpaka jioni. Je, itamtosha Askari huyu? Hali hii inasababisha Askari wetu wajihushe na masuala ya rushwa ili wakidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, nyumba wanazoishi Askari wa Magereza ni aibu, nyumba za Polisi Mtwara ni za tangu enzi za mkoloni na hazijaboreshwa. Jengo la Kituo cha Polisi cha Mtwara ni chakavu, kuta zina nyufa, hali inayosababisha kuwa na hatari kwa Askari wetu na wanaweza kuangukiwa na jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, tunaomba Jeshi la Polisi lisitumike vibaya kwenye masuala ya kisiasa. Jeshi hili lifanye kazi yao kwa weledi bila kuegemea upande wowote.

MHE. OMARI A. KIGODA: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali inayoongozwa na Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Waziri wake Mheshimiwa Kangi Lugola kwa ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, hali za Magereza yetu nchini ni mbaya, lazima kuwe na mkakati wa kufanya ili kunusuru hali hii. Ndani ya Magereza kuna wafungwa wenye vipaji vyao ambao wanaweza kutumika kama sehemu ya uzalishaji na sehemu ya kipato. Mfano, kuna wafungwa wenye taaluma ya *carpenter* (*utengenezaji wa furniture*), wengine ni wajenzi. Hao hao wangetumika kwenye matengenezo ya *furniture* za Magerezani au hata ujenzi wa ndani lakini pia *furniture* zingeuzwa kwenye Taasisi za Serikali ili waweze kupata mapato. Hii ingesaidia sana kuongeza hela ya bajeti mnayoomba, ingesaidia kwenye matatizo mengine kama kununua vitendea kazi kwa ajili ya wale wenye vipaji vyaa kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, hii ingetumika kwa taasisi zote kwa kuwa hata Polisi wapo wenye vipaji vyaa ujenzi, wawezeshwe kwa kupatiwa vifaa. Hizi nyumba tunazolalamika wanaweza kuzijenga wenyewe kwa kiwango kizuri. Tutumie sana vipaji vyao kuzalisha na kuingiza vipato. Ni aibu mtu anasimama hapa anaombea Askari mafuta. Tubadilike, hizi hela zinazopatikana zipelekwe kwenye maeneo ya uzalishaji na kuiwekeea mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, tuzipe hizi taasisi uhuru wa kuonesha vipaji vyao katika maendeleo na kuiweka wenyewe katika mazingira mazuri. Tuachane na mawazo ya kunufaisha watu wengine kwa kutumia neno tenda. Taasisi hizi zina uwezo wa kufanya vitu wenyewe na kuleta tija, tuwape nafasi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ASHA MSHIMBA JECHA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha majengo ya vituo vya Polisi na nyumba za makazi kwa Askari wetu. Naomba Serikali kutukamilishia ujenzi wa Kituo cha Polisi Dunga ambacho kinahitaji kiasi cha shilingi milioni 50 kwa matengenezo ya ndani; kuweka sakafu, madirisha, milango, plasta ya ndani na nje, *hard board* na uzio.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Makunduchi, nyumba za makazi ya Askari wa kawaida hali zake ni mbaya sana, mbovu. Tunaomba majengo hayo yajengwe upya.

Mheshimiwa Spika, naomba Maaskari wetu wapatiwe posho na stahili zao kwa wakati. Wapo Askari wameziomba posho hizo kwa kuandika barua, na katika ziara ya Mheshimiwa Waziri na Naibu pia, Askari wameziwasilisha changamoto hizo lakini hakuna hatua yoyote ya mabadiliko na hawajapatiwa hadi leo. Mbaya zaidi kuna Askari wameajiriwa mwisho kuliko wengine, tayari wamepatiwa posho hizi. Mfano, mwaka 2004 hawajapata posho lakini 2006 anapatiwa posho, wakati kazi yao ni moja, vyeo sawa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wapo Watanzania wengi hawajapatiwa Vitambulisho vya Taifa na wanashindwa kujitafutia fursa na kuzitumia kwa wakati stahiki. Basi tunaomba vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi vitumike katika kuzifikia fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Spika, mazingira ya kufanyika mikutano ya hadhara kwa Vyama vya Upinzani inaonekana kukataliwa na kutoruhusiwa mara nyingi na Jeshi la Polisi. Hivyo, kitendo hiki kinanyima fursa ya kidemokrasia kwa kukandamiza uhuru wa Vyama vya

Upinzani. Je, Polisi sasa wana mkakati gani wa kuondokana na dosari hii?

Mheshimiwa Spika, msongamano wa mahabusu na wafungwa kwenye Magereza bado ni mkubwa na hii inatokana na upelelezi kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kesi ya Mashehe wa Uamsho imechukua muda wa miaka sita sasa bila kujua hatma yao ni ipi, kwani hadi leo upelelezi haujakamilika. Ninaomba jambo hili vyombo vinavyohusika hasa wanaotafuta upelelezi lifanywe haraka ili haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupatikana kwa vitambulisho vyya Mtanzania bado haujaridhisha, kwani unaonekana ni ndoto kwamba hadi kufikia 2020 kupatikana kwa vitambulisho hivyo kwa Watanzania wote. Ninashauri Serikali iongeze mtambo wa kuzalisha Vitambulisho vyya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ubovu wa Kituo cha Konde, Pemba unatisha. Mvua zikinyesha maji yanahatarisha afya ya Askari. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati kituo hicho na Kituo cha Matongatuoni, Pemba ambacho ni kibovu?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mungu, Muumba wa Mbingu na Dunia kwa kuniwezesha nami niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2019/2020. Hotuba hii inakwenda kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoelekeza na kuhakikisha hali ya usalama kwa raia na mali zao unakua wa uhakika. Aidha, nichukue nafasi hii kwa mara nyingine tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa juhudhi kubwa inazoendelea kufanya kwa majeshi yetu

ya Polisi, Uhamiaji, Zimamoto pamoja na Magereza. Serikali imeendelea kufanya maboresho mbalimbali hasa kwa Askari wetu, makazi yao pamoja na mambo mengine mazuri yenye tija kubwa hasa katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao. Serikali imeendelea kudhibiti hali ya ulinzi na usalama nchini kwa kuboresha mazingira ya kuishi Askari na kufanya kazi, kutoa huduma bora za kubaini, kutanzua na kudhibiti uhalifu, kudhibiti vitendo vya rushwa ndani ya Jeshi la Polisi pamoja na kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kupambana na uhalifu nchini. Haya ni mambo mzuri ya kujivunia hasa katika kipindi hiki. Aidha, hali hii imechangia kupunguza makosa ya kiuhalifu kutoka makosa 37,602 mwaka 2017 hadi kufikia makosa 36,228 mwaka 2018.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kwa upande wa uhamiaji Serikali inatekeleza kwa mafanikio makubwa awamu ya pilii ya Mradi wa Uhamiaji Mtandao, ambayo inahusisha utoaji wa huduma ya viza pamoja na vibali vya ukaazi vya kielektroniki. Mradi huu ni wa kisasa kabisa na unaendana kabisa na dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile naipongeza Serikali kwa kuzindua mfumo huo hapo mnamo tarehe 26 Novemba, 2018, ambapo sasa unamwezesha mteja kufanya maombi yake kwa njia ya mtandao kama wafanyakyo nchi nyingine zilizoendelea. Hakika mfumo huo, utarahisisha utoaji wa huduma bora za uhamiaji, kuimarisha ulinzi na usalama, kuongeza udhibiti wa wageni wanaoingia nchini, ukusanyaji wa maduhuli ya Seriklai na kuchochaea kasi ya maendeleo ya kiuchumi kupitia sekta ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuendelea kuwawezesha Jeshi letu la Zima moto kwa kuwapa vifaa zaidi kama magari ili pindi yanapotokea matukio ya moto iwe rahisi kuyahimili. Pia naishauri Serikali kuangalia upya namna ya kuwatumia wafungwa waliopo Magerezani ili wawe wanazalisha kama alivyowahi kusema Mheshimiwa Rais wetu, wafungwa hawa watumike katika kuzalisha vitu mbalimbali kama mazao. Baadhi wana taaluma zao, pia wazitumie kuleta faida kwa jamii wakiwa huko huko Magerezani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutambua umuhimu wa usalama wa raia pamoja na mali zao, kama mdau mkubwa, nimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha vituo vya Polisi katika Jimbo langu vinajengwa. Nami kwa kushiriki kwa hali na mali na kuchangia mambo mbalimbali yanayohusu sekta hiyo kama ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari wetu, kukarabati gari la Polisi, tumejenga baadhi ya vituo vya Polisi kwa nguvu zetu wenyewe, lakini bado havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu sikuvi katika bajeti hii kwa umuhimu wa jambo hili sasa watusaidie kumalizia ujenzi wa vituo hivyo ili vianze kuwahudumia wananchi wangu. Tukifanikiwa kumalizia vituo hivyo, kwa kiasi kikubwa hali ya usalama Jimboni kwangu itazidi kuimarika. Aidha, tuna changamoto ya gari la Polis. Uhitaji wa chombo hicho ni muhimu kwani gari lilitopo halitoshelezi kuhudumia Jimbo zima. Tukipatiwa gari litasaidia kufanya doria za mara kwa mara ikizingatiwa Jimbo letu ni kubwa kiutawala.

Mheshimiwa Spika, naleta tena ombi hili kwa Serikali yangu sikuvi kutusaidia gari la Polisi katika bajeti hii. Halikadhalika, tumekuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji na kupelekea maafa. Nakuomba Mheshimiwa Waziri aje Jimboni kwangu kututembelea na kutatua changamoto iliyopo ambayo inahusisha pia na Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, bado tuna changamoto ya nyumba za Polisi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho aweze kutupatia majibu ya maombi yetu na changamoto nilizoiainisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Spika, awali naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kangi A. Lugola. Pia nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Masauni kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba bajeti inayopitishwa ifike kwa wakati ili kuweza kutekeleza shughuli ambazo zimepangwa kufanyaika katika kipindi cha mwaka 2019/2020 ili kufikia malengo yaliyopangwa kufikiwa. Upelelezi wa kesi mbalimbali nashauri ukamilike kwa wakati ili kuweza kuondoa msongamano wa watuhumiwa katika Magereza na mahabusu nchini.

Mheshimiwa Spika, Vitambulisho vya Taifa vinachukua muda mrefu hadi mwananchi kupata. Nashauri huduma hii ya utoaji vitambulisho iboreshwe ili kuharakisha; kila Mtanzania anayestahili kupata kitambulisho hiki, apewe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri Jeshi la Zimamoto lipatiwe vifaa vya uokoaji vya kutosha na vya kisasa ili kuweza kuharakisha uokoaji pindi majanga mbalimbali yatokeapo yaweze kushughulikiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iboreshe nyumba za Askari ili kuweza kuwa na makazi bora na ya kisasa zaidi maana nyumba zilizojengwa kwa mabati (*full suit*) zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali kwamba kwa wanawake wafungwa wanaojifungua katika Magereza wapewe muda maalum wa kuwatunza watoto wao, pia wapunguziwe kazi ili kuweza kupata nguvu baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ipunguze gharama za hati za kusafiria (*passport*) maana sio Watanzania wote wana uwezo wa kughamaria kupata *passport* na ukizingatia *passport* ni haki ya kila Mtanzania bila kujali uwezo wake wa kipato.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa Polisi Jamii. Sungusungu wengi hawana mafunzo na elimu ya kutosha katika kutekeleza majukumu yao ya kila

siku. Hivyo hupelekea migogoro na wakati mwingine husababisha mauaji kwa watu wasio na hatia.

Mheshimiwa Spika, nashauri elimu itolewe kwa wanachi ili kuondoa mila potofu za kuua watoto, vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi kwa njia ya kujipatia utajiri.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ijenge na iboreshe vituo vya Polisi ili kukidhi mahitaji. Pia kuwe na vitendea kazi hususan magari ili waweze kufika katika matukio kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na msongamano mkubwa katika vituo vya Polisi. Kutokana na shughuli za upotevu wa simu ili mwananchi kupatiwa *Loss Report* lazima aende Polisi. Hivyo, naishauri Serikali ianzishe kitengo maalum cha kushughulikia wananchi wanaokuja kuchukua *Loss Report* hususan za simu. Maana watu hujazana *CRO* na kusababisha wananchi wenye mahitaji ya dharura kushindwa kuhudumiwa kwa wakati, mfano, Dar es Salaam. Pia kiusalama katika vituo hivyo inakuwa siyo nzuri watu wa aina mbalimbali hujazana eneo moja kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namwomba Mungu azidi kuwapa afya njema Mheshimiwa Kangi na Naibu wake Mheshimiwa Masauni, pia umri mrefu katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru wewe na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kutoa mchango wangu katika hoja hii muhimu kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha 2019/2020 hali ya usalama wa raia na mali zao umeimarika. Pamoja na changamoto zilizojitokeza za mauaji ya watoto na kupotea kwa watoto katika Mikoa ya Njombe na changamoto za hapa na pale ambazo hazijakatisha tamaa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, kulinda raia na mali zao na wote tunaotambua na kuthamini kazi kubwa mnayoifanya,

tunawatia moyo endeleeni kuchapa kazi. Watanzania walio wengi wanawaunga mkono na kuwaombea dua njema. Taarifa imeandaliwa na Mheshimiwa Waziri na timu yake, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani; pamoja na kuipongeza Serikali kwa kupeleka fedha kwa kiwango cha zaidi ya asilimia 86, nashauri fedha ya Wizara hii ipelekwe yote na bajeti iongezwe kwa sababu majukumu ya Wizara hii ni muhimu na nyeti kwa usalama wa raia, mali na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Askari Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Serikali yetu kuhakikisha inaboresha maslahi ya Askari wetu kwa kuwapa mishahara bila kukosa, kuwapa posho ya chakula, nyumba na kadhalika bado tatizo kubwa lillipo ni maslahi ya Askari wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali itazame upya mambo yafuatayo:-

(a) Mishahara ya Askari iongezwe;

(b) Posho ya chakula iongezwe na itolewe kila inapofika tarehe 15 ya kila mwezi kuliko inavyotolewa sasa mwisho wa mwezi;

(c) Posho ya nauzi za likizo na safari za kikazi kwa Askari zilipwe kwa wakati kama inavyofanyika kwa watumishi wengine;

(d) Vitendea kazi kwa Askari wetu, mfano, *uniform* kwa sasa baadhi ya Askari wanunuwa wenyewe. Hili liangaliwe na zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya kununua nguo za Askari Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto;

(e) Stahiki za Askari wanapostaafu zitolewe mapema ili kuondoa usumbufu kwa Askari wanaokaa muda mrefu bila kulipwa stahiki zao. Napendekeza taratibu za malipo na kila

anachostahili Askari kupewa, kiandaliwe mapema kabla ya Askari kutoka kazini;

(f) Askari Polisi anapofiya na ndugu wa karibu kama vile baba, mama, mke au mume, Askari hapati fedha ya rambirambi kama ilivyo kwa watumishi wengine; na

(g) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa rambirambi kwa Askari anayefiwa na ndugu wa karibu kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine.

Mheshimiwa Spika, makazi ya Askari Polisi, Magereza, Zimamoto na Uhamiaji. Pamoja na kuipongeze Serikali kwa ujenzi wa makazi na vituo vya Polisi na pia kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli mnamo tarehe 7 Aprili, 2018 wakati akizindua nyumba za Askari Mkoani Arusha, alitoa shillingi billioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Askari ngazi ya chini ambayo fedha hiyo imesaidia kujenga nyumba 400 katika mikoa mbalimbali kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye hotuba yake. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, Serikali iandae mpango mkakati wa kujenga nyumba za Askari kwa kutumia rasilimali watu iliyopo katika Taasisi hizi kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo. Serikali ifufue kitengo cha ujenzi kilichopo katika Jeshi la Polisi na Magereza na kuwatutia wataalam wa ujenzi waliosajiliwa na Bodi ya Wahandisi; licha ya uchache wao wangeweza kusaidia kuboresha hali ya majengo kuititia kikosi cha ujenzi cha Polisi au Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi; lakini wafungwa wanapangiwa kazi za jumla vituoni (*general duties*) na Askari wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali itoe fedha tuweze kujenga nyumba za Askari kama ilivyo kuwa miaka ya nyuma. Askari Polisi na Magereza walijenga nyumba zao wenyewe kwa kutumia rasilimali fedha kidogo na rasilimali watu katika taasisi hizo. Swali, pia ningependa kujua kama Askari analipwa posho ya nyumba; na ni kwa asilimia ngapi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza utaratibu unaotumika wa kuwapandisha vyeo Askari Polisi, bado lipo tazito la baadhi ya Askari kutopandishwa vyeo kwa wakati, jambo ambalo linaleta manung'uniko yasiyo ya lazima kwa baadhi ya Askari. *PGO* ya Jeshi la Polisi inaeleza, Askari atapandishwa Daraja/cheo kila baada ya miaka mitatu endapo Askari anatimiza masharti kwa mujibu wa *PGO*.

Napenda kujua ni kwa nini wapo Askari ambao wanatimiza masharti ya *PGO* mpaka sasa wamekaa muda mrefu bila kupandishwa vyeo na wengine wanakaa kwenye cheo kimoja miaka zaidi ya mitatu hadi miaka 10 na wengine mpaka wanastaifu?

Mheshimiwa Spika, pia masharti ya upandishaji wa vyeo yamekuwa yakibadilika tofauti na Uhamiaji na Magereza. Hapa napenda kujua, sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, Serikali imejenga *blocks* sita za makazi, ghorofa tatu zinazokaliwa na jumla ya familia za Askari 24 kutoka mikoa ya Mwanza, Bukoba na Musoma bado hazijakamilika toka mwaka 2010. Napenda kujua nyumba hizi zitakamilika lini ili Askari Polisi waweze kuishi humo na hasa kwa kuzingatia kuwa walibomolewa nyumba walizokuwa wakiishi? Pia Jeshi la Polisi lilikuwa na mpango wa kujenga mahanga katika kila Mkoa wa kuishi Askari wapya 96 katika baadhi ya Mikoa michache tu ila mahanga hayajengwa. Napenda kujua je, mahanga yenye uwezo wa kubeba Askari wapya 96 kila Mkoa yatajengwa lini?

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ofisi za Polisi Mkoa na Wilaya ambazo hazijakamilika katika mikoa mbalimbali?

Mheshimiwa Spika, kuna vituo vya Polisi vimejengwa kwa nguvu za wananchi katika maeneo mbalimbali; mfano, Kituo cha mpakani mwa Malawi na Soko la lleje na Kituo cha Malimbe Mwanzo: Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga mkono nguvu za wananchi ili vituo hivyo viweze kukamilika na kutumika? Jeshi la Polisi lilianzisha mpango wa kujenga

nyumba za Askari katika baadhi ya Mikoa na Ofisi za Mikoa na Wilaya. Napenda kujua mpango huu umekwamia wapi?

Mheshimiwa Spika, swali, nyumba za Askari Mkoa wa Mara hazijakamilika na kutumika, tatizo ni nini? Nyumba za Askari Mkoa wa Mwanza hazijakamilika, tatizo ni nini? Ofisi mbalimbali zimeanzishwa, zimeisha kwenye misingi tu kama Manyara na Mara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Spika, zoezi la Vitambulisho vya Taifa kwenye Jimbo la Mikumi, zoezi la uandikishaji wa hivi vitambulisho vya Taifa limesimama kabisa. Jimboni Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla watu walishalipa fedha zao, shilingi 500/= kila mmoja lakini mpaka leo bado hawajapewa Vitambulisho vyao vya Taifa na mbaya zaidi hili tamko la Serikali kuhusu kusajili namba zote za simu nchini ukiwa na kitambulisho cha Taifa imeleta sintofahamu kubwa sana kwa wananchi wetu na Watanzania kwa ujumla. Naomba Waziri wa Mambo ya Ndani akija kuhitimisha atoe kauli ya Serikali kuhusu zoezi hili la vitambulisho na usajili wa namba za simu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, upotevu wa wananchi kumi wa Kijiji cha Ruhembe Jimbo la Mikumi; niliripoti Bungeni na kwenye vyombo mbalimbali vya usalama na vyombo vya habari kuhusu watu 10 waliopotea wakiwa pembezoni wa Hifadhi ya Mikumi, lakini mpaka leo tarehe 24 bado hakuna majibu ya Serikali kama hawa watu ni wazima, wamekamatwa au wamekufa tangu walipopotea tarehe 2 Aprili, 2019. Je, Waziri wa Mambo ya Ndani na vyombo vyake vya ulinzi na usalama wanatoa kauli gani juu ya upotevu wa ndugu zetu hawa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa na migogoro mfululizo ya wakulima na wafugaji Wilayani Kilosa, Serikali iliahidi kujenga vituo vya Polisi kwenye Kata za Tindiga, Ulaya, Kilangali, Malolo na Mabwerebwere: Je, Serikali itatimiza lini

ahadi yake hiyo ya kulinda wananchi na mali zao kwenye kata hizi?

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Mikumi ni muhimu sana na kina kazi kubwa sana ya kulinda wananchi wa Tarafa nzima ya Mikumi yenyе Kata saba za Mikumi, Malalo, Uleling'ombe, Mhenda, Ulaya, Kisanga na ukizingatia Mikumi ni Mji Mdogo wa Kitalii na idadi kubwa sana ya watu, kituo hiki hakina gari ya doria na mbaya zaidi *Cell* yao ni ndogo sana. Hakuna choo na mpaka leo watuhumiwa wanajisaidia kwenye ndoo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri akitupie jicho la huruma kituo hiki cha Mikumi ili Askari wetu wawze kufanya kazi yao kwa weledi na watuhumiwa wapate haki yao ya mazingira salama.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa masikitiko makubwa nimepitia hotuba ya Wizara hii lakini sikuona mahali ambapo wamepongeza jitihada za wananchi wa Kata ya Mtae, Tarafa ya Mtae Wilaya ya Lushoto ambao kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wameweza kukarabati jengo la Serikali ya kijiji na kuwa Kituo Kidogo cha Polisi katika Tarafa. Wananchi kwa kushirikiana na Mbuge pamoja na Kamanda wa Polisi Mkoa na Wilaya kwa pamoja kituo kimeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, vilevile kwa kuzingatia utawala bora na utawala unaozingatia sheria, wananchi wa Mtae wamewapatia nyumba ya kuishi familia mbili za Askari kati ya watatu waliopo katika eneo la kituo hiki. Napenda kuona Wizara hili ikitoa japo neno la shukrani kwa wananchi hata kama ni wajibu wao katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi Mbunge wa Mlalo na timu yangu kupitia Mfuko wa Jimbo tumeweza kuchimba kisima katika Gereza la Kilimo Mng'aro ambalo lina uhaba mkubwa wa maji. Tumeweza kutumia takribani shilingi milioni 20 kuwawekea kisima kirefu pamoja na tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 5000. Tunatamani kuona Wizara ikishirikiana nasi katika kuboresha miundombinu ya Gereza hili ambalo

limejengwa kwa tope na miti. Tunaomba Wizara itembelee Gereza hili la Kilimo cha Mpunga na Mbogamboga lenye uwezo wa kulisha wafungwa walioko katika Magereza ya Mkoa wa Tanga kwa asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, bado jengo la Polisi katika Makao Makuu lipo katika hali mbaya na ujenzi wa jengo jipya ulisimama kwa muda mrefu. Tungependa kuona ni kwa kiasi gani jambo hili linafikia mwisho.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda pia kushauri kuhusu Katibu Mkuu wa Wizara hii kusimamia mafungu mengi, hivyo kushindwa kuleta ufanisi katika Wizara hii. Afisa Masuuli wa Wizara hii ambaye ni Katibu Mkuu anasimamia Idara ya Uhamiaji, Idara za Zimamoto, Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi pamoja na *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe haya kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mlalo, basi angalau Wizara hii iweze kuwaunga mkono katika jukumu hili zito la ulinzi wa raia na mali zao.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu vifo vinavyotokana na ukatili wa Jeshi la Polisi. Hivi karibuni kumekuwa na matukio ya wananchi kunyanyaswa na baadhi ya Polisi na kuripotiwa katika maeneo mbalimbali. Mfano, Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Vlijini (Tanganyika) amekuwa akitumia baadhi ya Askari kunyanyasa wananchi wa Tanganyika. Wananchi wanawekwa ndani (rumande) wanabambikiziwa kesi mbalimbali, wanachomewa nyumba kwa maelekezo ya Mhando.

Mheshimiwa Spika, mmoja kati ya wananchi waliopigwa risasi na Askari na kufa anaitwa Shinje, Aprili, mwaka 2018. Jambo hili na mengineyo yanayoendelea kutokea katika mkoa wetu, yanachafua Jeshi la Polisi, lakini pia Serikali kupitia Jeshi la Polisi inashindwa kulinda mali za raia wake na usalama wao. Hii inapelekea watu kutokuwa na imani na jeshi la polisi.

152Mheshimiwa Spika, nataka Mheshimiwa Waziri akija hapa, ajibu ni kwa nini baadhi ya Askari wanafanya uovu na hawachukuliwi hatua; Wakuu wa Wilaya hawa Mheshimiwa Mhando wa Tanganyika na Mkuu wa Wilaya ya Mpanda? Je, sheria za kutoa amri kwa Polisi kuwakamata raia wanatoa wapi wateuliwa hawa? Jambo hili linakera na lisipofanyiwa kazi linaenda kuleta athari kubwa.

Mheshimiwa Spika, kingine ni kuhusu upotevu wa mali za raia katika vituo, vifaa nya raia vinavyokamatwa na Polisi, pikipiki, TV, Redio vitu vingine. Hii imekuwa ni kero kwa sababu unakuta mtuhumiwa anakamatwa; ushahidi na kesi inaenda Mahakamani, lakini baada ya muda vitu nya ushahidi vinapotea, vinauzwa au unakuta mali za wananchi ziko mtaani. Mheshimiwa Waziri ajibu, hili linakera na kuchafua Jeshi hili ambalo linatumika vibaya na baadhi ya Polisi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini *RCO*, Wakuu wa Vituo wanazuia Mikutano ya Hadhara na huku Polepole anaachwa akifanya mikutano ya ndani na nje? Intelijensia inapatikana kwa viongozi wa Upinzani tu ila kwa CCM hawapatikani na taarifa za intelijensia ambazo ni mbaya.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna Tarafa tatu, Kata 15, vituo nya Polisi vinavyofanya kazi ni viwili tu. Kwa kuzingatia kuwa Tunduru Kusini inapakana na Mto Ruvuma katika mpaka wa Msumbiji. Hivyo, tunaomba Kituo cha Polisi katika Kata ya Lukumbule, katika eneo la Lukumbule pamoja na Kituo cha Uhamiaji ili kudhibiti watu wa Msumbiji wanaoingia Tanzania bila kufuata utaratibu na sheria za nchi. Vilevile tunaomba Kituo cha Polisi katika Kata ya Misechela, Kijiji cha Misechela na katika Kata ya Namasakata katika Kijiji cha Namasakata ili kuwarahisishia katika Kata ya Mchateka ambayo ina idadi kubwa ya wakazi. Tunaomba kituo cha Polisi katika Kijiji cha Mchateka Katili ili kuhudumia wananchi

wa Kata hiyo. Lengo la kuomba Vituo hivi vya Polisi ni kupunguza kero kubwa kwa wananchi kutembea mwendo mrefuata huduma ya Kipolisi.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Namasakata hamna hata kituo kimoja cha Polisi. Tarafa hiyo ina Kata tano yaani Ligoma, Misechela, Tuwemacho, Mchuruka na Namasakata na hamna kituo cha Polisi hata kimoja. Huduma ya Kipolisi wataipata Makao Makuu ya Wilaya ya Tunduru Mjini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na vituo vya Polisi, tunaomba vituo vya Uhamiaji ili kupata huduma za *visa* kwani maeneo niliyotaja yamepakana na Msumbiji hivyo kuna mwillingiliano wa wananchi wa Msumbiji na Tanzania, lakini wananchi wa Tanzania wakienda Msumbiji wanapata shida sana kwa vile Askari wa Msumbiji wananyanyasa sana Watanzania kwa kuwapiga hatimaye kuwafunga na kuwanyang'anya mali zao wakati wao wakija Tanzania hawanyanyaswi hivyo. Kwa hiyo, tunaomba vituo vya Uhamiaji ili wananchi wa Tanzania wapate *visa* za kwenda Msumbiji kwa ukaribu zaidi badala ya kufuata Tunduru Mjini ambapo ni zaidi ya kilometra 80 kutoka mpakani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vituo vya Polisi, tunaomba Serikali kuangalia uwezekano wa kujenga nyumba za Askari katika Kituo cha Polisi Walasi na Kituo cha Polisi Masuguru ambaao karibu wote wanakaa uraliani na hata Askari walioopo Makao Makuu ya Polisi Wilaya hawana makazi ya kudumu. Kuna nyumba 300 za Polisi ziliungua moto miaka mitano iliyopita lakini hadi hivi leo nyumba hizo hazijajengwa. Tunaomba nyumba zile zijengwe ili kupunguza adha ya makazi kwa Askari wetu wanaofanya kazi katika mazingira magumu sana ya makazi kwa kuchanganyika na wananchi ambapo ni hatari kwa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, Serikali iongeze bajeti ya fedha kwa ajili ya kununua mafuta kwa ajili ya magari ya Polisi. Ni aibu kubwa sana kwa Jeshi la Polisi na Uhamiaji kuwa omboomba wa mafuta kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku na ndiyo maana Polisi wakiitwa mahali

kuna uhalifu hawafiki kwa wakati kwa sababu ya kukosa mafuta ya kufika eneo la tukio. Wakati mwингine wanalaзimika kuomba mafuta kutoka kwa mtoa taarifa ili waweze kufika eneo la tukio.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa kutayarisha na kuwalilisha kwa umakini vizuri hotuba hii. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, miradi ya ujenzi wa makazi, Ofisi na Vituo vya Polisi; napenda kuipongeza Serikali kwa kutambua na kuthamini uwepo wa upungufu wa makazi na ofisi/vituo vya Polisi katika nchi yetu. Hili ni jambo jema ambalo litasaidia kuwapatia utulivu Askari wetu na kuweza kufanya majukumu yao kwa ufanisi.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametuumba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika ujenzi wa miradi hii. Ushauri wangu katika suala hili ni kumwomba Mheshimiwa Waziri kututafuta Wabunge katika hatua za awali ili kutambua kwa pamoja maeneo husika. Kwa mfano, katika hotuba yake ukurasa wa 12 ametaja mikoa ambayo itajengwa makazi ya Polisi lakini mkoani eneo kubwa ambalo lina majimbo zaidi ya moja. Kwa hivyo, ni vyema Mheshimiwa Waziri angetaja sehemu maalum yanapojengwa ili kutambua ni Mbunge gani anahuksika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi; napenda kuipongeza Serikali kwa juhudzi zake inayochukua kwa kuendelea kuwatafutia vitendea kazi Maaskari wetu. Vitendea kazi ni chachu ya ufanisi mzuri wa kazi zao. Ushauri wangu katika suala hili ni kwamba, Serikali izidi kuwatafutia vifaa vya kisasa kutokana na ukuaji wa matendo ya uhalifu

vifaa ambavyo vitawarahisishia Askari wetu kuwatambua wahalifu kwa urahisi zaidi na kwa uhakika bila kubabaisha.

Mheshimiwa Spika, ajira kwa Maaskari; hivi sasa dunia inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kama inavyokabiliwa nchi yetu hivyo ni vyema Jeshi la Polisi likawa ni chanzo cha ajira katika nchi yetu. Ushauri wangu katika suala hili ni kwamba Serikali iwe makini sana katika kuchuja vijana ambaao wanaoajiri ili kuepuka kuajiri vijana ambaao hawana sifa na ambaao huku nje ni wahalifu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ni Wizara muhimu sana katika usalama wa raia na mali zao. Wizara hii inatakiwa Serikali kuwa na mikakati thabiti ya kutoa mafunzo kwa vijana wetu Askari ili kuwa imara kila wakati, kuboresha mazingira yao kwa kuwajengea nyumba, kupewa usafiri kama pikipiki, nyumba zao kuwekewa umeme, maji na kulipwa posho na kuongezewa mishahara yao. Pia kupandishwa vyeo kwa Askari hasa kitengo cha Polisi, Uhamiaji na Magereza, vyeo vyao vinachelewa sana, namaanisha kuwapandisha vyeo Askari wanaostahili kupandishwa. Naipongeza Serikali kwa kuwajengea nyumba Askari wa Uhamiaji wa hapa Dodoma. Hili ni jambo zuri sana kwa kuwajali Askari wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. MAKAME MASHAKA FOUM: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu kunijaalia afya njema, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ya kutekeleza majukumu ya kulijenga Taifa letu. Pia namshukuru Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, amani na utulivu tulionao ni kutokana na Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, watu wengi wanafanya makosa kutokana na kutozijua sharia, hivyo naiomba Wizara itumie njia mbalimbali za kuelimisha jamii ili iepukane na kutenda makosa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Magereza, naishauri Wizara kupanga mikakati na mipango mizuri ya kuhakikisha Jeshi la Magereza linazalisha chakula cha kutosha kujitosheleza. Sambamba na hilo wanayo maeneo mazuri kwa ajili ya mifugo. Naamini tunaweza kutoa maziwa, nyama na kadhalika kutokana na mifugo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pesa za maendeleo zipelekwe kwa wakati ili kutatua changamoto za majengo. Askari wetu wengi wanaishi katika nyumba duni, ili waweze kufanya kazi vizuri tuhakikishe wanapatiwa mazingira mazuri ya kuishi, Askari wetu wengi wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer Yussuf Masauni* kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya, naomba nipewe majibu sababu zipi zinasababisha askari wote wenyе cheo cha nyota moja kushuka chini wamewekewa ukomo wa kustaafu miaka 55. Hii sheria au kanuni haiwatendei haki askari hao; kwa nini Serikali isianganilie upya utaratibu huu na kuaweka katika utaratibu wa miaka 60 kama ulivyo kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya kupunguza ajali za barabarani hapa nchini bado ajali za pipipiki zinatishia uwepo wa vijana na nguvukazi ya Taifa. Kwa takwimu zilizopo kwa miaka 10 tu, watu waliopoteza maisha kwa bodaboda

ni 8,000, bado majeruhi, walemavu, yatima, wajane, wagane na jamii inayozunguka. Lazima Serikali kuja na mkakati mahsus i wa kupunguza/ kuondoa ajali za bodaboda zaidi ya mafunzo na elimu wanayotoa.

Mheshimiwa Spika, fedha inayotengwa kwenye vituo vya polisi kwenye wilaya zetu kuendesha shughuli za kila siku ni ndogo sana na kusababisha polisi kufanya kazi katika mazingira magumu sana. Polisi wanapewa lita tano za mafuta kwa siku kwa *patrol*/kwenye eneo kubwa kama Kaliua haiwezi kukidhi kabisa kazi zao kwa siku – matokeo yake matukio ya uhalifu yanatokea pembezoni, taarifa zinafika kituoni kwa muda lakini askari hawawezi kwenda kufuatilia kwa sababu hawana mafuta. Polisi wanaomba mafuta kwa watu binafsi au kwenye ofisi za halmashauri, wakipata waende, wakikosa wakae kimya. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha mafuta yapo?

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto kwenye wilaya nyingi hawana ofisi wala magari ya zimamoto, hawapo kabisa. Matukio ya moto yanatokea mara kwa mara nyumba zinateketea bila msaada wowote. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha wilaya zote zina ofisi za zimamoto na magari ya zimamoto yapo?

Mheshimiwa Spika, Wilayani Kaliua Jeshi la Magereza limechukua eneo la kujenga gereza la ekari 12 katika Kata ya Ushokora, Kijiji cha Pozamoyo kwa miaka sita sasa hakuna chochote pale kilichofanyika, hata watu waliohamishwa kwenye maeneo yao na kuacha mashamba yao hawajui hatma yao. Serikali ina mpango gani kuhusu eneo hili lilitengwa tangu 2012? Wananchi waliohamishwa maeneo yao nini hatma yao mpaka leo hawajui/ hawana pa kuishi, lini watalipwa fidia za maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, spidi ya utoaji wa vitambulisho vya uraia inakwenda taratibu sana na gharama za utekelezaji wa mradi huu zinaongezeka kila mwaka kwa namna ambayo muda unakuwa mrefu. Kwa kuwa mradi huu ultengewa fedha nyingi tangu mwaka 2012 kwa sababu ya umuhimu

wake na kuhakikisha Watanzania wanapata vitambulisho vya uraia. Serikali ieleze Bunge *time limit/time frame* ya zoezi hili muhimu kwa usalama na haki za raia wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi pekee ambayo mipaka yake mingi iko wazi na watu wa nje wanaingia kinyemela na wengi wanaishi humu ndani kama raia bila vyeti vya uraia. Wengine wamegombea nafasi za uongozi ndani ya nchi na wanaongoza watu leo. Vitambulisho vya uraia ndio mwarobaini wa tatizo hili, kila Mtanzania apate kitambulisho cha uraia.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na taasisi zake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, katika Nchi ya India kwa suala la usalama barabarani, wao ikifika saa tatu usiku huanza kuwakagua madereva wote ili kutambua kilevi kwa lengo la kuzuia vifo vingi vinavyotokana na ajali za barabarani wakati wa usiku. Kwa mfano huo wa Nchi ya India, naliomba Jeshi letu la Polisi liangalie uwezekano wa kuanzisha utaratibu huo wa ukaguzi wa kilevi kwa madereva wakati wa usiku ili kuzuia ajali nyakati za usiku ambazo nyingi zinasababisha vifo kutokana na ulevi wa madereva.

Mheshimiwa Spika, Madereva wa Serikali wadhibitiwe kwa kuendesha magari kwa kasi na kutoku-*overtake* sehemu za hatari.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nimechangia, lakini naomba tena kuchangia kwa maandishi hoja yangu ya mwisho ambayo sikutaka sana kuisemea kwa upana nilitaka kuandikia hapa na naomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, Mzee Ally Mwegango mkazi wa Kibirashi, Wilaya ya Kilindi ambaye alinunua gari kwa bwana Karl Muller kwa Sh.23,000,000 tarehe 7/7/2015 kwa akaunti namba 9120000187753 Benki ya Stanbic

na gari hii kukabidhiwa kwa Mzee Ally Mwegango . Tarehe 12/12/2017 gari hili lilikamatwa na Kampuni ya *COPS Auction Mart & Court Brokers* kwa maelekezo ya Benki ya *Redstone Financial Services*. Kimsingi muuzaji Mzee Karl Muller aliuza gari hili huku akijua amechukua mkopo kwenye *Financial Services*, kimsingi ni tapeli au mwizi. Jeshi la Polisi limeshindwa kuchukua hatua kwa mtu huyu na kumnyima haki Mzee Ally.

Mheshimiwa Spika, Mzee Ally huu ni mwaka wa pili sasa anafuatilia gari lake na lipo barabarani linafanya kazi. Nina imani kubwa sana na jeshi hili na pia naamini Mheshimiwa Waziri na wote waliopo chini yake wanalijua vema suala hili, hivi kama mimi Mbunge na mlalamikaji sote hatusikilizwi, hivi wanataka tuamini kwamba mhalifu huyo ana nguvu au yupo juu ya sheria?

Mheshimiwa Spika, ili kutenda haki kwa mlalamikaji Mzee Ally ambaye aliamini kabisa gari alilonunua lingemsaidia kujipatia riziki yake na familia, leo hii gari hili lipo kwenye mikono ya mtu mwingine, nina imani kubwa na nina uhakika suala hili linaweza kumalizika kwa kumkamata huyu tapeli au mwizi ambaye anafahamika wazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa ya kuchangia na uongozi mzuri huku Bungeni. Pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, /GPna Wakuu wote wa Majeshi yote, Zimamoto na Uokoaji, Magereza na Idara ya Uhamiaji kwa ufanisi mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo wizi wa magari umepungua sana, ajali barabarani zimepungua na hata wizi wa kuvunjiwa nyumba. Hizi zote ni juhudzi za Jeshi la Polisi, pongezi sana sana.

Mheshimiwa Spika, ombi, uongozi wa Jeshi la Polisi uone umuhimu wa kulipa deni kubwa la maji, linalodaiwa na Mamlaka ya Maji safi na Salama na Uondoaji wa Majitaka Moshi (*MUWSA*) Ref. Deni la *CCP-MSH*. Deni hili

limeshahakikiwa lakini ni zaidi ya miaka saba halilipwi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja alitolee maamuzi, la sivyo nitalazimika kushika shilingi kwenye mshahara wake japo sipendelei kabisa kufanya hivyo kwa Waziri makini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia. Niliuliza swalii kuhusu kutokuwepo kwa gereza lenye sifa ya kuwa gereza katika Wilaya ya Igunga. Gereza la Igunga halina ngome, hakuna gereza la wanawake na hulazimika kupeleka wafungwa wa kike kwenye Gereza la Wilaya ya Nzega. Gereza hilo pia halina nyumba za askari na halina ofisi za utawala. Kutokana na hali hiyo tunalomba Serikali itafute fedha za kufanya mambo yafuatayo:-

- (a) Ujenzi wa ngome;
- (b) Ujenzi wa jengo la utawala;
- (c) Ujenzi wa gereza la akinamama; na
- (d) Ujenzi wa nyumba za askari.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeanza kuwahamasisha wananchi na viongozi wa wilaya kuchangia ujenzi wa ofisi za utawala na nyumba za askari. Tunaomba sana Serikali ituunge mkono kwenye suala hili ili kuondoa adha wanayopata wafungwa na mahabusu katika Wilaya ya Igunga. Wilaya ya Igunga pia haina vitendea kazi kama magari na *computer* kwa ajli ya Jeshi la Polisi na hii inasababisha uduni wa huduma inayotolewa na Jeshi la Polisi. Wilaya ya Igunga ina vituo vya polisi katika Tarafa ya Manonga-Chome, Tarafa ya Simbo Simbo; Tarafa ya Igurubi, Igurubi; Tarafa ya Igunga, Igunga na Kituo cha Kata ya Nanga. Vituo vyote hivi vinahudumiwa na gari moja ambalo lipo katika Kituo cha Wilaya ya Igunga. Tunaomba Serikali

inunue magari kwa ajili ya Vituo vyote vya Polisi katika Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa viongozi wa Wilaya akiwemo *DC*, Mbunge, *DED* na wengine tumeanza mchakato wa kujenga Vituo vya Polisi vya Kata za Igunga (Mwanzugi) na Lugubu ili kukabiliana na ongezeko la watu katika maeneo hayo. Tunaomba Serikali ituunge mkono. Ahsante sana.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, kwa hekima na busara kubwa, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kushika kalamu na kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu kwa ustawi wa maisha ya jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kuwapongeza Mawaziri wote wanaohudumu kwenye Wizara hii sambamba na watumishi wote walioko kwenye Wizara hii. Pongezi za kipekee kwa askari wetu wa usalama barabarani kwa kazi nzuri wanayoifanya. Japo wapo askari wanaolitia doa Jeshi la Polisi kwa kupenda kwao vipesa vidogo vidogo, ushauri wangu kwa hao wachache wanaochafua jeshi letu ni basi wakadhibitiwa ipasavyo na pale wanapobainika basi adhabu kali iwe juu yao.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze kwenye makazi ya Askari Polisi na Magereza. Makazi ya askari wetu bado ni mabaya sana hassa kwa askari wa mikoani na kwenye magereza za pembezoni. Mfano, Wilaya ya Liwale ni wilaya ya tangu mwaka 1975 lakini hadi leo haina jengo la kituo cha polisi wala nyumba za askari licha ya halmashauri kutenga eneo zaidi ya heka 60. Jengo wananolitumia njengo la nyumba ya mtu binafsi. Kitendo cha polisi kukaa uraiani kunawapunguzia weledi wa kazi yao. Pamoja na hivyo lipopia Gereza la Kipule ambalo lilianzishwa tangu mwaka 1982 lakini hadi leo eneo linalomilikiwa na gereza hili halijalipiwa fidia toka kwa wananchi. Gereza hilo pia hadi leo lina majengo ya udongo na uzio wa miti na kufanya wale

wafungwa sugu au wa muda mrefu kulazimika kupelekwa Lindi.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi nya askari polisi; Wilaya ya Liwale imezungukwa na misitu, ni wilaya yenye mtawanyiko mkubwa lakini kuna uhaba mkubwa wa gari la askari polisi. Pamoja na mwaka huu kuletewa gari la *Canter* nalo ni kubwa linashindwa kuingia kwenye barabara za vijiji au vichochoroni. Hata hivyo napashwa kwa niaba yao nishukuru kwa hilo gari kwani ni hatua moja ya kutatua matatizo la usafiri kwa Polisi wa Wilaya ya Liwale. Ni matumaini yangu Serikali inaona umuhimu wa kuwa na gari la polisi sambamba na nyumba za askari.

Mheshimiwa Spika, katika Idara ya Uhamiaji bado kazi zao wanafanya kizamani sana, bado hawaendi na kasi ya Mheshimiwa Rais. Bado habari ya njoo kesho, njoo kesho ni nyingi hasa kwa raia wanaoomba uraia wa nchi yetu kwa wale wageni wa muda mrefu. Ni bora mwombaji apewe majibu mapema kama anaweza kupata au amekosa sifa za kupata uraia basi ni bora akafahamishwa. Kuacha kumpatia majibu kwa muda mrefu kunajenga mazingira ya rushwa. Ni bora Uhamiaji wakawa wazi kama mtu anakosa sifa za kupata hati ya uraia.

Mheshimiwa Spika, kikosi cha Zimamoto, ni kikosi muhimu sana kwa ulinzi wa mali zetu na ulinzi wa maisha yetu ya kila siku, lakini jeshi hili halijapewa umuhimu unaostahili. Jeshi la Zimamoto hawana magari ya kutosha na vifaa nya kukabiliana na majanga ya moto.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ziko wilaya ambazo hazina kabisa Jeshi hili la Zimamoto. Mfano Wilaya ya Liwale hakuna Askari hata mmoja wa Zimamoto na hivyo hata raia wa Liwale hawana uelewa wa kutosha juu ya kukabiliana na majanga ya moto, lakini wafanyabiashara bado wanalipa kodi ikiwemo ya zimamoto. Je, wanalipia huduma gani wakati hakuna ofisi ya zimamoto. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kuwa watu hawa wanalipia huduma ambayo hawatarajii kuipata?

Mheshimiwa Spika, mimi mpaka leo sioni faida ya watu kukaa magerezani kama wafungwa. Kwa nini wafungwa wawe mzigo kwa Taifa kwa kuwalisha bila wao kujitegemea. Nilitarajia kuona magereza yetu yakijitegemea, huko nyuma, magereza mengi yalikuwa na mashamba makubwa ya mazao ya chakula. Pia kulikuwa na viwanda vya kusindika mazao ya wakulima na kadhalika. Vilevile kulikuwa na viwanda vya mazao ya mifugo na uvuvi na mazao ya misitu. Kwa ushauri wangu kama magereza haziwezi kujitegemea hakuna haja ya kupeleka wafungwa magerezani na hivyo Serikali itafute njia nyingine ya kuwarekebisha wahalifu au wafungwa.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, katazo la mikutano ya Vyama vya siasa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa inasajiliwa kwa kuangalia vigezo toka mwaka 1992 tulipoingia kwenye mfumo wa vyama vingi, lakini tumeshuhudia kwenye Serikali ya Awamu ya Tano kumekuwa na zui o kwa vyama vya siasa kutimiza majukumu yao. Tunaomba Serikali itujibu inatumia sheria gani kuzuia mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, Askari kuwaadhibu wahalifu; Je, ni sheria gani inampa mamlaka Askari anapokuwa na mhalifu ambaye hajahukumiwa kuadhibiwa? Kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchijuu ya polisi pale wanapowakamata wahalifu jambo ambalo linaondoa upendo kati ya Jeshi la Polisi na raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti; Askari wa Usalama Barabarani kugeuka kuwa wakusanya mapato; hivi sasa kumekuwa na utaratibu kwa Askari wa Usalama Barabarani wakiwa na *EFD machine* na risiti muda wote, je, huo ndio mpango wa Wizara ili kuweza kumaliza ajali barabarani au ndiyo chanzo cha rushwa na kupelekea ajali zaidi?

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Polisi vinavyojengwa na nguvu ya wananchi; wananchi wamekuwa wakijitolea kujenga vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali nchini, lakini jitihada hizi za wananchi haziungwi mkono na Serikali

na kupelekea kuwavunja moyo wananchi hawa wanaojitolea.

Mheshimiwa Spika, vitambulisho vya Taifa; sio Watanzania wote ambao wamepata vitambulisho hivi, kwa hiyo jambo lolote litakalofanyika kwa sasa kwa kigezo cha kuwa na utambulisho litakuwa la ubaguzi, nashauri Serikali kwa kuwa bado kuna changamoto kwenye uzalishaji wa vitambulisho, Wizara iweke mkakati mahususi wa kuweza kumaliza changamoto hizo kwanza ili kuwapa haki wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la askari wenyе sifa na waliotimiza vigezo kupandishwa vyeo; kumekuwa na malalamiko kutoka kwa askari wanaojiendeleza kielimu kushindwa kupandishwa vyeo pale ambapo ameshajjiendeleza, suala hili linashusha moralikwa askari wetu kwani nao wana stahiki kupewa haki kama watumishi wengine nchini.

Mheshimiwa Spika, pesa za likizo; pamoja na uhamisho kwa askari wetu kumekuwa na malalamiko makubwa kwa askari kuhusu pesa za likizo na pesa za uhamisho, Wizara iangalie upya utaratibu wa kuwasaidia askari kuwapatia pesa hizo kwa kuwa ipo kisheria na ni haki zao.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Ulinzi na Usalama wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Kangi Lugola, Waziri na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Masauni, sisi Jimbo la Mbulu Vijijini tumejenga Kituo cha Polisi cha Yaeda Chini na kukimaliza kabisa tumebakia na nyumba za Walimu ili kituo kianzishwe hapo Yaeda Chini kwani wananchi wamejenga ili kupata usalama wa watu na mali zao. Sababu za kujenga kituo pametokea mauaji ya raia hapo nyuma bila watuhumiwa kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuna wizi wa mifugo ambao unaendelea, mifugo mingi imekuwa ikiibiwa na ikawaacha wananchi wakiwa hawana nchi zao ndiyo maana wameamua kujenga kituo cha polisi. Wanawake wengi wamekuwa wanabakwa sana hii ni kutokana na taarifa ambazo zipo. Ili kupunguza tatizo hilo tume ambazo zipo ili kupunguza tatizo hilo tumeamka kujenga kituo cha polisi ila tumeishiwa na nguvu za kuweza kuchangia hela na nyumba za askari tusaidieni hata nyumba moja. Mimi Mbunge nimechanga milioni nane za ujenzi wa kituo hiki cha polisi kushirikiana na wananchi. Ombi langu tupatiwe fedha za ujenzi wa nyumba za askari

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na kauli mpya tata na zenye ukakasi zinazotolewa na Jeshi la Polisi kwa siku za hivi karibuni; mfano, tutawapiga mpaka mchakae – *RPC Muroto*; tutapiga vifigo vya mbwa koko na nyingine zenye ukakasi kama hizo. Tafsiri ya kauli hizi ni ulevi wa madaraka, ubaguzi na kuwa juu ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kauli hizi hazisikiki tu kwa Jeshi la Polisi na hata kwa wanasiasa kama Mkuu wa Mkoa wa Tabora, akimtaka Mungu amshukuru Rais Magufuli na mengine kama haya. Ulevi wa madaraka, lakini kauli hizi zitafsiriwe kama zinaungwa mkono na Serikali ya Awamu ya Tano kwa kuwa, halamini tena katika *Government of the People for the People by the People*.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 28 – Polisi, limekuwa na upungufu mwingi sana katika matumizi ya fedha na haya yamesemwa na *CAG Report 2012/2013* mpaka leo hii. Mfano, zoezi la ujenzi wa vituo vya Polisi vya mfano chini ya mradi wa *STACA* uliodhaminiwa na Serikali ya Uingereza ukiwa na thamani ya zaidi ya *pound* milioni tatu (*Tsh. 10 billion*). Ujenzi wa hivyo vituo ulienda kinyume na *MOU*.

(1) *Budget ya estimates haikuendana na actual implementation.* Bajeti ya kukarabati vituo 35 vilikarabatiwa 16 tu ambayo ni asilimia 46 ya kazi.

(2) Ripoti za uwongo, mfano taarifa ya 2012/2013 kukamilika vituo vya Nachingwea, Nyakato na Kondoa.

(3) Ripoti ya 2013/2014 ilionesha hakuna kazi iliyofanyika katika vituo hivyo na walienda *site* hawakuona chochote.

(4) Mwaka 2014/2015 hakukuwa na ripoti iliyotolewa.

(5) Ujenzi wa vituo vingine bila mikataba na wakandarasi, mfano, *M/S Posh-alliance* kiasi cha Sh. 515,233,760.

(6) Ufisadi katika ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Mfano Makambako (*Model Police Station*).

(7) Milioni 25 zililiipwa kwa mkandarasi kwa ununuzi wa fenicha ambazo hazikununuliwa.

(8) kupotea kwa fedha ya wananchi mikononi mwa Polisi, wanaowekwa mahabusu au zinazokuwa vidhibiti; *Tsh. 145,410; Ksh. 25,900 na Euro 800.*

(9) *Delay in banking revenue collected of Tsh. 93,725,000. Delay in submission of revenue collected na traffic notification of over 24 million.*

(10) Kushindwa kukusanya *fines* zenyé thamani ya zaidi ya biliomini 4.4.

(11) Walifanya malipo ya milioni 234, zaidi kwa watoa huduma waliokuwa hawastahili, *Time General Supplies*.

(12) Malipo kwa watoa huduma ya milioni 103.4 bila kushindanishwa. *Single source procurement million 179.4; total of zaidi ya milioni 700 zimekiuka taratibu za manunuzi.*

(13) Matumizi ya zaidi ya milioni 345.9 ambazo hazikuidhinishwa na *IGP*kuanzia 2013 – 2017 na bila vithibitisho kinyume na *PGO* 121(2).

(14) Matumizi yasiyoeleweka ya kikao cha Viongozi Wakuu kilichofanyika Dodoma tarehe 17 – 19 Aprili, 2017 zaidi ya milioni 156,206,000 zilitumika na hazikuwa na ushahidi *out of 246.03 verification ilifanyika* kwa milioni 89.8 tu.

MHE. JAMES K. MILLYA: Mheshimiwa Spika, vitendea kazi vya Polisi. Jimbo la Simanjiro lina ukubwa wa *square kilometer* 21,000 takriban gari moja kwa wilaya kubwa kama hii, ni mateso na ni ngumu sana. Naomba jimbo hili liangaliwe kwa karibu. Kwa ukubwa huo Wilaya ya Simanjiro ni vyema pia mafuta ya mwezi wakaongezewa kutohana na ukubwa wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kesi zisizo na tija; Polisi Kituo cha Msitu na Tembo eneo ambalo lina rasilmali ya asili (Mto wa Nyumba ya Mungu) Mkuu wa kituo kile amekuwa na tabia ya kubambikiza wananchi kesi kwa sababu zisizo za msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mmoja wa mtu mmoja tajiri anayedhulumu wananchi wa Loliondo ardhi yao lakini Mkuu wa Kituo hiki ili kutuliza madai ya wananchi kutetea ardhi yao, ameamua kimkakati kushirikiana na tajiri huyo anayedhulumu wananchi eneo lao, kuwafungulia kesi nydingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza Jeshi la Polisi kwa ujumla wake kwa kazi nzuri inayofanywa na kikosi chini ya *IGP Sirro*. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri. Tunayo amani ya kutosha na eneo la Mererani ambalo hapo awali lilikuwa na matukio mabaya, kwa sasa lina amani ya kutosha. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, maaskari wasio waadilifu; ni vyema Wizara hii ilinde taswira ya Jeshi la Polisi kwa kuwaadhibu maaskari ambao sio waaminifu ili kulinda heshima ya Jeshi la Polisi. Polisi ni taswira ya nchi yetu. Naomba wahudumiwe kwa uhakika na mahitaji yao yaangaliwe na Wizara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya muhimu. Nawatachia kheri kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

MHE. MICH. DKT. GERTRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote niipongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Kangi Lugola kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ujambazi umepungua kwa kiasi kikubwa sana, tunatembea kwa uhuru, ajali za barabarani zimepungua mno na uvamizi wa mabenki pia umepungua sana. Hongereni.

Mheshimiwa Spika, naomba nyumba za askari Ifakara - Kilombero zijengwe, wana shida kubwa ya makazi. Pia tunaomba Mahakama ya Ifakara ijengwe, wakati wa masika, mafuriko yanaathiri wafungwa, mafaili, ofisi na ni kero kubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, posho za wazee wa Mahakama; Babati hawajawahi lipwa miaka miwili iliyopita, wazee wamehangainka bila mafanikio. Sasa naomba kufahamu wazee hawa wamehangainka sana watalipwa lini?

Mheshimiwa Spika, fidia ya wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa na jengo lao la Mahakama, Mkoa wa Manyara na Mahakama ya Wilaya ya Babati pale Mtaa wa Negamsii, Kata ya Bagara, Jimbo la Babati Mjini tangu 2004 hadi leo wananchi hawajalipwa fidia japo Mahakama imeshajenga majengo yao na wananchi hawajalipwa. Naomba kufahamu Mahakama kama chombo cha haki ni kwa nini imewanyima wananchi fidia yao na lini watalipwa?

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Spika, nampa hongera Mheshimiwa Waziri Kangi Lugola kwa majukumu. Nachukua fursa hii kukumbusha juu ya wito wa Serikali kwa wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tarafa ya Chipanga, Wilayani Bahi waliamu kujenga Kituo cha Polisi cha Tarafa toka mwaka 2003 na kukamilisha lakini hadi sasa hakijafunguliwa takribani miaka 16 sasa. Wananchi walichangia zaidi ya milioni 40 wakati huo, lakini wamekatishwa tamaa na Jeshi kutokukipokea kituo hicho na kukifungua. Kituo hicho kina umuhimu mkubwa kikifunguliwa kwa kulinda usalama wa mali na wananchi. Naomba sasa kifunguliwe. Ahsante.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, katika Wilaya ya Missenyi, Kata ya Kakunyu nimepokea malalamiko mengi ya baadhi ya watu kupewa *PI - Persona non grata* na kutakiwa kuondoka ndani ya saa 24.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie orodha ya majina ya Utaifa wa watu waliokuwa wanakaa Kata ya Kakunyu na wakapewa '*PI*'. Katika mikutano yangu ya hadhara katika Kata ya Kakunyu nilipokea malalamiko mengi, pia ya baadhi ya wananchi kukamatwa usiku nyumbani kwao na kupigwa viboko na kulazimishwa wakubali kwamba wao si Watanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri afafanue kama vitendo vya kukamatwa watu usiku na kuwapiga viboko ndiyo utaratibu mpya wa kuwatambua Watanzania na wasiokuwa Watanzania hasa katika Kata ya Kakunyu, Wilayani Misenyi.

SPIKA: Ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, Mwongozo!

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

MWONGOZO WA SPIKA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, ninaomba niombe Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7). Kwa busara kabisa na hekima kubwa, nimemsikiliza sana sana *Chief Whip* wa upande wa upinzani, wakati akitoa maelezo yenye hekima na busara kubwa kuhusu jambo ambalo lilitokea leo ndani ya Bunge lakini lilianza kutokea toka jana.

Mheshimiwa Spika, mjadala huu katika nyakati tofauti ulijadiliwa na kutawaliwa na maneno ambayo yalikuwa yanavunja Kanuni ya 61(1)(g) na wakati mwingine lugha zilizotumika zilikuwa ni lugha za kuudhi na zinazodharirisha watu wengine, na hasa jeshi letu la polisi ambalo linafanya kazi kubwa sana ya kulinda raia na mali zao katika nchi ya Tanzania, amani na utulivu katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Selasini ameliweka vizuri sana jambo hili na ametaka katuonyesha kilichotokea kwa Mbunge wa upande wa upinzani, haikuwa ni dhamira ya Wabunge wa upinzani, ilikuwa ni dhamira ya aliyesema.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako, ili jambo hili tuliweke vizuri na kuhakikisha kwamba jeshi la polisi tunapomaliza mjadala wa hotuba ya bajeti ya jeshi la polisi liondoke likiwa na heshima yake kama ilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini usitoe nafasi kwa Mbunge husika, aweze kuomba radhi jeshi letu na kufuta ile kauli na hasa alipoliita jeshi letu la polisi kwamba ni kansa ya nchi yetu. Ili tukitoka hapa tuwe wamoja kama Wabunge na tuendelee *ku-retain* heshima ya jeshi. Lakini nikubaliane na maneno ya busara sana aliyyoyasema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, kabla sijatoa mwongozo huo, nimuombe tena kwa mara nyingine *Chief Whip* wa *Opposition* kwa uzito wa jambo hili, kwa dakika moja hivi, kama kambi yako inakubaliana na huyo Mbunge au vipi au chochote unachowenza kusema, karibu.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, ni msimamo wa kambi yetu kwamba sisi tunaunga mkono kazi nzuri ambazo jeshi la polisi limekuwa likifanya na vilevile tunalishauri jeshi la polisi, katika yale mambo ambayo tunaona kwamba sheria na taratibu hazifuatwi, basi liweke sawa. Ni kweli kauli iliyotolewa jana haikuwa kauli nzuri.

Mheshimiwa Spika, na kama unavyojuua nimeshakuandikia mezani kwako nikikuomba kwamba nimuite Mbunge anayehusika ili asimame aliweke vizuri hilo suala, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Nakubaliana na viongozi hawa, na nimeitisha *Hansards* ninazo hapa zaidi ya moja, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, pamoja na mengine ulisema; "Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, kwenye polisi, maana yake hawa ndiyo kansa ya Taifa."

Nakupa nafasi ama usimame nayo maelezo yako, ama uyaweke vizuri maelezo yako, dakika mbili tu, dakika mbili tu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema na kama ulivysoma *Hansard* ya jana, nikiwa ninajadili katika Wizara hii, ni kweli kabisa nilizungumza kwamba Jeshi la Polisi ni kansa ya Taifa. Kama Mbunge ninayefuata kanuni, ninaomba nifute na itolewe kwenye *Hansard* hilo neno la kansa ya Taifa na kwa waliokwazika naomba wanisamehe, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Sophia, kwa ustaarabu huo, nizidi kuwaasa, Waheshimiwa Wabunge

tunapochangia tujitahidi sana *ku-control* munkali, kwa sababu sisi ni viongozi, na hasa tunapoongelea majeshi yetu ya nchi au vyombo vya ulinzi na usalama, hawa ni watu ambaao wanafanya kazi kubwa sana kwa ajili yetu. (*Makof!*)

Hawa ni watu ambaao wamekula viapo vya kuyaweka maisha yao kwa ajili yetu sisi. Watu wa aina hiyo wana heshima popote pale, hata muende kwenye hilo taifa kubwa lililotuletea mifumo hii mingine, hilo la Marekani, wanamheshimu sana mtu ye yeyote ambaye ni Askari, wanamheshimu sana mtu ye yeyote ambaye amewahi kupigana vita, wanawaheshimu sana kwa ajili ya Taifa lao. (*Makof!*)

Kwa hiyo, kama umekumbana na magumu ya hapa na pale kwa mtu mmoja, wawili, lakini siyo vizuri kujumuisha jeshi zima ukalipiga *labels* kama hizo, ni jambo ambalo halikubaliki, si msingi ambaao tuujenge katika nchi yetu, si msingi hata kidogo, hasa sisi kama viongozi. Kwa hiyo, ni vizuri sana kuwa makini sana na kauli zetu, kwa sababu zina *consequences* kubwa sana, kubwa sana, si vema kabisa kuwalipa Askari wetu hawa kwa maneno ya namna hiyo, tabu wanazopipata tunazijua. Wanaishi katika mazingira magumu sana, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, kipato chao ni kidogo, lakini wanavumilia yote, nchi yetu ni salama.

Halafu juu ya yote hayo tena sisi Wabunge tukaishia tena kuwatwisha kwa maneno ya namna hiyo, hili ni jambo ambalo halikubaliki hata kidogo, yako mambo lazima tuwe tunakubaliana wote, yako mambo hayana cha kambi. Kwa hiyo, nikushukuru sana na kama Spika, niwaombeni radhi sana Jeshi la Polisi. (*Makof!*)

Najua mmeumia sana, lakini tumelifuta jambo hili kwenye *Hansard* kila mahali, Bunge la Tanzania tunasimama na jeshi la polisi, tunawapongezeni kwa kazi nzuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, kuititia kwako, Mheshimiwa Naibu, jambo hili tunaliombea radhi sisi

kama Wabunge wote, ni jambo ambalo tunaamini halitajirudia tena, akisimama tena Mbunge mwingine huko siku zijazo, akaenda kihivyo, basi pamoja na adhabu za hapa Bungeni, mengine labda hukohuko uwanjani, watu watajifunza *the hard way*.

Jioni tutahitimisha hoja yetu ataanza Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu Waziri na utaratibu utaendelea kama kawaida, nitaomba ni vizuri mfike ili muweze kumsikia Waziri akijibu hoja zetu ambazo mmezitoa kwa siku mbili, ni vizuri tukawepo.

Kwa vile sitarudi hapa jioni atakuwepo Mwenyekiti, nisemee neno moja, kama kwa kulirudia kidogo. Mheshimiwa Zitto Kabwe hayuko hapa, amekuwa mwepesi sana kwenye kutoa taarifa fulani fulani, hasa zinazotoka kwenye ma-book yanayotoka Ofisi ya Ukaguzi wa Taifa, yanayokuwa yamewekwa Mezani hapa, na watu wengi wanamtatsri kama shujaa fulani hivi. Kwa sababu walioko nje ya Bunge hawaelewi taratibu zetu, kwa kawaida hizo taarifa za ukaguzi, kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, wengine mmezizoea sana kuziita taarifa za CAG, ni *English version*, kama vile ni kazi ya mtu mmoja, wakati ni kazi ya ofisi yenye watu wengi sana.

Utaratibu wetu zikishawekwa mezani hapa zitakwenda kwenye kamati zinazohusika, na kamati zake ni mbili, Kamati ya PAC, na Kamati ya LAAC. Kwenye kamati kule watachambua kila kitu, hoja kwa hoja na kadhalika. Hata huyo mwanachama wa CHADEMA ataitwa PAC, hata hao sijui nini, polisi sijui *uniforms* zimefanyaje, litajulikana vizuri kule. Kama nilivyosema wakati fulani, zile ni hoja, ni *queries*, lakini watu wanawaaminisha watanzania, kila kinachoandikwa na CAG au hiyo ofisi, kila kilichoandikwa mle kwamba ni ukweli wa asilimia 100, siyo hivyo, yako mambo mle si kweli hata kidogo. (*Makofii*)

Tena mengi, ninyi tena si mmekuwa wajumbe PAC, wale mliokaa miaka, au bado kabisa, mbona mnaruhusiwa kuhudhuria kwenye zile kamati, muwe mnaenda, mengine kiambatanisho tu hakikuweko, mengine sijui nini, mifano iko

mingi, yaani *book* lile linachambuliwa zinabaki hoja ngapi sijui zile, ndiyo tunawapa Serikali, sasa hizi malizieni, zingine zote zimefungwa, zimefungwa, ilikuwa sijui kiambatanisho gani hakipo, sasa kimeonekana, ilikuwa vocha fulani haipo, imeonekana. Kwa hiyo, kusambaza kama anavyofanya Mheshimiwa Zitto, kuwaaminisha wakati hiki kitu lazima kichambuliwe, kama kiongozi lazima uwe na *patience*, kazi ile inawenyewe. Anachong'ang'ania Mheshimiwa Zitto ni kutaka kuendelea kuwa Mwenyekiti wa *PAC* kinyemela! (*Makofi*)

Ndiyo ukweli, kwa nini unatangulia mbele, *CAG* kasema hiyo tuhuma, weka neno, katuhumu, kama unataka. Maana yake unawafanya wananchi nchi nzima waamini kwamba kuna mahela, madudu gani yamefanya hivi, sijui halamshauri ya wapi, halmashauri yake ya Kigoma kule hati chafu mwaka wa pili huu mfululizo. (*Makofi*)

Iko kwenye ripoti mle, hasemi, na yenye nayo itaitwa! Itapewa haki ya kusikilizwa, ndiyo maana Wabunge waliovengi wamenyamaza siyo kwamba hawajui kusoma yake ma-*book*, ni kwa sababu hiyo kazi ina mchakato wake na mwisho tutaelewa nini ambacho kiko ndani.

Tukilliweka Taifa hili katika misingi ya kwamba kila kinachoandikwa na ofisi ya *CAG* kwamba sasa ndiyo, hatutakuwa tunalitendea haki. Lazima mtu ambaye amewekewa swali, apate nafasi ya kujibu! (*Makofi*)

CAG ni *external auditor*, anapoleta hoja *external auditor*, hoja zile huwa zinatakiwa zipitiwe zipate majibu! Sasa kama katika hoja zile kuna hoja ya polisi, wanapewa polisi wanashughulika na huyo mtu, kama hoja ile ni ya Serikali wanapewa Serikali, wanajua nini cha kufanya na kadhalika. (*Makofi*)

Sasa mwenzetu huyu ni harakahara, anapeleka kwa, ili ye ye aonekane, ye ye kama ye ye *is the best*, lakini Bunge na Wabunge wote hawajui kusoma taarifa na kadhalika. Jambo ambalo sisi, si sawasawa sana. Hatumkatazi, havunji

kanuni yoyote, lakini ni kule kuwahiwahi ambako, sijui tunakuitaje kule, yaani! Kwa hiyo, anaonekana wa maana kweli huko eti ana taarifa, taarifa ziko wazi, ziko wazi, ni vizuri tukajua taratibu namna ya kwenda tutakwenda vizuri tukienda hivyo. Na katika maisha, jizue sana kuwatuhumu watu, kama kiongozi wa kisasa au kiongozi ye yote, jizue sana, ni dhambi kwa Mungu.

Wape nafasi hao watu walijotajwa, wajieleze, wakishajieleza kama hawana maelezo, sasa toka nje, unashida gani, una haja ya kuwahi, toka nje sasa eleza kuna watu wameitwa hawakujieleza, hawana lolote na hawajachukuliwa hatua na kadhalika, itakuwa ni jambo ambalo ni sahihi. Lakini taarifa tu mezani, tayari! Hata huyo wa CHADEMA tunaweza tukamtuhumu hapa kumbe labda alikuwa sahihi, acheni aitwe, aje ae leze vizuri hilo gari lilikuwaje na ataltwa, kama ni Mbunge si Mbuge wataitwa, na ndiyo kazi yangu kuhakikisha nawaita, kwenye Kamati ya PAC, asiyefika, namleta kwa pingu, si mnajua madaraka mmenipa, sasa kuna atakayeshindikana kuitwa pale. (*Makof*)

Yuko wapi huyo atakayeshindikana, hakuna hata mmoja, wajipange na majibu ya hoja, ni haki yao wasikilizwe, watoe maelezo, itatusaidia tukienda kwa utaratibu huo vizuri zaidi.

Vinginevyo nawatakia Muungano mwema. Kesho kama tulivyo eleza, kutakuwa na mechii jioni saa tisa, ni vizuri tukafika pale Uwanja wa Jamhuri, wenzetu Baraza wa Wawakilishi watakuwepo na mambo yatakuwa mazuri sana pale. Yako maandalizi mazito mazito pale, na yale mambo yatatusaidia, kama hayo ya michezo, yanatuweka pamoja vizuri. Tukikutana pale hivi vimbwaga vyote vinakuwa havipo, tunafurahi tunashangilia, inatuweka vizuri zaidi na inatuunganisha zaidi kama Bunge moja.

Basi baada ya maelezo hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi leo Jioni saa 11.00.

(Saa 7.00 Mchana, Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa ambazo ninazo, wachangiaji wote wameshamalizika, sasa tunaanza na upande wa Serikali, Mheshimiwa Mkuchika dakika kumi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja hii muhimu sana ya Wizara hii ambayo ni uhai wa Taifa letu. Nataka nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyowezesha Jeshi la Polisi kutekeleza kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Kangi Lugola anavyotekeleza majukumu yake kama Waziri wa Mambo ya Ndani. Pia nataka niwapongeze watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani, kuna majeshi ya kila aina katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, nataka kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi katika nchi hii. Nitatoa mifano ya namna gani Jeshi la Polisi limetunusuru katika majanga ambayo tulikuwa nayo katika nchi hii. Tabia ya binadamu ni kusahau, ndiyo maana kila siku tunakwenda Msikitini, tunakwenda Kanisani kukumbushwa mambo. Siyo kama hatujayasikia, lakini kwa sababu tunasahau, ndiyo maana tumepangia kila Jumapili na kila Ijumaa twende kusali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge, natoka Mtwara. Ili utoke Mtwara kwenda Dar es Salaam lazima upite Ikwiriri – Kibiti. Tulivamiwa Kibiti - Ikwiriri na watu ambao hatuwajui. Watu wengi wameuawa, usiku kulikuwa hakupitiki, Jeshi la Polisi limepambana, Kibiti kumetulilia, Ikwiriri kumetulilia, sisi watu tunaotoka Kusini tunapita Ikwiriri - Kibiti hata saa nane

usiku, hakuna tatizo. Kazi hiyo imefanywa na Jeshi la Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, katika nchi yetu hii kuna mapori makubwa yaliyopo katikati ya Mji na Mji; Kasulu, Kibondo, mabasi yakitembea hasa giza likiingia lazima Askari wa Polisi wa-*patrol* kuhakikisha kwamba tunakuwa salama. Wanafanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, wale ambao wanabeza kazi ya Polisi, kaa, tafakari, hebu juilize itokee siku moja Jiji la Dar es Salaam halina Mapolisi kwa muda wa nusu saa, hakuna Mapolisi wa kuongoza *Traffic* Dar es Salaam, badala ya kuwa *traffic jam* itakuwa imesimama kabisa. Polisi wanafanya kazi nzuri. Polisi wamepunguza ajali katika nchi hii. Ajali zimepungua, Mapolisi wanafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa umri wangu, jana nimeumia sana kuona kwamba watu wanasimama hakuna hata ile shukrani. Halafu jambo lingine nimelishangaa kwa utu uzima wangu, watu wameuliza maswali juu ya raia waliokufa ambao hawajulikani waliko; lakini hakuna aliyesimama anasikitika Mapolisi waliouawa wakiwa kazini wakifanya kazi ya kututetea sisi. Kwa mwendo huu mnataka kuwafanya vijana wakati mwingine sasa waseme eeh, kumbe ukienda Jeshi la Polisi wewe ni *target?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu wengi wamepoteza maisha, siyo kwamba walikuwa wanalinda shamba la baba yao; siyo kwamba walikuwa wanalinda duka lao; walikuwa wanatulinda sisi Watanzania wote bila kubagua wewe umetoka Mtwara, umetoka Lindi, umetoka Kilimanjaro, umetoka Kigoma nakadhalika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Nchi hii bila Polisi; hapa tu jioni magari yajae, maana yake leo watakuwepo watu kumpongeza Mheshimiwa Waziri kama atapita na Inshallah atapita. Magari yatajaa hapa. Ili tutoke hapa, bado mnataka Askari Polisi katuondoa tu hapa Ukumbini. Je, Dar es Salaam!

Kwa hiyo, nasema *Traffic* wanafanya kazi nzuri, mimi nimesimama hapa kuwapongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Polisi hawa wanaitwa Askari wa Usalama wa Raia. Usalama wa Raia maana yake wanaangalia usalama wetu sisi. Sasa jana hapa palikuwa na hotuba za lawama tele, Polisi hawafanyi hiki, fulani amepotea hatujui aliko; sijui imekuwaje! Polisi anafanya kazi ya kulinda nchi hii kwa kusaidiwa kupewa taarifa na raia wema ili wafuatilie waweze kubaini ni watu gani wanauchafua usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tunaambiwa na tumepewa namba kwamba bwana una jambo la kuwataarifu Polisi? Piga hiyo namba. Hupigi namba; tangu mwaka 2018 tumemaliza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, watu wamekaa kimya, hawana mawasiliano na Polisi, hawajawapa taarifa ya Polisi, wanasubiri leo hotuba ya Mheshimiwa Kangi Lugola, waseme tena fulani hatumwoni na fulani ilikuwa hivi; na fulani. Umewapa taarifa Polisi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Polisi walivyo wachache, sisi Watanzania tullobaki milioni 55 ondoa hiyo idadi ya Polisi ambayo ni ndogo sana ukilinganisha na hao milioni 55, watawezaje kupata taarifa kama sisi wakereketwa wa nchi hii, wenye uchungu wa nchi hii hatuwapi taarifa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusisitiza hapa, tuwape taarifa ya ushirikiano Jeshi la Polisi. Polisi pekee hawawezi kufanya yote ya kulinda usalama wa nchi yetu kama sisi hatutawapa taarifa. Kuja hapa na kutoa tu hotuba fulani hatumwoni, fulani kaibiwa, fulani imekuwa hivi, umewapa taarifa Polisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi sitaki malumbano, nimesimama hapa kueleza kwamba tuna haja ya kushirikiana na Jeshi la Polisi ili nchi yetu izidi kuwa nchi ya amani na usalama. Siyo vizuri kutoa tuhuma humu dari bila kuwapa taarifa Jeshi la Polisi ili waweze kufanya uchunguzi,

waweze kufuatilia kwa sababu Polisi kwa kawaida yao, wamesomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nataka kuzungumza habari ya utawala bora, imegusiwa hapa na pale. Ndugu zangu na Watanzania huko mliko, niwatoe hofu Watanzania wenzangu, Tanzania tuko salama. Nchi yetu, vyombo vyaa usalama vimedhibiti. Niambieni Afrika Mashariki yote hii leo, nchi gani watu wakipata matatizo ya vita kwao, wakipata *civil war*, wapi wanakimbilia kama siyo Tanzania? Hivi Tanzania pangekuwa mahali pa vurugu mechi wangekimbilia? Wanakimbilia Tanzania kwa sababu ni nchi ambayo ina amani, tuko shwari, vyombo yetu vinafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana juzi niliumia hapa, mmoja akataka mjadala, tumjadili *CDF* kasema hivi. *CDF* kasema tu jamani eeh, sisi tutawafuatilia wakorofi wote, tukiwapata, tutawashughulikia. Hivi Askari kazi yake nini? Si kughulikia maadui wa nchi? Ukaja mjadala humu, *CDF* tumjadili; mnajadili nini? Askari tunapoapishwa na Rais, tunakula kiapo cha kulinda nchi yetu. Alichosema yeeye na wanajeshi wenzake, wataendelea kulinda nchi yetu ili isichezewe. Ikawa nongwa. Unakuja mjadala humu! He! *Freedom* ya kukaa tunamjadili *CDF* aliyesema kwamba tutashughulika na wote wanaoleta chokochoko katika nchi yetu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalizie, maana dakika kumi naona ni chache. Upande wa utawala bora, nataka kuzitoa takwimu hizi; Watanzania tuna tabia ya kubenza mafanikio yetu. Tuko tayari kusifu mambo ya wenzetu lakini yetu hatusifu. Ndiyo maana hata humu ndani hata wenzangu wale wenye *interest* za mpira, ukimwambia panga timu ya mpira wa Ureno, atamweka *goalkeeper*, yote iko kichwani; lakini mwambie *Taifa Stars* juzi walicheza nani na nani? Hajui. Ndiyo tulivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niseme upande wa utawala bora; na hapa uniruhusu kusoma. Nataka

kusema, kwa utawala bora sisi katika nchi za Afrika tunang'ara. Maana mengi yaliyokuwa yanazungumzwa hapa ni ya kubeza utawala bora uliopo katika nchi hii. Kiashiria cha *transparency International*, hili ni *NGO* moja ya ki-*International*, inaeleza habari ya utawala bora dunia mzima. Wanasema kwamba Tanzania tunafanya vizuri. Tumepanda katika utawala bora, tulikuwa nafasi ya 193, sasa tuko nafasi ya 99, wanasema kwa utawala bora Tanzania iko juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu wa *Afrobarometerhawa* wanasema mwaka 2014 ilionesha kuwa asilimia 66 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimeongezeka; mwaka 2017 wakasema kiwango cha rushwa kimepungua, watu asilimia 85; *TWAWEZA* wakasema Tanzania utawala bora umeongezeka, rushwa imepunguza. Wale *REPOA* wakasema hivyo hivyo. Tungeweza kutoa mifano mingi sana...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKTI: Nimekuongezea dadika tatu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa huruma yako. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ndugu zangu, Watanzania tujivunie mafanikio tuliyonayo. Tanzania kama isingelikuwa nchi ya amani, mbona tuna wakimbizi hapa? Wamekimbilia kwao. Mbona hawajakimbilia nchi fulani, mbona hawajakimbilia na nchi fulani na nchi fulani? Wamekimbilia Tanzania kwa sababu hapa wakija hakuna ile unamwona tu fulani, kabila gani huyuo ua! Kabila gani huyo, ua! Utawala bora nchi hii uko juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na matatizo hapa ya mauaji ya Albino, tumepambana, nchi imetulia; mambo hayo bado wapo mmoja mmoja, lakini na hao mipango

tumeiweka kwa usalama wa nchi hii, hatutaki mtu auawe tu kwa sababu ni kilema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja. Nawaomba Wabunge wenzangu, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, Polisi wanafanya kazi nchi hii. Polisi na vyombo vyote vya usalama vinafanya kazi nchi hii, ndiyo maana ukipewa fursa ya kuongea, unaongea jinsi unavyotaka. Nchi nyine wanavyoongea baadhi ya watu hapa, ilikuwa ukitoka tu hapa tayari anakusubiri pale uende ukakae ndani huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa watu mnaongea huru hapa, mnaongea mambo mengine ya ajabu ajabu, Mheshimiwa Rais ananunua vitu, amekuwa yeze ndiyo mnunuzi. Mmeambiwa hapa, Mheshimiwa Rais hajaenda *shopping* hata siku moja kwa ndege za Serikali, wala kwa jambo lolote la Serikali, vitu vyote vimenunuliwa kwa taratibu za manunuzi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

MWENYEKITI: Ahsante. Polisi wanafanya kazi vizuri sana, ni kweli, lakini wapunguze punguze kidogo ushabiki wa jangwani kule. (*Kicheko/Makofi*)

Sasa nina mgeni anaitwa Shehe Bahadi Muhamrami Saleh, karibu Bungeni, namwita Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Eng. Masauni dakika 15.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuendelea kuniamini kwa nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba niendelee kumhakikishia kwamba nitaendelea kutokumwangusha na kuchapa kazi inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa msaada wao mbalimbali ambao unanisadia kutekeleza majukumu yangu vizuri. Pia nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kangi Lugola ambaye kwa kweli ni Waziri wa aina yake. Tumefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa; pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakuu wa Vyombo pamoja na Makamanda wote nchi nzima na Wakuu wa Taasisi mbalimbali wakiwemo *NIDA* na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siyo kwa umuhimu, niishukuru sana familia yangu kwa kuniunga mkono na kuweza kunistahimilia pale ambapo natekeleza majukumu ya Kitaifa. Baada ya shukrani hizo, sasa nataka niende moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka nizungumze kwa sababu ya ufupi wa muda, nimeamua kuliweka hili mwanzo kwa sababu ni jambo nadhani ni muhimu sana. Jambo hili kwa bahati mbaya linaonekana kuleta taswira mbaya na kuichafua Serikali yetu adhimu ambayo wakati wote imekuwa ikifanya kazi kwa uadilifu, kwa ufanisi na kwa bidii kubwa na juhudini kubwa katika kuwatumiwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuhuma hizi zisipojibiwa kwa uwazi kama ambavyo nataka nijitahidi kuzijibu hapa leo, zikiendelea kubakia kuzungumzwa kila siku zinaweza kusababisha kutengeneza chuki kati ya wananchi na Serikali yao, chuki ambazo madhara yake kwa mustakabali wa amani ya nchi yetu zinaweza zikawa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna tuhuma kwamba vyombo hasa Jeshi la Polisi na kwa maana ya Serikali kwa ujumla wake, tumekuwa tukifanya kazi zetu kwa kukandamiza baadhi ya raia kulingana na aina ya dini wanayoiamini au sehemu walijotoka. Labda nitoe mfano mmoja hai ambao umekuwa ukizungumzwa miaka mingi,

wamekuwa wakitoa mfano wa watu ambao wanawaita Mashehe wa Uamsho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri kwamba binafsi kwa kupata fursa ya kutumikia Serikali hii, najiridhisha pasi na shaka yoyote kwamba Serikali yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake ambavyo tunavisiimamia wakati wote tumekuwa tukifanya kazi kwa kufuata misingi ya sheria. Kama ingelikuwa nimeshuhudia aina yoyote ya upendeleo, ubaguzi kwa misingi yoyote ile, leo ningelimwandikia barua Mheshimiwa Rais ya kuijuzulu nikakaa kule *backbencher*, nikawa mimi ndiyo mionganoni mwa watu wa kushiriki kупingana na hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naamini kabisa kwamba kwanza Serikali ya aina hiyo itakuwa ni Serikali ambayo inatenda dhambi kwa Mwenyezi Mungu, lakini ni Serikali ambayo itakuwa inaandaa misingi mibovu ya amani ya nchi hii. Tumeshuhudia Mataifa mbalimbali ambayo haikuwa na misingi mizuri kama misingi ambayo Waasisi wa Taifa hili waliojenga kwa Tanzania inayosababisha mpaka sasa hivi tuendelee kubakia na umoja na mshikamano bila kujali jambo lolote ambalo mhusika analo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua jambo hili bahati mbaya linazungumzwa na baadhi ya wanasiasa kwa sababu za kisiasa, jambo ambalo ni hatari sana, lakini hatuwezi kuendelea kukubali. Tuhuma hizi za hawa watu wa Uamsho zimekuwa za muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka katika vikao vya bajeti vilivyopita ilikuja hoja ya kwamba watu hawa wa Uamsho wanafanyiwa vitendo vya udhalilishaji na tukapata maelezo kutoka vyombo vyetu tukiwasilisha Bungeni kueleza kwamba haya ambayo yanazungumzwa siyo kweli. Nami binafsi nilifanya ziara ya kwenda Gereza la Ukonga na kuzungumza nao watu hawa. Nilipofika niliwauliza kwamba je, kuna jambo lolote la kinyume na utaratibu ikiwemo udhalilishaji ambapo vyombo vyetu vilivyopo chini ya Wizara

ya Mambo ya Ndani ya Nchi vimewafanya? Wakaniambia hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyofika niliwauliza kwamba, je, kuna jambo lolote la kinyume na utaratibu ikiwemo udhalilishaji ambavyo vyombo vyetu viliyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi vimewafanya? Wakaniambia hakuna, nikawaauliza je, kuishi kwenu hapa kuna mashaka yoyote ya ukiukwaji wa haki za binadamu? Wakaniambia hakuna, tuko vizuri kabisa. Baadaye wakanieleza pamoja na mambo mengine, jambo la kwanza wakaniambia kwamba sisi changamoto yetu hapa ni kuchelewa kwa kesi yetu. *Concern* hiyo ndiyo *concern* ambayo Serikali tunayo siyo kwa wao tu bali kwa Mahabusu wote nchi nzima na kila siku tumekuwa tukieleza mikakati mbalimbali ya jinsi ambavyo tunataka tuhakikishe kwamba wanaotuhumiwa kesi zao zinakwenda haraka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mikakati mingi ya kutumia wafungwa kwa ajili ya kuijendeleza katika Jeshi la Magereza ambayo tutaizungumza baadaye; kwenye kilimo, kwenye viwanda, tunahitaji nguvu kazi. Kwa hiyo tunaamini kabisa wale ambao hawana hatia waachiwe huru, waliokuwa na hatia wafungwe ili kama hata wanaendelea kutumia rasilimali za nchi, lakini waweze kuzalisha vilevile. Kwa hiyo hakuna hata siku moja Serikali hii imekaa ikawa inapendelea kuona raia wake wanaendelea kubaki mahabusu. Jambo hili bahati nzuri tulilizungumza kwa mapana yake. Aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Profesa Kabudi alilizungumza akaeleza ni changamoto gani zinakabili tuhuma hizi, tuhuma za ugaidi ni kwa nini kesi zimechelewa na jitihada gani Serikali tunaingiza katika kuona mambo haya yanakwisha haraka, limeelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo waliniuliza, wakanipatia maandiko ambayo walieleza kwamba wao wanataka, wanaona kwamba wameshajifunza vyta kutosha na kwa hiyo basi wanaomba waachiwe na kwa namna hiyo basi watakapokuwa wameachiwa hawatakubali tena

kufanya siasa au kutumika kwenye siasa. Sasa nikajiuliza; kwani kesi ambayo inawakabili hawa watuhumiwa ni kesi ya siasa au kesi ya ugaidi? Nihavyofahamu ni kwamba tuhuma zile ni za ugaidi siyo za siasa, sasa unazungumza siasa imetoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kauli hiyo ikanikaa sana kwenye kichwa na ndiyo maana ninapokuja sasa huku kwenye Bunge na maeneo mengine, naona sasa nikishabihisha na matukio yalijyotokea kipindi cha nyuma napata mashaka. Naona hapa kuna jambo lingine na kama jambo ni siasa hivi kweli Waheshimiwa Wabunge tuko tayari kuligawa Taifa hili kwa sababu ya siasa? Kama kweli hoja ni siasa na nikashabihisha baadhi ya sera za Chama Kikuu cha Upinzani kilichokuwa Zanzibar za kuendelea kudhani kwamba wataendelea kupata *popularity* kwa kugawa wananchi. Sera za kusema hawa Wapemba, hawa Waunguja kwamba labda watu wa Unguja wameona kwamba sera hizo hazikufanikiwa kuwaambia watu wa Unguja ambao ni ndugu za damu na wenzao wa Pemba kwamba watu wa Unguja hawawapendi Wapemba ili kupata kura tu. Au sera za kusema kwamba hawa Watanzania Bara, hawa Wazanzibari na ndiyo haya mambo ambayo yalifanyika katika kipindi cha nyuma, nikashangaa vihi dini gani ambayo inashabihisha kugawa watu? Dini gani ambayo inazungumzia masuala ya Muungano mbaya? Hivi kweli hakuna jambo hata moja zuri la Muungano? Badala ya kuwaambia wananchi watumie fursa zilizopo nyngi za Muungano, wanatumia changamoto ambazo pengine tunazikabili kila siku na kuzipunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikapata mashaka sana na hilo jambo na ndiyo maana nikasema kwamba yale mambo ambayo yalijitokeza kipindi kile na watu wengi ni mashahidi, tulishuhudia jinsi ambavyo baadhi ya Masheikh wengine mpake leo wana makovu na majeraha kwenye uso ya kumwagiwa tindikali, kuna Mapadre walipigwa risasi, kuna mabomu yalitegwa, ni kwa sababu ya kuendekeza na kuchanganya na yote yalifanyika kwa kutumia dini lakini kumbe leo nimegundua haya kumbe yalikuwa na malengo ya kisasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatari na nimeona niyazungumze hivyo kwa mapana kwa sababu tumechoka kuona kwamba Serikali yeu inaendelea kuchafuliwa hali ya kuwa ukweli hawa wanasiasa wanaufahamu. Nataka niwahakikishie kitu kimoja tu kwamba, karne hii tuliyokuwanayo hatutakubali kuruhusu undumilakuwili wa kisiasa, hatutakubali kuona dini inatumika kujenga chuki, kujenga uadui kwa kuitia kwenye siasa. Yaliyotokea yamekuwa ni funzo kwetu sisi na ndiyo maana nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa *statement* nzito na muhimu sana aliyotoa Zanzibar juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda Zanzibar pamoja na tuliona kwamba kuna hatari ya kunyemelea kwa taratibu zile zile ambazo zilitufikisha pale tulipokuwepo na tukapata kazi kubwa sana na hivyo basi naendelea kusisitiza kauli ya Mheshimiwa Waziri na hii kauli ambayo aliwaelekeza Jeshi la Polisi. Kutokana na kazi za kisiasa ambazo zimeendelea kufanywa na wale wale ambao sasa wamehamia vyama vingine kwa kisingizio kwa mikutano ya ndani halafu leo wanakuja hapa wanalamika wanasesma mikutano ya ndani inazuiliwa, mikutano ya hadhara inazuiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano ya ndani ambayo itakuwa inafanywa kwa utaratibu kama ambavyo wamekuwa wakifanya wao kule Zanzibar, utaratibu wa kutumia mikutano ya ndani kueneza chuki, utaratibu wa kutumia mikutano ya ndani kutukana viongozi na kugawa wananchi, mikutano hiyo haitakuwa na uhalali, hata kama ni mikutano ya ndani. Mikutano ya ndani ambayo unafanya unaweka maturubai na mabomba nje na kuziba njia wananchi wasifanye shughuli zao, kupiga ngoma barabarani, kuchinja wanyama sijui mbuzi na kumwaga damu barabarani, mikutano hiyo marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza kauli ya Mheshimiwa Waziri kwamba kama kuna Askari ambao wanadhani kwamba baadhi yao, najua kama watakuwepo kwa Zanzibar watakuwa wachache kama wapo, kama yaliyotokea kipindi kile cha siasa na dini kwenda pamoja

wakaacha mambo haya yakaenda mpaka yakafikia yalipofikia, kama wamefanya hivyo iwe kwa uzembe, iwe kwa utashi wao na mapenzi yao kwa chama chochote kile cha upinzani wachukuliwe hatua. Wasipochukuliwa hatua, wakubwa wao tutawachukulia hatua sisi na watakaokuwa nje ya mamlaka yetu tutatoa mapendelekezo kwenye mamlaka husika wachukuliwe hatua. Hili jambo hatuwezi kuliruhusu, tunataka sheria ifuatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya mikutano hii najua Mheshimiwa Waziri atalizungumza, madhumuni ni kwamba sisi tunataka demokrasia hii iwe na tija kwa wananchi, demokrasia itafsiri hali halisi ya kupambana na umaskini ndiyo tafsiri ya demokrasia yetu na ndiyo maana tunasema kwamba wakati huu ni wakati wa kufanya kazi. Kwa hiyo mikutano ya hadhara inayofanywa itafanywa wakati husika. Hatuwezi tukafika hapa tukarithishana tu demokrasia za watu wengine. Wamarekani wanawake wameanza kuruhusiwa kupiga kura mwaka 1920, tokea karne na karne za nyuma zilizopita. Kuruhusiwa watu weusi kupiga kura, kushiriki uchaguzi imechukua miaka zaidi ya 100.

MWENYEKITI: Haya malizia Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tafsiri ya Demokrasia yetu ilete tija kwa wananchi na tunafanya hivyo kwa kufuata sheria kwa sababu Jeshi la Polisi linaposema kwamba linataka kuangalia intelijensia ikoje, intelijensia ni uwanja mpana. Kwa mfano; unapozungumzia intelijensia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri malizia.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa intelijensia ya Polisi inaona kwamba sisi tunahitaji Askari wetu waende wakaangalie hali ya usalama ya wezi, hali ya usalama ya majambazi ili

Wananchi watekeleze shughuli zao za maendeleo hatuwezi ku-deploy Polisi wetu wakalinda mikutano ya fujo na chuki.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Kwa hiyo tuko hapa tunasimamia kwa mujibu wa sharia, kwa hiyo tunataka Askari wote watambue hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kumalizia; nataka nichukue fursa hii kuwaambia Askari wetu kwamba kama kuna Serikali ambayo inawapenda ni Serikali ya Dkt. John POmbe Magufuli. Katika kipindi cha muda mfupi kwa haraka haraka, toka Serikali ya Dkt. Magufuli imeingia madarakani kuna mambo makubwa Jeshi letu la Polisi limefanyiwa ambayo ni ya kutolea mifano na hayajafanyika kwa miaka mingi nitataja machache:-

Mheshimia Mwenyekiti, mafao ya wastaaifu ni moja ya changamoto kubwa kwa Askari wetu na takwimu hapa zinaonesha ni kwa kiasi gani tumefanikiwa. Masuala ya ucheleweshwaji wa mishahara kwenye vyeo ilikuwa ni changamoto kubwa kwa Askari wetu, sasa hivi mambo haya yamepata ufumbuzi kwa kiasi kikubwa sana. Mheshimiwa Waziri wa Utumishi amezungumza, tunatarajia kupandisha vyeo vingine zaidi mwaka huu wa fedha pamoja na kuajiri askari wapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho mbalimbali ziko katika hatua za kuongezwa, mpaka hata sasa makazi ya Askari yanaboreshwani. Serikali hii ya Dkt. Magufuli inaimarisha vitendeakazi ikiwemo vyombo vyaya usafiri na teknolojia za kisiasa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi. Hali kadhalika, katika masuala...

MHE. MICH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: ...ya mafunzo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kaa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: ...masuala ya mafunzo pamoja na...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kaa kwanza

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: ...Serikali hii imeangalia kwa karibu sana. Kwa hiyo hoja za Wapinzani hazina mashiko. Serikali hii...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri ahsante wka mchango mzuri, ahsante nimekuongeza dakika saba.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofî)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Mtoho hoja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kutokana na hotuba yangu...

MWENYEKITI: Dakika 45.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: ...kutokana na hotuba yangu ya taarifa ya utekelezaji wa mpango na

Bajeti kwa Mwaka 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 niliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 24 Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu imechangiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo imetoa maoni na ushauri kwa Wizara na Serikali kwa ujumla katika maeneo mbalimbali. Kwa dhati kabisa naishukuru Kamati hii kwani imekuwa ikitoa maoni ya msingi kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 92 wamechangia hotuba hiyo, kati ya hao Wabunge 45 wamechangia kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge 47 wamechangia kwa maandishi. Pamoja na maelezo ya ufanuzi nitakayoyatoa, hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zitawasilishwa rasmi kwa maandishi katika Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima nianze kutoa majibu kutokana na ushauri mbalimbali ambaao umetolewa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, lakini kwa sababu ya muda nitagusia maeneo machache na ushauri mwingine ambaao umetolewa na Kamati naomba uingie kwenye *Hansard* kwa sababu Wizara ushauri wote uliotolewa tumeizingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametoa ushauri kwamba Serikali itenye shilingi bilioni nane ili kuendeleza Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto pale Mchicha, Dar es Salaam. Tumezingatia ushauri wa Kamati kwamba kwa kuwa tumehamia Dodoma na sasa tumeanza kujenga Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na uokoaji Mjini Dodoma, lile jengo tumeunda Kamati Ndogo ya Wataalam ili waweze kutushauri kwa ajili ya kubadilisha matumizi na kwa sababu tuna chuo, tunaweza tukafanya kuwa Tawi la Chuo chetu cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati yako ilishauri kwamba mchakato wa kukamilisha Sheria ya Usalama barabarani umechukua muda mrefu. Nikuhakikishie pamoja na Bunge lako tukufu kwamba katika Mwaka huu wa fedha, sheria hii iko katika hatua nzuri tutakuwa tumeiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwewnyekiti, pia ushauri mwininge ambao tumeuzingatia ni kuendelea kutumia utaratibu wa Bodi ya *Parole* ya kupata adhabu mbadala kwa ajili ya kupunguza msongamano kwenye Magereza wa wafungwa pamoja na mahabusu. Si hilo tu, ni pamoja na kuendelea kutumia msamaha wa Mheshimiwa Rais ikiwa ni pamoja na kujenga magereza hapa nchini kama ambavyo tunaelekea kumaliza Gereza la Ruangwa pamoja na Chato pamoja na ukarabati na kupanua mabweni kwenye magereza mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwininge ambao ni vyema nikaugusia ni kwamba Kamati ilishauri Serikali itoe fedha za maendeleo bilioni 5.79 zilizoidhinishwa kwa ajili ye ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa, Wilaya na vituo, hata hivyo fedha hizo kwamba hazikutolewa. Ni kwamba Wizara imeendelea kuwasiliana na Hazina na mpaka sasa tunaendelea na mawasiliano kuhakikisha kwamba hizo fedha kabla ya mwaka wa fedha haujawkisha zinatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ushauri waliooutoa ambao ni vyema nikaugusia ni huu wa wahamiaji haramu kwamba wahamiaji haramu wapatao 3,260 wako kwenye magereza yetu hapa nchini na wametoa ushauri, tumezingatia na hasa ikizingatiwa kwamba Tanzania, Ethiopia pamoja na Kenya tumefanya mkutano wa pamoja, yako mambo ambayo tumekubalina kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la wahamiaji haramu. Kwa hiyo ushauri wote ambao Kamati imetupatia sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tumeuzingatia na tutaufanya kazi na hatutakuwa na mzaha. Naamini ninavyozungumza hapa, Naibu Waziri anajua, Naibu Katibu Mkuu na Katibu Mkuu wote wamesikia na Wakuu wote wa vyombo wamesikia, tutafanya

kazi kama mchwa usiku na mchana kuhakikisha kwamba yote haya tunayatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kugusia hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zingine ambazo zimetolewa kwa maandishi, zingine kwa kusema na zinahusu vyombo nya ulinzi na usalama mbalimbali ambavyo viko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kabla sijafikia hatua hiyo, nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na nataka niuthibitishie umma wa Watanzania kwamba mkiona vyaelea vimeundwa. Amani na usalama na utulivu wanaouona katika nchi hii ni kwa sababu ya kazi nzuri, kazi ambayo imefanywa na vyombo nya ulinzi na usalama na hususan Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa nchi yenyeheshima duniani na kuheshimika kwa kuwa na amani na usalama wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, nataka niwafahamishe Wabunge; kazi namba moja kabisa ya Jeshi la Polisi ni kumlinda Mheshimiwa Rais pamoja na Taasisi yake na ndio maana alipo Mheshimiwa Rais, Jeshi la Polisi tupo. Hainiingii akilini baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kusimama na kubeza kazi nzuri zinazofanywa na Jeshi la Polisi na kulibatiza majina mengine ya kejeli, kitu gani ambacho unakifanya wewe mpaka uone kwamba Jeshi la Polisi linahitaji kubatizwa majina ya namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi, siku mia tatu sitini na tano na robo hawana cha Jumamosi, hawana cha Jumapili, hawana cha Sikukuu, hawana cha mvua, hawana cha jua. Askari hawa wanafanya kazi kubwa halafu humu ndani anaibuka Mbunge anasema hata Askari kung'atwa na mbu hiyo ni kazi yao, ni majukumu yao na maneno hayo yanazungumza na mtu ambaye anaheshimika, Mheshimiwa ambaye ni Mchungaji na sisi waumini hatumwiti tu Mchungaji, tunamuita Baba Mchungaji, lakini anasema maneno ya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu hapa wanasema Jeshi la Polisi wanatumia lugha ambazo ni za

kuudhi, za kejeli, hazina staha. Nataka nikuhakikishie; wakati ule CAG aliposema Bunge hili ni dhaifu wapo baadhi ya Wabunge hapa walitetea kauli hizo ambazo ndizo za kejeli, kauli ambazo zinadhaliilisha Bunge lakini leo Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma, Kamanda ambaye amefundishika, Kamanda ambaye anajua kutumia lugha za Kibunge anasema "ole wao watakaoandamana kesho, watapigwa na watachakaa" hiyo ni lugha ya kufundishwa Askari ambaye amefundishika, hiyo ndio lugha ya kipolisi". (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie sisi Jeshi la Polisi tunazo lugha nydingi ambazo tukiongea hapa wengine hamtatuelewa. Kwa mfano, wewe unaitwa Mheshimiwa Zungu sisi Polisi tunakuита Zulu *uniform* Novemba *uniform* ndivyo tunavyokuita sisi, hawa hawatatuelewa. Tunaposema kwamba tunatumia lugha hizi, lugha hizi zinatokana na *preemption model*. *Preemption model*/kwenye Jeshi maana yake nini, nifungue darasa kwa wale walioikosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linapoona kwamba kuna mambo ambayo yanataka kufanyika, mikusanyiko isiyoruhusiwa, Jeshi la Polisi tunajiandaa kwenye vifaa ndiyo maana mtaona askari wanamwaga mahali wanatembea kikakamavu, wanafanya hivi kuona kesho uandamane uone cha mtema kuni. Wakati mwingine tunatumia lugha hizi kwamba ole wake na wale tunaowaambia lugha hizi ni wale watakaokuwa wahalifu, hii ni lugha ya kushughulikia wahalifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa Mheshimiwa Msigwa mara kwa mara namuona ananyanya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niende kwenye hiyo hoja ya mikutano ili tumalizane na akina Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Ruth Mollel na wote wale ambao mmekuwa mkiuliza ni sheria gani inawanyima haki ya mikutano ya ndani, inawanyima haki ya mikutano ya hadhara na mnisikilize vizuri ili leo tumalizane hapa. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipo apa kwenye Uwanja wa Taifa aliapa kuilinda, kuhifadhi na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais anapokuwa analinda na kuitetea ni kuhakikisha yale yote yaliyoandikwa humu yanatekelezwa na hayavunjiwa na mtu yejote na yeje kama Mkuu wa Nchi anasimamia hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20(1) unayoinua inasema hivi: "Kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo". (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20(3) inasema hivi: "Bunge laweza kutunga sheria inayoweka masharti yatakayohakikisha kuwa vyama vyaya siasa vinazingatia mipaka na vigezo vilivyowekwa na masharti ya ibara ndogo ya (2) kuhusu uhuru na haki ya watu kushirikiana na kujumuika.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 30 ya Katiba inaweka masharti ya mipaka na inasema hivi: "Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika sehemu hii ya Katiba hii, yanayofafanua misingi ya haki, uhuru na wajibu wa binadamu, hayaharamishi, naomba nirudie, hayaramishi sheria yoyote iliyotungwa wala kuzuia sheria yoyote kutungwa au jambo lolote halali kufanywa kwa mujibu wa sheria hiyo kwa ajili ya-

(a) Kuhakikisha kwamba haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma haviathiriwi na matumizi mabaya na uhuru na haki za watu binafsi. (*Makof/ Vigelegele*)

(b) Kuhakikisha ulinzi, usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii, afya ya jamii, mipango ya maendeleo mijini na vijijini haviathiriwi". (*Makof!*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa, Mheshimiwa Rais alipopiga marufuku mikutano hii ni kwa mujibu wa Katiba hii kwenye vifungu niliviyovieleza kwa maana kwamba mikutano hii...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: *Order, order.*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Sikiliza basi Mheshimiwa Msigwa.

MWENYEKITI: *Order, order.*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana kwamba mikutano hii isije ikavuruga mipango ya maendeleo, nimesoma Ibara hii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa Mbunge ukitaka kuongea unafuata utaratibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hebu ngoja kwanza. Waheshimiwa Wabunge, kama Serikali inajibu watu wote tukae kimya.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Hapana, ndiyo muda wake wa kujibu.

MBUNGE FULANI: Anadanganya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, anajibu ndiyo muda wake, sasa mnapoanza ku-*provoke*, mnakifanya Kiti kianze kuwa...

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa, kifungu cha 11(1) kinasema hivi: "Kila chama chenye usajili wa muda na usajili wa kudumu kitakuwa na hadhi ya-

(a) Kufanya mikutano katika sehemu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kutoa taarifa kwa Afisa Msimamizi wa Polisi wa eneo husika kwa ajili ya kujitangaza kwa umma na kutafuta wanachama. (*Makofii*)

(b) Kupata ulinzi kwa ajili ya usalama wa mikutano ingawa vyama vyenye usajili wa muda havitaruhusiwa kuweka mgombea au kufanya kampeni katika uchaguzi wowote wa Ubunge, Uwakilishi au Urais au Uchaguzi wa Serikali za Mitaa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (2) kinasema: "Bila kuathiri sheria nyingine, vifungu 43, 44, 45 na 46 vya Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322 vitatumika katika mikutano yote itakayofanyika ndani ya Jamhuri ya

Muongano na chama chochote hata kama kina usajili wa kudumu au usajili wa muda".

MBUNGE FULANI: Vifungu hivyo vinahusu ulinzi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (3) kinasema: "Kila chama chenye usajili wa kudumu kitakuwa na hadhi ya kuweka mgombea na pia kufanya kampeni kwa ajili ya mgombea yejote katika uchaguzi wa Wabunge, wawakilishi wa Urais au uchaguzi wa Serikali za Mitaa". (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (4), Mheshimiwa Ruth Mollel sasa unisikilize vizuri ili uone ni sheria gani tunatumia ya kuzuia mikutano yako ya ndani. Kifungu cha (4) kinasema: "Pale ambapo chama cha siasa kinapokuwa na nia ya kufanya mikutano au maandamano katika eneo lolote la wazi, hiyo ndiyo ya hadhara, au sehemu yoyote, maana yake sehemu ya ndani au wapi, kinatakiwa kutoa taarifa si chini ya saa 48 kabla mkutano husika kufanyika. Taarifa hiyo ni lazima iwe kwa maandishi itakayowalishwa kwa Afisa wa Polisi Msimamizi wa eneo husika ambapo mkutano husika unatarajiwa kufanyika. Ikitokea chama cha siasa Kimewasilisha taarifa kulingana na kifungu kidogo cha (4) chama hicho kinaweza kuendelea na mkutano kama ulivyopangwa isipokuwa kitakapopokea amri kutoka kwa Afisa wa Polisi Msimamizi wa eneo husika kutoendelea na mkutano husika, mkutano huo hautafanyika". (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zio hili ambalo linahusisha Sheria ya Vyama vya Siasa limeenda kutafsiriwa kwenye Sheria ya Jeshi la Polisi. Sheria ya Jeshi la Polisi, kifungu cha 42 kinasema hivi: "Mtu yejote atakayekaidi amri au kudharau au kutekeleza amri iliyotolewa katika kifungu kidogo cha (1) hapo juu atakuwa ametenda kosa na atakamatwa bila hati ya ukamataji na endapo atatiwa hatiani anaweza kuuhukumiwa kulipa faini au vifungo au vyote". (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kinaendelea kusema: "Pale ambapo mtu atawalisha taarifa ya maandishi kama ilivyoelezwa kwenye kifungu kidogo cha (1) anaweza kuendelea kuandaa au kukusanya watu au kuandamana kama ilivyopangwa isipokuwa tu pale anapopokea amri kutoka kwa Afisa wa Polisi Msimamizi wa eneo husika juu ya kusanyiko hilo au maandamano kutofanyika kama ilivyoelekezwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichotaka kuwaambia hawa Wapinzani ni nini? Tatizo la wenzetu hawa hawataki kutekeleza na kufuata Katiba. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wenzetu hawa hawataki kufuata sheria za Vyama vya Siasa na Jeshi la Polisi. Sasa mimi niwaambie, najua haya yote yanawasumbua kwa sababu mmekosa hewa ya *oxygen* upande mliopo. Ushauri wangu wa bure kwenye chama kingine cha siasa bado kuna *oxygen* ya kumwaga na kutosha, kama mnaona kufanya siasa huko hakuwezekani nendeni kwenye vyama vyenye *oxygen*. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe maelekezo kwa Jeshi la Polisi na naamini *IGP* unanisikia kwamba vyama vyote vya siasa na najua uchaguzi unakuja Novemba, najua kuna watu wanaokaidi na kutotaka kuzingatia sheria na najua sikio la kufa halisikii dawa, endeleeni kuhakikisha kwamba mikutano isiyoruhusiwa ni kweli hairuhusiwi na wale watakaokaidi waendelee kukamatwa. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja za Mheshimiwa Msigwa, mimi nakuheshimu sana. Mambo mengi sana yamesemwa humu kuhusiana na watu kupotea, kuuwawa, kutekwa lakini Mheshimiwa Msigwa alienda mbali zaidi akawa ananitaka mimi Waziri kwa niaba ya Serikali nitoe majibu kuhusiana na upigwaji risasi wa Mheshimiwa Tundu Lissu, kutoonekana kwa kina Ben Saanane na wengine aliotwaja. Maneno yote haya yanaletwa kwa sababu moja tu na sababu yenyewe ni kutaka Serikali na wananchi kuchonganishwa. (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Aaaa.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali pale ambapo tunaona Mheshimiwa Mbunge anatoa maneno ambayo kila kukicha tunapotoa maelezo lakini hataki kusikia, anabaki na kazi moja tu. Kazi moja hiyo kwa sababu ni Mchungaji, ukisoma kwenye Kutoka 23:1 inasema: “Usivumishe habari za uongo; usitie mkono wako pamoja na mwovu, kuwa shahidi wa udhalimu”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu ambaye ni mchonganishi ana shetani ndani yake. Biblia inasema mtu ambaye ni mchonganishi anakuwa ni mmiliki halali wa ibilisi shetani. Biblia inasema mtu ambaye ni mchonganishi anakuwa ni mtumwa wa shetani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba Bunge hili mnisikilize vizuri, nimekuwa nikieleza hapa nyakati mbalimbali kwamba taarifa zote za watu kupotea, kutekwa, kuuwawa, ambazo zimeripotiwa kwenye vituo vya Polisi zote hizi zina mafaili na upelelezi unaendelea. Katika mazingira ambayo upelelezi unaendelea, sisi tuna Jeshi la Polisi lenye weledi na teknolojia katika kufuatilia uhalifu ambao umetokea wa watu niliowataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulaumu Jeshi la Polisi na kutaka kuonesha kidole kwamba matukio hayo yanafanywa na Serikali, sisi kama Serikali hatutakubali. Ziko nchi nyingi ambazo wananchi wake tena wengine maarufu

wamepotea, wameuwawa lakini mpaka leo waliofanya matukio hayo hawajapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, nchi ya Marekani ambayo ina *FBI, Central Intelligence Agency* pamoja na taasisi nyingine 24 za Serikali kwa ajili ya usalama kuanzia mwaka 1947, miaka zaidi ya 72 alikufa pale Elizabeth Short aliyejewa anataka kujunga na *Hollywood* kwa ajili ya *movie*, mpaka leo pamoja na vyombo vyote hivyo wanaendelea kuchunguza, hawajampata aliyejewa na tukio hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani hapo hapo, kuna mwanamuziki Tupac Shakur, leo ni miaka 23 wanaendelea kuchunguza lakini hawajampata nani amefanya tukio hilo. (*Makofii*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata
utaratibu)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sisi Tanzania ambao tunaendelea na uchunguzi pale ambapo hatujapata mtuhumiwa aliyejewa tukio, kwa nini baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaonesha kidole kwa Serikali? Hii yote wanafanya kwa sababu ya kuchonganisha Serikali na wananchi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme bayana matukio mengine kama nilivyowahi kusema upelelezi unachukua siku nyingi na sisi Jeshi la Polisi tunashindwa kuunganisha *dot* za upelelezi kwa sababu baadhi ya wahusika hawataki kutoa ushirikiano. Umezungumzia kesi ya Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Msigwa nilikilize vizuri, unataka kusikia Serikali inasema nini kuhusu nani aliyempiga risasi Mheshimiwa Tundu Lissu, nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu baada ya tukio hili kutokea Polisi tulianza uchunguzi na hata kabla hatujaanza uchunguzi Madaktari wa Serikali kwa nia njema ya kunusuru uhai wa Mheshimiwa Tundu Lissu walikuwa mstari wa mbele kabisa na baada ya hapo kupitia

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma alimtaka dereva aliyekuwa na Mheshimiwa Tundu Lissu aje kwenye kituo cha Polisi atoe maelezo. Polisi hawa sio Mungu, Polisi hawa wanahitaji binadamu ambaye alikuwa kwenye tukio aje atoe maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu wakati huo dereva wa Mheshimiwa Tundu Lissu kwa jina Adam amekimbia na hataki kuonekana kuja kutoa maelezo kwenye kituo cha Polisi. Sasa sisi Jeshi la Polisi huwa tunaangalia na mazingira yanayozunguka tukio lilitokea. Kwa kuwa risasi zilizopigwa ni nyingi zaidi ya 38; na kwa kuwa risasi hizo zilimpiga Mheshimiwa Tundu Lissu kutokea alikokuwa amekaa kuelekea upande alikokuwa dereva lakini dereva alitoka akiwa hana kovu hata ukucha wake kupigwa risasi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inatia mashaka na ndiyo maana Jeshi la Polisi wanamtaka Adam aje atoe maelezo nini kilitokea. Pili kwenye gari mule walikuwa wawili tu dereva Adam na Mheshimiwa Tundu Lissu, yeye ni mtu muhimu sana wa kusaidia Jeshi la Polisi.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Sisi Jeshi la Polisi tunakosa usaidizi...

WABUNGE FULANI: Mwongozo, mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa wote mnaofanya fujo nawaona na nawa-note.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Hapana, Serikali inajibu na kama mtu ana hoja baadaye atatoa siyo sababu ya kufanya fujo ndani ya Bunge.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Unapomkatisha Waziri unakifanya Kiti kichukue hatua za Kikanuni. Nimekuona hapo Mheshimiwa. Endelea Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Wewe Mheshimiwa Heche tulia, hizi ajali gani kuanzia Chacha Wangwe dereva anatoka mzima, anakuja Mheshimiwa Tundu Lissu anatoka mzima halafu tuiseme?

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

WABUNGE FULANI: Kakae huko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, endelea.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo...

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Toa dozi, toa dozi Mheshimiwa Kangi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya watu wamekuwa wakitaka Jeshi la Polisi litumie sheria inayoitwa *Mutual Assistance on Criminal Matters* kwamba tunaweza tukam-summon mtu yejote ambaye yuko nje ya nchi akaja akatoa ushahidi. Hata hivyo, katika kesi hii matumizi ya sheria hii yangelenga kwa mtu ambaye anajificha asiweze kuja kwa hiari yake, kwa hiyo, tunatumia vyombo na nchi nyingine kumlazimisha huyo mtu aje lakini kwa dereva wa Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Tundu Lissu wenyele wanatakiwa waje kwa hiari yao na hivyo hatulazimiki kutumia sheria ya namna hiyo. Kwa

hiyo, katika mazingira ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu ametekeleza kesi yake, katika mazingira ambayo Adam hatakuja kutoa ushahidi, isitokee tena Jeshi la Polisi kulaumiwa katika mazingira ya namna hii.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo lingine, niende kwenye ujisadi ambao umeelekezwa kwenye Jeshi la Polisi. Wako Waheshimiwa Wabunge hapa wameelezea kuwepo kwa ujisadi ndani ya Jeshi la Polisi lakini taarifa za ujisadi huu wamezipata kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali na kama Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunahakikisha kabisa kwamba hakuna chombo chochote cha ulinzi na usalama ambacho kitakuwa na matumizi mabaya ya fedha, kitafanya ujisadi na ndio maana pale ambapo tunabaini kwamba ujisadi umefanyika tumekuwa tukichukua hatua ikiwa ni pamoja na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria ambao wanahuksika na ujisadi huu. Ujisadi mwingine ambao umetajwa kwenye taarifa ya CAG lazima niwe bayana CAG pamoja na mambo mengine amelihusisha Jeshi la Polisi na kashfa ya sare hewa na kwamba sare hewa hizi ni za shilingi bilioni 16.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, kwa moyo mkunjufu, kwa mikono yangu myeupe nikiwa kama Waziri makini, nikiwa kama Waziri ambaye ninaitakia mema nchi hii, nikiwa kama Waziri ambaye ninatetea rasilimali za Watanzania na tumuogope Mungu, sijawahi kuona mtu muongo kama CAG katika nchi ya Tanzania. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani sare zinazodaiwa kuwa hewa mimi Waziri ambaye nimekwenda kwenye *ma-container* na *ma-godown* ya Jeshi la Polisi. Ambapo nimekuta sare nyingi ambazo zimeletwa halafu CAG

anapeleka taarifa kwa Mheshimiwa Rais ya uwongo kwamba, hakuna sare za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nanyanya mikono juu, itakapofika jioni kama mimi nasema uwongo kwamba, hakuna sare hewa, kama nasema uwongo najivua nguo. Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tukiwa tumeambatana na maafisa wa *CAG* twende *main store* akaangalie ma-*container* zaidi ya 15 yenye futi 40, ma-*godown* matano ambayo yamesheheni sare za vitambaa, viatu, kofia na mikanda, halafu *CAG* anapeleka taarifa mbele ya Rais kwamba, Jeshi la Polisi wamepokea sare hewa na kulipa shilingi bilioni 16.6 na ninaweka uwaziri wangu rehani kama nasema uwongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuogope Mungu. Na kama tutaendelea kuwa na mtu anayefanya ukaguzi halafu anaenda anasema uwongo kwamba, kule kuna sare hewa, huyo mtu tumuogope kama ukoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilanza kuwa na wasiwasi inakuwaje Jeshi la Polisi liwe na Sare hewa? Sare ambazo nimeziona kwa macho yangu mimi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumuogope Mungu, sare hizo zipo, hakuna hewa...

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche kaa chini, mda wetu mdogo.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Heche kaa chini.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni na Katiba zinavunjwa.

MWEMNYEKITI: Mheshimiwa Heche utaratibu maamuzi yote ni ya Kiti. Kaa chini.

MBUNGE FULANI: Aaah!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, liligusiwa pia, suala la Lugumi. Kwamba, suala la Lugumi lilianza nikalichukua, sasa limeishia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya kubaini kwamba, chombo kingine cha Serikali (TAKUKURU) kwamba, wameanzisha uchunguzi na wakati ule nilikuwa tayari nimeshamuita Lugumi kwa ajili ya kuchukua hatua, suala hilo nililiacha mikononi mwa TAKUKURU, ili waendeleenalo na pale ambapo watakuwa wamelimaliza, jambo hilo litawekwa hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwathibitshie kwamba, wale wote waliokuwa wamekwapua fedha za *NIDA*. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tuliweza kuyaita makampuni tukanusuru fedha aslimia 84 ya fedha ambazo zilikuwa zimekwapuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hoja mbalimbali pia za Wabunge ambazo ni vema nikazigusia, hasa Vitambulisho vya Taifa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jana wakati umeelekeza mwongozo wa Mheshimiwa Felister Bura kwamba, kutakuwa na usajili wa simu na watanzania wanayo hofu. Napenda niendelee kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba, usajili wa Vitambulisho vya Taifa tunaendelea vizuri na ni lengo letu itakapofika Disemba mwaka huu malengo yetu ya kufikia milioni 24 ya Watanzania tutakuwa tumefikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana nikasema kwa kuwa mpaka sasa tumekwishafikia katika kusajili na kuweza kuandaa namba ya utambulisho wa Taifa, tumefika milioni 16 ambapo Watanzania milioni 16 wana uwezo wa

kwenda kusajili simu zao kwa mujibu wa masharti ya *TCRA*. Wale ambao hawataangukia kwenye hiyo milioni 16 sisi kama Serikali tumesema kwamba, si makosa ya wanaomiliki simu, tutaweka utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba, hakuna Mtanzania ambaye simu yake itakapofika Disemba itazimwa kwa sababu hajawa na namba ya utambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ambalo ni vema nikagusia, Naibu Waziri amezungumzia masuala ya ujenzi wa vituo vya Polisi, makazi ya askari kwenye Jeshi la Polisi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza tayari tumekwishaanzisha *The Police Force Cooperation Soul*, yaani hili ni shirika ndani ya Jeshi la Polisi. Tayari mkurugenzi mkuu tumemteuwa na wale wakurugenzi wa idara tumewateuwa, tayari wajumbe wa bodi tumewateuwa. Ni imani ya Wizara kwamba, watakwenda kukusanya fedha nyingi sana ambazo ni imani yetu kwamba, watakwenda kumaliza tatizo la makazi na vituo vya Polisi ndani ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye Jeshi la Magereza. Kwenye Jeshi la Magereza pia nigosie kwamba, tunaendelea kuhakikisha kwamba, ule mfumo wa ujenzi wa nyumba bunifu wa kila gereza tunauendeleza vizuri, ili kila mwaka kila gereza tumeshalielekeza lazima liwe na nyumba zisizopungua tatu mahali ambapo kuna gereza ili kuhakikisha kwamba, askari wetu wanapata nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri amezungumzia stahiki mbalimbali za askari, posho:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie askari wote kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, najua mnanisikiliza; la kwanza ambalo tumelifanya ni kuhakikisha kwamba, tunapitia sheria zote pamoja na kanuni zote, ili kubaini na kuorodhesha posho zote ambazo ni stahiki ya askari kwa sababu, kuna baadhi ya posho ambazo ziko kwenye kanuni au kwenye sheria, lakini askari hawajaanza kuzipata. Ni imani yangu kwamba, tutakapokuwa tumekamilisha zoezi hilo lazima tuhakikishe kwamba, askari

wanapata hizi posho ambazo zipo kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nijielekeze kwenye madeni ya wazabuni mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge wengine kwa maandishi mmezungumza hapa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli inaendelea kulipa madeni ya wazabuni na watoa huduma. Na ndio maana wapo wazabuni kwenye vyombo hivi vya ulinzi na usalama tumeanza kuwalipa fedha. Wale ambao madeni yao yamekwishahakikiwa naomba waendelee kuamini kwamba, madeni yao yatakwenda kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja ya Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Kagera, hususan kwenye suala la uhalifu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara kwenye Mkoa wa Kigoma, alipofanya ziara kwenye Mkoa wa Kigoma, pamoja na mambo mengine na taarifa ya Ulinzi na Usama aliyoipata ni kweli kabisa kwamba, mazingira ya Mkoa wa Kigoma na sehemu ya Mkoa wa Kagera hali ya uhalifu wa kushtukiza na hasa wenye silaha za moto kutoka nchi jirani ya Rwanda au Burundi wamekuwa wakiingia. Na ni kweli kabisa tukiweza kufunga milango ya mipakani ni kweli tutapunguza uhalifu wa silaha ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari tumeanza kutekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu ambapo Jeshi la Polisi wanaendelea na mchakato wa kutathmini na kuangalia vigezo ambavyo vinasababisha maeneo gani ambayo yanaweza yakatengwa, halafu tukayatafutia mkoa maalum wa kipolisi au kanda maalum ya kipolisi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaotoka maeneo yale naomba muwe na amani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigosie jambo lingine la wahamiaji haramu. Wahamiaji haramu Mheshimiwa Kitandula amegusia, Wataita pamoja na Wakamba maeneo ya Mkinga wana maingiliano na nchi ya Kenya na kwamba, kuna usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge. Na ndio maana hata juzi Waheshimiwa Wabunge kutoka Kigoma mliweza kutusifia *Immigration* kwamba, sasa ile kero ya kutumia pua au kuimba wimbo wa Taifa kwamba, huyu ni Mrundi au sio Mrundi imeanza kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie Wabunge kwamba, tutaendelea kudhibiti mipaka na tutaendelea kupambana na uhamiaji haramu mpaka tutakapoutokomeza. Na ndio maana wahamiaji haramu wengine ambao tayari tumekwisha wakamata tunafanya mpango wa kuwarudisha makwao. Na ndio maana katika kuwarudisha makwao tumeendelea pia kupata taarifa za madalali au watu wengine Watanzania wenzetu ambao wanashiriki katika kuwatafutia usafiri ama kuwahifadhi, ili tuweze kuvunja mitandao hii ya uhamiaji haramu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigosie suala kwa ujumla la usalama barabarani ikiwa ni pamoja na kero ya bodaboda:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie na niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, kama kuna eneo ambalo sasa tunafanya vizuri ni kwenye kikosi cha usalama barabarani ndani ya jeshi la Polisi. Sasa hivi kikosi cha usalama barabarani zile rushwa zile ambazo ziliikuwa zinatuhumiwa sasa zinaenda kwisha. Na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwa sababu, wengine pia mlikuwa mkiombwa, lakini siku hizi hamusemi kwa maana hali inaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, ajali zimepungua kwa asilimia 38.7. Na kielelezo kwamba, tunafanya vizuri ni kupungua kwa ajali na hasa ambazo ziliikuwa zinachukua vifo

vya watu wengi ikiwa ni pamoja na watu kupata vilema, pamoja na uharibifu wa mali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana huko mbele tunakokwenda, hilo shirika la Polisi nililolisema litaenda mbele zaidi kuhakikisha kwamba, wanapata wawekezaji ambao wana fedha na sisi Serikali hatutoi hata senti tano kwa ajili ya kuanzisha vituo maalum vya ukaguzi wa magari katika nchi nzima. Tutakapokuwa tumemaliza hilo ni imani yangu kwamba, magari mabovu yote yatatoka barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda nimeshatoa maelekezo na hayo maelekezo ni vema nikayarudia. Ibara ya 4 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia kwamba, Serikali zote mbili zitatumia nguvu zake zote kuhakikisha kwamba changamoto kubwa nne zinafanyiwa kazi. Changamoto ya kwanza ni kuondoa umasikini. Changamoto ya pili ni kutatua tatizo la ajira hasa kwa vijana na changamoto ya tatu ni vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali na ya nne ya mwisho ni kuendelea kudumisha amani, usalama, utulivu na kulinda maisha ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bodaboda ni eneo ambalo wamejitekeza kama kujiajiri na hawa ni vijana wanajiajiri. Nimetoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi kwamba, bodaboda hawa kwanza lazima wafuate sheria za usalama barabarani kama chombo kingine chocchote ambacho kiko barabarani. Hawaruhusiwi kubeba mshikaki, hawaruhusiwi kutokuwa na leseni, hawaruhusiwi kutovaa kofia lazima wavae, lazima waende *speed* inayotakiwa, sheria zote na watengeneze bodaboda zao. Lakini tumepeiga marufuku namna walivyokuwa wanakamatwa na nikaelekeza kwamba, bodaboda za aina tatu tu ndizo zitakazokamatwa na kupelekwa kwenye kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la kwanza la bodaboda ni bodaboda ambayo imehusika kwenye uhalifu. Bodaboda ya pili ni iliyo husika kwenye ajali na bodaboda ya tatu ni ile ambayo ni ya kuokota, haina mwenywewe. Bodaboda ambazo haziko kwenye makundi hayo

zisikamatwe na kupelekwa kituoni, tunachofanya ni nini, na nimetoa maelekezo; pale ambapo Askari wa Usalama Barabarani hakumuonya, akaamua kumpiga *fine*, atampiga *fine* na ye ye atakwenda atafute *fine* yake kwa muda wa siku saba sawa na wenye magari. Na atakaposhindwa ndani ya siku saba nimeelekeza namna ya kuwapata hawa bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia kwa kuwa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 inawataka pia, halmashauri wawe na hawa Polisi *auxiliary*. Ma- wote nchi nzima washirikiane na wakurugenzi wa halmashauri zote nchi nzima. Hizi halmashauri zina viongozi kuanzia vitongoji, vijiji na kwa mijini kwenye mitaa yote, kila bodaboda hapa nchini lazima aisajili kwa kiongozi wake mahali anapoishi. Atasajili namba ya bodaboda yake, jina la dereva au mmiliki wa bodaboda, baadaye orodha zile zitakusanywa ndani ya ile halmashauri, mkurugenzi ataingiza kwenye *database* halafu atazalisha *database* ile ataipeleka kwa *DTO*, yani Mkuu wa *Traffic* katika wilaya ile. Na asubuhi askari wa usalama barabarani watakapokuwa wanaenda kazini mojawapo ya kitendea kazi ni orodha ya bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bodaboda atakapokuwa ametenda kosa ataangalia namba, akiangalia kwenye orodha yake bodaboda haipo atajua huyu hajasajiliwa mahali kwa hiyo, hilo nalo tutadhibiti wizi wa bodaboda. Na bodaboda hiyo ambayo hajjasajiliwa lazima atoe maelezo na ile ambayo ataikuta kwenye orodha ata-*indicate* kwamba wewe tarehe fulani unatakiwa uwe umelipa *fine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huo katika nchi yote ya Tanzania hakuna bodaboda atakayetuchenga na hatutahangaika na bodaboda kwa sababu tutakuwa tunajua mahali walipo na namna ambavyo tunaweza tukawasaidia kwa sababu, lengo sio kuwasumbua bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa wafanyabisahara ndogondogo, almaarufu mamantilie au mamalishe. Vijana wanachoma chips wanakaanga chips:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na sintofahamu wakati mwininge, llani hii inasema waondoe umasikini; sasa kama mamantilie anasumbuliwa biashara zake, babalishé anasumbuliwa biashara zake. Lazima Jeshi la Polisi mahali walipo watafute namna bora ya kuwalea hawa wafanyabiashara ndogondogo. Na pale ambapo wanajihuisha na makosa ya kipolisi ya kijinai, waweze kuwaelekeza namna bora ya kuendesha biashara yao na sio kila wakati kuwafunga mashati halafu wanashindwa kufanya biashara zao watu masikini hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la kusisitiza kesi za kubambikiza pamoja na dhamana. Wamesema Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba, kweli kwenye magereza zetu hapa nchini kuna baadhi ya kesi ndogondogo ambazo watu wako mahabusu kule magereza au kesi ndogondogo mtu amefungwa yuko kule magereza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliarifu Bunge lako Tukufu tumeishakubaliana na Waziri wa Katiba na Sheria namna ambavyo tutakwenda kutumia hizi *Mobile Courts*, namna ambavyo ushauri uliotolewa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ya kuhakikisha kwamba, tunatengeneza kamati za kutembelea magereza kila wakati kwenda kuwabaini wale ambao kwa kweli wako kule, lakini hakuna sababu za msingi kuendelea kulundikana kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimuombe Mheshimiwa Esther Matiko katika hili wewe ni shuhuda mzuri, kuna watu walikuwa wanasema msongamano magerezani wengine wanatoka na ukurutu, wengine wanatoka na vifua, lakini tumeshuhudia Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Mbobe wametoka kule wako vizuri tu kwa hiyo, magereza yetu wanakula vizuri na wanalala vizuri na wanatoka wakiwa na afya njema kama mnavyomuona Mheshimiwa Esther Matiko anavyong'ara. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala alilolisema Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Esther Matiko mpaka sasa bado mimi Waziri haijaniingia akilini kwamba, kwenye kituo cha Polisi na ukavitaja baadhi ya vituo vya Polisi kwamba, wako Polisi wetu ambao wanalawiti watuhumiwa kinyume na maumbile, watuhumiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo kama kweli litakuwa na ushahidi kwa sababu, kuna mambo yanaweza kufanyika, lakini yakiwa na ushahidi. Nimuombe Mheshimiwa Esther Matiko aligusia wakati anachangia kwamba, kuna *RCO* alienda magerezani pale kwa hiyo, niombe unisaidie jina la huyo *RCO*, ili tupate mahali pakuanzia, pengine tunaweza tukaona kwamba, jambo hili lilitokea kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi mmehitaji vituo kwenye maeneo yenu, mmehitaji magari au pipipiki akiwemo na ndugu yangu Mheshimiwa Suzan Kiwanga, Mbunge wa Mlimba. Changamoto ya Mlimba pale naifahamu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na ndiyo maana nimekuwa nikiongea na Halmashauri zilizopo kule; Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, kwamba sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunapokuwa hapa Bungeni, tunagawana sungura mdogo huyu. Tunapomaliza kugawana, baadhi ya Wizara wanakwenda kule kwenye Halmashauri zao wanagawana sungura mwingine tena. Sisi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi tunakosa fursa kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni Madiwani kwenye Halmashauri zetu. Nimezunguka, kuna baadhi ya Halmashauri kwa kweli wanatenga fedha. Kuna maeneo ambapo wananchi wameshaonyesha nguvu zao, yapo maboma; nawaomba kwenye hizo Halmashauri pia, vyombo hivi vya ulinzi na usalama na vyenyewe vinatoa huduma kama ambavyo darasa linatoa huduma. Kama ambavyo kwenye elimu mwalimu anahitaji nyumba; nasi Askari tunahitaji nyumba. Mahitaji ni yale yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge kwenye Halmashauri zenu mjaribu kushawishi, nami nitaendelea kuwasiliana na Waziri mwenzangu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili tuone namna ambavyo tunaweza tukasaadia maeneo hayo. Mheshimiwa Suzan Kiwanga ahadi yangu ya kuja Mlimba bado iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mkuchika, masuala yanayohusu mishahara, maslahi pamoja na vyeo, ametoa kauli ya Serikali hapa leo. Pia ni wahakikishie Askari wote kwenye vyombo vyote vya ulinzi na usalama na katika hotuba yangu nimeeleza, nimeeleza...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa Waziri, muda wako umekwisha.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba Askari wapo ambao tumewapandisha vyeo hivi karibuni na wapo wale ambao mchakato wa kuwabaini na kuwapandisha vyeo unaendelea. Kwa hiyo, wafanye kazi bila kuchoka kwa sababu mchakato wa kuangalia maslahi ya vyeo unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nataka ni wahakikishie Watanzania na Bunge hili kwamba pamoja na kasoro ndogo ndogo ambazo zinajitokeza kwa baadhi ya askari, endeleeni kuliunga mkono Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama, wanafanya kazi kubwa. Hatuwezi kukata tamaa, na ndiyo maana wale wachache ambao wanataka kuharibu taswira ya Jeshi la Polisi, tumeonyesha kwenye hotuba yetu kwamba tumekuwa tukichukua hatua

za kuwashusha vyeo na wengine kuwafukuza kwa aibu. Kwa hiyo, nasi hatuvumilii na kukaa na watu kama hao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna nyongeza ya wageni walioingia Bungeni jioni hii. Wageni waliopo Jukwaa la Spika, ni wageni sita wa Mheshimiwa Spika kutoka nchini Ujerumania ambaao ni *Honorable Eva-Maria Schreiber Member of Parliament, Federal Parliament of Germany, welcome to the Parliament.* (*Makof*)

Mr. Manuel Faber, Staff Member MPs office, Mrs Katrin Voss, Officer Left Party National Office, Dr. Renate Wolf Translator, Dr. Richard Shaba Head of German Liaison Office, Dodoma and Dorothee Braun, Country Director Rosaluxemburg Foundation, karibuni Dodoma. (*Makof*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, ni wageni 65 wa Mheshimiwa Jasmine Tisekwa ambaao ni wanachuo wa Chuo cha Kilimo cha Sokoine kilichopo Mkoani Morogoro; Ndg. Boniface Elias Mgeni kutoka Dar es Salaam ambaye amekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. (*Makof*)

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kif. 1001 – *Admini. and
HR Management.....Sh.14,437,065,109/=*

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu michango mingi wakati inaelezwa na wakati Mheshimiwa Waziri anajaribu kujibu, amegusia suala la tuhuma za ubadhirifu wa fedha kupitia manunuzi ya sare na vitu mbalimbali; sasa tunafahamu kwamba kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG*, Jeshi la Polisi ni moja kati ya vyombo ambavyo vinatakiwa kuonyesha mfano na malalamiko haya yamekuwa ni endelevu na Ripoti ya *CAG* kila inapotoka Jeshi la Polisi lipo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamani sana kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri atuambie kama Bunge na kama maelezo hayatajitosheleza nitashika shilingi na nitaomba Wajumbe waniunge mkono, tunataka kufahamu, nini msimamo wa Serikali kupitia Wizara juu ya mwendelezo wa upotevu wa mali hizi ambazo zinaendelea kuonekana na ubadhirifu wa *billions* za fedha zinaendelea kupotea ndani ya Jeshi la Polisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti na Kanuni yetu ya 37(7) tumewahisha taarifa. Sasa hivi Kamati ya *PAC* na Kamati ya *LAAC* inafanya kazi Ripoti ya *CAG* na Serikali sasa hivi inaandaa majibu. Kwa hiyo, sitampa

fursa tena Mheshimiwa Mbunge kwa sababu umewahisha shughuli na shughuli hii itarudi Bungeni mwezi wa Tisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Jitu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba katika mchango wangu niliochangia kwa maandishi, ningependa Mheshimiwa Waziri atolee ufanuzi au atupe majibu kuhusu jambo la Wizara hii na majeshi ambayo yapo chini yake hususan Jeshi la Magereza na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; ni jinsi gani Wizara na Serikali kwa ujumla wamejipanga kuhakikisha kwamba majeshi haya yanapatiwa zana, uwezo na vifaa vya kutosha ili kwa mfano, kwa upande wa Magereza waweze kuzalisha na kusaldia kuendeleza elimu kwa wale ambao wamefungwa kusudi wakitoka wawe na ujuzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Magereza ina wataalam wa kutosha tatizo kubwa ni nyenzo za kufanya kazi. Wizara na Serikali imejipangaje kuwawezesha hata kwa mkopo badala ya kupitia kwa mfumo wa bajeti ili waweze kukopeshwa kama taasisi nydingine yoyote waweze kuijendeleza na waweze kutoa huduma nzuri ili waweze kufanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nao badala ya kutegemea bajeti ya kununua vifaa, kwa nini pesa ya mabilioni tunayokusanya kutokana na ada mbalimbali kwa jina la Zimamoto (*Fire Inspection Fee*); kwa nini asilimia 20 ya fedha zile zisiende moja kwa moja iwe *ring fenced*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zinatosha kabisa kununua vifaa vya kuzimia moto na kama wana uhakika kila mwaka kutakuwa na bajeti, wanaweza wakatumia ile kukopea na vifaa vingine wakawa wanalipa kila mwaka kutokana na fedha ambazo zinakusanya kwa jina la Zimamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu na kama majibu hayataridhisha, basi nitaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tujadili na waunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashika shilingi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja yake Mheshimiwa Mbunge, naomba nimtaarifu kwamba kwa upande wa Jeshi la Zimamoto, bajeti iliyopita tumeweza kupata shilingi bilioni tatu ambazo zinasaidia kwa ajili ya kununua baadhi ya magari ya kuzimia moto. Kama hiyo haitoshi, pia tumeweza kuwa na utaratibu wa kupata masharti ya mikopo nafuu kupitia Austria ambapo tunataraja kupata vifaa lakini tunaimarisha na mahusiano na nchi nydingine ili kuweza kupata vifaa kwa njia ya mahusiano kati ya Jeshi la Zimamoto la nchi yetu na nchi nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Magereza, kuna jitihada ambazo zimefanyika tayari. Tunavyozungumza, tumeya-mark Magereza 10 ya kimkakati na katika Magereza hayo tumepeleka matrekti kwa ajili ya kuweza kusaidia kukamilisha malengo haya ikiwemo pia kwenye Gereza la Kwitanga kule Kigoma kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu za kufufua zao la michikichi. Kule peke yake tumepeleka matrekti mawili pamoja na vifaa vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa ujumla tunajitahidi kadri ya hatua kwa hatua kuweza kupunguza changamoto ya vitendea kazi katika majeshi yetu haya mawili.

MWENYEKITI: Sasa hivi wana miradi yao ya ujenzi, kwa hiyo, wanapata *extra funds*. Mheshimiwa Jitu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono tujadili

suala hili kwa sababu ni maeneo yote mawili muhimu sana Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lakini pia kwa upande wa Jeshi la Magereza kuboresha huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu najua ni ndogo na kutokana na mapato yetu ya ndani, lakini kuna njia nyingi sana...

MWENYEKITI: Toa hoja.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wenzangu waniunge mkono ili hoja hii ijadiliwe. Naomba kutoa hoja.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa jana kuna maswali nilimwuliza Mheshimiwa Waziri na kwa bahati mbaya niseme katika majibu yake aligeuza Bunge kama Mkutano wa Hadhara na hakutoa majibu. Niliiomba Serikali itoe taarifa ya kina kwa sababu Jeshi la Wananchi linawatumikia wananchi, nasi wananchi tunayo haki ya kujuu utendaji wa Jeshi la Wananchi. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hatupendezwi na vitendo vibovu ambavyo Askari wetu kwa mfano kule Kibiti walipoteza maisha, hakuna raia mwema wa Tanzania atakayefurahia kitendo hicho. Nilieleza na nikatoa mfano kwamba mpaka Mheshimiwa Rais aliliambia Jeshi la Polisi kwamba Watanzania sio wajinga kuhusiana na tukio la Mo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezungumza pia tukio la Mheshimiwa Lissu kwamba dereva wake hakupatikana, ndiyo maana mmeshindwa kufanya upelelezi. Nilitoa mfano kwamba Mheshimiwa Nape alionyeshwa bastola, ni kituo gani ambacho Mheshimiwa Nape amehojoja maelezo yake? Kwa sababu tukio la Mheshimiwa Lissu umesema mmeshindwa kufanya kazi kwa sababu Adam hakuja. Mheshimiwa Nape ni wapi amehojoja toka ameonyeshwa bastola hadharani? Azory, ripoti iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka, ili tuwe *comfortable* na Jeshi, tunalipenda Jeshi la Polisi na msipotoshe kwamba hatulipendi; tunalipenda sana. Hata huko vituoni kuna wakati huko Majimboni wanakuwa hawana mafuta, tunatoa tunasaidiana, huko kwetu; na tunawahitaji sana. Tunataka Jeshi la Polisi liwe *transparent* ili wananchi tuwe na imani nalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa namna gani Polisi au Serikali inatoa ripoti ya uwazi kwa matukio makubwa haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiporidhika na majibu yake, nitaomba nitoe shilingi na Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuchangia. Kwa hiyo, namtaka Mheshimiwa Waziri atuambie, aji-*commit* namna gani wanatoa maelezo ya kina kwa hawa watu ambao nimewataja; akina Roma Mkatoliki, Azory, Mawazo yaani yale matukio makubwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu Baba Mchungaji aniacchie mshahara wangu, kwa sababu hayo matukio yote aliyojasema, nimeeleza Bunge lako Tukufu kwamba matukio hayo yote bado Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi. Sasa anataka taarifa ya namna gani? Kwa sababu taarifa ndiyo hiyo kwamba matukio hayo bado tunaendelea na upelelezi. Upelelezi utakapokuwa umekamilika, kama tutakuwa tumepata wahusika, tutawafikisha Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumzia la Mheshimiwa Nape. Mheshimiwa Nape ilikuwa ni juu yake ye ye ambaye kama ameona ametendewa tukio, ndiye angeenda kwenye *the nearest Police Station* akaripoti kesi yake, lakini mpaka leo hatuna RB yoyote kwenye kituo chochote cha Polisi ambapo ameripoti.

Kwani wewe Mheshimiwa Msigwa, wewe ni Baba Mchungaji, kwani waumini wakati wa matoleo (sadaka), hicho watakachokitoa, ukikuta ni kidogo wakati unahesabu, utarudisha mabakuli na kuwaambia tena kwamba toeni tena sadaka hazijatosha? Unataka maelezo ya namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba anirudishie tu mshahara wangu.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Kangi. Naomba nitoe hoja Wabunge tujadili kuhusiana na majibu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kabisa, naendelea kung'ang'ania mshahara wake. Naomba kutoa hoja.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwamba bado Serikali haijatupa majibu ya kina Watanzania juu ya raia wengine ambao wameuawa kama Mawazo; juu ya raia ambao wanapigwa risasi kama Mheshimiwa Tundu Lissu; ambao wamepotea kama Ben Saanane, Simon Kanguye aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri kule Kigoma mpaka leo na wengine wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona Kamanda Baro alivyopigwa risasi Mwanza, haikuchukua muda polisi wakawa wamesema wamewakamata wale watuhumiwa. Ni kwa vipi sasa hawa raia wengine ambao wanaendelea kupotea na

kuuawa hatupati majibu ya kina, badala yake Mheshimiwa Waziri anakuja hapa anatuambia mambo mengine lazima yasubirie taarifa zitakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi lina intelijensia ya kutosha kuweza kuchunguza na kujuu hawa watu waliompiga risasi kwa mfano Mheshimiwa Tundu Lissu, hawa watu waliomteka Ben Saanane, hawa watu ambao wameondoka na Simon Kanguye ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri kutokana na CCM mpaka leo hajulikani alipo; hawa watu waliomuua Mawazo mpaka leo hatujajua ni akina nani, ingawa kuna taarifa, lakini hakuna hata mtu ambaye amekamatwa, atupe majibu ya kina...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mollel.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hoja ya Mheshimiwa Mchunguaji Msigwa kwa sababu hakuna kazi kubwa kama kuchunguza kesi ambaye anayesababisha tukio ndio wa kwanza kumkuta kwenye kilio na akilazimisha uchunguzi ufanyie. Mheshimiwa Waziri amesema hajakataa haya yote kufanyiwa kazi, lakini ameonesha jinsi ambavyo uchunguzi ulivyo mgumu, kama ambavyo leo dereva aliyekaa na Mheshimiwa Tundu Lissu pembedi mpaka leo haonekani lakini ye ye hajaguswa na risasi; kama ambavyo tumeona kwamba baada ya mikutano mingi kuahirishwa imeonekana hata matukio ya mauaji yamepungua. Maana yake kuna mahusiano makubwa ya ile mikutano na wale watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa anakumbuka vizuri ambavyo figo za Mheshimiwa Tundu Lissu zilipata shida kurekebishwa kwa zaidi ya miezi miwili Kenya kutokana na makosa yake ye ye mwenyewe kwa kung'ang'ania kukaa kwenye ndege ambayo Madaktari walitakiwa wakae, hatujui ni kwa nini aling'ang'ania kukaa pale akanyima Manesi kukaa kwenye

ndege na mwisho wa siku tukamfikisha Mheshimiwa Tundu Lissu hospitali...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa kwa sababu kuu mbili; kwanza ukisoma hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani imejaa matusi, kejeli na udhalilishaji wa Jeshi la Polisi. Serikali yetu inafanya kazi kubwa sana, hususan Jeshi la Polisi, uchunguzi hauletwi Bungeni, uchunguzi unapelekwa mahakamani. Matokeo yake kesi inasikilizwa na watuhumiwa wanahukumiwa, lakini hauletwi humu Bungeni, kwa hilo siungi mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kueleza tu masikitiko yangu kwa jinsi tunavyojadili hili jambo, tunazidi kuifedhehesha Serikali, tunazidi kulifedhehesha Jeshi la Polisi. Kwa sababu Waziri alivyozungumza ni kana kwamba tayari wana tetesi na mhusika, kwa nini asikamatwe? Dereva alikuwa hapo Kenya, Kenya sisi tuna uhusiano mzuri katika Nchi za Afrika Mashariki, lakini nikwambie siku ile ya tukio mimi nilikuwepo na RCOndio aliyeniomba mimi nimtafute dereva ili aende akatoe gari na mimi nilimwagiza Mheshimiwa Komu dereva akapatikana gari likaenda kuondolewa; mlikuwa mnamuhitaji dereva kwa nini msimkamate? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini isitoshe, kitaalam risasi inaweza ikajulikana imetengenezwa wapi, imenunuliwa na nani, imepigwa kwenye bunduki gani, na *CCTV cameras* zipo. Mheshimiwa Kangi amezungumza habari ya dereva wa Chacha Wangwe, amesahau dereva wa Chacha Wangwe

alishtakiwa na akahukumiwa? Kwa hiyo msijaribu kufanya hili jambo ni la kisiasa, namna mnavyolijadili ndiyo namna mnavyoonesha Serikali inahusika na polisi hawataki kufanya kazi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Heche.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili maisha ya watu, hawa tunaozungumzia ni binadamu na ni bahati mbaya sana kwamba Bunge hili linatumika kwa watu wengine ambao wana tuhuma za mauaji na mama zao walikuwa Mawaziri wakapenyea hapo, kuja kuhalalisha mambo ya kuendelea mauaji humu ndani. Tunataka majibu akina Azory Gwanda wako wapi, wana watoto kama wewe Mheshimiwa Kangi; tunataka majibu waliomuua Mawazo ni akina nani na ni kazi ya Jeshi la Polisi kutupa hayo majibu. Hatuwezi sisi wenyewe kwenda kuchunguza, wenyewe vyombo na wenyewe utaratibu wa uchunguzi ni Jeshi la Polisi na ndicho anacho-*demand* Mheshimiwa Mchungaji Msigwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeleta *politics* za nini hapa, kwenye jambo ambalo tunazungumza kwamba watu wamepoteza maisha, wameacha wake zao wajane, wameacha watoto wao yatima, wameacha mama zao, halafu tunaleta mambo ya mzaha kwenye maisha ya watu. Tunaliweka Taifa kwenye *risk* kwa mambo ya kihuni kabisa ambayo hayatakiwi kuja humu Bungeni, mambo ya mzaha hayo kafanyieni huko barabarani.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Marwa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuseme ukweli, hivi kwa nini CHADEMA wanamkatalia dereva wa Mheshimiwa Lissu, kuna siri gani? Nashauri ni vizuri hawa akina Mheshimiwa Heche na wenzake wakamatwe ili wawe mashahidi wa nani alihuksika kwenye tukio la Mheshimiwa Tundu Lissu kwa sababu haiwezekani leo dereva wa Mheshimiwa Lissu wamkatalie, Mheshimiwa Lissu mwenyewe sijui wamemficha wapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikie sehemu tuache mizaha, hawa akina Mheshimiwa Heche na wenzake wakamatwe wakawe mashahidi nani aliyempiga Mheshimiwa Lissu. Haiwezekani Taifa tukaendelea kwa namna hii, hawa ni wahusika wakubwa hawa, hususan huyu Mheshimiwa Heche huyu, nina mashaka na huyu Mheshimiwa Heche. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Boniphace.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Naomba Mheshimiwa Mchungaji Msigwa amrudishie Waziri shilingi yake. Waziri amejieleza vizuri na kuna vitu vingine mtu alisema hapa kwamba kuna watu wanafanya mambo ya kisiasa yawe siasa; tumeona Marekani, Marais zaidi ya wanne walliuawa, lakini Rais maarufu sana John Kennedy alliuawa hadharani, taarifa zake zilienda Bungeni zikaahirishwa mpaka leo, kwa mujibu wa Marekani ni miaka 30 inapopita watu watoe taarifa hadharani, lakini ya John Kennedy ilivyofika miaka 30 haikutolewa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema anaendelea kufanya uchunguzi, tuone inavyokwenda, lakini huyu mnayeita mgonjwa aliye pigwa risasi. Mgonjwa wa kwanza duniani kutoka kitandani na kwenda kuhubiri mambo mabaya ya nchi yake. Ni wapi sasa alipopigwa au kuna njama zingine? Maana yake zipo taarifa kwamba huyu dereva wake alimwekea *bullets* ambazo hazina athari kwake. Hivi ni kwa nini huyu dereva na huyu mgonjwa anayetembea duniani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Alberto.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sioni kwa nini tunafanya *spinning* katika jambo muhimu kama hili, au kulidogosha, kulifanya kama jambo la

Mheshimiwa Tundu Lissu. Hili sio jambo la Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Tundu Lissu ni mtu mmoja tu; tunachodai ni Serikali kuchukua fursa hii ili ijisafishe, isafishe Jeshi, kwa sababu kuna lawama kubwa ya watu kupotea, ya watu kupigwa, ya watu kuteswa, *there is no need ku-argue.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Mheshimiwa Juma Kombo aliuliza swali, kisha akasema anapenda iundwe tume kuchunguza kwa nini Jeshi letu la Polisi lime-retrogress mpaka kuwa lina lawama kubwa ya kutesa, ya kupiga, ya kupoteza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jamani anachotaka Mheshimiwa Mchungaji Msigwa; *tusifanye politics, we should not spin this,* hii ni kwa ajili ya nchi yetu. Tutengeneze mazingira, kwa mfano, polisi hata siku moja hawajatuambia kama, ya Akwilini walituambia *case closed.* Tumeridhika japo kwa wengine wakakamatwa kwa *case closed* akina Mheshimiwa mzee Mbobe na wengine wakashtakiwa kwa *case closed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachotaka ni kwamba ili tujenge taswira ya Jeshi letu, ili tuwe na imani na nchi yetu yatengenezwe mazingira tuone, tusione mzaha kusema kwamba babu yangu alipotea mwaka gani, katika Umoja wa Mataifa kuna kitengo kinacho-dea/na watu waliopotea, je, mnataka tukaripoti huko, halafu mtuambie kwa nini tusimalizane hapa? Tunaweza kwenda kuwaambia Umoja wa Taifa kwamba kuna *list* ya watu kadhaa wamepotea na wakaja wakachunguza kama wanavyokwenda nchi nyingine, lakini tunatoa fursa kwa Serikali *you should clean your house, if you clean your house you clean our house as well.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sophia, ajiandae Mheshimiwa Khamis.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa juu ya suala la polisi kuwajibika kwa kazi yao kutuambia watu wanaopotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja akipotea hata kama ana miezi miwili, hata kama ni mimba ikitoka na ukaitoa kwa bahati mbaya au kwa makusudi lazima uwajibishwe. Kwa hiyo, naunga mkono hoja hii, kwamba tunahitaji kupata taarifa kwa sababu leo tunazungumzia habari ya akina Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini kesho hatujui ni nani anafuatia. Wajibu wa polisi ni kuhakikisha maisha ya watu yako salama na wale ambao wamepotea tunahitaji tupate taarifa zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumze katika Bunge hilli kwamba tunapoleta sasa, mtu mmoja ametoka kusema hapa CHADEMA tunajua; sisi tulisema kama ninyi mnashindwa tulete watazamaji wa kimataifa, kama ni Mheshimiwa Mbewe, kama ni sisi tukamatwe na tuhukumiwe kwa makosa tuliyoyafanya, lakini mkasema mnaweza kufanya ninyi wenyewe. Sasa kama inachukua miaka 72 kama anavyosema Mheshimiwa Waziri tusubiri miaka 72 tupate taarifa za akina Azory Gwanda na wengine, mimi nafikiri si sawa, nafikiri tufanye kazi kama taifa kwa ajili ya usalama wa Watanzania tukiwepo na sisi Wabunge na watoto wetu na watu wengine pia ambao wanapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusimamia hoja ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa. Ahsante sana.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa. Mimi kwanza kwa masikitiko makubwa kwa Wabunge wenzetu ambao ni wananchi wa Tanzania na kwa sababu mambo haya hayajawakuta wao wanaona kwamba ni jambo la kawaida, lakini kule Zanzibar kuna mtu anaitwa Ally Juma Suleiman, huyu mtu alikwenda akafuatwa nyumbani kwake, akatekwa, akapigwa, akateswa, mwisho akatupwa msituni na akapelekwa hospitali siku ya tatu amefariki, hakuna mtu yejote mpaka leo

aliyekamatwa wala uchunguzi wa kesi hii. Halafu leo mtu anakuja hapa anasema kwamba hakuna jambo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mwananchi wangu, mpigakura wangu jimboni anafanya shughuli zake Dar es Salaam, anaitwa Khalfan, anafanya shughuli za sonara, amekwenda kuchukuliwa dukani kwake. Huu ni mwaka wa pili sasa ameambiwa atarudishwa mpaka leo hajarudishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Bwege ametoa malalamiko hapa na ametoa na barua akampa Mwenyekiti kwenye Kiti hapa kwa *ku-quote* na mambo aliyoftuilia juu ya watu wake ambao wamepotea, wametekwa, wamepigwa risasi na hakuna maelezo. Mheshimiwa Kangi mwenyewe amepewa hizo barua wala hajatoa taarifa zozote, kwa hiyo tusifanye mchezo hili jambo ni jambo la kitaifa, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atupe majibu yanayoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kwa sababu nataka kuweka rekodi sawasawa na kwa sababu nimetajwa kama mmoja wa waathirika katika mazungumzo yanayoendelea hapa. Kwa miaka miwili na zaidi nimekuwa nikitajwa na jambo hili nimekuwa nikivumilia, nimekaa kimya muda mrefu sana. Si busara kufanya siasa maisha ya watu. Nataka kwa unyenyekevu sana niombe, si busara kufanya siasa maisha ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili liliponitokea ni miaka miwili na kitu iliyopita, lilipotokea alikuwepo Kamanda wa Polisi wa Mkoa kwenye eneo la tukio, alikuwepo *OCD*, walikuwepo polisi wa kutosha wakati jambo hili linatoka mbele ya macho yao; hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Aliyenyooshewa bastola ni mimi, namfahamu aliyefanya tukio hili, lakini amekuwa akitajwa kwa majina yake na anakofanya kazi na hakuna hatua zilizochukuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuiomba Serikali yangu kwa unyenyekevu sana, naamini hakutumwa na Serikali kufanya alichokifanya, alifanya kwa ujinga wake wa kutotumia busara kutekeleza kazi aliyatumwa. Serikali ni vizuri ikajitenga na matukio haya kwa sababu siamini kama mnawatuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, busara ndogo tu ya kumaliza mambo haya na itasaidia sana ili wanaoutumwa kwenda kutekeleza majukumu wakatumie busara badala ya kuondoa ubinadamu na kujiweka pemberi. Naiomba Serikali yangu... (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Obama, ajiande Mheshimiwa Rehani.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namwomba Mheshimiwa Mchungaji Msigwa arudishe shilingi kwa sababu Waziri wa Mambo ya Ndani amesema vizuri kabisa, kwanza amekiri kwamba ameshayafungulia faili moja baada ya lingine. Kwa hiyo, kwa kuwa yako kwenye ngazi mbalimbali za uchunguzi na kwa kuwa majibu ya uchunguzi hayajatoka na hatuwezi kuyapata hapa Bungeni basi libaki jukumu la Waziri na Serikali. Pindi itakapokuwa imeonekana kuna mambo ya kuweza kutuambia waje watuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kwa muda huu ambao tunapitisha bajeti na kwa kuwa mambo yako kwenye uchunguzi na uchunguzi ukisemwa hapa utaharibu uchunguzi unaoendelea, kwa hiyo naona kwamba Serikali iendelee na kazi yake ya kufanya uchunguzi na ikitokea waje watuambie, lakini shilingi yake apewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Rehani.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nimwombe rafiki yangu, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, arudishe shilingi kwa sababu kwa muda huu wa bajeti kusema kwamba unazuia shilingi na mshahara wa Waziri haitaleta afya wala haitasaidia, kwa sababu uchunguzi ni *process* na ina *stages* zake. Naiomba Serikali iende na mchakato huu, lakini ifike mahali itoe majibu ili hili suala liwe na mwisho kwa sababu kusipokuwa kuna mwisho kila siku litaendelea kuwa linarudiwa. Sasa ifike mahali Serikali itoe maelezo ambayo yataweza kuwa ni kikomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliamini kabisa Jeshi la Polisi, lina vitengo mbalimbali na intelijensia ambayo ni ya hali ya juu ya kuweza kugundua au kuweza kufika mahali kama jambo haligunduliki hatujui, yaani uchunguzi umefika mwisho, kwamba hapa hatuelewi kinachoendelea kama ulivyofanyika uchunguzi katika maeneo mengine kwamba vitu vimekosa kabisa majibu, basi Serikali ifike mahali itoe majibu ya mwisho kwamba hili limeshindikana na hatukupata jibu lake, kwa sababu suala la kupotea watu sio Tanzania, karibu nchi zote matukio yanatokea na hakuna kitu kama hicho kusema kwamba tunazuia bajeti isipite kwa sababu ya uchunguzi wa watu fulani. Uchunguzi uachwe uendelee kwa sababu ni wajibu wa askari na ni *process*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee kusema kwamba hakuna Mtanzania wala mtu mwenye wadhifa Serikalini ambaye akisikia au akiona mtu ameuawa au amepotea ama ametekwa akaona ni jambo la kawaida. Wanachokisema hao na sisi tuna dhamira hiyo hiyo, kwamba matukio haya ambayo yanaripotiwa

kutokea sisi kama Serikali hatuko kimya na hatuvezi kila siku kila kitu tunachochunguza na kukipata halafu kuna mahali tunapeleka mrejesho. Kwa sababu kuna mambo mengine ya kiuchunguzi, hatusemisemi tu kila mahali unapofika, kwa sababu sisi binadamu tulivyo masuala haya ya uchunguzi unawenza ukasema jambo mahali ukidhani unalisema kwa nia njema kwamba Mbunge amesema utee taarifa kumbe taarifa hiyo inaharibu uchunguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Wajumbe waliamini Jeshi la Polisi na katika kuliamini Jeshi la Polisi ambapo sisi tunaendelea na uchunguzi, hakuna kitu chochote ambacho sisi tutaficha. Tutaficha kwa sababu gani? Pia niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, tusichanganye mtu kupotea, mtu kutekwa au mtu kuuawa; makundi hayo matatu yanatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mwingine ambaye anaweza akawa haonekani, mimi nimeshuhudia, nimetembelea migodi wakati ule niko Naibu Waziri kwenye Mazingira, kuna watu nimewakuta kwenye migodi ambao naamini kwao walishafanya na matanga, kwamba huyu alishafariki, kumbe yuko kwenye mgodi harudi nyumbani kwao, lakini huku wanasema kapotea kwa hiyo kafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, huyo ambaye ametekwa lazima tuwe na ushahidi wa huu utekaji vinginevyo tutalaumu Jeshi la Polisi bure. Katika kulilaumu ndipo hapo wanadhani kwamba Serikali inahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema, mambo haya yanapokuwa yanaendelea kusemwa na kusemwa ndio kuharibu uchunguzi. Watuachie sisi Jeshi la Polisi na watuamini tuendelee na uchunguzi. Tena mengine wanachanganya ambayo hatusemi kwa mfano kesi ya Mawazo, kesi ya Mawazo si lazima tuseme kuna watuhumiwa mpaka sasa wako Geita pale. Sasa mnataka tu-*disclose* na vitu vingine ambavyo bado tunaendelea kufuatilia? Hapa wanasema waliomuuwa Mawazo hawajakamatwa lakini

wapo pale Geita. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Msigwa wala asifike hatu ya kupiga kura, anirudishie tu shilingi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, funga hoja yako.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nilitaka hili Bunge Tukufu ambalo sisi ni *elite* katika nchi hii, mia tatu tisini na kitu watu wametuamini, wanategemea tutafanya maamuzi yenye busara kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Sisi ni *tax payer presentative and the best thing God is watching* lakini more than that wananchi waliotupigia kura wanatuangalia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, katika hatua hii sasa...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye hoja, ndiyo na-conclude.

MWENYEKITI: Kama hujaridhika toa hoja.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, si ndiyo nazungumza mpaka nijenge hoja ili kuonyesha sijaridhika.

MWENYEKITI: Aaah, huna haja, umeshajenga hoja toka mwanzo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, si nina dakika zangu? Hizi ni dakika zangu.

MWENYEKITI: Mimi ndiye ninayepanga dakika sasa hivi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, si Kanuni?

MWENYEKITI: Sasa hivi ni mimi hata ukienda kwenye Kanuni.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Kanuni imesema.

MWENYEKITI: Mimi ndiyo nina-*determine*. Kanuni ya mwanzo ulipojenga hoja ni dakika tano, kila aliyechangia hapa ni dakika tatu, sasa hivi napanga mimi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unanipa dakika ngapi?

MWENYEKITI: Sasa nasema hivi, maelezo ya kutosha ulishatoa...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ni-*conclude*.

MWENYEKITI: Hapa *conclusion* yako ni mawili, umeridhika na majibu kama umeridhika unatoa hoja.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *I want to cement my...*

MWENYEKITI: *No, no, no*, toa hoja tumalize hii biashara.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wanaotaka mauaji yaendelee waonekane na sisi wengine tunapingga mauaji. Kwa hiyo, mimi nasema tupige kura ili wananchi waone nani anataka mauaji na nani anataka Jeshi la Polisi...

MWENYEKITI: Wala hiyo siyo hoja...

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MWENYEKITI: Hoja hapa ni shilingi ya Waziri, kaa chini Mheshimiwa Msigwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, kaa chini *please*.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu kuondoa shilingi ya Waziri.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shally Raymond.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama baada ya kujitahidi sana kuelezea kuhusu madeni ya Mamlaka za Maji Tanzania nzima, hizo ni kwenye *utility*, madeni ya maji na umeme. Imekuwa hivyo na siwezi kuzungumzia kila Mamlaka lakini ninayoifahamu zaidi ni ile ya Moshi (MUWSA).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napozungumza sasa hivi MUWSA wanaidai Wizara hii shilingi 2,049,396,154. Mamlaka ndogo kama ile inavyodai hela nyingi kama hizo na Mheshimiwa Waziri anasimama hapa anatoa wito anasema, natoa wito kwa msisitizo Mamlaka za Maji wakarabati visima vyao, watatoa wapi hela ya kukarabati visima? Nimemsikia Mheshimiwa Waziri alivyoeleza kwamba tusubiri mambo yatafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeamua kushika shilingi hii, ni kwamba hata kwenye bajeti hela iliyotolewa ya shilingi 22,800,000 kwa mwaka huu Fungu 28, ukienda lile Fungu 29 unakuta shilingi 24,600,000 hata ingedundulizwa namna gani haitoshi kulipa deni hili. Mamlaka kama MUWSA inazidi kupauka, wafanyakazi 250 pale wanafanya kazi kwa shida, Mamlaka hiyo ndiyo inategemewa kupeleka maji kule kwenye Mamlaka za Miji Midogo ambapo imeshindwa kwenye Wilaya zote Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliwakatia maji CCPikawa ni kilio, Makuruta wakaleta fujo sana. Nina barua hapa zitakuja, barua zikaandikwa Wizara ya Fedha, fedha ikatoka lakini fedha hizo hazikupelekwa Mamlaka ya Maji, Mikoa mingine kama Arusha wakalipwa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kwa nini nisisimame hapa nikakuomba nipate maelezo ya kina na kama sitaridhika basi nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeza sana Mheshimiwa Shally Raymond, kwa kweli hili jambo limemgusa na sisi tunafarijika kuona Waheshimiwa Wabunge kama ye ye wanaguswa sana na changamoto kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba deni hili halikulipwa kwa mwaka wa fedha ambaao unamalizika kama ambavyo madeni mengine yamelipwa, mwaka uliopita tulikuwa na karibu shilingi 15,000,000,000 kwa ajili ya kulipa madeni mbalimbali, kwenye maji peke yake tulilipa karibu shilingi 4,000,000,000 kwa sababu uhakiki haukumalizika kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba uhakiki umeshafanyika na tayari tumeshapeleka Hazina kwa ajili ya malipo kwa mwaka wa fedha ujao. Ni imani yetu kuwa katika mwaka wa fedha ujao deni hili litapatiwa ufumbuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa uhakiki umeshafanywa na na Waziri wa Fedha anatikisa kichwa, kwa hiyo, nafikiri Juni mambo yatakuwa tayari, mkubalie tu Waziri.

MHE. SHALLY J. RAYMOND, Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa na kwa vile nakuamini wewe sana na kwa vile tuko kwenye ile Kamati, nimekubali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi. Kuna methali ya Kiswahili inasema kwamba: "Ukila na kipofu usimshike mkono'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamejinasibu na wamejigamba sana hapa kwamba wataongeza posho, stahiki na mishahara ya wafanyakazi hawa wa Jeshi la Polisi kwa wakati. Hata hivyo, kuna lugha hii ya kwamba tangu niingie kwenye Bunge hili tukizungumza suala la stahiki za askari wanasema kwamba wanarekebisha sheria na kanuni ili kuona kwamba askari hawa wanapata posho zao stahiki na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini askari ambao tunawatetea sisi ni hawa askari wadogo wa chini, nina hakika Inspekta Jenerali Simon Siro baada ya kupandishwa kuwa */GP* mshahara na stahiki zake anazipata. Nina hakika Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri stahiki zao wanazipata lakini askari wadogo hawa hawapati stahiki zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishampa Mheshimiwa Waziri nilishakupa majina ya askari ambaye ametumikia cheo cha Koplo kwa miaka minne hajalipwa mshahara wa Koplo. Amekwenda kozi ya *Sergeant* amejillipia mwenyewe ghamama za kozi sasa hivi ni *Sergeant* hajalipwa mshahara wa Koplo, hajalipwa hizo *areas*. Hawa ndio askari ambao sisi tunawazungumzia na hawa ndio askari ambao wanakupa wewe kiburi na jeuri cha kujitwanga hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka *commitment* ya Serikali utuambie lini watalipwa? Serikali inasema ina fedha za kutosha ni lini mtawalipa askari hawa, walalahoi hawa, wavuja jasho hawa, pesa yao, haki yao. Baada ya mwaka mmoja ukimkuta askari amestaafu utafikiria kama aliyetafunwa akatapikwa kwa sababu kazi hizi zina *stress*, ni ngumu, stahiki zao hamuwapi kwa nini? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitaridhika na majibu ya Waziri nitazuia shilingi yake pamoja na urafiki tulionao.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Mheshimiwa Yussuf, Mbunge wa Chambani, ni rafiki yangu sana wa pete na kidole. Sasa urafiki huu ambao tunanyang'anyana mshahara huu ni urafiki wa kutiwa dowa huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba askari ambao Waheshimiwa Wabunge wote hapa mmewatetea na mmeonyesha jinsi kazi yao ilivyo muhimu katika Taifa hili, wanafanya kazi katika mazingira magumu. Askari hawa tunahitaji kuwapandisha vyeo wapate mishahara mizuri na posho zao, naomba Mheshimiwa aamini kwamba kanuni na sheria tutazipita zote ili kuona stahiki za askari ambazo wamekuwa hawapati ili kuhakikisha wanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba siku za nyuma kulikuwa na kasoro ambazo wenzetu kwenye *payroll point* pale walikuwa wanafanya uzembe kurekebisha mshahara wa askari kwa kupeleka *documents* Utumishi na kwenda Wizara ya Fedha inavyotakiwa. Niliwapa *deadline* na naamini hata haya nayoyasema sasa kuonyesha *seriousness* kwamba Mkuu ye yote wa chombo cha Ulinzi na Usalama kwenye *Payroll points* ambapo nitabaini, maana nimeshawaambia walete mrejesho wa askari wote kuonyesha hawana kasoro, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sina mzaha, hao ambao watakuwa wamekalia hizo stahiki za askari ilhali wanastahili kupata stahiki zao sitawaonea huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu shilingi hiyo unirudishie kwa sababu hii *commitment* niliyoitoa ni dhahiri kabisa kwamba yote yataenda kurekebisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf, hiyo ni kazi ya Kamati na sasa hivi tunaivalia njuga kuhakikisha vyombo hivi vyote vya ulinzi kuanzia Jeshi, Polisi, Magereza, Uhamiaji, *Fire*, wanalipwa stahiki zao. Nikuhakikishie zoezi hilo tunalifanya. Nkuombe tu umrudishie shilingi yake rafiki yako, swahiba wako, jioni mtakunywa mtori pamoja hapo. (*Kicheko*)

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyezekiti, Mheshimiwa Waziri urafiki wetu utakatika kwa saa. Katika stahiki za watu mimi hilo sina mchezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa sababu nilitaka *commitment* aseme ni lini lakini ameshindwa na Serikali inajigamba kwamba fedha inazo, mwaka wa nne bado mnapitia sheria na kanuni tu, mbona zenu mnalipwa kwa wakati, hawa wadogo tu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba suala hili wenzangu waniunge mkono tulijadili ili tupate jibu leo askari hawa watalipwa lini haki zao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud, unachangia au unaunga mkono hoja.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nachangia.

MWENYEKITI: Mheshiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Mbarouk, Mheshimiwa Rukia, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Ndaki na Mheshimiwa Almas. Tunaanza na Mheshimiwa Rukia.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Yussuf Salim. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyezekiti, askari hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, wana-*risk* maisha yao, wanakaa kwenye malindo usiku kucha wanaliwa na mbu watu wamelala ndani, wanafanya kazi ngumu sana halafu

stahiki zao hawapewi hii kwa kweli ni shida. Kwa sababu tukiwa tunawanyima stahiki zao tusipige kelele kama wanachukua rushwa wakati mwingine wanakuwa na hali ngumu ya maisha. Pengine yuko kazini afikiria watoto wake watakula nini, watoto wataka kwenda shule wanataka madaftari, kwa hiyo, akipewa rushwa hawezi kuikataa. Ili tuepukane na rushwa ni lazima hawa watu wapewe stahiki zao. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Yussuf.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ukubali useme ni lini marekebisho haya yatafikia mahali pake, hata kama mimi ni mjambe lakini yanaenda kuathiri hata kiinua mgogo cha askari. Askari ametoka *Sergeant Major* amekwenda kwenye Inspeksa mpaka muda wake wa kustaafu unafika lakini mshahara wake haukupandishwa imekwenda kuathiri mpaka kiinua mgogo chake na wapo wengi na majina yameletwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki niseme mengi kwa sababu waliopo uchawini hawasemi sana wachawi wenzao kwa sababu mimi ni mjambe. Niseme tu waziwazi kwamba hili jambo ni la muda mrefu, kama ni mapitio ya sheria na kanuni yamechukua muda mrefu, toa ahadi ya siku/wakati maalumu haya mambo yatamalizika lini, wWewe ni mwanasiasa mbobezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja Mheshimiwa Yussuf, sisi askari tunawapenda kweli na ndiyo maana tunawatetea. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Almas.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kuniruhusu sana nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi hapa Mheshimiwa Waziri wa Utumishi katika Ofisi ya Rais ametoa tamko la Serikali la kuboresha na kupandisha vyeo stahiki watumishi wote ikiwa ni pamoja na Jeshi la Polisi. Nina hakika tamko la leo la Serikali limefanya *commitment* kwamba askari hawa ni mionganoni mwa watumishi wote wa Serikali ambao wataangaliwa kupandishwa mishahara yao na kulipwa mishahara mizuri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Yussuf.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nataka kusema ni kwamba, najua hata Waziri mwenyewe atakuwa nataka askari wake waweeze kuongezewa mishahara. Unajua ni jambo la kushangaza sana kwamba sisi tunapiga kelele sana huku Upinzani tunataka Polisi waongezewa mishahara na kila siku tunalalamika tunapigwa na Polisi lakini bado tunataka Polisi waongezewa mishahara ninyi huko CCM mnasubiri nini na mko wengi? Hebu tuamue Polisi hawa tuwaongezee mshahara, tukishawaongezee mshahara watafanya kazi vizuri. Askari hawa wanafamilia zao na watoto hawana hata nyumba za kuishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri akubali kwamba hizi fedha ziongezwe na Serikali yetu inakusanya mapato ya kutosha. Polisi nao sasa hivi nao sasa hivi wanakusanya mapato hebu tuwaongeze fedha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Anatropia.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nadhani hili la kuwaongezee mshahara askari siyo la kwetu ni la wale wenye Wabunge wengi ambao ni CCM.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anatropia, toa mchango wako, acha mambo ambayo haya maana yoyote humu ndani.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu...

MWENYEKITI: Unajua lengo lako ni kutaka kuleta *division*, kaa chini. Mheshimiwa Mbarouk. (*Kicheko*)

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi nianze kwa kusema siku zote hakuna shujaa anayekwenda vitani kwa gherama zake. Sasa moja kwa moja niungane mkono na Mheshimiwa Yussuf, Mheshimiwa Waziri ahakikishe ya kwamba anaongeza fedha na anatoa *commitment* ya Serikali kwamba askari wetu waongezewe mishahara na aseme lini wataongezewa mshahara huu kwa sababu askari nao ni binadamu wana watoto, nyumba wanazoishi inabidi wafanye marekebisho wenyewe kwa mishahara midogo waliokuwa nayo na wanasomesha watoto kama sisi. Sasa inakuwaje basi hata roho ya kibinadamu hakuna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Yussuf Waziri aseme lini wanaongezwa mishahara. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndaki, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kinachotaka kujengwa hapa ndani ni kana kwamba Mheshimiwa Waziri ametazama tu jambo hili la kuongeza mishahara na kupandisha vyeo watumishi au maaskari lakini siyo hivyo. Mheshimiwa Waziri amesema anaifuata kanuni, taratibu na sheria ili kwamba aweze kuwaongeza maaskari mishahara yao na wale ambao wanapandishwa vyeo waweze kupata stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hivyo, wewe umetamka hapo kwamba suala hili kama Mwenyekiti umelivilia njuga na kwamba litarekebishwa. Kwa hiyo, si kwamba maaskari hawa Bunge hili au Mheshimiwa Waziri anakataa kuongeza mishahara na stahiki zao, hapana, zitaongezwa lakini kwa kufuata utaratibu ambao umewekwa katika Serikali nzima, siyo kitu cha idara moja. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto.

MHE. VENANCE K. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimuombe Mheshimiwa akubali shilingi ya Mheshimiwa irudishwe kwake kwa sababu jambo hili siyo la kufanya siasa kwamba ionekane kuna upande ambao hautaki polisi wapandishwe mishahara, la hasha! Na Mheshimiwa Mwakajoka amelizungumza vizuri kwamba kama ni kipigo wanapigwa wao, lakini bado wanaombea askari wapewe pesa.

Kwa hiyo, mimi niseme tu kwa kuwa tayari kamati zimeshakaa, zimejadili, na uwezekano mkubwa wa kuongeza fedha upo na mishahara kwa sababu Serikali yetu inakusanya vizuri fedha. Niombe tu tukubali Mheshimiwa alifanyie kazi na Mheshimiwa Mbunge arudishe shilingi ili askari wapewe fedha lakini tusifanye siasa kwenye jambo hili kwa sababu tayari fedha zitaongezwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUUKA, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba mtoa hoja airudishe shilingi kwa Mheshimiwa Waziri, na ninasema hivi kwa sababu kinachoendelea sasa hivi na hasa kwa upande wa *Opposition* tunataka kupotosha mjadala huu kwa kukiuka Kanuni.

Mheshimiwa Mwneyekiti, Kanuni ya 105 haisemi katika maamuzi haya ya sasa kwamba Bunge lako lifanye maamuzi ama ya kuongeza fedha kwenye kifungu chochote, ama

kupunguza fedha kwenye kifungu chochote, kama hoja hiyo iko kimsingi Kanuni ya 105 ndiyo itakayokwenda kutumika. Kwa hiyo kama sasa hivi Bunge hili litafanya mchezo wa kutaka kutengeneza hoja ya kisiasa kwa kufanya maamuzi ya kuonesha kwamba labda upande mmoja unakataa ama upande mmoja haukubali...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUUKA, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: ...si sahihi. Kwa hiyo, sasa hivi kwa hatua tuliyofikia tutafanya maamuzi kwa kuzingatia Randama na hoja iliyopo hapa mezani na hoja nydingine yoyote ambayo kama kuna Mbunge anafikiri inatakiwa kubebewa uzito, itakwenda kwa Kanuni ya 105 na kama kuna Mbunge anataka kuisoma nitaisoma, lakini ni lazima tuheshimu Kanuni na tuzingatie utaratibu wa Bunge.

MWENYEKITI: Ahsante, mtoa hoja hitimisha.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect* kwako wewe ni muislamu na nakuheshimu sana...

MWENYEKITI: Mheshimiwa hatuna masuala ya dini.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Ninachosema, hoja yangu isipotoshwe. Mimi nilitaka Waziri aniambie ni lini askari hawa watapewa stahiki zao? Mshahara mtu akipandishwa cheo cha Koplo unajulikana kwa nini akae miaka minne hapewi? Wakati unajulikana mshahara wa Koplo. Hiyo kanuni ni kanuni gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipotoshwe hii mada, nataka kauli ya Mheshimiwa Waziri lini utawapa, mtu umempandisha Koplo miaka minne hujampa pesa yake utampa lini? Pesa unayo, kanuni ipo isizungushwe hii mkaitia katika siasa, hii ni haki ya watu, nipe, lini utawapa wenyewe

wapo wanakusikia hapo na wewe watakukamata hivyo hivyo ikiwa hukuwapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

MheshimiwaMwenyekiti, ni kweli anachosema Mheshimiwa kwa sababu wengine waliochangia walikuwa wanapotosha hoja ya Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba kama kuna wakati ambapo hatutakiwi kucheza na stahiki za askari na hasa hizo ambazo tayari huyu ameshapandishwa na tunapopandisha maana yake tuliji-*committ* kwamba tutakuwa na uwezo wa kuwalipa, huyo atakuwa anachezea mboni ya jicho la Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeeleza hapa kwamba tumebakiza takribani asilimia 8.1tu katika marekebisho na kasoro ambazo zilikuwepo na zilikuwa kwenye *payroll points* ambapo nimesema, nimekwishawapa *deadline* kwamba ifikapo mwezi Mei, wawe wamekwisha kamilisha zile kasoro ndogo ndogo.

MheshimiwaMwenyekiti, lakini kuna mnyama mmoja anaitwa panya wanasema panya huwa anauma na kupuliza, wametukana mapolisi wangu weee, wametukana, sasa wamefika pahala wanapuliza wanataka kuwaaminisha askari kwamba wao wanawajali sana. Ahsante sana. (*Kicheko*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Yussuf, Waziri ameshatoa *commitment* bado asilimia nane. hoja yako naifunga mimi kwa mujibu wa Kanuni ya 5. Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Ahsante, Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mattar umefuta hoja yako?

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo, nikushukuru kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia katika mchango wangu, Zanzibar kuna vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi ambapo viko kihalali, viko kwa mujibu wa sheria na vitambulisho hivi vilikuwa vina-*function* katika kupatia *passport* na huduma nyingine. Lakini vitambulisho hivi kwa sasa havipatii *passport* na huwezi kutumia kwa huduma nyingine yoyote.

Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekula hasara kubwa kuhakikisha wananchi wake wanapata vitambulisho hivi, na Idara ya Vitambulisho bado ipo na inafanyakazi, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, niiombe *commitment* yake ya uhakika, ni lini vitambulisho hivi vitafanyakazi katika kupatia *passport* kama kitambulisho cha Mtanzania ili wananchi wa Zanzibar waweze kupata huduma hii ya kupata *passport* kwa mujibu wa utaratibu na sheria ya nchi yetu? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ambacho anasema Mheshimiwa Mattar kuhusu vitambulisho hivi. Vitambulisho hivi ni vitambulisho vizuri, vitambulisho muhimu sana, na tunavithamini sana na vinasaidia sana kwa kweli na ndio maana kwa kutambua hilo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwanza kuna mahusiano mazuri kati ya Mamlaka ya Vitambulisho - *NIDA* na Mamlaka ya Vitambulisho - Zanzibar. Lakini jambo ambalo limefanya huu mchakato uchelewe, ni kutokana na mchakato wa maboresho wa vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi ambao unaendelea. Kwa hiyo, mara mchakato huo utakapokuwa

umekamilishwa, mifumo hii miwili itaunganishwa na baada ya hapo vitambulisho vyote viwili vitawezu kutumika. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi niombe avute subira.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mattar hukutoa nia ya kutoa shilingi majibu hayo.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Nimetoa Mheshimiwa nia ya kutoa shilingi, hukunisikia, lakini nimetoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaridhishi na siko pamoja nayo, kwa hiyo ninaomba kutoa hoja Wabunge wenzangu wanisaidie kulijadili hili suala ili Wazanzibar kwa ujumla wapate haki yao ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Hoja haijaungwa mkono, haijafika watu kumi. Tunaendelea Mheshimiwa Kamala. Jamani tuna kanuni hapa na kuna watu wanatazama kanuni zinavyoendesha, hata *referee* akipitisha *penalt za "mazabe"* anashitakiwa. Dkt. Kamala

MHE. BALOZI DKT. DIODOROUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii muhimu, maeneo mengi ya mipakani Tanzania tunapakana na nchi nyingi ndani ya Afrika Mashariki na nyinginezo, lakini kuna utaratibu ambao umebuniwa wa watu kutengeneza fedha kwa kutafsiri sheria wanavyotaka wao na utaratibu wenyewe uliotengenezwa huu baadhi ya maafisa wanatoa kitu kinaitwa *order of departure*. Kwa hiyo wakimtafuta mtu yeoyote yule anayekaa maeneo ya mipakani, kama wanaona ana chochote ambacho anaweza kunyang'anywa, basi ili wamnyang'anye hicho kitu wanamwambia wewe tuna mashaka na uraia wako, kwa hiyo sasa tunakupa *order uondoke*, ukitazama *order zenyewe ninazo nakala hapa*. *Order* yenyewe unakuta amesaini afisa fulani, lakini *paper* yenyewe inatakiwa aliyeipokea asaini hayupo, inatakiwa aliyeifanya kazi asaini hayupo, kwa hiyo huu ni utaratibu

ambao umetengenezwa ndani ya Wizara wa kutengeneza fedha tu na kubughudhi watu eti kwa sababu wanakaa maeneo ya mpakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi wanaenda pale maeneo mengi ya mpakani, kama wakisema fulani mwanaume wana mashaka na uraia wake, wanampa *order of departure*, halafu zile mali ambazo ameachia, mke wake au wake zake wanataka kuzinyang'anya, wananyang'anya mali hizo, lakini Tanzania hatujaweka utaratibu wa watu wanaonyang'anya mali, hizo mali nani anakabidhiwa? Labda Mheshimiwa Waziri akiniambia hiyo leo hii.

Kwa hiyo nitaomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo kwa nini manyanyaso haya yanaendelea ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini baadhi ya watu wanafuatwa usiku wa manane nyumbani kwao, wanatekwa, wanapigwa viboko, halafu baadae wanapewa wanasema *order of departure* wakati hivi vitu vinafanywa na watu wachache tu ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo bila kufanya hivyo nitaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ili pamoja na urafiki nillionao na wewe nichukue walau shilingi...

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini tu Mheshimiwa Balozi Dkt. Kamala ni mtani wangu huyu, nimuombe tu kwamba anirudishie shilingi hiyo wala asiichukue kwa sababu Idara yetu ya Uhamiaji wanaendelea kupambana kwa nguvu zote na wahamiaji haramu na wanapambana nao kwa mujibu wa sheria na hata hiyo *order of departure* ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge ni mojawapo ya sheria ambazo tunazitumia. Sheria nyingine ambayo tunatumia ya kuwaondoa watu nchini hapa ambao wanabainika kwamba wamekuwa ni *prohibited immigrant*, kwa hiyo, tunatoa *notice* kwa ajili ya kuwaondoa hao *prohibited migrant*, lakini

nakubaliana naye kwamba kwa nyakati fulani kumekuwa na malalamiko yanayokuja mpaka Wizarani kwamba wako watu wengine ambao pengine ni *foreigners* wanakuja nchini, wanafanya biashara, biashara inaposhamiri wenzao ambao wanafanya nao biashara ile wanawazunguka na kuwazushia makosa mbalimbali ili waweze kuondoshwa hawa waache mali yao katika nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na inaonekana anam-refer yule dada anaitwa Asimwe ambaye nilienda kwenye kijiji chake cha Bugingo pale, kwamba walimuondosha mume wake na mali zake wakachukua ikiwemo migomba pamoja na ardhi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge hizo karatasi nimemuomba anipatie na pale inapotokea kwamba maafisa wetu wa *Immigration* ambao pengine si waaminifu wanaweza wakawa kweli wame-side na upande fulani kwaajili ya kutaka kudhulamu mali ya mtu malalamiko hayo yafikishwe kwa viongozi wa *Immigration* wa ngazi ya juu ili waweze kuchukua hatua na hizo karatasi nimeziona zinaonesha kwamba sehemu mbili ambako yule aliyepokea ile *order of departure* alipaswa asaini na yule ambaye ameitekeleza alipaswa asaini kwamba zinamapungufu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wananchi ambao wako ndani ya *East Africa* kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki wao ndiyo hizi *order of departure* ambazo tunazitoa, kwa hiyo nimuombe hizo karatasi anikabidhi ili niweze kuzifanyia kazi, na pale itakapobainika kwamba kweli baadhi ya maafisa wetu wanafanya mambo ambayo ni ya rushwa katika kunyang'anya mali za watu tutachukua hatua. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Balozi aiache tu shilingi yangu niende nayo nyumbani kwa ajili ya familia yangu. Ahsante

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi mpe karatasi Mheshimiwa Waziri.

MHE. BALOZI DKT. DIODOROUS B. KAMALA: Mheshimiwa naomba niseme kwa kuwa amekubali hili na

kwa kuwa mimi nilishashiriki kumuongezea mshahara mkubwa zaidi hata ya huu sina sababu ya kutoa shilingi yake.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa muda wetu umefika tunaingia kwenye *guillotine*.

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kif. 1001 –*Administration and HR*

ManagementSh.14,437,065,109/=

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 458,961,054/=

Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 611,426,105/=

Kif. 1004 –*Probation and Community*

Services Division.....Sh. 2,739,329,341/=

Kif. 1005 – *Government Communication*

Unit.....Sh. 168,130,611/=

Kif. 1006 – *Management Information*

System Unit.....Sh.438,468,914/=

Kif. 1007 – *Internal Audit Unit*.....Sh. 202,875,447/=

Kif. 1008 – *Procurement Management*

UnitSh. 323,553,918/=

Kif. 1009 – *Complaints Division*.....Sh. 200,506,101/=

Kif. 1010 – *Legal Services Division*.....Sh. 468,905,738/=

Kif. 2001 – *Registrar of Societies*.....Sh. 118,048,000/=

Kif. 4001 - *Refugees Unit*.....Sh. 739,502,662/=

(Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Kif. 3001 – *Fire and Rescue Services*..... Sh.19,588,035,000/=

Kif. 3002 - *Fire and Rescue Services*

Training Institute.....Sh. 580,509,000/=

Kif. 3003 – *Fire Safety*..... Sh. 140,800,000/=

Kif. 3004 – *Operations*.....Sh. 991,050,000/=

Kif. 3005 – *Dar es Salaam Regional Office*....Sh. 837,900,000/=

Kif. 3006 - *Arusha Regional Office*..... Sh. 592,600,000/=

Kif. 3007 - *Dodoma Regional Office*..... Sh. 491,750,000/=

Kif. 3008 – *Mwanza Regional Office*..... Sh. 772,750,000/=

Kif. 3009 - *Mbeya Regional Office*..... Sh. 381,400,000/=
Kif. 3010 – *Kinondoni Regional Office*..... Sh. 719,109,000/=
Kif. 3011 – *Mara Regional Office*..... Sh. 384,650,000/=
Kif. 3012 – *Kigoma Regional Office*..... Sh. 327,050,000/=
Kif. 3013 – *Pwani Regional Office*..... Sh. 581,450,000/=
Kif. 3014 – *Manyara Regional Office*..... Sh. 350,750,000/=
Kif. 3015 – *Geita Regional Office*..... Sh. 275,500,000/=
Kif. 3016 – *Temeke Regional Office*..... Sh. 788,700,000/=
Kif. 3017 – *Singida Regional Office*..... Sh. 337,900,000/=
Kif. 3018 – *Tabora Regional Office*..... Sh. 463,700,000/=
Kif. 3019 – *Iringa Regional Office*..... Sh. 465,800,000/=
Kif. 3020 – *Rukwa Regional Office*..... Sh. 288,900,000/=
Kif. 3021 – *Ruvuma Regional Office*..... Sh. 413,450,000/=
Kif. 3022 – *Kagera Regional Office*..... Sh. 395,250,000/=
Kif. 3023 – *Mtwara Regional Office*..... Sh. 410,200,000/=
Kif. 3024 – *Lindi Regional Office*..... Sh. 317,150,000/=
Kif. 3025 - *Njombe Regional Office*..... Sh. 282,300,000/=
Kif. 3026 – *Shinyanga Regional Office*..... Sh. 480,100,000/=
Kif. 3027 – *Ilala Regional Office*..... Sh. 780,059,000/=
Kif. 3028 – *Kilimanjaro Regional Office*..... Sh. 527,650,000/=
Kif. 3029 – *Morogoro Regional Office*..... Sh. 550,100,000/=
Kif. 3030 – *Katavi Regional Office*..... Sh. 265,800,000/=
Kif. 3031 – *Tanga Regional Office*..... Sh. 528,100,000/=
Kif. 3032 – *Simiyu Regional Office*..... Sh. 239,150,000/=
Kif. 3033 – *Songwe Regional Office*..... Sh. 206,089,000/=

(Vifungu vilichotajwa hapo juu viliptishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 28 - Jeshi la Polisi

Kif. 1002 – *Finance and Acounts Unit*..... Sh. 413,000,000/=
Kif. 2001 – *Police Main Force* Sh.255,545,860,500/=
Kif. 2002 – *Police Marine*..... Sh. 2,527,516,000/=
Kif. 2003 – *Railway Police Division*..... Sh.1,992,900,000/=
Kif. 2004 – *Police Signals Branch*..... Sh. 2,348,450,000/=
Kif. 2005 – *Police Zanzibar*..... Sh.8,193,620,000/=
Kif. 2006 – *Police Airwing*..... Sh.2,851,200,000/=
Kif. 2007 – *TAZARA Police* Sh.2,428,749,000/=
Kif. 2008 – *Field Force Unit*..... Sh. 2,013,520,000/=

Kif. 2009 – <i>Traffic Police</i>	Sh.1,975,238,000/=
Kif. 2010 – <i>Police Airport</i>	Sh.2,673,294,000/=
Kif. 2011 – <i>Police Dog and Horses</i>	Sh.1,664,259,000/=
Kif. 2012 – <i>Dar ea Salaam Special Zone</i>	Sh.5,373,320,000/=
Kif. 2013 – <i>Police Ilala</i>	Sh.10,904,204,000/=
Kif. 2014 – <i>Police Klnondoni</i>	Sh.11,256,619,000/=
Kif. 2015 – <i>Police Temeke</i>	Sh. 8,865,952,000/=
Kif. 2016 - <i>Police Arusha</i>	Sh.13,817,260,000/=
Kif. 2017 - <i>Police Iringa</i>	Sh. 8,843,130,000/=
Kif.2018 – <i>Police Kilimanjaro</i>	Sh.10,885,192,000/=
Kif.2019- <i>Police Kigoma</i>	Shs.10,036,860,000/=
Kif.2020 – <i>Police Kagera</i>	Sh.12,207,551,000/=
Kif. 2021 – <i>Police Lindi</i>	Sh.6,206,053,000/=
Kif.2022 – <i>Police Mwanza</i>	Sh.12,767,309,000/=
Kif. 2023 – <i>Police Mara</i>	Sh. 8,334,866,000/=
Kif.2024 – <i>Police Tarime, Rarya</i>	Sh. 6,310,016,000/=
Kif.2025 – <i>Police Mbeya</i>	Sh.12,126,067,000/=
Kif. 2026 – <i>Police Mtwara</i>	Sh. 7,257,097,000/=
Kif.2027 – <i>Police Morogoro</i>	Sh.13,788,460,000/=
Kif. 2028 – <i>Police Manyara</i>	Sh. 8,234,406,000/=
Kif.2029 – <i>Police Singida</i>	Sh. 8,338,274,000/=
Kif. 2030 – <i>Police Pwani</i>	Sh.10,183,397,000/=
Kif.2031 – <i>Police Ruvuma</i>	Sh. 7,196,183,000/=
Kif.2032 – <i>Police Rukwa</i>	Sh. 5,858,935,000/=
Kif. 2033 – <i>Police Shinyanga</i>	Sh. 6,716,774,000/=
Kif. 2034 – <i>Police Tabora</i>	Sh. 7,647,496,000/=
Kif.2035 – <i>Police Tanga</i>	Sh. 10,016,715,000/=
Kif.2036 – <i>Police Mjini Magharibi</i>	Sh.12,907,458,000/=
Kif. 2037 – <i>Police Kusini Unguja</i>	Sh. 5,887,400,000/=
Kif. 2038 – <i>Police Kaskazini Unguja</i>	Sh. 5,345,317,000/=
Kif. 2039 – <i>Police Kusini Pemba</i>	Sh. 4,222,627,000/=
Kif. 2040 – <i>Police Kaskazini Pemba</i>	Sh. 4,309,822,000/=
Kif.2041 – <i>Police Dodoma</i>	Sh.10,679,628,000/=
Kif. 2042 – <i>Police Geita</i>	Sh. 7,084,352,000/=
Kif. 2043 – <i>Police Katavi</i>	Sh. 4,068,456,000/=
Kif. 2044 – <i>Police Njombe</i>	Sh. 4,349,880,000/=
Kif. 2045 – <i>Police Simiyu</i>	Sh. 4,844,894,000/=
Kif. 2046 – <i>Police Songwe</i>	Sh.105,000,000/=
Kif. 2047 – <i>Police Rufiji</i>	Sh.104,000,000/=
Kif. 3001 – <i>Police College Moshi</i>	Sh. 5,302,495,000/=

Kif.3002 – Police CollegeSh.2,442,357,000/=
Kif. 4001 – Police Vehicles Maintenance
Unit.....Sh. 3,493,558,000/=
Kif. 5001 – Police Medical UnitSh.2,692,892,000/=
Kif. 6001 – Police Building Brigade.....Sh. 6,679,900,000/=
Kif. 7001 – Criminal Investigation Division ...Sh. 8,014,321,500/=
Kif. 7002 – Stock Theft Prevention Unit.....Sh. 1,155,090,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 29 – Jeshi la Magereza

Kif.1001 – Prisons Headquaters.....Sh. 7,932,270,000/=
Kif. 1002 – Finance and Accounts.....Sh. 304,550,000/=
Kif. 2001 – Parole Department.....Sh. 1,052,339,000/=
Kif.2002-Prisons Welfare and
Rehabilitation.....Sh.148,182,167,000/=
Kif. 2003 – Resettlement of OffendersSh. 4,244,827,000/=
Kif. 2004 – Prisons ArushaSh. 863,836,000/=
Kif. 2005 – Prisons Dar es SalaamSh. 2,072,375,000/=
Kif. 2006 – Prisons Dodoma.....Sh. 950,765,000/=
Kif. 2007 – Prisons Kigoma.....Sh. 494,345,000/=
Kif. 2008 – Prisons Tanga.....Sh. 713,968,000/=
Kif. 2009 – Prisons Kagera.....Sh. 612,739,000/=
Kif.2010 – Prisons Mwanza.....Sh. 1,005,914,000/=
Kif. 2011 – Prisons Tabora.....Sh. 707,075,000/=
Kif. 2012 – Prisons Mbeya.....Sh. 930,963,000/=
Kif. 2013 – Prisons Singida.....Sh. 546,359,000/=
Kif. 2014 – Prisons Coast.....Sh. 872,154,000/=
Kif. 2015 – Prisons Lindi.....Sh. 601,522,000/=
Kif. 2016 – Prisons Manyara.....Sh. 464,496,000/=
Kif. 2017 – Prisons Mtwara.....Sh. 721,645,000/=
Kif. 2018 – Prisons Ruvuma.....Sh. 523,632,000/=
Kif. 2019 – Prisons Rukwa.....Sh. 611,899,000/=
Kif. 2020 – Prisons Mara.....Sh. 635,005,000/=
Kif. 2021 – Prisons Iringa.....Sh. 616,423,000/=
Kif. 2022 – Prisons Kilimanjaro.....Sh. 734,744,000/=
Kif.2023 – Prisons Morogoro.....Sh. 1,607,633,000/=
Kif. 2024 – Prisons Geita.....Sh. 34,140,000/=

Kif. 2025 – *Prisons Katavi*.....Sh. 22,240,000/=
Kif. 2026 – *Prisons Njombe*.....Sh. 22,900,000/=
Kif. 2027 – *Prisons Simiyu*..... Sh. 26,240,000/=
Kif. 2028 – *Prisons Shinyanga*.....Sh. 540,143,000/=
Kif. 3001 – *Ukonga Prisons Staff College*.....Sh. 3,307,400,000/=
Kif. 3002 – *Kingolwila Prisons Driving School*.....Sh. 477,983,000/=
Kif. 3003 – *Ruanda Prisons Trade School*.....Sh. 945,839,000/=
Kif. 3004 – *Prisons College Kiwira*.....Sh. 1,668,791,130/=
Kif. 4001 – *Prison Building Brigade*.....Sh. 1,055,740,000/=
Kif. 4002 – *Prison Industries*.....Sh. 587,161,000/=
Kif. 4003 – *Prison Farms*.....Sh. 1,246,452,080/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

Kif. 2001 – *Immigration Zanzibar*.....Sh. 5,520,684,000/=
Kif. 2002 – *Immigration Head Quarter*.....Sh. 37,017,707,000/=
Kif. 2003 – *Immigration Ilala*.....Sh. 34,200,000/=
Kif. 2004 – *TZ Regional Immigration Training Academy*.....Sh. 94,612,000/=
Kif. 2005 – *Immigration Kinondoni*.....Sh. 34,800,000/=
Kif. 2006 – *Immigration Temeke*.....Sh. 34,200,000/=
Kif. 2007 – *Immigration Arusha*.....Sh. 56,340,000/=
Kif. 2008 – *Immigration Dar-es-Salaam*.....Sh. 82,290,000/=
Kif. 2009 – *Immigration Dodoma*.....Sh. 51,756,000/=
Kif. 2010 – *Immigration Geita*.....Sh. 53,620,000/=
Kif. 2011 – *Immigration Iringa*.....Sh. 46,050,000/=
Kif. 2012 – *Immigration Kilimanjaro*.....Sh. 45,369,996/=
Kif. 2013 – *Immigration Kigoma*.....Sh. 71,290,000/=
Kif. 2014 – *Immigration Katavi*.....Sh. 61,550,000/=
Kif. 2015 – *Immigration Kagera*.....Sh. 70,330,004/=
Kif. 2016 – *Immigration Lindi*.....Sh. 45,119,996/=
Kif. 2017 – *Immigration Mwanza*.....Sh. 50,220,000/=
Kif. 2018 – *Immigration Manyara*.....Sh. 58,220,004/=
Kif. 2019 – *Immigration Mbeya*.....Sh. 70,639,996/=
Kif. 2020 – *Immigration Morogoro*.....Sh. 72,760,000/=
Kif. 2021 – *Immigration Mtwara*.....Sh. 52,559,996/=

Kif. 2022 – <i>Immigration Mara</i>	Sh. 57,880,000/=
Kif. 2023 – <i>Immigration Njombe</i>	Sh. 41,780,000/=
Kif. 2024 – <i>Immigration Pwani</i>	Sh. 53,120,000/=
Kif. 2025 – <i>Immigration Ruvuma</i>	Sh. 52,859,996/=
Kif. 2026 – <i>Immigration Rukwa</i>	Sh. 56,630,004/=
Kif. 2027 – <i>Immigration Simiyu</i>	Sh. 49,280,004/=
Kif. 2028 – <i>Immigration Singida</i>	Sh. 43,180,000/=
Kif. 2029 – <i>Immigration Shinyanga</i>	Sh. 49,640,000/=
Kif. 2030 – <i>Immigration Tanga</i>	Sh. 70,480,004/=
Kif. 2031 – <i>Immigration Tabora</i>	Sh. 56,790,004/=
Kif. 2032 – <i>Immigration Songwe</i>	Sh. 62,330,004/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 14 - Zimamoto na Uokoaji

Kif. 3001 – <i>Fire and Rescue Service</i>	Sh. 4,500,000,000/=
--	---------------------

Fungu 28 - Jeshi la Polisi

Kif. 2001– <i>Police Main Force</i>	Sh. 792,924,679/=
Kif. 2005 – <i>Police Zanzibar</i>	Sh. 500,000,000/=
Kif. 2020 – <i>Police Kagera</i>	Sh.1,400,000,000/=
Kif. 2025 – <i>Police Mbeya</i>	Sh. 50,000,000/=
Kif. 2041 – <i>Police Dodoma</i>	Sh. 0
Kif. 2044 – <i>Police Njombe</i>	Sh. 0
Kif. 2045 - <i>Police Simiyu</i>	Sh. 50,000,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 29 - Jeshi la Magereza

Kif. 2002 – <i>Prisons Welfare and Rehabilitation</i>	Sh. 0
Kif. 4001 – <i>Prison Building Brigade</i>	Sh. 0

Kif. 4002 – *Prison Industries*Sh. 2,000,000,000/=
Kif. 4003 – *Prison Farms*.....Sh. 5,000,000,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji

Kif. 2002 – *Immigration Head Quarter*.....Sh. 0

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. MOSSY LUKUVI - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea. Tukae. Mtoa hoja.

TAARIFA

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hongera sana wewe na Naibu wako, lakini pamoja na makamanda wote wa vyombo hivi vya ulinzi vya Wizara ya Mambo ya Ndani, ni kweli mnafanya kazi nzuri sana lakini suala la watu kupewa *PI* kwa kweli linaumiza watu na sheria tunapitisha Bunge, *PI* haandiki kila mtu kuna mtu mwenye cheo maalum ambaye ndiye anatakiwa aandike. Sasa mkiachia kila mtu anaandika *PI* kuwafukuza watu sababu tu wanaelewana mitaani, haki za watu zinakosekana. Kwa hiyo, mlisimamie na hizo karatasi mzichunguze, kama kuna hujuma yoyote aliyofanyiwa mtu kunyimwa haki yake chukueni hatua kwa wote ambao waliohusika.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo na tangazo hili limesisitizwa na Mheshimiwa Spika; Waheshimiwa Wabunge wote kwamba *referee* wa mchezo wa kesho wa soka kati ya *Bunge Sports Club* na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, atakuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. (*Makofi*)

Aidha, washika vibendera kwenye mchezo huo watakuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Job Ndugai na Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zuberi Maulid. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wahudhurie mpambano huo, mchezo utaanza saa kumi jioni kwenye uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma, wote mnakaribishwa. (*Makofi*)

Baada ya maneno haya nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyofanya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Bunge lilahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 29 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)

